MAFUNDISHO

YA

BUDDHA



GURUDUMU LA DHARMA

Gurudumu la Dharma ni tafsiri ya neno la Sankrit "Dharmacakra". Kama lilivyo gurudumu la mkokoteni liendealo kuzunguka linaonyesha alama ya Mafundisho ya Buddha kadri yanavyozidi kuenezwa kwa mapana bila kikomo. Midenge minane katikati ya gurudumu inawakilisha Njia Kuu nane za U-Buddha, Mwelekeo muhimu zaidi wa Matendo. Njia Kuu nane ni mtizamo sahihi, mawazo sahihi, matamshi sahihi, tabia sahihi, maisha sahihi, juhudi sahihi, fikara sahihi na tafakuri sahihi. Katika siku za kale kabla ya sanamu na mifano mingine ya Buddha havijatengenezwa, Gurudumu hili la Dharma lilitumika kama kifaa cha kuabudu. Kwa wakati huu, Gurudumu linatumika Kimataifa kama alama muafaka ya U-Buddha.

Haki ya chapa © 1966 na **BUKKYŌ DENDŌ KYŌKAI**

Sehemu yoyote ya kitabu hiki inaweza kunukuliwa bila kungoja ruhusa. Tunaloomba tu ni kwamba shukrani za kunukuru ziwaendee **Bukkyō Dendō Kyōkai**, Tokyo na nakala moja ya toleo itumwe kwetu.
Tunatoa shukrani.

BUKKYŌ DENDŌ KYŌKAI
(Taasisi ya Uenezaji wa U-Buddha)
3-14, 4-Chome, Shiba,
Minato-Ku, Tokyo, Japan, 108-0014
Simu: (03) 3455-5851
Fax: (03) 3798-2758
E-mail:bdkmibwm@tky.3web.ne.jp
Toleo 1a kwanza, 1998

Kimechapishwa na
Kampuni ya uchapishaji ya Kosaido
Tokyo, Japan.

Hekima ya Buddha ni pana kama bahari na Roho yake imejaa Huruma tele.

Buddha hana umbo wala sura bali hujibainisha Mwenyewe kwa ubora wake na hutuongoza kwa moyo wake wote wa Huruma.

Kitabu hiki ni cha thamani kubwa kwani kinabeba kiini cha mafundisho ya Buddha kama yalivyoandikwa katika juzuu zaidi ya elfu tano. Mafundisho haya yametunzwa na kurithishwa kwa zaidi ya miaka elfu mbili na mia tano yakienea nje ya mipaka ya nchi na vizingiti vya rangi za ulimwenguni.

Maneno ya Buddha yaliyomo ndani ya kitabu hiki hugusa sehemu zote za maisha ya binadamu na huyafanya yawe na maana.

DHAMMAPADA

Chuki haimalizwi na chuki katika dunia hii. Chuki humalizwa na upendo peke yake. Hii ni kanuni ya zama za kale.

Mjinga anayefikiri kuwa yeye ni mjinga, kwa wazo hilo yu mwerevu. Mjinga ajifikiriaye kuwa mwerevu ni mjinga hasa.

Hata kama angeteka watu elfu mara elfu katika uwanja wa mapambano, ni bure; ni heri yeye aitekaye nafsi yake, huyo yu shujaa mwenye enzi.

Hata kama ataishi miaka mia moja bila kuona utakaso wa kweli ni kazi bure, ni bora yule aishiye siku moja na kuuona utakaso wa kweli.

Taabu ipo kwenye uzawa kama binadamu, taabu ndiyo maisha ya mauti, Taabu ndiyo isikikayo katika utakaso wa kweli, Taabu pia ni katika kuonekana kwa Buddha.

Bila kutenda maovu, bali kupanda wema, kutakasa roho zetu, - Huo ndio ushauri wa Mabuddha.

Hakuna wana wa kuwekewa kinga, hakuna kinga ya baba wala mwanaukoo kwani yeye aliyeshindwa na kifo hawezi kupata ulinzi wowote kutoka kwa nduguye.

YALIYOMO

BUDDHA

SURA YA KWANZA : Shakyamuni Buddha 2
I Maisha ya Buddha 2
II Mafundisho ya Mwisho ya Buddha 10
SURA YA PILI : Utukufu wa Buddha 14
I Huruma na Maadili yake 14
II Msaada na Wokovu aliotuletea Buddha 17
III Buddha Aishiye milele 21
SURA YA TATU : Umbile la Buddha na Maadili Yake 24
I Sura Tatu za mwili wa Buddha 24
II Buddha anavyojitokeza 27
III Maadili ya Buddha 30

DHARMA

SURA YA KWANZA : Chanzo 36
I Unne wa Ukweli Bora 36
II Chanzo 39
III Chimbuko Tegemezi 40
SURA YA PILI : Nadharia ya Ubinafsi 44
I Ubinafsi usio wa kudumu 44
II Nadharia ya Tabia ya Binadamu 47

III Hali Halisi ya Mambo 49
IV Njia Panda 54
SURA YA TATU : Hali ya Buddha 61
I Moyo wa Utakaso 61
II Hali yake 66
III Kutokuwa na Ubinafsi 71
SURA YA NNE : Uchafu 76
I Uchafu wa Binadamu 76
II Hali na Tabia ya binadamu 83
III Maisha ya Binadamu 84
IV Ukweli wa Maisha ya Binadamu 89
SURA YA TANO : Faraja iletwayo na Buddha 96
I Nadhili za Amida Buddha 96
II Nchi iliyo takatifu ya Amida Buddha 104

NJIA YA UTENDAJI

SURA YA KWANZA : Njia ya Kutakata 108
I Utakaso wa Moyo wa Binadamu 108
II Matendo mema 115
III Mafundisho ya hadithi za Kale 126
SURA YA PILI : Kufanikiwa kwa Vitendo 139
I Kutafuta Ukweli 139
II Njia za Matendo 150
III Njia ya Imani 162
IV Methali Takatifu 168

UNDUGU

SURA YA KWANZA : Wajibu wa Undugu 178
I Ndugu wasio na makao 178
II Wafuasi wa Ulei 183
SURA YA PILI : Mwongozo wa Kuishi kwa Vitendo 194
I Maisha ya familia 194
II Maisha ya Wanawake 203
III Maisha ya Huduma 210
SURA YA TATU : Ujenzi wa Nchi ya Buddha 220
I Udugu wenye Masikilizano 220
II Nchi ya Buddha 227
III Walioupokea Utukufu Katika Nchi ya Buddha 232

Chimbuko la Rejea

I Historia Fupi ya Buddha 250
II Kuenezwa kwa Mafundisho ya Buddha 259
III Historia ya "Mafundisho ya Buddha" 262
IV Faharisi ya "Mafundisho ya Buddha" 264
V Sherehe ya Sanskrit 273
VI Aṅguttara Nikāya 279

BUDDHA

SURA YA KWANZA

SHAKYAMUNI BUDDHA

I
MAISHA YA BUDDHA

1. Watu wa ukoo wa Shakya waliishi kandokando ya Mto Rohini utiririkao kusini katika mitelemko ya milima ya Himalaya. Mfalme wao Shuddhodana Gautama, alianzisha maskani yake Kapilavastu na akajenga ngome kubwa, akatawala kwa busara, hivyo akapendwa na watu wake wote.

Malkia aliitwa Maya. Alikuwa binti wa mjomba wake Mfalme ambaye naye alikuwa mfalme wa jirani kutoka pia katika nasaba ya Shakya.

Kwa muda wa miaka ishirini hawakupata mtoto. Ila usiku mmoja Malkia Maya alipata ndoto ya ajabu, alimwona tembo mweupe akiingia tumboni mwake kupitia upande wa kulia wa kifua chake naye akawa mja mzito. Mfalme na watu wake walikuwa na shauku kubwa ya kupata mtoto wa kifalme. Kufuatana na desturi zao Malkia ilimpasa arudi kwa wazazi wake ili ajifungue, na alipokuwa njiani, wakati wa kijua kikali cha vuli aliamua kupumzika katika Bustani ya Lumbini.

Kila upande alikuwa amezungukwa na maua mazuri ya Ashoka. Kwa furaha aliinua mkono wake wa kulia kukongonyoa tawi na katika kufanya hivyo mtoto wa kiume alizaliwa. Watu

wote walionyesha furaha zao za dhati kwa utukufu wa Malkia na mtoto wake, Mbingu na dunia vilishangilia. Siku hii ya kukumbukwa siku zote ilikuwa siku ya nane ya mwezi wa Aprili.

Mfalme alijiwa na furaha ya kupindukia na akamwita mtoto, Siddhartha lenye maana "Kila ombi limetimizwa".

2. Hata hivyo furaha katika maskani ya Mfalme ilifuatwa na huzuni, kwani baada ya siku chache Malkia mpendwa Maya alikufa ghafla. Mahaprajapati, mdogo wake marehemu Malkia alimchukua mtoto na kumlea kwa mapenzi makubwa.

Mtawa mmoja aitwaye Asita, aliyeishi katika milima ya karibu, aliona mwanga mkali katika ngome ya mfalme. Akiitafsiri kuwa ni ishara ya nyota njema alikuja nyumbani kwa Mfalme na akaonyeshwa mtoto. Alitabiri kuwa "kama huyo mwana wa Mfalme angeishi ndani ya Ikulu angekuwa Mfalme mkuu wa ajabu na kwamba angetawala dunia nzima. Lakini kama angeghairi maisha hayo na kufuata maisha ya kidini, angekuwa Buddha, Mwokozi wa dunia."

Mwanzoni Mfalme alifurahiwa sana na utabiri huo, lakini baadaye alianza kuingiwa na waisiwasi juu ya mwanae wa pekee, kuacha maskani yake na kuishi maisha ya upweke.

Alipopata umri wa miaka saba mwana wa Mfalme alianza mafunzo ya maendeleo ya jamii na kijeshi lakini mawazo yake yalielekea kwenye mambo mengine. Siku moja mnamo majira ya

vuli alitoka nje ya mji na babaye. Wakiwa wanamwangalia mkulima mmoja akilima kwa plau shambani mwake alimwona ndege akishuka ardhini na kumchukua mnyoo aliyefunuliwa na plau. Aliketi chini katika kivuli cha mti na kuwaza juu ya tukio hilo huku akinong'ona:

"Lo! je, viumbe vyote hai huuana?"

Mwana huyo wa Mfalme, aliyekuwa amempoteza mama aliguswa sana na mkasa wa viumbe hao wadogo.

Jeraha hilo liliongezeka rohoni mwake siku hadi siku kadri alivyoendelea kukua; jinsi liwavyo kovu dogo juu ya mti mchanga, maumivu katika maisha ya binadamu yalizidi kupenyeza kwa nguvu ndani ya moyo wake.

Mfalme aliendelea kuwa na mashaka alipokumbuka utabiri wa yule mtawa kwa hiyo alijitahidi kwa kila hali kumchangamsha na kumtia moyo mwanae ili amgeuze mawazo yake.

Mfalme alimwoza mwanae alipofikisha umri wa miaka 19, kwa Binti Yashodhara. Alikuwa binti yake Suprabudha, Hababi wa ngome ya Devadaha ambaye pia alikuwa kaka yake marehemu Malkia Maya.

3. Kwa muda wa miaka kumi Mwana wa Mfalme alizunguka katika vibanda wakati wa majira mbalimbali akazama katika muziki, ngoma na anasa lakini kila wakati mawazo yake yaliguswa na swala la mateso na kwa huzuni alijitahidi kuelewa maana halisi

ya maisha ya binadamu.

"Anasa za barazani kwa Mfalme, afya nzuri ya mwili huu, raha hizi za ujana, vina maana gani kwangu? " aliwaza. "Kuna siku tutakuwa wagonjwa, tutazeeka, kifo hakiepukiki. Kiburi cha ujana, kiburi cha afya nzuri, kiburi cha kuwa hai - watu wote werevu wanapaswa kuyatupilia mbali mambo haya."

"Mtu apambanaye na maisha hana budi kutafuta kitu cha thamani. Kuna njia mbili za kuangalia - njia adilifu na njia potofu. Akitazama katika njia potofu anatambua kuwa magonjwa, uzee na kifo haviepukiki, lakini hutafuta kinyume cha hayo.

"Akiangalia katika njia adilifu anatambua ukweli juu ya magonjwa, uzee na kifo na kutafuta maana ambamo kwayo mateso ya binadamu yamefichika. Katika maisha yangu ya anasa mwelekeo wangu ni katika njia potofu."

4. Hivyo mapambano ya kiroho yaliendelea katika moyo wa mwana wa mfalme hadi mtoto wake wa pekee, Rahula, alipozaliwa wakati yeye akiwa na umri wa miaka 29. Tukio hilo liliyaelekeza mambo kwenye upeo, kwani hatimaye aliamua kuhama katika maskani ya kifalme na kutafuta suluhisho la kutotulia kiroho katika maisha ya kimaskini yasiyo na makao. Usiku mmoja aliondoka kwenye ngome akiwa tu na mwendesha gari la kukokotwa aitwaye Chandaka, pamoja na farasi wake mweupe aitwaye Kanthaka.

Uchungu haukumwishia na mashetani wengi walimjaribu

wakisema: "Ingefaa urudi katika ngome yako kwani hivi karibuni dunia nzima itakuwa yako. Lakini alimwambia ibilisi kuwa hana haja na dunia nzima. Hivyo alinyoa nywele na kuelekeza hatua zake kusini akiwa amebeba bakuli la omba omba mkononi mwake.

Kwanza mwana wa Mfalme alimwendea Mtawa Bhagava na kuangalia majaribio yake ya utawa. Pia alikwenda kwa Arada Kalama na Udraka Ramaputra kujifunza njia zao za kupata Wongofu kwa njia ya taamuli, lakini baada ya kuyafanyia mazoezi kwa muda, aliamini kuwa hayatamfikisha katika Wongofu. Hatimaye alikwenda katika nchi ya Magadha na kuishi maisha ya utawa katika msitu wa Uruvilva ukingoni mwa mto Nairanjana, utiririkao katika bonde la kijiji cha Gaya.

5. Majaribio ya utawa aliyoyafanya yalikuwa magumu kupindukia. alisukumwa na wazo kuwa:

"Hapajakuwepo mtakatifu yeyote katika enzi zilizopita, wala zilizopo na hata zijazo ambaye alitafuta au atatafuta wongofu kuliko nifanyavyo mimi."

Bado mwana wa mfalme hakuweza kufaulu kufikia lengo lake. Baada ya miaka sita msituni aliacha maisha ya majaribio ya utawa.

Alikwenda kuoga mtoni na akakubali bakuli lenye maziwa la Sujata, mwanamwali aliyeishi katika kijiji cha jirani.

Waandamizi watano walioishi na mwana wa Mfalme katika muda wa miaka 6 ya maisha yake ya utawa walishtushwa na kitendo chake cha kupokea maziwa kutoka mkononi mwa mwanamwali; Walimwona kama amejidhalilisha nao wakamuacha.

Hivyo basi Mwana wa Mfalme aliachwa peke yake. Alikuwa bado dhaifu lakini hata katika hatari ya kupoteza maisha yake alijaribu tena kipindi cha kutafakari, akijisemea moyoni mwake. "Damu yaweza kuchoka, mwili waweza kuoza, mifupa yaweza kutawanyika lakini katu sitapaacha mahali hapa hadi nipatapo njia ya wongofu."

Mapambano yake yalikuwa ya nguvu na yasiyo na mfano. Aliingiwa na mawazo mchanganyiko na kukaribia kukata tamaa, vivuli vya giza vilitishia roho yake, na alisongwa sana na vishawishi vyote vya mashetani. Kwa saburi na uangalifu mkubwa alivichambua kimoja baada ya kingine na mwisho alivikataa vyote. Yalikuwa ni mapambano magumu hasa yaliyosababisha damu yake kupungua, mwili wake kusinyaa na mifupa yake kupasuka.

Lakini nyota ya asubuhi ilipotokea katika anga ya mashariki, mapambano yalimalizika na moyo wake ukawa safi na kung'ara kama jua la asubuhi. Hatimaye, alikuwa amegundua njia sahihi ya Wongofu. Ilikuwa siku ya nane mwezi wa Desemba, na Mwana wa Mfalme alikuwa Buddha akiwa na umri wa miaka 35.

6. Kuanzia wakati huo Mwana wa Mfalme alijulikana kwa

majina mbali mabali: Wengine walimwita Buddha, Mwongofu Aliyekamilika Tathagato, Wengine walimwita Shakyamuni, mwenye hekima katika ukoo wa Shakya, wegine walimwita Aheshimiwaye na dunia.

Kwanza alikwenda Mrigadava Varanasi ambapo omba omba watano alioishi nao katika maisha ya majaribio ya utawa kwa muda wa miaka sita walipokaa. Mwanzoni walimpuuza, lakini baada ya kuzungumza naye, walimwamini na wakawa wafuasi wake wa kwanza. Kisha alielekea katika Ngome Rajariha kumwongofya Mfalme Bimbisara aliyekuwa rafiki yake wa siku nyingi. Kutokea hapo alizungukia nchi nzima akiishi kwa sadaka huku akiwahubiri watu kukubali na kupokea njia ya maisha yake.

Watu walimwitikia kama kiu kitafutavyo maji na njaa itafutavyo chakula. Wanafunzi wa kwanza wawili, Sariputra na Mandgalyayana, pamoja na wafuasi wao elfu mbili walikuja kwake.

Hapo mwanzo baba yake Buddha, Mfalme Shuddhodana, akiwa bado ana uchungu kwa ajili ya uamuzi wa mwanae kuhama maskani yake alikaa pembeni ila baadaye akawa mwanafunzi wake mwaminifu. Mahaprajapori alikuwa mama yake wa kambo na Buddha, na Binti Mfalme Yashodhara, mke wake na wanaukoo wote wa Shakya walianza kumfuata. Umati wa watu wengine walimwamini na kuwa wafuasi wake watiifu.

7. Kwa muda wa miaka arobaini na tano Buddha alizunguka

akihubiri na kushawishi watu kufuata njia yake ya maisha. Lakini alipopata umri wa miaka themanini, akiwa Vaisali na njiani kutoka Rajagriha kwenda Shravasti, aliugua na akatabiri kuwa baada ya miezi mitatu ataingia Nirvana. Hata hivyo aliendelea na safari yake hadi Pava ambapo aliugua sana kutokana na chakula alichopewa na mhunzi aliyeitwa Chunda. Hatimaye, ingawaje alikuwa na maumivu na unyonge wa mwili, alifika katika msitu ukingoni mwa Kusinagara.

8. Chini ya uongozi wa Ananda, mwanafunzi aliyempenda sana Buddha, mwili wake ulichomwa moto na marafiki zake huko Kusinagara.

Watawala saba majirani pamoja na Mfalme Ajatasatru walidai vitu na mabaki ya Buddha vigawanywe kati yao. Watu wa Kusinagara kwanza walikataa madai hayo kiasi cha mzozo huo kutaka kuishia kwenye vita, lakini kwa ushauri wa mtu mmoja mwenye busara aitwaye Drana, mzozo ulikwisha na mabaki yakagawanywa kati ya nchi kubwa nane. Majivu ya lundo la kuni la kuchomea maiti pamoja na gudulia la kutunzia mabaki yaligawiwa kwa watawala wengine yakapewa pia heshima ile ile. Hivyo basi minara mikubwa kumi kwa ukumbusho wa Buddha ilijengwa kuhifadhi mabaki na majivu yake.

II
MAFUNDISHO YA MWISHO YA BUDDHA

1. Chini ya miti iitwayo Sala huko Kasinagara, katika maneno yake ya mwisho kwa wanafunzi wake, Buddha alisema:-

" Kuweni mwanga. Jitegemee, msimtegemee mtu awaye yoyote. Fanya mafundisho yangu mwanga wenu. Yaamini hayo tu: Msitegemee mafundisho mengine yoyote.

Fikiria miili yenu: Fikiri unajisi wake. Mkijua ya kwamba maumivu na furaha yake vyote ni chimbuko la mateso, unawezaje kujihusisha katika tamaa zake? Fikiria nafsi yako, fikiria kupita kwake, unaweza kudanganyikaje, ukijivuna na kutamani huku ukijua kuwa mwisho wa yote ni mateso? Fikiria vitu vyote, nini kati ya hivyo vinadumu? Je vyote si kusanyiko ambalo kitambo tu vitatenganika na kusambaratika? Msihadaiwe na mateso ya ulimwengu, bali fuata mafundisho yangu, na hata baada ya kifo changu mtaondokana na uchungu. Fanya hivi na hakika mtakuwa mitume wangu."

2. "Mitume wangu, mafundisho niliyokupeni si ya kusahauliwa au kuachwa. Ni ya kutunzwa, ya kufikiriwa na ya kujaribiwa. Mkifuata mafundisho haya mtakuwa wenye faraja siku zote.

"Maana ya mafundisho ni kuiongoza roho yako. Epukana na tamaa na tabia zenu zitakuwa njema, roho zenu zitakuwa safi

na maneno yenu yatakuwa ya kuaminika. Daima, kwa kufikiria ufupi wa maisha yenu, mtaweza kushinda tamaa na hasira na mtaweza kujiepusha na maovu yote.

"Mkiona roho zenu zinajaribiwa na kuzingirwa na tamaa yawapasa kuyakandamiza na kuyashinda majaribu,kuweni na amri juu ya nafsi zenu.

"Nafsi ya mtu inaweza kumfanya awe Buddha au inaweza kumfanya awe mnyama. Akitawaliwa na makosa, anakuwa Ibilisi, akiongoka huwa Buddha. Kwa hiyo itawale nafsi yako na kamwe usipotoke.

3. Heshimianeni ninyi kwa ninyi, fuata mafundisho yangu, kwenu pasiwepo faraka, msitengane kama maji na mafuta, lakini changanyikaneni kama maji na maziwa.

Someni kwa pamoja jifunzeni kwa pamoja. Msipoteze mawazo na muda wenu katika uzembe na mabishano. Furahieni maua ya wongofu wakati wa msimu wake na vuneni matunda ya njia ya kweli.

"Mafundisho niliyokupatieni nami niliyapata kwa kuifuata njia hiyo. Inakupaseni kufuata mafundisho haya na kuzingatia maadili yake kila wakati.

"Ukiyapuuza, ina maana kuwa kwa hakika hukuwahi kuwa nami. Hii ina maana kuwa uko mbali na mimi ingawa kwa kweli

upo pamoja nami, lakini ukiyakubali na kuyazingatia mafundisho yangu, basi upo karibu sana nami hata kama utakuwa mbali nami."

4. "Wanafunzi wangu, mwisho wangu umekaribia, kuachana kwetu ku karibu lakini msisikitike. Daima maisha yanabadilika, hakuna mtu awezaye kukwepa kuteketea kwa mwili. Tendo hili nitalionyesha muda huu kwa kifo changu mwenyewe, mwili wangu ukiporomoka kama mkokoteni uliofyatuka fungato.

"Msiomboleze bure, lakini muelewe kuwa hakuna kinachodumu na kutokana na haya mjifunze udhaifu wa maisha ya binadamu. Msiendekeze imani potofu kuwa linalobadilika linaweza lisibadilike.

"Shetani wa vishawishi vya kila hali, wakati wote anatafuta nafasi ya kuihadaa nafsi. Iwapo kuna nyoka mwenye sumu anayeishi chumbani mwako, nawe unataka kusinzia kwa amani basi ni sharti umfukuze nyoka huyo kwanza.

"Yakupasa kuzivunja pingu za tamaa za dunia na kuzifukuzia mbali kama jinsi utakavyofukuza huyo nyoka. Inabidi ulinde nafsi yako kwa dhati."

5. "Wanafunzi wangu, mwisho wangu umefika bali msisahau kuwa kifo ni mwisho tu wa kiwiliwili. Mwili ulizaliwa kutokana na wazazi na ulilishwa kwa chakula, vivyo hivyo hapana budi pawepo maradhi na hatimaye kifo.

"Lakini Buddha wa kweli siyo mwili wa binadamu bali ni Wongofu. Binadamu lazima afe, lakini Hekima ya Wongofu itadumu milele katika ukweli wa Dharma, na katika kuizingatia Dharma. Yule auangaliaye tu mwili wangu hakika hanioni mimi. Bali yeye tu anayeyakubali mafundisho yangu hakika aniona mimi. Baada ya kifo changu, Dharma atakuwa Mwalimu wako. Fuata Dharma na utakuwa mkweli kwangu.

Katika miaka arobaini na tano ya maisha yangu sikuficha lo lote katika mafundisho yangu. Hakuna siri ya mafunzo wala kuficha maana na kila kitu kimefundishwa bayana na kwa ufasaha. Wanafunzi wangu wapenzi huu ndio mwisho. Kwa muda huu nitaweza kupitia Nirvana. Hivyo ndivyo nilivyoagizwa.

SURA YA PILI

BUDDHA ATUKUZWAYE NA WA AZALI (MILELE)

I
HURUMA NA NADHIRI ZAKE

1. Roho ya Buddha ni ile yenye upendo mwingi, upole na huruma tele. Fadhili kuu ni moyo wa kuokoa watu wote kwa njia na hali yoyote ile. Huruma kuu ni moyo unaoisukuma kuugua pamoja na wagonjwa na kuteswa mateso yao.

"Mateso yenu ni mateso yangu na furaha yenu ni furaha yangu" alisema Buddha, na ni kama mama daima ampendavyo mwanae. Hasahau moyo huo hata kwa kitambo kidogo tu, kwani ni asili ya u-Buddha kuwa na huruma.

Moyo wa Buddha wa huruma unatiwa hamasa kulingana na matakwa ya binadamu, imani ya mtu ni urejeo wa moyo huu na humwongoza katika wongofu, kama mama atambuaye uzazi wake kwa kupenda mwanae, naye mtoto kwa kuyaona mapenzi hayo hujisikia yu salama na ana amani.

Pamoja na yote hayo watu hawaelewi moyo huu wa Buddha na huendelea kuteseka kutokana na ndoto na tamaa zitokanazo na ujinga wao, wanateswa na matendo waliyojikusanyia kutokana na uchu wa dunia na kutangatanga katika milima ya hadaa huku wakibeba mizigo mizito ya

madhambi yao.

2. Usifikiri kuwa huruma ya Buddha ni maisha ya sasa tu, ni ufunuo wa huruma isiyo na mwisho ya Buddha wa milele na milele ambayo imefanya zama za kale, binadamu alipoasi kutokana na ujinga.

Buddha wa milele huwatokea watu katika namna mbalimbali za kirafiki na huwaletea taratibu za busara zilizojaa faraja.

Shakyamun Buddha, Mwana wa Mfalme katika ukoo wa Shakya, aliacha starehe za nyumbani kwake na kuishi maisha ya kujinyima na ya upweke. Kwa njia ya taamuli aliupata Wongofu.Alifundisha Dharma (Mafundisho) kati ya ndugu zake na kuyadhihirisha kwa kifo chake hapa ardhini.

Kazi ya u-Buddha ni ya kudumu kama ujinga wa binadamu usivyokuwa na mwisho, na kama kina cha ujinga kisivyokuwa na mwanzo, vivyo hivyo huruma ya Buddha haina mipaka.

Buddha alipoamua kujitenga na maisha ya dunia aliweka nadhiri kuu nne: 1) Kuwaokoa watu wote 2) Kukana tamaa zote za dunia, 3) Kujifunza mafundisho yote, 4) Kupata wongofu wa kweli. Nadhiri hizi ni udhihirisho wa upendo na huruma ambavyo ni vya msingi katika asili ya u-Buddha.

3. Kwanza Buddha alijifunza kuepuka na dhambi ya kuua

kiumbe chochote, alitaka watu wote wangejua baraka za maisha marefu.

Buddha alijifunza kuepuka dhambi ya wizi, alitamani watu wote wangekuwa na kila kitu wakihitajicho.

Buddha alijifunza kuepuka uzinzi, alitumaini watu wote wangejua baraka za moyo safi badala ya kuhangaishwa na tamaa zisizoisha.

Buddha, akilenga katika utimilifu, alijizoeza kujiepusha na vishawishi vya kila aina, alitamani watu wote wangejua utulivu na amani ya moyoni ambavyo vingefuatia katika kusema ukweli.

Alijifunza kuepukana na uongo na hila, alitamani watu wote wangejua furaha ya ushirikiano.

Alijizoeza kuepuka kuwatukana wenzake, na akatamani wote wangekuwa na moyo mkunjufu ambao ungefuatiwa na kuishi pamoja kwa amani.

Alijifunza kujiepusha na maseng'enyo, na akatamani watu wote wangejua baraka za ushirika katika maono ya wengine.

Buddha, akilenga katika ukamilifu, alijifunza kuepukana na uchoyo, na kwa tendo hili la uadilifu alitamani watu wote wangejua amani ambayo ingepatikana kutokana na maisha haya

huru.

Alijifunza kuepuka hasira, na alitamani watu wote wangependana.

Alijifunza kuepuka ujinga, na alitamani watu wote wangeelewa wala siyo kutojali sheria za asili ya mambo.

Kwa hiyo huruma ya Buddha inawakusanya watu wote na mawazo yake ya kila mara ni faraja ndani yao. Huwapenda watu kama wazazi wawapendavyo watoto wao na huwatakia baraka nyingi ili waweze kuvuka ng'ambo ya bahari hii ya kufa na kupona.

II
FARAJA ZA BUDDHA NA WOKOVU KWETU

Siyo rahisi kwa maneno ya Buddha aliyoyasema kutoka ukingoni mwa wongofu kuwafikia kwa urahisi watu waliopo kwenye mapambano ya dunia ya hadaa. Hivyo Buddha hurudi katika dunia hii yeye mwenyewe na kutumia njia zake za wokovu.

"Sasa nitawapa hadithi" Buddha alisema. Palikuwepo na tajiri mmoja ambaye nyumba yake ilishika moto. Tajiri huyo alikuwa mbali na mji wake na aliporudi aliwakuta watoto wake

wakicheza ndani bila ya taarifa ya moto. Baba yao alipiga yowe, "Toka nje watoto! Toka ndani ya nyumba! Haraka!" Lakini watoto hawakumjali.

Kwa hofu baba aliita tena, watoto nina zawadi za vitu vya kuchezea vya ajabu hapa, toka ndani ya nyumba mkazichukue! "Kwa kusikia hivyo, safari hii watoto walikimbia na kutoka nje ya nyumba iunguayo.

Dunia hii ni nyumba iunguayo. Watu bila kutambua kuwa nyumba inaungua wako katika hatari ya kuungua hadi kufa, kwa hiyo Buddha kwa huruma hubuni mbinu za kuwaokoa.

2. Buddha alisema: " Nitakutolea mfano mwingine. Zama za kale Mwana pekee wa tajiri mmoja aliondoka nyumbani kwao na akaishi kwenye umaskini.

"Baba yake alisafiri mbali kumtafuta mwanae bali hakumwona. Alifanya kila njia ya kumpata mwanae bila ya mafanikio.

"Miaka mingi baadaye, mwanae akiwa katika hali duni" alizungukia kwenye makazi ya baba yake.

"Baba yake alimtambua mwanae na akawatuma watumishi wamlete mwana huyo mpotevu nyumbani, ambaye akishangazwa na jumba la fahari lilivyokuwa alihofu kuwa alikuwa akidanganywa na hakuwa huru kufuatana nao.

Hakutambua kuwa aliyemtaka alikuwa ni baba yake.

"Baba yake alituma watumishi wake tena kumpatia fedha awe mtumishi kati ya watu wa nyumbani mwa Bwana wao. Mwana alikubali shauri na akarudi nao katika nyumba ya baba yake na akawa mtumishi.

"Baba yake alimpandisha cheo taratibu akawa msimamizi wa mali na hazina zote, lakini bado hakutambua kuwa ndiye baba yake mzazi.

"Baba yake alipendezwa na uaminifu wa mwanae na mwisho wa maisha yake ulipokaribia aliwaita ndugu na marafiki zake na akawambia: "Ndugu zangu, huyu ndiye mwanangu pekee; Mwanangu niliyemtafuta kwa siku nyingi. Tangu leo, mali yangu yote na hazina ni mali yake."

"Mwanae alishangazwa sana na tendo la kukiri kwa baba yake na akasema: Sio kwamba nimempata baba yangu tu bali mali hii na hazina ni vyangu vyote."

Tajiri katika mfano huu anafananishwa na Buddha, na mtoto mpotevu ni badili ya watu wote. Huruma ya Buddha inawagusa wote kwa mapenzi ya baba kwa mwanae wa pekee. Katika upendo huo huweka njia za kuwaongoza, kuwafundisha na kuwatajirisha na hazina ya wongofu.

3. Kama mvua inyesheavyo mashamba yote, vivyo hivyo

huruma ya Buddha huwafikia watu wote bila ubaguzi. Jinsi mimea mbalimbali inavyofaidika kutokana na kila mvua inyeshapo ndivyo watu wa hali na maumbile mbalimbali wanavyobarikiwa katika njia mbalimbali.

4. Wazazi huwapenda watoto wao wote, lakini mapendo yao hujidhihirisha kwa huruma na matunzo ya pekee kwa mtoto mgonjwa.

Huruma ya Buddha ni sawa kwa wote, bali hujidhihirisha kwa uangalifu wa pekee kwa wale ambao kutokana na ujinga wao, wanabeba mizigo mizito ya dhambi na mateso mengi.

Jua hupambazuka katika anga ya Mashariki na huangaza kufukuza giza la dunia bila ubaya au upendeleo na kusambaza mwangaza katika eneo lolote. Vivyo hivyo huruma ya Buddha huwazunguka watu wote ikiwatia nguvu kutenda mema na kuwaongoza kuepukana na dhambi. Kwa hiyo hulifukuza giza la ujinga na kuwaelekeza watu kwenye Wongofu.

Buddha ni baba katika huruma yake na mama katika mapendo yake. Watu hutenda kwa nguvu nyingi katika ujinga na utumwa wao ili kutimiza tamaa za dunia. Buddha naye ana juhudi lakini katika huruma kwa watu wote. Watu hawana msaada wowote bila huruma ya Buddha na hawana budi kupokea njia zake za wokovu kama watoto wake.

III
BUDDHA WA MILELE

1. Watu wa kawaida huamini kuwa Buddha alikuwa mtoto wa mfalme na akajifunza njia ya Wongofu akiwa fukara; Ukweli ni kwamba, Buddha amekuwepo muda wote katika dunia isiyokuwa na mwanzo wala mwisho.

Akiwa Buddha wa milele, amewafahamu watu wote na hutumia njia zote za faraja. Hakuna uongo katika Dharma ya milele aliyoifundisha Buddha kwani hufahamu vitu vyote vilivyo duniani na huwafunza watu wote.

Ni kweli, ni vigumu kuelewa dunia jinsi ilivyo, kwani ingawa dunia inaonekana sahihi, siyo sahihi, na ingawa inaonekana danganyifu siyo danganyifu. Watu wajinga hawawezi kujua ukweli wa dunia.

Buddha pekee anaifahamu dunia ilivyo kwa ufasaha na hasemi ni sahihi au danganyifu, nzuri au potovu. Huielezea na kuifafanua dunia ilivyo.

Buddha anachofundisha ni hiki "Watu wote wastawishe mizizi ya wema kwa minajiri ya asili yao, matendo yao, na imani zao." Mafundisho haya yanazidi mathibitisho na makanusho yote ya dunia hii.

2. Buddha hafundishi kwa maneno tu bali pia kwa maisha

yake. Ingawa maisha yake hayana mwisho, ili kuwaamsha watu wachoyo, hutumia njia ya kifo chake.

"Wakati mganga fulani alipokuwa safari ya mbali, kwa bahati mbaya watoto wake walikunywa sumu. Mganga huyo aliporudi aligundua ugonjwa na akatengeneza dawa inayoharibu nguvu ya sumu. Baadhi ya watoto ambao hawakuwa wameathirika sana waliinywa hiyo dawa wakapona, lakini wengine walikuwa wameathirika sana na hata wakakataa kunywa dawa.

Mganga huyo akisukumwa na upendo wa mzazi kwa mtoto, aliamua kutumia njia kali ya kuwafanya wapone. Aliwaambia wanae: "Yanipasa kufunga safari ya mbali. Nimezeeka na ninaweza kufa siku yoyote. Nikiwa pamoja nanyi nitawatunza lakini nikifa mtazidi kuwa na hali mbaya. Mkipata habari za kifo changu ninawasihi mnywe hiyo dawa ili mjitibu na hii sumu". Hatima yake akasafiri mbali. Baada ya muda, akatuma mjumbe kuleta taarifa ya kifo chake kwa watoto wake.

Watoto walipopokea tanzia, walihuzunika sana kwa kifo cha baba yao na kwa kutambua kuwa hawataendelea kufaidi matunzo mema waliyoyapata kutoka kwa baba yao, wakikumbuka ombi lake wakati anaondoka, kwa mahangaiko na masikitiko, walikunywa dawa na wakapona.

Watu hawapaswi kulaani uongo wa mzazi huyo. Buddha ni

kama mzazi huyo. Naye pia hutumia hadithi ya uzima na kifo kuponya watu walionaswa katika hatamu za tamaa.

SURA YA TATU

UMBILE LA BUDDHA NA HULKA ZAKE

I
HALI TATU ZA MWILI WA BUDDHA

1. Msihangaike kumjua Buddha kwa sura kwani Buddha siyo sura au tabia. Buddha ni Wongofu wenyewe. Njia sahihi ya kumjua Buddha ni kusadiki Wongofu.

Ikiwa mtu aonapo umbo zuri sana la Buddha na akafikiri anamfahamu Buddha, kosa lake ni kama la jicho jinga, kwa kuwa Buddha halisi hawezi kuonekana katika umbile au kuonekana kwa macho ya binadamu. Haiwezekani kumfahamu Buddha kwa maelezo sahihi ya tabia yake. Haiwezekani kueleza sifa za Buddha kwa maneno ya binadamu.

Ingawa tunazungumzia umbile lake, Buddha wa milele hana umbile mahsusi, lakini anaweza kujibainisha katika umbile lolote. Ingawa tunaeleza sifa na tabia zake, kumbe Buddha wa milele hana tabia mahsusi, bali anaweza kujibainisha katika tabia iwayo yoyote nzuri.

Hivyo basi, yeyote aonapo dhahiri umbile la Buddha, au atambuaye tabia yake kwa ufasaha, na kumbe haambatani na umbile au sura yake, basi huyo ana uwezo wa kumwona na kumjua Buddha.

2. Mwili wa Buddha ndio Wongofu wenyewe. Kule kutokuwa na umbile wala asili, siku zote ndivyo ilivyo na mara zote itakuwa hivyo. Siyo mwili ambao lazima ulishwe chakula. Ni mwili wa milele ambao uthabiti wake ni hekima. Kwa hiyo Buddha, hana hofu wala maradhi, daima habadiliki.

Kwa hiyo Buddha hatapotea ilimradi Wongofu upo. Wongofu hujitokeza kama mwanga wa Hekima uamshao watu katika upya wa maisha na kuwafanya wazaliwe katika dunia ya Buddha.

Wale watambuao huwa wana Buddha, hushika Dharma yake, huheshimu mafundisho yake na kuwarithisha watoto wao. Hakuna miujiza izidiyo uwezo wa Buddha.

3. Mwili wa Buddha una utatu ndani yake. Kuna sura ya Asili au Dharma-kaya, kuna sura ya Nguvu zisizoonekana au Sambhoga-kaya, pia sura ya ufunuo au Nirmana-kaya.

Dharma-kaya ndiyo uthibiti wa Dharma, yaani ni nguvu ya kweli yenyewe. Katika hali ya Asili ya Buddha, hana umbo wala rangi, na kwa kuwa hana umbo wala rangi, hana atokako wala aendako. Buddha hutanda juu ya kila kitu kama mbingu ilivyo na kwa kuwa yeye ni wote hapungikiwi kitu.

Buddha haishi kwa kuwa watu hufikiri hivyo, wala hapotei kwa kuwa watu humsahau. Hana ulazima wowote wa kuonekana kwa vile watu wana raha, au ulazima wa kutoonekana wakati

watu si waangalifu na wazembe. Buddha hujipenyeza mahali popote katika mawazo ya binadamu.

Katika mtizamo huu mwili wa Buddha, ujaza kila pembe ya ulimwengu huu, hugusa kila sehemu, huishi milele na milele hata kama watu wanamwamini au wana mashaka na kuwepo kwake.

4. Sambhoga-kaya huashiria uasili wa Buddha, Maunganiko ya Huruma na Hekima, roho isiyokuwa na sura, ijipambanuavyo kwa ishara za uzazi na kifo, kupitia katika ishara za kuweka nadhiri, kufundisha na kulitangaza jina lake takatifu ili kuwaelekeza watu katika wokovu.

Huruma ndiyo asili ya mwili huu na katika roho yake Buddha hutumia njia zote kuwakomboa wale wote walio tayari kwa ukombozi. Kama moto ambao ukisha washwa hauzimiki hadi mafuta yakauke ndani ya chombo, ndivyo ilivyo Huruma ya Buddha, haitafifia hadi mateso ya duniani yamekwisha. Kama upepo upeperushavyo vumbi, ndivyo Huruma ya Buddha katika mwili huu ipeperushavyo mavumbi ya mateso ya binadamu.

Nirmana-kaya hudhihirisha kuwa, ili kukamilisha faraja ya Buddha wa ufunuo, Buddha alikuja ulimwenguni katika umbile la binadamu na akaonyesha watu katika maumbile yao na uwezo wao hali za uzawa wao, namna ya kuyakana mambo ya dunia hii na upatikanaji wa wongofu. Katika kuwaongoza watu, Buddha katika mwili huu hutumia njia yoyote ile kama vile maradhi na kifo.

Umbile la asili la Buddha ni Dharma kaya moja, lakini kutokana na jinsi tabia za watu zinavyotofautiana vivyo hivyo umbile la Buddha hujitokeza tofauti. Ingawa umbile la Buddha hutofautiana kutokana na matakwa mbali mbali, matendo na uwezo wa watu, Buddha hujihusisha tu na ukweli wa Dharma.

Ingawa mwili wa Buddha una utatu ndani yake, roho yake na madhumuni yake vina lengo moja, kuwaokoa watu wote.

Katika hali yoyote ile Buddha ni dhahiri katika utakatifu wake, kumbe ufunuo huu siyo Buddha kwa sababu Buddha hana maumbile. U-Buddha hujaza kila kitu. Hufanya mwili wake kama wongofu, na huwatokea wale wote wenye uwezo wa kutambua ukweli.

II
KUJITOKEZA KWA BUDDHA

1. Buddha huonekana katika dunia hii kwa nadra. Sasa Buddha huonekana, hupata Wongofu, huonyesha Dharma, huvunja wimbi la mashaka, hung'oa vishawishi vya tamaa na kuziba chemichemi za maovu. Bila kizuizi yeye uhiari kuizuru dunia yote. Hakuna kitu bora kama kumheshimu Buddha.

Buddha huonekana katika ulimwengu wa mateso kwa sababu hawawezi kuachana na watu watesekao. Dhumuni lake pekee ni kueneza Dharma na kuwabariki watu wote katika

ukweli wake.

Ni vigumu kutangaza Dharma katika dunia iliyojaa maonevu na uwongo, dunia inayopambana bure na tamaa zisizoisha na maudhi. Buddha hupambana na shida zote kwa sababu ya upendo wake na huruma.

2. Buddha ni rafiki mwema wa watu wote. Buddha ampatapo mtu atesekaye kutokana na mzigo mzito wa mateso ya duniani, hujazwa na huruma na kugawana naye mzigo huo. Akutanapo na mtu anayehangaika na madanganyiko hufukuzia mbali madanganyiko hayo na kumwashia nuru ya hekima yake.

Kama ndama anavyofurahia maisha awapo na mama yake, vivyo hivyo wale waliokwisha yasikia mafundisho ya Buddha hukataa katu kuachana naye kwa kuwa mafundisho yake huwaletea faraja.

3. Mwezi unapozama, watu husema kuwa mwezi umepotea na mwezi unapoandama, husema kuwa mwezi umeonekana. Ukweli ni kuwa mwezi hauendi wala kuja, bali hung'aa muda wote angani. Buddha ni kama mwezi. Yeye hapotei wala kurejea; Huelekea kuwa hivyo kutokana na upendo wake kwa watu ili awafundishe.

Watu huita sura mojawapo ya mwezi Mwezi mpevu, huita na sura nyingine mwezi Mwandamo; Ukweli Mwezi ni mviringo bila kuzidi wala kupungua. Dhahiri Buddha ni kama mwezi.

Machoni mwa binadamu, Buddha huelekea kubadilika katika umbo, ila ukweli Buddha habadiliki.

Mwezi huonekana kila pahali, juu ya mji, kijiji kilichotambaa, kwenye milima, mto, huonekana katika kina cha bwawa, katika mtungi wa maji, katika tone la umande likining'inia juu ya jani. Mtu atembeapo mamia ya kilometa mwezi huandamana naye. Kwa binadamu mwezi huelekea kubadilika lakini mwezi haubadiliki. Buddha ni kama mwezi katika kuwafuata watu wa dunia hii kwenye hali zao zote za maisha akijibainisha katika sura mbali mbali, lakini katika Asili yake habadiliki.

4. Ukweli kwamba Buddha hutokea na kutoweka unaweza kuelezwa kwa utendaji: Yaani, wakati tendo na hali ni vya heri, Buddha hutokea, wakati matendo na hali ya mambo haviridhishi na wala si vya heri, Buddha huelekea kutoweka katika dunia hii.

Hata kama Buddha anajitokeza au kutoweka, u-Buddha daima unabakia jinsi ulivyo. Kwa kuielewa kanuni hii, mtu yampasa kuishika njia ya Wongofu na kupata Hekima kamili, bila ya kusumbuliwa na mabadiliko yasiyo ya kweli katika picha ya Buddha, katika hali ya ulimwengu, au katika mabadiliko ya mawazo ya binadamu.

Imeelezwa kuwa Buddha hana mwili wa kibinadamu ila yeye ni Wongofu. Mwili unaweza kufikiriwa kama chombo au mfuko ambao ukijazwa na Wongofu, unaweza kuitwa Buddha.

Kwa hiyo, mtu yeyote akijihusisha tu na mwili wa Buddha na akalilia kutoweka kwake, kamwe hataweza kumwona Buddha wa kweli.

Kwa hakika Chanzo halisi cha vitu vyote hakiwezi kufafanuliwa kwa kupambanua, kati ya kuwepo na kutokuwepo, ya kwenda na kurudi, ya zuri na baya: Vitu vyote havina hakika na kabisa ni vya hali moja.

Mpambanuo wa namna hii husababishwa na hukumu batili ya wale wayaonao mambo haya. Maumbile ya kweli ya Buddha hayatoki wala hayapotei.

III
HULKA ZA BUDDHA

1. Buddha hupokea heshima kubwa ulimwenguni kutokana na maadili matano: Tabia bora, Ushauri bora, Hekima sahihi, Uwezo bora wa kuhubiri na Uwezo mkubwa wa kuwaongoza watu kuyashika mafundisho yake.

Kwa nyongeza, maadili mengine nane humwezesha Buddha kutoa baraka na faraja kwa watu: Uwezo wa kuleta fadhila ulimwenguni katika kuyafuata mafundisho yake, uwezo wa kuhukumu lipi ni haki kati ya zuri na baya, sahihi na kosa, uwezo wa kuwaongoza watu kwenye Wongofu kwa kuwafundisha kwa njia sahihi, uwezo wa kuongoza watu wote kwa usawa, uwezo

wa kukwepa kiburi na majivuno, uwezo wa kutenda ayasemayo, uwezo wa kusema aliyoyatenda, na hivyo kutimiza nadhiri za moyo wake wa huruma.

2. Buddha ni baba na mama wa watu wote duniani. Kwa muda wa miaka 16 tangu mtoto amezaliwa baba na mama huzungumza naye katika lugha ya kitoto; na baadaye humfundisha hatua kwa hatua jinsi ya kuzungumza kama mtu mzima. Kama wazazi waleavyo watoto, vivyo hivyo Buddha kwanza huwalea watu wake, kisha huwaacha wajitegemee. Kwanza huyaacha mambo yaende kwa mkondo wake, kisha huyaleta katika himaya yake.

Anachokihubiri Buddha katika lugha yake, watu hukipokea na kukitumia katika lugha yao kana kwamba kilikuwa tu kimeandaliwa kwa ajili yao.

Akili ya Buddha huzidi akili ya binadamu; haiwezi kuelezwa kwa maneno, inaweza tu kudokezwa kwa mfano au hadithi.

Maji ya mto Ganges husukwasukwa kwa mwendo wa farasi na tembo na kunogwa na samaki na kaa; lakini mto huendelea kutiririka tu bila wasiwasi wa misukosuko hiyo. Buddha ni kama mto mkubwa. Samaki na kaa wa mafundisho mengine huogelea katika kina chake na kupambana na mawimbi yake bila mafanikio yoyote. Dharma ya Buddha huendelea kutiririka ikiwa safi bila wasi wasi wowote.

3. Hekima ya Buddha, ambayo ni kamilifu, hujitenga na udhalimu na uhifadhi kiasi na upole ambavyo haviwezi kuelezeka kwa maneno matupu. Akiwa yeye ni chimbuko la busara hujua fikra na hisia za watu wote na hutambua kila kitu katika ulimwengu huu kwa muda mfupi sana.

Kama nyota za angani zinavyoakisi mwanga kwenye bahari tulivu,vivyo hivyo ndivyo mawazo na hisia vinavyo akisiwa katika kina cha hekima ya Buddha. Hii ndiyo maana Buddha anaitwa Mwongofu mkamilifu, ajuwaye kila jambo.

Hekima ya Buddha hubadilisha akili zilizochakaa, huwatia nuru na kuwafunza umuhimu wa dunia hii, chanzo chake na maana ya kuwepo na kutokuwepo. Hakika, bila msaada wa Hekima ya Buddha, ni sura ipi ya ulimwengu ingeweza kufahamika kwa watu?

4. Buddha hajitokezi kama Buddha kila mara. Wakati mwingine hujitokeza katika hali ya utu na uovu wake, mara nyingine kama Mwanamke., kama Mungu , kama mfalme au kama Mtawala wa nchi. Hujitokeza katika danguro au katika nyumba ya kucheza kamari.

Katika magonjwa hujitokeza kama mponya na katika vita uhubiri na kushauri uvumilivu na huruma kwa wanaoumwa, kwa wale wanaoamini kuwa mambo ni ya milele, huwahubiri juu ya mambo ya kupita na yasiyo na uhakika, kwa wajivunao na kujisifu, huwahubiri unyenyekevu na kujitoa mhanga, kwa wale

waliotekwa katika anasa za duniani huwabashiria taabu za dunia.

Kazi za Buddha ni kuwa bayana katika mambo yote na nyakati zote ambavyo ni hali halisi takatifu ya Dharma-kaya (hali kamili ya Buddha), hivyo basi ni wema na huruma utiririkao kutoka Dharma-kaya ndani ya maisha yasiyo na mwisho na mwanga usiokuwa na mipaka, ikileta wokovu kwa binadamu.

5. Dunia ni kama nyumba iunguayo ambayo daima hubomolewa na kujengwa upya. Watu wakiwa wamevurugwa na giza la ujinga wao, hupoteza akili zao katika hasira, chuki, husuda, udhalimu, na mateso ya dunia. Wako kama watoto wachanga wanamwitaji mama, kila mmoja yampasa kuutegemea msamaha, wema na huruma ya Buddha.

Buddha ni baba wa dunia hii, watu wote ni watoto wa Buddha. Buddha ni mtakatifu wa hali ya juu sana kati ya watakatifu. Dunia inawaka moto kwa uchakavu na kifo, kuna mateso kila mahali. Lakini watu, wakiwa wamekumbwa katika juhudi za kipumbavu za kutafuta anasa, wamepungukiwa na busara kutambua hilo.

Buddha aliona kuwa dunia hii ya hadaa, ilikuwa hasa nyumba iunguayo, hivyo aliiacha na kutafuta hifadhi na amani katika msitu mtulivu. Akiwa huko, kwa huruma yake kuu hutuita, "Dunia hii ya mabadiliko na mateso ni yangu; watu wote huwa wajinga, wasiosikia ni watoto wangu, ni mimi pekee niwezaye kuwakomboa kutoka kwenye majaribu na taabu."

Umbile la Buddha na Hulka zake

Buddha akiwa Mfalme Mkuu wa Dharma, Anaweza kuwahubiri watu wote Apendavyo. Buddha huwepo duniani kuwabariki watu. Kuwaokoa katika mateso, huwahubiri Dharma, lakini masikio ya watu yamezibwa na uchoyo nao si wasikivu.

Lakini wale wasikiao mafundisho yake hujinusuru katika majaribu na taabu za maisha. "Watu hawawezi kuokolewa kwa kutegemea hekima zao wenyewe." Alisema, "na ni kutokana na imani ndipo wataingia katika mafundisho yangu." Kwa hiyo, yampasa kila mtu kusikiliza mafundisho ya Buddha na kuyafuata.

DHARMA

SURA YA KWANZA

MWANZO

I
UTUKUFU WA KWELI WENYE SURA NNE

1. Dunia imejaa mateso. Kuzaliwa ni mateso, Uzee ni mateso, Ugonjwa na kifo ni mateso. Kukutana na mtu umchukiaye ni mateso, kutenganishwa na mtu umpendaye ni mateso, kuhangaika bure ili kutosheleza mahitaji ya mtu ni mateso. Kwa kweli maisha yaliyojaa tamaa na uchu mara zote hayakosi taabu. Hii inaitwa ukweli wa mateso.

Asili ya mateso ya binadamu kwa hakika inapatikana katika kiu ya mwili wa binadamu na katika mauzauza ya tamaa ya dunia. Ikiwa kiu hii na mauzauza haya vitafuatiliwa katika vyanzo vyake vitagunduliwa kuchimbuka katika shauku za silika za kimwili. Hivyo tamaa, ikiwa na nia ya kuishi kwa mizizi yake, hutafuta kile ikitakacho hata kama ni kifo. Hii inaitwa ukweli wa Asili ya mateso.

Ikiwa tamaa, ambayo ipo katika shina la mateso ya binadamu ingeweza kuondolewa basi mateso yatakoma na taabu ya binadamu itakwisha. Hii huitwa ukweli wa kikomo cha mateso.

Ili kuingia katika hali ambayo hakuna tamaa wala taabu,

yampasa mtu kufuata njia fulani. Hatua za Njia hii Yenye Mikondo Minane Bora ni: Mtizamo sahihi, mawazo sahihi, mazungumzo sahihi, Tabia njema, Nafuu sahihi, Juhudi sahihi, Utulivu sahihi na fikra sahihi. Hii inaitwa Ukweli wa Njia Bora kwenye Kikomo Cha Asili ya Mateso.

Yawapasa kuweka kweli hizi kwa ufasaha katika mioyo yao, kwa kuwa dunia imejaa mateso na yeyote atakaye kuepukana na mateso, yampasa kuepukana na uhusiano wa tamaa za dunia hii ambayo ni asili pekee ya mateso. Njia ya maisha ambayo imejitenga na taabu na mateso ya duniani yaweza kutambulikana kwa Wongofu; na Wongofu unaweza kupatikana tu kupitia nidhamu ya Njia Yenye Mikondo Minane Bora.

2. Wale wote waufuatao Wongofu yawapasa kuelewa U-nne wa Ukweli Bora. Bila kuelewa hili watatangatanga pasipo mwisho katika mshangao na mashaka ya madanganyo ya dunia. Wale waelewao U-nne wa ukweli Bora wanaitwa, "Watu waliopata macho ya Wongofu."

Kwa hiyo wote wale wanaohitaji kufuata mafundisho ya Buddha yawapasa kufikiria sana juu ya U-nne wa Ukweli Bora na kuelewa bayana maana yake. Nyakati zote Mtakatifu kama ni Mtakatifu wa kweli basi ni yule aielewayo maana hii na kuifundisha kwa wenzake.

Binadamu anapoelewa kwa ufasaha U-nne wa Ukweli Bora basi Njia Yenye Mikondo Minane Bora inamwondolea

choyo, na kutokana na kujikomboa kutokana na choyo, hatagombana na hataua, wala kuiba, kuzini, kudanganya, kutukana, kujipendekeza, husuda, kukasirika, kusahau kuwa maisha ya binadamu ni ya muda tu na wala hawezi kuwa dhalimu.

3. Kufuata Njia Bora ni sawa na kuingia katika chumba chenye giza ukiwa na taa mkononi, giza litaondoshwa na chumba kitajaa mwanga.

Watu wanaoelewa maana ya Kweli Bora na wamejifunza kufuata Njia Bora wanao mwanga wa hekima ambao utafukuzia mbali giza la ujinga.

Buddha huwaongoza watu kwa kuwaashiria tu kwenye U-nne wa Ukweli Bora. Wale waelewao ukweli huo vizuri watapata Wongofu, Wataweza kuwaongoza na kuwapa nguvu wengine katika dunuia ya mashaka na wataaminiwa. Hakika U-nne wa Ukweli Bora unapoeleweka kwa ufasaha,chemichemi na taabu za ulimwenguni hukauka.

Kutoka katika U-nne wa Ukweli Bora, mitume wa Buddha watapata kweli nyingine za thamani, watapata busara na hekima ya kuelewa maana zote, na watakuwa na uwezo wa kuihubiri Dharma kwa watu wote wa ulimwenguni.

II
MWANZO

Kuna mambo yanayosababisha mateso yote ya binadamu, na kuna njia ambayo kwayo hayo yanaweza kuisha, kwa kuwa jambo lolote duniani ni tokeo la migongano ya sababu na mazingira, na kila kitu hupotea jinsi sababu na mazingira vibadilikavyo na kutoweka.

Mvua hunyesha, pepo huvuma, mito hustawi, majani hukua na kupevushwa. Mambo haya yote yanahusiana na mazingira na sababu, na yanasababishwa nayo, na hupotea jinsi mazingira na sababu (tabia za maumbile) vinavyobadilika.

Mtu huzaliwa kutokana na uzazi. Mwili wake hukuzwa na chakula, roho yake hulelewa na mafundisho na uzoefu.

Kwa hiyo, mwili na roho vinahusiana na mazingira yanapobadilika.

Kama wavu ulivyotengenezwa kwa mfululizo wa mafundo mengi, vivyo hivyo vitu vyote ulimwenguni vimeunganishwa kwa mfululizo wa mafundo. Yeyote afikiriaye kuwa tundu la wavu linajitegemea na limetengwa pekee anajidanganya.

Unaitwa wavu kwa sababu umetengenezwa kwa mfululizo wa matundu yaliyounganishwa na kila tundu lina nafasi na wajibu wake kwa ushirikiano na mahusiano na matundu mengine.

3. Maua hutokea kutokana na mfululizo wa hali ifanyayo yastawi. Majani hupeperushwa kutokana na mfululizo wa hali iyasababishayo yawe hivyo. Maua hayatokei kwa utashi wake, wala jani halianguki lenyewe, ila ni kutokana na majira. Hivyo basi kila jambo lina kuwepo kwake na kutoweka kwake; hakuna kinachoweza kujitegemea bila badiliko lolote.

Ni kwa kanuni ya milele na isiyobadilika ya ulimwengu huu kwamba kila kitu kiliumbwa kwa kanuni ile ile, kila kitu hubadilika, hakuna kitu kikaacho daima bila kubadilika.

III
MWANZO TEGEMEZI

1. Kipi ni chanzo cha huzuni, maombolezo, uchungu au maumivu? Je hakipatikani katika kweli kuwa watu kwa wastani wamejaa tamaa?

Wanang'ang'ania kwa ukaidi maisha ya utajiri na heshima, starehe na anasa, msisimko na kujifurahisha, hawajui ukweli kuwa na uchu wa mambo haya ni chanzo cha mateso ya binadamu.

Tangu mwanzo, dunia imejaa msongamano wa maafa mbali na mambo yasiyoepukika kama maradhi, uzee na kifo.

Hata hivyo mtu akifikiri kwa makini ukweli wote, ataridhika kuwa chimbuko la mateso linaambatana na kanuni ya

kukumbwa sana na tamaa. Ikiwa uchu na tamaa vinaweza kuondolewa, mateso ya binadamu yatakoma.

Ujinga hubainishwa katika choyo ijazayo akili za binadamu. Inatokana na ukweli kuwa binadamu hawatambui sababu sahihi ya mfululizo wa mambo.

Kutokana na ujinga na uchoyo huzuka tamaa mbaya kwa mambo ambayo kwa hakika hayapatikani lakini ambayo binadamu huendelea kuyasaka bila kuchoka wala kujua.

Kwa sababu ya ujinga na uchoyo, watu huufikiria ubaguzi ambapo, kwa kweli hakuna ubaguzi wowote. Kama ilivyo, hakuna mpaka wa ubaguzi wa zuri au baya katika tabia ya binadamu, bali binadamu, kwa sababu ya ujinga wao hufikiria juu ya mgawanyiko huo na kuamua kuwa lile ni baya au zuri.

Kwa sababu ya ujinga wao, kila wakati watu wote hufikiria mawazo mabaya na mara nyingi hupoteza mtizamo sahihi na kwa kung'ang'ania ubinafsi wao, hutenda maovu. Matokeo yake hujinasisha kwenye maisha ya udanganyifu.

Kwa kuyafanya matendo yao kuwa uwanja wao wa ubinafsi, kupandikiza kazi za ubaguzi wa moyo kama mbegu, kufunika moyo kwa ujinga, wakiurutubisha kwa mvua ya kupenda sana tamaa wakiumwagilia kwa maji ya utashi wa ubinafsi, haya yote huongezea dhana ya uovu, na kuendeleza kubeba mzigo wa madanganyo.

2. Ukweli, kwa hiyo ni akili zao ziletazo madanganyo ya huzuni, maombolezo, uchungu na maumivu makali.

Ulimwengu huu wote wa madanganyo si kitu ila ni kivuli kiletwacho na akili. Na kumbe ni kutokana na akili ile ile ambayo huzaa Wongofu.

3. Katika ulimwengu huu kuna mitazamo mitatu batili. Yeyote mwenye mitizamo hii, inampasa kuyakana mambo yote ya ulimwengu huu.

Kwanza, wengine husema kuwa maisha ya binadamu yanategemea Utaratibu ulivyopangwa, pili wengine huamini kuwa kila kitu kiliumbwa na mwenyezi Mungu na kutawaliwa kwa utashi wake; tatu, wengine husema kuwa kila kitu hutokea kwa nasibu bila kuwa na sababu au hali ya maumbile.

Ikiwa yote yameamriwa kwa utaratibu uliopangwa, matendo mema na maovu yanaamriwa mbeleni, neema na misiba vimepangwa mbeleni. Hakuna kitakachoishi bila kuamriwa mbeleni. Hivyo mipango yote na juhudi za mwanadamu kwa ajili ya maendeleo vingekuwa kazi bure na kusingekuwepo na matumaini ya binadamu.

Ndivyo ilivyo hata kwa mitizamo mingine, ikiwa kila kitu hatima yake iko mikononi mwa Mungu asiyejulikana, au katika bahati nasibu, yapi ni matumaini ya binadamu kama si kujitoa

muhanga? Siyo ajabu watu waaminio dhana hizi hukata tamaa na kudharau juhudi za kutenda kwa busara na kukwepa dhambi.

Kwa kweli, dhana hizi tatu au mitazamo hii yote ni batili: kila kitu ni mfululizo wa matokeo ambayo chimbuko lake ni mkusanyiko wa sababu na hali.

SURA YA PILI

NADHARIA IHUSUYO MOYO PEKEE NA HALI HALISI YA MAMBO/VITU

I
KUTODUMU NA KUTOKUWEPO U-MIMI

1. Ingawa vyote mwili na moyo vipo kutokana na chimbuko zinazohusiana, haina maana kuwa kuna tabia ya u-mimi. Kama kiwiliwili cha mtu kilivyo mkusanyiko wa chembe chembe tofauti,kwa hiyo si cha kudumu.

Kama mwili ungekuwa na tabia ya u-mimi ungefanya hili na lile upendavyo.

Mfalme ana uwezo wa kusifu au kuadhibu jinsi apendavyo, lakini naye huugua mbali na mapenzi yake, huzeeka bila kupenda na bahati na matumaini yake mara nyingi hushindwa kuwiana.

Moyo nao si wa tabia ya u-mimi. Moyo wa binadamu ni mkusanyiko wa sababu na hali za maumbile. Daima unaendelea kubadilika.

Kama moyo ungekuwa na tabia ya u-mimi, Ungefanya lile na lile jinsi upendavyo, lakini moyo mara nyingi hukwepa kufanya unachofahamu kuwa ni sahihi na kwa unyonge hufuata uovu. Hata hivyo, hakuna linaloelekea kutokea kama jinsi nafsi

ipendeleavyo.

2. Kama mtu akiulizwa kuwa mwili haubadiliki au haudumu, atalazimika kujibu kuwa "haudumu."

Kama mtu akiulizwa kuwa ufupi wa maisha ni furaha au mateso, kawaida atasema ni "mateso."

Ikiwa mtu anaamini kuwa kitu kisichodumu, kinachobadilika na kimejaa mateso, ni tabia ya u-mimi, basi atakuwa amekosea sana.

Moyo wa binadamu pia sio wa kudumu na umejaa mateso, hauna chochote ndani mwake cha kufanya uonekane kuwa wa tabia ya u-mimi.

Mwili wetu halisi na roho vinavyotengeneza maisha ya mtu, pamoja na mazingira ya dunia yanayomzunguka, havina uhusiano wa dhana ya "mimi" na ya "changu".

Kwa kuwa vyote mwili na mazingira yake ni vya chimbuko na hali zinazohusiana kimaumbile, daima vinaendelea kubadilika na havitakuwa na kikomo.

Moyo wa binadamu, katika kubadilika kusikokoma, ni kama mto utiririkao au ulimi wa moto wa mshumaa, na kama afanyavyo nyani, daima moyo huruka ruka huko na huko bila kutulia hata kwa kitambo kidogo tu.

Nadharia ihusuyo Moyo pekee na hali Halisi ya mambo/vitu

Mtu mwenye busara, akiona au kuyasikia haya, yampasa kutojihusisha na mwili au roho iwapo anataka kupata Uongofu.

3. Kuna mambo matano ambayo hakuna yeyote wa kuweza kuyatimiza katika ulimwengu huu: kwanza ni kuacha kuzeeka wakati anazeeka; pili ni kuacha kuugua; tatu ni kuacha kufa; nne; ni kukana kuisha kabisa na kutoonekana tena katika uso wa dunia; tano; kukana kumalizika kwa kila kitu.

Watu wa kawaida katika dunia hii hatima yake hujiingiza katika mambo haya, na watu walio wengi huumizwa na mambo haya lakini wale waliokwisha sikia mafundisho ya Buddha hawaumii kwa sababu wanajua kuwa hayo ni mambo yasiyoepukika.

Kuna kweli nne katika ulimwengu huu: kwanza, vitu vyote hutokana na kutokujua; mambo yote ya tamaa si ya kudumu, si ya uhakika na ni ya mateso; tatu, vitu vyote vilivyopo ni vya muda tu, si vya uhakika na ni vya mateso; nne hakuna kitu kama "mimi" na hakuna kitu kama "yangu" au "changu" ulimwenguni kote.

Kweli hizi zilizotajwa kwamba kila kitu si cha kudumu, na ni cha muda tu, cha kupita na kisicho na u-mimi, haziwezi kuwa na uhusiano na kuwepo au kutokuwepo kwa Buddha katika dunia hii. Kweli hizi ni bayana, Buddha huzijua zilivyo na hufundisha Dharma kwa watu wote.

II
DHANA YA MOYO PEKEE

1. Madanganyo na wongofu vyote vimetokana na moyo, na kila kitu kilichopo au chenye uhai hutokana na matakwa ya moyo kama jinsi vitu vijitokezavyo katika mkoba wa mtu afanyaye mazingaombwe.

Matendo ya moyo hayana kikomo, yanatengeneza mazingira ya maisha. Akili chafu hujizungushia mambo machafu na roho safi hujizungushia mambo yaliyo safi na salama. Hivyo basi, mazingira hayana mipaka kuliko yalivyo matendo ya moyo.

Kama jinsi msanii achoravyo picha ndivyo mazingira yalivyoumbwa na matendo ya moyo. Wakati mazingira yaliyotengenezwa na Buddha ni matakatifu yasiyo najisi, yale yaliyotengenezwa na watu baki hayako hivyo.

Moyo hubuni maumbo mbalimbali kama msanii bora abunivyo michoro mbalimbali iliyomo kwenye dunia hii. Hakuna kitu chochote duniani ambacho hakikuumbwa na moyo. Buddha ni kama nyoyo zetu; viumbe wenye busara sana ni kama Ma-Buddha. Kwa hiyo hamna tofauti kati ya mioyo ya Ma-Buddha na viumbe wote wenye busara katika uwezo wa kuumba vitu vyote.

Buddha ana uwezo mkubwa wa kuelewa mambo yote yapangwayo na mioyo inayokufa. Kwa hiyo wale wote wajuao

ukweli huu wana uwezo wa kumwona Buddha halisi.

2. Lakini moyo ambao hujitengenezea mazingira yake hauwezi kabisa kukwepa kuwa na kumbukumbu, hofu au maombolezo, siyo tu katika nyakati zilizopita, bali pia katika nyakati hizi na nyakati zijazo, kwa kuwa haya yametokana na ujinga na uchoyo.

Ni kutokana na ujinga na choyo ambapo dunia ya maovu imezaliwa, mifumo yote migumu ya kuunganisha maumbile na hali ya mazingira ipo ndani ya moyo wala si pengine.

Uhai na kifo vyote hutoka moyoni na huishi ndani yake, kwa hiyo moyo ambao hujihusisha na uhai na kifo unapopitia ndipo dunia ya uhai na kifo nayo hupitia.

Maisha yasiyo ya wongofu hutokana na moyo unaofadhaishwa na dunia yake ya madanganyo. Tukijifunza kuwa hakuna dunia ya madanganyo nje ya moyo, moyo uliofadhaika huwa safi, na iwapo tunaacha kutengeneza mazingira machafu, tutapata Uongofu.

Kwa njia hii dunia ya uhai na kifo imeumbwa kutokana na moyo, imeunganishwa na moyo, inatawaliwa na moyo, moyo ndio unaotawala kila hali. Dunia ya mateso inaletwa na moyo uliokufa kwa madanganyo.

3. Kwa hiyo, vitu vyote kimsingi vinasimamiwa na

kutawaliwa na moyo, na vinaumbwa na moyo. Kama magurudumu yafuatavyo maksai avutaye mkokoteni ndivyo mateso yamfuatavyo mtu asemaye na kutenda kwa moyo mchafu.

Lakini mtu asemapo na kutenda kwa moyo mzuri na safi, furaha humfuata kama kivuli chake. Wale watendao maovu hufuatwa na wazo, "Nimetenda kosa", na kumbukumbu ya tendo hilo hutunzwa ili mwisho iweze kufanya kazi yake ya upatilizo katika maisha ya mbeleni. Lakini wale watendao kwa nia njema hutangazwa na furaha kwa wazo, "Nimetenda wema," na huwa na furaha zaidi kwa fikra kuwa tendo jema huleta furaha ya kudumu katika maisha yajayo usoni. Ikiwa moyo haukutakasika, utaifanya miguu kusererека ikitembea katika njia chafu na ngumu, hii itafuatiwa na mieleka mingi pamoja na maumivu makali. Lakini kama moyo umetakasika njia itakuwa safi na safari itakuwa ya amani.

Yule wa kufurahia utakaso wa moyo na mwili anaifuata njia ya u-Buddha, anakata kamba za uchoyo, mawazo mabaya na tamaa mbovu. Yule aliye mtulivu moyoni hupata amani na hivyo huweza kuutengeneza na kuutuliza moyo wake usiku na mchana kwa bidii na uangalifu zaidi.

III
USAHIHI WA VITU/MAMBO

1. Kwa kuwa kila kitu katika ulimwengu huu hutokana na

hali na sababu, hapawezi kuwepo tofauti za msingi kati ya vitu. Tofauti dhahiri zipo kwa sababu watu wana mawazo ya kipuuzi na kibaguzi.

Huko angani hakuna tofauti kati ya Mashariki na Magharibi; binadamu huunda tofauti hizi kutokana na mioyo yao na kuziamini kuwa ni za kweli. Namba za hisabati tangu moja hadi mwisho usiojulikana kila mojawapo ni namba kamili, na kila mojawapo katika yenyewe haina utofauti wa wingi, lakini watu huunda utofauti huo kwa matakwa yao ili kuonyesha utofauti wa kiasi au kadri.

Kwa asili hakuna tofauti kati ya njia ya uhai na njia ya mauti; watu hufanya upambanuzi na kuiita njia hii ni ya uzazi na ile ni ya kifo. Kimatendo hakuna upambanuo kati ya tendo zuri na baya, lakini watu huweka utofauti huo kwa manufaa yao.

Buddha hukaa mbali na mipambanuo hiyo na huiangalia dunia kama wingu lipitalo. Kwa Buddha kila kitu au jambo lenye ukamilifu au tamati ni madanganyo; anajua kuwa lolote lile lishikwalo na moyo na kutolewa nje halina maana; hivyo Buddha hujitenga mbali na vipingamizi vya fikra na upambanuzi wa mawazo.

2. Watu hufikiria na kuyafanya mambo yawe yalivyo ili kukidhi matakwa kwa ajili ya manufaa na faraja zao.
Hushikiria utajiri na hazina na utukufu, hung'ag'ania kwa kukata tamaa maisha ya mauti.

Hufanya tofauti zisizo na kanuni kati ya kuishi na kutokuishi, zuri na baya, sahihi na kosefu. Kwa watu, maisha ni mfululizo wa mishikamano na miunganisho, na tena kwa sababu ya hii wanalazimika kubeba mzigo wa madanganyo uliojaa maumivu na mateso.

Hapo kale kulikuwa na mwanamume aliyekuwa akisafiri kwenda mbali na akafika kwenye mto. Akanong'ona: "upande huu wa mto ni mgumu na wa hatari kupitia, na upande mwingine unaelekea kuwa rahisi na salama zaidi, lakini nitavukaje kufika huko? "

Hivyo alitengeneza chelezo kwa kutumia matawi na matete na akavuka salama. Kisha akafikiri,"Chelezo imekuwa ya manufaa sana kwangu katika kuvuka mto, sitaiacha ukingoni ioze ila nitaibeba niende nayo. "Kwa hiyo kwa hiari yake alibeba mzigo usio wa lazima." Je mtu huyu anaweza kuitwa mwenye busara?

Mfano huu unafundisha kuwa hata kitu kizuri, kinapokuwa mzigo bila sababu yapasa kitupiliwe mbali; Kama inavyopaswa kufanyika kwa kitu kibaya. Buddha aliifanya kuwa kanuni ya maisha yake ya kuepuka majadiliano yasiyofaa na yasiyo ya lazima.

3. Mambo hayaji na kutoka; wala hayatokei na kutoweka; kwa hiyo mtu hapati vitu au kupoteza vitu.

Buddha hufundisha kuwa vitu havitokei wala kutoweka

kwa kuwa vitu hivi huvuka uthibitisho wa kuwepo na kukana kuwepo. Yaani kila kitu kikiwa ni upatanifu na mfululizo wa sababu na hali kitu chenyewe hakipo kwa hiyo inaweza kusemwa kuwa hakipo. Wakati ule ule, kwa kuwa kwa kiasi kimeunganishwa na sababu na hali, kinaweza kutamkwa kuwa ni kitu kisichokuwepo.

Kushikamana na kitu kwa sababu ya umbile lake ni chimbuko la madanganyo. Kama umbile halikushikiliwa na kung'ang'aniwa, fikra hii potovu na udanganyifu wa kipuuzi havitakuwepo. Wongofu ni kuona ukweli huu na kuwa huru kutokana na madanganyo hayo ya kipumbavu.

Dunia kwa kweli ni kama ndoto na hazina za dunia ni sarabi itamanishayo. Kama umbali uonekanavyo katika picha, vitu havina uhakika ndani mwake bali ni kama ukungu.

4. Kuamini kuwa vitu vilivyoumbwa kwa mfululizo wa sababu zisizohesabika na vinaweza kudumu milele ni kosa kubwa na inaitwa nadharia ya kudumu, lakini ni kosa kubwa vilevile kuamini kwamba vitu hutoweka kabisa, hii ni nadharia ya kutokuwepo.

Aina hizi za uzima wa milele na kifo, kuwepo na kutokuwepo, hazihusishwi na hali halisi ya vitu, bali ni katika sura zake kama zionekanavyo kwa macho ya binadamu yaliyochafuka. Kutokana na tamaa ya binadamu, watu hujishikiza na

kujiambatanisha na sura hizi, ila katika hali yenyewe ya vitu, wako mbali na yale yote ya ubaguzi na maunganisho yake.

Kwa kuwa kila kitu kimeumbwa kwa mfululizo wa sababu na hali sura za vitu zinabadilika kila wakati, yaani hakuna uthabiti juu yake kama inavyopasa kuwa juu ya vitu thabiti. Ni kwa sababu ya mabadiliko ya daima ya sura yatufanyayo kutofananisha vitu na sarabi na ndoto. Ila, pamoja na mabadiliko ya daima ya sura vitu katika hali zake za kiroho ni za kudumu na hazibadiliki.

Kwa binadamu mto huonekana kama mto, lakini kwa pepo mbaya mwenye njaa aonaye moto kwenye maji, mto huelekea kuwa moto. Kwa hiyo, kumwambia binadamu kuwa mto unaishi itakuwa na maana, lakini kwa pepo huyo itakuwa haina maana.

Kwa mtizamo huo, inaweza kusemwa kuwa vitu ni kama madanganyo: Vinaweza kusemwa kuwa vinaishi ama haviishi.

Pamoja na hayo, haiwezi kusemwa kuwa mbali na dunia hii ya mabadiliko na sura, kuna dunia ya hali ya kudumu na kweli. Ni kosa kuiona dunia hii kama ni ya muda ama ni halisi.

Lakini watu wajinga wa dunia hii husadiki kuwa dunia hii ni halisi na huendelea kushughulikia wazo hilo potofu. Lakini jinsi dunia hii ilivyo madanganyo tu, matendo yao huyashikiza kwenye makosa, huwaelekeza tu kwenye maumivu na mateso.

Mtu mwenye busara, atambuapo kwamba dunia ipo na ni

ya madanganyo matupu, hatendi kana kwamba dunia ni halisi, kwa jinsi hiyo huyakwepa mateso.

IV
NJIA YA KATI

1. Kwa wale wachaguao njia iendayo kwenye Wongofu, kuna ncha mbili ambazo zapaswa kuepukwa kwa uangalifu. Kwanza kuna ncha ya kutumbukia katika tamaa za mwili. Pili kuna ncha ya maisha ya kuepukana na Maovu kwa kujitesa mwili na roho bila sababu.

Njia bora ivukayo ncha hizi mbili na kuelekea kwenye wongofu na hekima na amani ya moyo inaweza kuitwa Njia ya Kati. Ipi ni njia ya kati? Ina njia Nane Bora ndani yake: Mtizamo sahihi, wazo sahihi, mazungumzo sahihi, tabia njema, maisha sahihi, nguvu sahihi, uchunguzi sahihi, na mkazo ulio sahihi.

Kama ilivyokwisha semwa, vitu vyote hutokea na kutoweka kwa sababu ya mfululizo wa vyanzo usiokoma. Watu wajinga huyaona maisha kama ya kudumu au kutokudumu lakini werevu huona mbali ya kudumu na kutokudumu, kitu kishindavyo vyote, huu ni msimamo wa Njia ya kati.

2. Fikiria gogo lielealo mtoni. Kama gogo hilo halikwami mahali, ama kuzama, ama kuoza, ama binadamu kulitoa nje ya mto hatima yake litafika baharini. Maisha ni kama gogo

lililobambwa kwenye wimbi la mto mkubwa. Ikiwa mtu hakujihusisha katika maisha, hatajihusisha na maisha ya kujitesa, kama mtu hatajivunia vipawa vyake au hatajihusisha na matendo maovu; ikiwa katika kutafuta Wongofu, hatayapuuzia madanganyo wala kutoyaogopa, basi mtu huyu anatafuta Njia ya kati.

Jambo la maana katika kufuata njia ya Wongofu ni kukwepa kunaswa katika ncha mojawapo, yaani kufuata Njia ya kati kila wakati.

Kujua kwamba vitu havidumu au vinadumu, kukumbuka hali ya kindoto ya kiasili ya kila kitu, mtu yampasa kuepuka kutawaliwa na kiburi cha ubinafsi au kujisifu kwa matendo mema; au kujiingiza na kujinasisha katika jambo lolote lile.

Ikiwa mtu ataepuka kunaswa katika wimbi la tamaa zake yampasa kujifunza tangu Mwanzo kutoshikilia vitu vinginevyo atazoea na kujikuta ametawaliwa na vitu hivyo. Yampasa asitawaliwe na vitu vihusuvyo kuwepo au kutokuwepo au kutawaliwa na lolote ndani au nje, wala kwa vitu vizuri au vibaya, vitu sahihi au visivyo sahihi.

Pale anapoanza kutawaliwa na vitu, kwa wakati huo huo, na vyote kwa mara moja, maisha ya madanganyo huanza. Yule afuataye Njia Bora ya kwenye Wongofu hatakubali majuto wala kuhifadhi matazamio, ila kwa moyo adilifu na mtulivu atakutana na yajayo.

3. Uongofu hauna sura mahususi au asili ambayo unaweza kujibainisha nayo; hivyo katika Wongofu wenyewe, hakuna cha kuongoa.

Uongofu upo na huishi tu kwa sababu ya madanganyo na ujinga; na kama haya yakiisha, Wongovu nao utakwisha. Na kinyume chake ni sahihi pia: hakuna Wongofu kama hakuna madanganyo na ujinga; hakuna madanganyo na ujinga pasipo Wongofu.

Kwa hiyo, kuweni macho, katika kushindana na fikra kuwa Wongofu ni "kitu" cha kushikiliwa vinginevyo hii itakuwa kizuizi. Wakati moyo uliokuwa ndani ya giza unapopata mwanga wa Wongofu, giza lake hupotea na njia lipoteleapo ndipo kitu kiitwacho Wongofu nacho hupitia.

Kwa vile watu hutamani kuwa Waongofu na na kutaka kuushikilia Wongofu ina maana kwamba bado wana madanganyo; kwa hiyo watu wanaofuata njia ya kuelekea kwenye Wongofu hawapaswi kuufikiria na iwapo wataufikiria basi wasisite kwa muda mrefu kuwa ndani yake.

Watu wapatapo Wongofu katika hali hii ina maaana kuwa kila kitu ni Wongofu kama kilivyo; Wongofu hadi mateso ya duniani na Wongofu vitakapokuwa kitu kilekile katika fikra zao.

4. Dhana hii ya umoja wa ulimwengu - kwamba vitu katika maumbile yake havina alama za utofautisho - inaitwa "Sunyata".

Sunyata maana yake ni kutokuwa thabiti, ambacho hakijazaliwa, kisichokuwa na hali ya upweke, bila "uwili". Ni kwa kuwa vitu vyenyewe havina umbo au tabia tunazoweza kusema kuwa vitu hivi ni vya kuzaliwa ama kuharibiwa. Hakuna chochote juu ya hali halisi ya vitu kinachoweza kuelezwa kwa njia ya upambanuzi, ndiyo sababu vitu vinaitwa visivyo yakini.

Kama ulivyokwisha dokezewa, vitu vyote hutokea na kutoweka kutokana na sababu na hali. Hakuna kitu kinachoishi peke yake, kila kitu kinahusiana na kingine.

Penye mwanga pana kivuli, penye marefu pana mafupi,penye weupe pana weusi, kwa jinsi hii hali ya upekee ya vitu haiwezi kuwepo, vinaitwa visivyo - yakini.

Kwa mantiki ileile, Wongofu hauwezi kuwepo bila ujinga, hakuna ujinga pasipokuwepo Wongofu. Kwa kuwa vitu havitofautiani katika hali halisi, haiwezekani kuwepo na "uwili".

5. Kwa mazoea yao watu hujifikiria kuwa wao wameunganishwa na kuzaliwa na kufa, ila kwa hakika hakuna dhana za namna hiyo.

Watu wanapoweza kutambua ukweli huu,basi wametambua ukweli wa kutokuwepo uwili katika kuzaliwa na kufa.

Ni kwa sababu watu huhifadhi wazo la ubinafsi na

kung'ang'ania wazo la kuwa na mali, lakini kwa kuwa hakuna kitu kama "nafsi" haiwezekani kuwepo na vitu kama mali, watu wakiweza kutambua ukweli huu, wataweza kutambua ukweli wa"kutokuwepo - uwili".

Watu huendelea kutofautisha kati ya lililotakasika na lisilotakasika, lakini katika hali halisi ya mambo, hakuna tofauti hizo, ila tofauti inakuwepo kutokana na picha zisizoelekea na za uwongo zilizimo ndani ya mioyo yao.

Katika hali kama hiyo watu hutenganisha mema na mabaya, lakini mema na mabaya hayaishi kuwa tofauti. Wale wafuatao njia ya kwenda kwenye wongofu hawatambui uwili huo na huongoza katika kutotukuza wema na kulaani maovu, wala kutweza wema na kusamehe maovu.

Kawaida watu huchukia balaa na kutamani bahati; lakini tofauti yake ikiangaliwa kwa makini, balaa mara nyingi hugeuka bahati njema na bahati njema kuwa balaa. Mtu mwerevu hujifunza kupambana na mambo ya maisha yanayobadilika kwa roho adilifu bila ya kufurahishwa na mafanikio wala kusikitishwa na kutofaulu. Hivyo mtu hutambua ukweli wa kutokuwepo - uwili.

Kwa hiyo maneno yote yaelezayo uhusiano wa uwili - kama vile kuishi na kutoishi, tamaa za dunia na maarifa ya kweli utakaso na uchafu, wema na uovu - hakuna hata moja kati ya haya yanayohitilafiana inayoweza kuelezwa au kutambuliwa asili yake

halisi katika fikra za mtu. Watu wanapokuwa huru kutokana na kauli kama hizo na hasira zitokanazo na kauli hizi, wanatambua ukweli uliowazi kwa wote wa Sunyata.

6. Kama ua safi la yungiyungi liotavyo katika matope ya bwawa badala ya kuota katika ardhi yenye rutuba iliyopo kwenye mwambao, Vivyo hivyo ndivyo Wongofu wa u-Buddha uchipukavyo kutoka kwenye uchafu wa tamaa za duniani. Hata maoni potofu ya wazushi pamoja na madanganyo ya tamaa za dunia vinaweza kuwa mbegu za u -Buddha.

Ikiwa mpiga mbizi anataka kupata lulu lazima azame hadi chini ya bahari huku akikwepa hatari zote za marijani yaliyochongoka pamoja na papa wabaya. Hivyo binadamu yampasa kupambana na hatari ziambatanazo na tamaa ya dunia kama anataka kupata lulu ya Wongofu. Yampasa kwanza apotelee katika majabali ya milima ya ubinafsi na choyo, kabla ndani mwake hajapata mwamko na kuwa na hamu ya kutafuta njia ambayo itamwelekeza kwenye Wongofu.

Kuna hadithi ya mtawa aliyekuwa na uchu wa kutafuta njia ya kweli hadi akapanda mlima wa Panga na kujitupa motoni huku akivivumilia kwa sababu ya kuwa na matumaini. Yeye anayekubali kujitoa mhanga kukabiliana na hatari za njiani atakutana na upepo mwanana ukivuma kwenye milima ya Panga zilizojaa hamaki na uroho na kati ya mioto ya chuki na; mwisho wake, atakuja kutambua kuwa uroho na tamaa za dunia ambavyo alikuwa akipambana na kuteseka dhidi yake ndio Wongofu

wenyewe.

7. Mafundisho ya Buddha, hutuelekeza kwenye pasipo uwili, kutoka katika dhana za upambanuzi wa mitizamo inayohitilafiana. Ni kosa kwa watu kutafuta jambo linalodhaniwa kuwa zuri na sahihi, na kukwepa lingine linalodhaniwa kuwa baya na ovu.

Ikiwa watu watasisitiza kuwa vitu vyote ni shinda na ni vya kupita tu hili ni kosa kubwa kama ilivyo kusisitiza kuwa vitu vyote ni hakika na havibadiliki. Ikiwa mtu anang'ang'ania kwenye ubinafsi ni kosa kwa sababu haiwezi kumuokoa kutokana na kutoridhika au kuteseka. Kama anaamini kuwa hakuna nafsi, ni kosa pia na itakuwa kazi bure kwake kufuata Njia ya Ukweli. Ikiwa watu watadai kuwa kila kitu ni furaha, hilo ni kosa vilevile. Buddha hufundisha Njia ya kati akizishinda dhana hizi potofu, ambapo njia panda huungana na kuwa kitu kimoja.

SURA YA TATU

TABIA - BUDDHA

I
MOYO WA UTAKASO

1. Kati ya binadamu kuna aina na viwango vya akili: wengine ni werevu, wengine ni wajinga, wengine wana tabia njema, wengine wana harara, wengine wanaongozwa kwa urahisi, wengine ni wagumu kuongoza, wengine wana mioyo safi na wengine wana mioyo ya kutu lakini tofauti hizi hazina maana kwenye kuchangia kuupata Wongofu. Dunia ni kama bwawa la yungiyungi lililojaa mimea kila aina, kuna maua ya rangi mbalimabali. Baadhi ni meupe na mengine ni samawati, mengine ni bluu na mengine njano. Baadhi huota ndani ya maji, mengine hutandaza majani yake sambamba na maji, mengine hutoa majani yake juu ya maji. Binadamu ana tofauti nyingi zaidi. Kuna tofauti ya jinsia, ingawa si tofauti muhimu, kwani kwa mafunzo sahihi, wanaume kwa wanawake wote wanaweza kupata Wongofu.

Ili kuwa Mwalimu wa tembo, yampasa mtu awe na sifa tano; afya njema, ujasiri, bidii, nia njema na hekima. Ili kufuata Njia Bora ya Wongofu ya Buddha yampasa mtu awe na sifa zilezile nzuri tano. Ikiwa mtu anazo hizi sifa, bila kujali jinsia yake inawezekana kuupata Wongofu. Haitaji muda mwingi kujifunza mafundisho ya Buddha kwa kuwa binadamu wote wana asili ya kuwa na hamu sana ya Wongofu.

2. Katika kushika njia ya wongofu, watu humwona Buddha kwa macho yao na humwamini kwa mioyo yao. Macho yamwonayo Buddha na mioyo imwaminio ni macho yale yale na mioyo ile ile ambavyo mpaka siku hiyo vilikuwa vikitangatanga huko na huko katika ulimwengu wa kuzaliwa na kufa.

Ikiwa mfalme atachokozwa na maharamia yampasa kuchunguza kwanza kambi lao kabla ya kufanya mashambulizi. Hivyo basi, mtu akisongwa na tamaa za dunia, yampasa kwanza achunguze chanzo na chimbuko lake.

Mtu awapo ndani ya nyumba na akafumbua macho yake ataona kwanza upande wa ndani wa chumba kabla ya kuona yaliyo nje kupitia kwenye madirisha. Vivyo hivyo hatuwezi kuwa na macho ya kuona maudhari ya nje kabla ya jicho kutambua mambo yaliyomo ndani ya nyumba.

Kama kuna moyo ndani ya mwili, yaupasa kujua kwanza mambo yaliyomo ndani ya mwili, ila kawaida watu hupendelea mambo yaliyo nje na huelekea kujua au kujali kidogo mambo yaliyomo mwilini.

Ikiwa moyo upo nje ya mwili, haupaswi kuwa na uhusiano na mahitaji ya mwili, lakini ukweli ni kuwa mwili huhisi moyo unachojua na moyo hujua mwili unachohisi. Kwa hiyo haiwezi kusemwa kwamba moyo wa binadamu upo nje ya mwili wake. Wapi basi asili ya moyo ilipo?

3. Tokea katika zama zile zisizojulikana, wakiwa wameshurutishwa na matendo yao yaliyopitishwa na kanuni mbili za dhana potofu, watu wametangatanga katika ujinga.

Kwanza waliamini kuwa moyo wa upambanuzi ambao hutanda chini ya maisha haya ya kuzaliwa na kufa, ilikuwa hali yao halisi, na pili, hawakujua kuwa walikuwa na moyo safi wa Wongofu uliofichika nyuma ya moyo wa upambanuzi.

Mtu anapokunja ngumi yake na kuinua juu mkono wake, macho huiona na moyo huipambanua, lakini moyo huo unaoipambanua ngumi hiyo siyo moyo halisi.

Moyo pambanuzi ni moyo tu wa kupambanua tofauti za kufikiriwa ambazo zimeumbwa kutokana na aina nyingine ya hisia zihusuzo nafsi.

Moyo pambanuzi unashurutishwa na sababu na hali, hauna asili ya vitu, na unabadilika mara kwa mara. Lakini kwa kuwa watu wana imani kuwa moyo huu ni moyo wao halisi, madanganyo huingia katika sababu na hali vinavyozaa mateso.

Mtu hufungua mkono na moyo huubaini, lakini ni kitu gani kinachojongea? Je ni moyo au mkono? Au si mojawapo ya hivyo? Mkono unapojongea na moyo nao hujongea na vivyo hivyo moyo unapojongea mkono hujongea nao. Lakini moyo unaojongea ni ule wa umbo la juu juu tu sio moyo ulio wa kweli na hakika.

4. Kimsingi kila mmoja ana moyo Safi,lakini moyo huo hufunikwa na uchafu na vumbi za tamaa za dunia zilizotokana na manzili. Moyo huu mchafu siyo wa asili halisi ya binadamu; kuna kitu kimeongezwa kwake kama awavyo mvamizi au mgeni ndani ya nyumba ambayo si yake.

Mwezi mara nyingi hufunikwa na mawingu, lakini hayauyumbishi na usafi wa mwezi utabaki vile vile. Kwa hiyo watu wasidanganyike kwa kufikiri kuwa moyo huu mchafu ni moyo wao wa kweli.

Yawapasa daima kujikumbusha juu ya ukweli huu kwa kujitahidi ndani mwao kuamsha moyo wa Wongofu ulio safi. Wakiwa wameingiwa na moyo wenye uchafu na unaobadilika na wakiwa wamedanganywa na mawazo yao potofu hutangatanga huko na huko katika dunia ya madanganyo.

Bugudha na uchafu wa moyo wa binadanu huamshwa na choyo pamoja na urejeo wa moyo huo kwenye manzili zibadilikazo.

Moyo ambao haujabughudhiwa na mambo yanapotokea, hubakia safi na mtulivu, kwa manzili yo yote ile ni moyo wa kweli na unapaswa kumiliki jambo.

Hatuwezi kusema kuwa hoteli hutoweka kwa kuwa mgeni ameondoka: Wala hatuwezi kusema utu na nafsi kweli ya mtu vimetoweka wakati moyo mchafu ulioamshwa na manzili ya

maisha yabadilikayo unapotoweka. Lile linalobadilika kufuatana na mabadiliko ya hali haliwi hali ya kweli ya moyo.

5. Na tufikirie chumba cha mihadhara kinachong'ara wakati jua linawaka lakini kinajaa giza jua linapochwea.

Tunaweza kufikiria mwanga ukitoweka na jua na giza likiingia na usiku, lakini hatuwezi kufikiria moyo utambuao mwanga na giza.

Moyo ambao ni mwepesi kuona mwanga na giza hauwezi kurudishwa kwa mwanga na giza wala hauwezi kurudishwa kwa mtu yeyote, unaweza kurudi tu kwenye maumbile ya kweli ambayo ndiyo asili ya msingi wake.

Ni moyo tu wa "muda" ambao kwa kitambo huona mabadiliko ya mwanga na ya giza wakati jua liwapo na lichweapo.

Ni moyo tu wa "muda" ambao una hisia tofauti kitambo hadi kitambo manzili ya maisha ibadilikavyo. Moyo huo siyo wa hakika na kweli. Moyo wa msingi na kweli unaotambua mwanga na giza ni asili ya kweli ya binadamu.

Hisia za muda juu ya zuri na baya, upendo na chuki ambazo zimechochewa na mazingira na hali ibadilikayo kutoka nje, ni marejeo ya kitambo ambayo yana chimbuko kutoka katika uchafu uliokusanywa na moyo wa binadamu.

Nyuma ya tamaa na maumivu ya dunia yanayopendwa na moyo ndipo ilipojituliza kweli na asili ya moyo safi usio na uchafu.

Maji ni duara katika chombo duara, na mraba katika chombo mraba, lakini maji yenyewe hayana umbo maalum. Watu mara nyingi husahau ukweli huu.

Watu huona lile ni baya na lile ni zuri, wanapenda hili na kuchukia lile, na hutenganisha kuishi na kutoishi na zaidi wakiwa wamejinasisha katika vikwazo hivi na kufungamana navyo, wanateseka.

Endapo tu, watu wangejisalimisha na kuacha kujihusisha na maswala haya ya kufikiria na kufanya mipambanuo isiyo ya kweli na wakarudi kuhifadhi utakaso ulio kwenye mioyo yao ya asili, basi miili yao pamoja na mioyo yao vyote vingekuwa huru pasipo uchafu na mateso; wangejua amani itokanayo na uhuru huo.

II
TABIA - BUDDHA

1. Tumezungumzia juu ya moyo uliotakasika wa kweli kuwa ndio msingi, ndio Uasili-wa-Buddha, yaani ndiyo mbegu ya u-Buddha.

Mtu anaweza kupata moto aishikapo lenzi kati ya jua na kianga lakini moto watokea wapi? Lenzi ipo masafa marefu toka

kwenye jua, lakini moto hutokea kwenye kianga kwa njia ya lenzi. Lakini kama kianga kisingekuwa na asili ya kushika moto, moto usingetokea.

Katika misingi hiyo, ikiwa mwanga wa binadamu, asili yake ya kweli ambayo ndiyo u-Buddha itawaka na mwanga wake mkali utaangaza mioyo ya watu na itaamsha imani katika Buddha. Yeye hushika lenzi ya Hekima mbele ya mioyo ya watu wote ili imani zao ziharakishwe.

2. Mara nyingi watu hupuuzia mvuto uliomo kwenye mioyo yao ya kweli kwa ajili ya hekima ya Buddha iliyoongoka, na kwa sababu yake wamenaswa katika mtego wa tamaa za dunia, wanazidi kujiingiza katika mpambanuo juu ya mazuri na mabaya na tena husononeka juu ya kujibainisha na kuteseka kwa mambo hayo.

Kwa nini watu wenye moyo huu wa asili na uliotakasika wanazidi kung'ang'ania madanganyo na kujihukumu kutanga tanga katika dunia ya madanganyo na mateso,wakijifunika kwa uasili wa Buddha wakati mahali walipo pote pamezungukwa na mwanga wa hekima ya Buddha?

Hapo kale bwana mmoja aliangalia katika upande wa pili wa kioo na aliposhindwa kuona uso wake na kichwa chake alirukwa na akili. Ni jinsi gani isivyo muhimu kwa mtu kurukwa na akili kwa sababu tu ya kutokuwa mwangalifu wakati ameangalia tu upande wa nyuma wa kioo!

Ni kama ilivyo ujinga na kutokuwa na umuhimu kwa mtu kuendekea kuteseka kwa sababu ameshindwa kupata Wongofu alipotegemea kuupata. Hakuna kushindwa katika Wongofu, kushindwa kupo ndani ya watu, ambao, kwa muda mrefu, wametafuta Wongofu katika mioyo yao ya kupambanua, bila ya kugundua kuwa mioyo yao siyo ya kweli bali ni mioyo ya kufikirika iliyosababishwa na mlundikano wa choyo na udanganyifu vilivyoufunika na kuuficha moyo wao wa kweli.

Ikiwa mlundikano wa imani batili umesafishwa, Uongofu utatokea. Bali jambo la kushangaza, watu wapatapo Uongofu, watabaini kuwa bila ya kuwepo imani batili Uongofu hauwezi kuwepo.

3. Uasili wa Buddha silo jambo lenye mwisho. Ingawa watu wabaya waweza kuzaliwa kama hayawani au pepo wenye njaa au kuangukia jehanamu, hawawezi kamwe kupoteza uasili wao wa Buddha.

Hata kama ungezamishwa vipi katika uchafu wa mwili au kufichwa katika mizizi ya tamaa za dunia na hata ikisahaulika vipi, uvutano wa mtu kuelekea kwenye u-Buddha haupotezwi kamwe.

4. Kuna hadithi ya zamani juu ya mtu mmoja aliyepatwa usingizi wa ulevi. Rafiki yake alimsubiri kadri alivyoweza na baadaye alilazimika kuondoka lakini kwa kuhofia kuwa rafiki yake anaweza

kuwa na mahitaji ya baadaye , aliamua kuficha johari katika nguo ya mlevi. Yule mlevi alipozinduka bila kujua kuwa mwenzake alikuwa ameficha johari ndani ya nguo yake aliendelea kutanga tanga kwa njaa na umaskini. Baada ya muda mrefu watu hao wawili walikutana tena na rafiki alimwambia yule maskini juu ya johari na akamshauri aitafute.

Kama alivyo bwana mlevi katika hadithi, watu hutanga tanga wakiteseka katika maisha haya ya kuzaliwa na kufa, bila kutambua kilichofichwa ndani ya asili yao, kitu kilicho safi na kinang'ara, ambacho ni hazina isiyo na malipo ya uasili wa Buddha.

Hata vipi watu watakuwa hawatambui ukweli kwamba kila mmoja ndani mwake ana asili hiyo bora na hata kama wamejawa na dharau na ujinga walio nao, Buddha hapotezi imani juu yao kwa sababu anajua kuwa hata katika kidogo kati yao, kwa upeo mkubwa kuna uadilifu wote wa u-Buddha.

Kwa hiyo Buddha huamsha imani ndani mwao wale wadanganywao na ujinga na hawawezi kuona Asili yao ya Buddha, huwaondoa katika madanganyo na huwafundisha kuwa kimsingi hakuna tofauti kati yao na u-Buddha.

5. Buddha ni yule aliyepata u-Buddha na watu ni wale ambao wana uwezo kupata u-Buddha; hiyo tu ndiyo tofauti kati yao.

Lakini ikiwa mtu atafikiri kuwa amepata Uongofu,

anajidanganya kwani, hata kama anaelekea njia ile, bado hajaufikia u-Buddha.

Uasili wa Buddha haupatikani bila kuwa na uangalifu na kuweka bidii yakinifu wala kazi haikamiliki hadi u-Buddha umepatikana.

6. Hapo kale Mfalme aliwakusanya baadhi ya vipofu karibu na tembo na akawataka wamweleze jinsi tembo anavyofanana. Mtu wa kwanza aligusa pembe na akasema kuwa tembo ni kama karoti kubwa ajabu, mwingine alibahatisha kugusa sikio na akasema yu kama feni kubwa, mwingine aligusa mkonga wake na akasema tembo ni kama mwichi, bado mwingine aliyebahatisha kugusa mguu wake, alisema ni kama kinu, na mwingine, aliyeshika mkia wake alisema kuwa alikuwa kama kamba. Hakuna hata mmoja kati yao aliyeweza kumwambia mfalme umbo halisi alilonalo tembo.

Kama mfano huu ulivyo, mtu anaweza kueleza juu juu uasili wa mtu lakini hawezi kueleza asili ya kweli ya binadamu, uasili wa Buddha.

Kuna njia mojawapo tu inayowezekana ambayo ni asili ya mtu ya milele, Asili yake ya Buddha ambayo haiwezi kuyumbishwa na tamaa za duniani au kuharibiwa na kifo, inaweza kubainika, nayo ni Buddha na kwa mafundusho bora ya Buddha.

III
BILA UBINAFSI/U-MIMI

1. Tunakuwa tunazungumzia uasili wa Buddha kana kwamba ni kitu kinachoweza kuelezeka na kana kwamba ulishabihiana na "roho" ya mafundisho mengine, lakini haupo hivyo.

"Dhana ya nafsi ya mtu" ni jambo ambalo limekuwa likifikiriwa na moyo pambanuzi ambao kwanza uliishika na kujibainisha kwayo lakini ambao yaupasa kuachana nayo. Kinyume chake, Uasili wa Buddha ni jambo lisiloelezeka linalopaswa kugunduliwa kwanza. Kwa namna fulani inafanana na nafsi ya mtu lakini siyo "nafsi" katika maana ya "ni mimi" au "angu".

Kuamini katika kuwepo kwa "nafsi" ni imani potofu inayodhania kuwa kuwepo ni kutokuwepo.

Hii inaweza kuelezwa katika mfano. Mama mmoja alimpeleka mtoto wake mgonjwa kwa daktari. Daktari alimpatia mtoto dawa na akamweleza mama huyo asimnyonyeshe mwanae hadi dawa imeanza kutumika mwilini.

Mama huyo aliyapaka matiti yake kwa dawa chungu ili mwanae asiyanyonye kwa hiari yake. Baada ya dawa kuwa imeyeyuka tumboni mama huyo alisafisha matiti na kumwachia mtoto anyonye. Mama alitumia njia ya namna hii ili kumwokoa mwanae kwa kuwa alimpenda.

Kama mama katika mfano huu, Buddha katika kuondoa kutoelewana vema na kuvunja fungamano na nafsi ya mtu, hukana kuwepo kwa nafsi, na pindi fungamano na kutoelewana vema vinapotokomezwa, ndipo auelezeapo uhakika wa moyo wa kweli ambao ni uasili wa Buddha.

Kufungamana na umimi huwapotosha watu na kuwaelekeza katika madanganyo, lakini imani katika uasili wa Buddha huwapeleka kwenye Uongofu.

Ni kama mwanamke katika hadithi aliyerithishwa sanduku. Bila kujua kuwa sanduku lilikuwa na dhahabu aliendelea kuishi maisha ya kimaskini hadi mtu mwingine alipolifungua na kumwonyesha dhahabu yake. Buddha hufungua mioyo ya watu na kuwaonyesha utakaso wao wa uasili wa Buddha.

2. Ikiwa kila mtu ana uasili wa Buddha, kwa nini kuna mateso mengi kutokana na watu kudanganyana au kuuana? Na kwa nini kuna tofauti kubwa ya vyeo na ukwasi, tajiri na maskini?

Kuna hadithi juu ya mpiga mieleka mmoja aliyezoea kuvaa pambo la kito cha thamani kwenye paji la uso wake. Siku moja alikuwa akicheza mieleka na kito hicho kiliseteka katika nyama ya uso. Alifikiri amepoteza kito chake na akaenda kwa daktari amfunge jeraha. Mganga alipoanza kumfunga jeraha akakuta kito kimeingia ndani ya nyama na kufunikwa kwa damu na uchafu. Aliinua kioo na kumwonyesha mcheza mieleka kile kito.

Uasili wa Buddha ni "kama kito" cha thamani katika hadithi hii: unafunikwa na uchafu na vumbi la mambo mengi na watu hufikiri kuwa wameupoteza, lakini mwalimu mwema huurejesha tena kwa ajili yao.

Uasili wa Buddha upo katika kila mtu bila kujali ni kwa kina gani umefunikwa na choyo, hasira na ujinga au umezikwa kwa matendo na upatilizo wake. Uasili wa Buddha hauwezi kupotea au kuharibiwa, na pindi uchafu wote unapoondolewa hapo hapo au kitambo uasili hujitokeza tena.

Kama mcheza mieleka katika hadithi alivyoonyeshwa kito kilichoseteka ndani ya nyama na damu kwa msaada wa kioo, hivyo watu huonyeshwa asili ya Buddha yao ilivyozikwa chini ya uchu na tamaa zao za dunia kwa njia ya mwanga wa Buddha.

3. Uasili wa Buddha daima ni mtakatifu na mtulivu bila kujali ni jinsi ipi umefunikwa kwa utofauti wa hali ya nchi na mazingira yao. Kama maziwa ya ng'ombe yalivyo meupe wakati wote bila ya kujali rangi ya ngozi ya ng'ombe, awe ni mweupe, mwekundu au mweusi, ndivyo isivyo na maana kwa utofauti upi matendo ya watu yanaweza kugeuza maisha yao ama ni vipi matokeo ya tofauti yanaweza kuathiri matendo na mawazo yao.

Huko India kuna methali juu ya mmea wa dawa wa ajabu uliokuwa umefichika katika nyasi ndefu zilizo kwenye milima ya Himalayas. Kwa muda mrefu watu wengi waliutafuta mmea huo bila mafanikio hadi hapo mwerevu mmoja alipougundua kwa

utamu wake. Kwa muda wa maisha yake alikusanya dawa hiyo na kuiweka katika pipa, lakini baada ya kifo chake dawa hiyo tamu na ya kuongeza maisha ilibaki mbali mafichoni kwenye kijito huko milimani na maji matamu ndani ya pipa yalibadilika yakawa chachu na yenye madhara pamoja na mionjo mbalimbali.

Vivyo hivyo uasili wa Buddha umefichika kati ya pori lililooteshwa kwa tamaa za dunia na haupatikani kwa urahisi lakini Buddha aliutafuta na kuudhihirisha kwa watu na kadri waupokeavyo kwa werekevu tofauti ndivyo uletavyo maonjo tofauti kwa kila mmoja.

4. Almasi ambayo ni ngumu kuliko vitu vyote vijulikanavyo haiwezi kusagwa. Mawe na mchanga huweza kusagwa na kuwa vumbi lakini almasi haidhuriki. Uasili wa Buddha ni kama almasi, hivyo hauwezi kuvunjwavunjwa.

Asili ya binadamu, vyote mwili na moyo, vitakwisha, lakini uasili wa Buddha hauwezi kuharibika.

Uasili wa Buddha ni tabia moja tu nzuri sana katika asili ya binadamu. Buddha hufundisha kuwa, ingawa katika asili ya mwanadamu kuna namna tofauti zisizoisha kama vile wanawake na wanaume, hakuna mbaguano katika uasili wa Buddha.

Dhahabu safi hupatikana kwa kuyeyusha mwamba na kuondoa uchafu wote. Ikiwa watu wangeyeyusha miamba ya mioyo yao na kuondoa uchafu wote na ubinafsi uambatanao na

tamaa za dunia, wote wangerejesha uasili mtakatifu za Buddha.

SURA YA NNE

UCHAFU (NAJISI)

I
UCHAFU WA BINADAMU

1. Kuna aina mbili za tamaa za dunia zichafuazo na kufunika utakaso wa hali ya Buddha. Kwanza ni tamaa ya kuchambua na kujadili ambavyo husababisha watu kuchanganyikiwa wakati wa kutoa maamuzi. Pili ni tamaa ya jazba itokanayo na uzoefu ambayo kwayo thamani ya utu hupotoshwa.

Madanganyo yatokanayo na kufikiri na yale yatokanayo na majaribio yote yanaweza kufikiriwa kama ni ya mchanganuo wa uchafu wote wa binadamu, lakini ukweli ni kwamba kuna chimbuko mbili duniani ambapo matatizo haya yameegemea. Kwanza ni ujinga na pili ni tamaa.

Madanganyo ya kufikiria yameegemea kwenye ujinga na madanganyo ya majaribio yameegemea kwenye tamaa kwa hiyo mambo yote hakika yamekuwa ni jambo moja tu na kwa pamoja ni chanzo cha mihangaiko yote.

Kama watu ni wajinga hawawezi kufikiri kwa usahihi na kwa usalama. Wanaposalimu amri kwa tamaa ya kuishi, mambo mengine hujiambatanisha kama vile kushikilia vitu, na kujishikiza kwa kila jambo. Ni kutokana na njaa hii ya kila mara itamanishayo kila kitu kizuri kionekacho au kusikika ambayo watu hujikuta

wameelekea kwenye madanganyo ya tabia. Baadhi ya watu husalimu amri hata kwa tamaa ya kifo cha mwili.

Kutokana na chimbuko hizi za mwanzo, vyote kama choyo, ujinga, kutokuelewana, mambo yapitayo, wivu, ulaghai, uongo, majivuno, matusi, ulevi, ubinafsi, huongezeka na kuzidi kujitokeza.

2. Choyo hutokana na mawazo potofu ya kujiridhisha, hasira hotokana na mawazo potofu yahusuyo hali ya maadili ya mtu na mazingira aliyomo, ujinga hutokana na kutoweza kujua matendo mazuri ni yapi.

Mambo haya matatu yaani - choyo, hasira na ujinga huitwa mioto mitatu ya dunia. Moto wa choyo huunguza wale waliopoteza akili zao za kweli kupitia kwenye choyo, moto wa hasira huunguza wale waliopoteza akili zao za kweli kwenye hasira, moto wa ujinga huunguza wale waliopoteza akili zao za kweli kutokana na kushindwa kwao kuyasikia na kuyafuata mafundisho ya Buddha.

Kwa hakika, dunia hii inaungua pamoja na mioto mingi ya aina mbalimbali. Mioto hii ni moto wa choyo, moto wa hasira, moto wa ujinga, moto wa tamaa na wa ubinafsi, moto wa kuishiwa nguvu, magonjwa na kifo, moto wa maombolezo, masikitiko, mateso na uchungu. Kila mahali mioto hii inawaka. Haiunguzi nafsi ya mtu peke yake bali pia husababisha wengine kuteseka na kuwaelekeza kwenye matendo maovu ya mwili;

maneno na akili. Vidonda visababishwavyo na mioto hii huzaa usaha ambao huambukiza na kutoa sumu ya kuharibu wale wote wanaoikaribia mioto hii na huwaelekeza kwenye njia za dhambi.

3. Choyo huchimbuka kutoka kwenye hali ya kutaka kuridhika, hasira hutokana na hali ya kutoridhika, na ujinga hutokana na mawazo yasiyo safi. Ibilisi wa choyo ana uchafu kidogo lakini ni mgumu kuondoa, ibilisi wa hasira ana uchafu mwingi lakini ni mwepesi kuondolewa, ibilisi wa ujinga ana uchafu mwingi na mgumu mno kumwondoa.

Kwa hiyo, watu yawapasa kuzima mioto hii popote na wakati wowote inapojitokeza kwa kufanya maamuzi sahihi juu ya mambo yanayoweza kuleta kuridhika kuliko kwa haki na kweli, na kwa kutawala mioyo yao juu ya mambo yasiyoridhisha katika maisha, na kwa kuyakumbuka mafundisho ya Buddha juu ya utu na hekima. Iwapo moyo umejazwa na mawazo yenye busara, yaliyoi safi yasiyo ya uchoyo, basi hapatakuwepo nafasi ambapo mizizi ya tamaa za ulimwengu yaweza kuchipukia.

4. Choyo, hasira na ujinga ni kama homa. Binadamu apatapo homa hii hata akilala kwa utulivu chumbani mwake bado atasikia maumivu na kuteseka kutokana na ukosefu wa usingizi.

Wale wasio na homa hii hawana taabu yo yote kupata usingizi wa amani, hata wakilala kwenye usiku wa baridi wakati wa masika juu ya udongo uliofunikwa tu na majani kidogo au wakati wa usiku wa kiangazi kwenye chumba kidogo

kilichofungwa.

Mambo matatu haya, choyo, hasira na ujinga ndivyo hasa chanzo cha mateso yote ya binadamu. Ili kuondoa vyanzo hivi vya mateso, mtu yampasa kuyashika mafundisho, yampasa kujizoeza kutuliza fikra yake kwa makini na kuwa na busara. Kuyashika mafundisho kutaondoa uchafu wa choyo, kuituliza fikra yake kwa makini kutaondoa uchafu wa hasira na busara itaondoa uchafu wa ujinga.

5. Tabia za binadamu hazihesabiki. Ni kama mtu mwenye kiu anywapo maji ya chumvi, hayaimalizi kiu yake bali huiongeza.

Vivyo ndivyo ilivyo kwa mtu anayejitahidi kufurahia tamaa zake, hufaidi tu ongezeko la kutoridhika, na kuzidisha majanga yake.

Furaha ya tamaa kamwe hairidhishi; kila wakati huacha nyuma wasi wasi na uchungu ambavyo haviwezi kutulizwa, na kama furaha ya tamaa zake itazimwa, itamfanya awe "kichaa".

Katika kuridhisha tamaa zao, watu watapambana na kupigana wao kwa wao, mfalme kwa mfalme, raia kwa raia, mzazi kwa mtoto, ndugu kwa ndugu, dada kwa dada, rafiki kwa rafiki, watagombana hata kuuana wao kwa wao ili kuridhisha tamaa zao.

Watu huangamiza maisha yao katika jitihada za kutosheleza

tamaa. Wataiba, kudanganya na kuwa wazinzi; na kisha watakapokamatwa, watateseka kutokana na aibu hiyo na adhabu zake.

Watafanya dhambi kwa miili yao na maneno yao, watafanya dhambi kwa mioyo yao wakijua fika kuwa furaha hatima yake italeta huzuni na mateso; kwa kweli tamaa ina nguvu. Baadaye yatakuja mateso mengi kwa dunia inayofuata yakiambatana na uchungu mwingi.

6. Kati ya tamaa za dunia ngoa ndiyo inayoongoza. Tamaa nyingine zote duniani hufuata katika reli hiyo.

Ngoa huelekea kuleta udongo ambamo tamaa nyingi hustawi. Ngoa ni kama pepo mbaya amezaye matendo yote mema ya duniani. Ngoa ni kama nyoka mwenye sumu kali ajifichaye katika shamba la maua; huwauma wale wote wajao shambani kufuata urembo. Ngoa ni kama mzabibu upandao mti na kutambaa juu ya matawi yake na kuusonga. Ngoa huingiza mikono yake katika mahangaiko ya binadamu na kunyonya busara nzuri ya moyo mpaka moyo unapokauka. Ngoa ni chambo cha pepo mbaya ambaye wajinga humfumbata na mwisho husukumwa katika vina vya dunia ovu.

Ikiwa mfupa mkavu utapakwa damu mbwa atauguguna hadi atakapochoka na kukata tamaa. Ngoa kwa binadamu ni sawa sawa na mfupa kwa mbwa, mtu ataitamani hadi atakapochoka.

Ikiwa kipande cha nyama kitatupiwa kwa nyang'au wawili, watagombana na kuraruana ili kukipata. Mtu mjinga akibeba mwenge huku akipingana na upepo bila shaka atajiunguza. Kama nyang'au hao wawili na mjinga, watu hujiumiza na kujiunguza kwa sababu ya tamaa za dunia.

7. Ni rahisi kuukinga mwili wa nje kutokana na mishale yenye sumu lakini ni vigumu kuukinga moyo kutokana na mishale ya sumu ipenyezayo kutoka ndani mwake. Uroho, chuki, ujinga na hila za ubinafsi - hii ni mishale minne ya sumu ipenyezayo kutoka ndani ya moyo wenyewe na kuushambulia kwa sumu kali sana.

Kama watu wataambukizwa na uroho, chuki na ujinga, watasema uongo, watadanganyana, watatukanana na wataseng'enyana, tena watakamilisha maneno yao kwa kuua, kuiba na kuzini.

Hizi hali tatu ovu za moyo, maneno manne maovu na matendo matatu maouvu yakijumlishwa pamoja hufanya maovu makuu kumi.

Iwapo watu watazoea kuongopa, wataendelea kutenda kila baya bila hata wao wenyewe kujitambua. Kabla ya kutenda mabaya lazima waongope, na mara waanzapo kuongopa watatenda dhambi bila kujali.

Uroho, tamaa mbaya, uwongo, chuki, balaa na huzuni, yote yanatokana na ujinga. Hivyo basi ujinga ni sumu kuu.

8. Kutokana na tamaa matendo hufuata,, kutokana na matendo, mateso hufuata; tamaa, matendo na mateso ni kama gurudumu lizungukalo daima.

Mzunguko wa gurudumu hili hauna mwanzo wala mwisho, watu hawawezi kuepuka kufanyika upya kwa maisha. Maisha mapya hufuata maisha mengine kufuatana na mzunguko wa mhamo usio kuwa na mwisho.

Kama mtu angerundika majivu na mifupa yake inayoungua katika mhamo huu wa milele, huenda lundo hilo lingekuwa mlima mrefu; kama mtu angekusanya maziwa ya akina mama aliowanyonya wakati wa majira ya mhamo huo yangekuwa mengi kuliko hata bahari.

Ingawa watu wote wana asili ya u-Buddha , asili hii inafichwa na kuzamishwa katika uchafu wa tamaa za kidunia bila kujulikana kwa muda mrefu. Hii ndiyo sababu mateso ni kwa watu wote na maisha ya taabu yanaendelea kuwepo.

Lakini, kwa kukubali uroho, chuki, na ujinga matendo maovu hukusanywa na mambohuanza upya, hivyo, kwa kufuata mafundisho ya Buddha, vianzo viovu vitasafishwa, na kurudi upya katika dunia ya mateso kutakwisha.

II
TABIA NA HALI YA BINADAMU

1. Tabia ya binadamu ni kama msitu mnene usio na njia ya kuingia na ambao ni vigumu kupitika. Kwa ulinganifu tabia ya mnyama ni rahisi kuielewa. Bado, kwa ujumla tunaweza kupambanua tabia ya binadamu kwa msingi wa tofauti nne madhubuti.

Kwanza, kuna sababu ya mafundisho batili, kuna watu ambao huishi kwa uhasama na kujiletea kuishi kwa mateso. pili, kuna wale ambao, kwa ukatili, kama wizi, kama kuua au kama matendo mengine yasiyo ya huruma, huwafanya wengine kuteseka. Tatu, kuna watu wawafanyao wengine wateseke pamoja nao. Nne, kuna wale wasioteseka bali huwaokoa wenzao kutokana na mateso. Watu hawa katika kundi la mwisho, kwa kufuata mafundisho ya Buddha, hawafuati uroho, chuki au ujinga, bali huishi maisha ya amani, utulivu, huruma na hekima bila kuiba au kuua.

2. Kuna aina tatu za watu duniani. Aina ya kwanza ni kama herufi zilizoandikwa juu ya mwamba; wanapokea chuki kwa urahisi na kuishi na mawazo ya chuki kwa muda mrefu. Aina ya pili ni kama herufi zilizoandikwa katika maji yatiririkayo; hawashiki mawazo yapitayo; hawajihusishi na matusi wala maseng'enyo; mioyo yao haina vurugu na ni mitakatifu.

Kuna aina nyingine za watu. Kwanza ni wale wajivunao;

watendao bila kufikiri; na hawatosheki; tabia zao zinaeleweka kwa urahisi. Pili kuna wale wenye heshima na adabu na kila mara hutenda baada ya kufikiri; tabia zao ni vigumu kuzielewa. Pia kuna wale walioshinda tamaa kabisa; haiwezekani kuwaelewa tabia zao.

Hivyo watu wanaweza kuainishwa katika njia tofauti, lakini tabia zao ni vigumu kuzielewa. Ni Buddha tu peke yake awaelewaye, na, kwa hekima yake huwaongoza katika mafundisho mbalimbali.

III
MAISHA YA BINADAMU

1. Kuna kisa kifafanuacho maisha ya binadamu. Hapo kale kulikuwa na mtu akiendesha mtumbwi kwenye mto. Mtu mmoja ufukoni alimwonya, "Wacha kupiga kasia kwa furaha kuelekea kwenye mkondo mkali; kuna maporomoko na kizingia cha maji hatari na kuna mamba na majini vikisubiri katika mapango ya mawe.

Katika kisa hiki, "mkondo mkali" ni maisha ya tamaa mbaya; "kupiga makasia kwa furaha" ni kuruhusu tamaa za binafsi; "kizingia cha maji" ina maana ya furaha; "maporomoko mbele" ina maana ya maumivu na mateso; "mamba na majini" inahusu kifo na kuoza ambayo hufuata maisha ya anasa na tamaa mbaya; "mtu aliye ufukoni aonyaye," huyo ni Buddha.

Kuna kisa kingine. Mtu aliyetenda kosa la jinai anakimbia; walinzi wanamfukuza na katika kutaka kujificha anatumbukia katika kisima kwa kutumia mizabibu iliyoota kandokando yake. Anapotelemka kisimani anawaona nyoka sehemu ya chini ya kisima, kwa hiyo kwa usalama wake anaamua kung'ang'ania kwenye mizabibu.

Baada ya muda wakati na mikono yake imeanza kuchoka, anawaona panya wawili mmoja mweupe na mwingine mweusi wanauguguna ule mzabibu.

Mzabibu ukikatika ataanguka kwenye nyoka na kuangamia. Ghafla, kwa kuangalia juu anaona juu ya uso wake mzinga wa nyuki na matone ya asali yakidondoka. Huyu bwana, kwa kusahau hatari zote anaonja asali kwa furaha.

"Mtu" ina maana ya yule anayezaliwa, kuteseka na kufa pekee. "Walinzi" na "nyoka" inahusu mwili na tamaa zake. "Mizabibu" ina maana ya mwendelezo wa maisha ya binadamu. "Panya wawili, mmoja mweupe na mwingine mweusi" inahusu muda, usiku na mchana, na miaka ipitayo. "Asali" inaashiria furaha za asili za mwili zinazoghilibu mateso ya miaka ipitayo.

2. Kuna kisa kingine tena. Mfalme anawaweka nyoka ndani ya sanduku na kumkabidhi mtumishi alitunze. Anamwamrisha mtumishi huyo kuwatunza vizuri na kumwonya kuwa akiwaudhi hata mmoja wao atapewa adhabu ya kifo. Kwa kuogopa,

mtumishi analitupilia mbali sanduku na kutoroka.

Mfalme anatuma walinzi kumkamata. Kwanza wanamwendea yule mtumishi katika hali ya urafiki kwa nia ya kumrudisha kwa usalama, lakini kwa kutoamini urafiki wao anatorokea katika kijiji kingine.

Baadaye, katika njozi, sauti inamwambia kuwa katika kijiji hiki hakuna makazi ya usalama, na kuwa pia kuna maharamia sita watakaomshambulia, kwa hiyo anakimbia mpaka anapokutana na kizuizi cha mto mpana. Huku akifikiria hatari zinazomfuata anatengeneza chelezo na anafaulu kuvuka mkondo mkali na ng'ambo yake hatimaye anapata amani na usalama.

"Nyoka wanne katika sanduku" inaashiria ardhi, maji, moto na hewa vitengenezavyo mwili. Mwili umewekwa kwenye hukumu ya tamaa mbaya na ni adui wa moyo. Kwa hali hiyo anajitahidi kuukimbia mwili.

"Walinzi watano wamwendeao kwa urafiki" ina maana ya vipengere vitano - umbo, kuhisi, kutambua, hiari na ufahamu wa nafsi - vinavyojenga mwili na moyo.

"Makazi salama " ni fahamu sita, ambazo si "makazi salama hata hivyo, na" maharamia sita" ni vigezo sita vya fahamu sita. Kwa hiyo anapoona hatari katika fahamu sita anakimbia tena na kurudi kwenye mkondo mkali wa tamaa za dunia.

Kwa hali hiyo hujitengenezea chelezo ya mafundisho mema ya Buddha na hatimaye huvuka mkondo mkali kwa usalama.

3. Kuna nyakati tatu zenye hatari wakati mwana hawezi kumsaidia mama yake na wala mama hawezi kuwa wa msaada kwa mwanae:- moto, mafuriko na wizi wa uvunjaji. Kumbe, hata katika nyakati hizi za hatari na huzuni kuna bado nafasi ya kusaidiana.

Lakini kuna nyakati tatu ambapo haiwezekani kabisa kwa mama kumwokoa mwanae wala mwana kumwokoa mama yake. Nyakati hizi tatu ni wakati wa magonjwa, wakati wa kuzeeka na watati wa kifo.

Mwana awezaje kuchukua nafasi ya mama yake wakati amezeeka? Mama awezaje kuchukua nafasi ya mwanae aliye mgonjwa? Je, wanawezaje kusaidiana kifo kinapokaribia? Hata kama wangependana kupindukia au kuwa karibu sana au marafiki sana, hakuna wa kumsaidia mwenzake katika wakati kama huo.

4. Siku moja, Yama, Mfalme wa Jehanum katika hadidhi za mapokeo, alimuuliza bwana mmoja aliyeingia jehanum juu ya maovu yake katika maisha yake, kama katika muda wa maisha yake aliwahi kukutana na wajumbe watatu wa mbinguni. Yule bwana alijibu: Hapana, mheshimiwa, sikukutana na watu wa namna hiyo."

Uchafu

Yama alimuuliza kama aliwahi kukutana na mtu mzee aliyepinda mgongo huku akitembea kwa mkongojo. Yule bwana alijibu: "Ndiyo, Bwana wangu, nimekutana na watu wa namna hiyo mara kwa mara." "Kisha Yama akamwambia: Unateseka kwa adhabu hii kwa sababu hukutambua kutokana na yule mzee, mjumbe wa mbinguni aliyetumwa kukutahadharisha kuwa ubadilishe mwenendo wako haraka sana kabla hata wewe hujawa mzee."

Yama alimuuliza tena ikiwa aliwahi kumwona mtu maskini, mgonjwa na asiye na rafiki yeyote. Yule mtu alijibu: "Ndiyo, Bwana wangu nimeona wengi wa jinsi hiyo. "Basi, Yama akamwambia: "Umekuja hapa kwa sababu umeshindwa kutambua kati ya wagonjwa hawa, wale wajumbe wa mbinguni walitumwa kukutahadharisha juu ya ugonjwa wako mwenyewe.

Ndipo Yama alipomwuliza kwa mara nyingine kama amewahi kumwona mtu mfu. Yule bwana akajibu: "Ndiyo Bwanangu, nimehudhuria kwenye vifo mara nyingi." Yama akamwambia: "Hii ni kwa sababu hukuweza kutambua kuwa kati ya watu hawa mitume walitumwa kwako kukutahadharisha kuwa umeletwa kwenye kifo. Kama ungeweza kuwatambua mitume hao na kuchukuwa onyo lao ungebadilisha mwelekeo wako, pia usingekuja kwenye nafasi hii ya mateso.

5. Siku moja palikuwa na mama mmoja aitwaye Kisagotami, mke wa bwana tajiri aliyerukwa na akili kutokana na kifo cha mtoto wake. Alibeba maiti ya yule mtoto akazunguka nayo

nyumba moja hadi nyingine akiwaomba watu wamfufue mwanae.

Bila shaka hakupata mtu wa kumsaidia, lakini hatimaye alikutana na mfuasi wa Buddha naye akamshauri amwone Aliyebarikiwa ambaye kwa wakati huo aliishi Jetavana, hivyo akaipeleka maiti ya mtoto kwa Buddha.

Mbarikiwa alimwangalia kwa huruma na kusema: "Kumfufua mtoto nahitaji mbegu za mti uitwao mtia usingizi; nenda ukaombe mbegu nne au tano za mti huo toka kaya moja ambayo haijapatwa na kifo hata siku moja."

Kwa hiyo huyo mama aliyechanganyikiwa alizunguka kila mahali asipate nyumba ambayo haijafikiwa na kifo. Mwisho alilazimika kurudi kwa Buddha. Katika utulivu wa Buddha akili ya yule mama ilimrudia na akaelewa maana ya maneno ya Buddha. Alichukua mwili wa marehemu mtoto wake akauzika na akarudi kwa Buddha akawa mmojawapo wa wanafunzi wake.

IV
UKWELI WA MAISHA YA BINADAMU

1. Watu wa dunia hii wangependa na kuzoea ubinafsi na ukatili; hawajui namna ya kupendana na kuheshimiana; wanabishana na kugombana juu ya mambo yasiyo na maana yoyote bali tu kwa madhara na mateso yao, na maisha yanakuwa

ya mzunguko wa ukiwa na huzuni.

Bila kujali kama ni matajiri au maskini, wana wasiwasi juu ya pesa yao; Wanateseka kutokana na umasikini wao na wanateseka kutokana na utajiri wao. Kwa kuwa maisha yao yanatawaliwa na uroho, hawaridhiki wala hawatosheki kamwe.

Mtu tajiri husumbuka juu ya shamba lake kama analo; anasumbukia jambo lake pamoja na mali zake nyingine. Ana wasiwasi wa kupatwa na hasara, jumba lake kuungua, wezi kuvunja nyumba na kuiba, yeye mwenyewe kutekwa nyara. Tena anahangaika juu ya kifo na kupanga kutumia mali yake. Kwa hakika yu pekee katika njia yake ya kifo na hakuna anayefuatana naye katika kifo.

Maskini kila siku anateseka kutokana na uchache na upungufu, na hii, husaidia kuamsha tamaa zisizoisha - kwa ardhi na nyumba. Akiwa amewashwa na tamaa huchakaa kimwili na kimoyo na mwisho hufariki katikati ya maisha yake.

Dunia nzima huwa ya kumsikitikia, hata njia ya kuelekea kwenye kifo huelekea kuwa ya upweke kama vile ana njia ndefu mbeleni isiyo na marafiki wa kumsindikiza.

2. Sasa, kuna maovu matano duniani. Kwanza kuna ukatili; kila kiumbe, hata wadudu, wanashindana wao kwa wao. Mwenye nguvu anashambulia asiye na nguvu, wanyonge wanawadanganya walio na nguvu; kila mahali kuna mapigano na

ukatili.

Pili, hakuna mpaka dhahiri kati ya haki za baba na mwanae; kati ya mkubwa na mdogo; kati ya mume na mke ; kati ya mwanajamii mkubwa na mdogo ; kwa kila tendo kila mmoja hujitahidi kuwa juu ya mwenzake ili kufaidika kuliko wengine wote. Wanadanganyana, kuna hadaa na wamejawa na unafiki.

Tatu, hakuna mpaka dhahiri kati ya tabia ya wanawake na wanaume. Kila mmoja kwa wakati mwingine ana mawazo machafu na potofu na tamaa ambayo huwaelekeza katika matendo ya ajabu na mara nyingi wanakuwa katika ugomvi, mapigano, udhalimu na uovu.

Nne, kuna uelekeo wa watu kutoheshimu haki za wenzao, kujikuza wao kwa gharama ya wenzao, kuwa mifano mibaya kitabia, na, kutokuwa waadilifu katika maneno yao, kudanganya, kusingizia, na kukashifu wengine.

Tano, kuna maelekeo ya watu kutojali wajibu wao kwa wenzio. Hufikiria sana juu ya faraja na tamaa zao; Husahau upendeleo na fadhila walizokwisha kupokea na kusababisha maudhi kwa wengine ambavyo mara nyingi huleta udhalimu mkubwa.

3. Watu yawapasa kuhurumiana; yawapasa kuheshimiana kwa tabia zao nzuri na kusaidiana katika shida; lakini, badala yake ni wachoyo na wana mioyo migumu; wanakashfiana kwa

kushindwa kwao na wanachukia wengine kwa manufaa yao. Kwa kawaida, karaha hizi huzidi kuwa mbaya na baada ya muda hazivumiliki tena.

Hisia hizi za chuki haziishii hivi mapema katika matendo ya ujeuri na ukatili; bali hupanda sumu katika hisia za chuki na hasira ambazo huchorwa kwa makini katika mioyo yao ambayo kwayo watu hubeba alama katika mzunguko wa kufanyika kuwa mwili.

Kweli, katika dunia hii ya tamaa kuu (ngoa), mtu huzaliwa pekee na kufa pekee, na hakuna mtu wa kusaidiana au kugawana naye adhabu baada ya kifo.

Kanuni ya chanzo na matendo ni ya ulimwengu wote; Kila mtu ataubeba mzigo wake wa dhambi na kuelekea kwenye upatilizo. Kanuni hii vilevile hutawala matendo mema. Maisha ya huruma na upole yatazaa bahati nzuri na furaha.

4. Kadri miaka inavyopita na watu kugundua jinsi walivyotekwa na choyo, tabia na mateso, kwa nguvu, wanasikitika na kukata tamaa. Katika kutaka tamaa mara nyingi hugombana na wenzao na huzama katika dhambi na kuacha kujaribu kutembea katika njia ya kweli; kila mara maisha yao hukatishwa bila kutegemewa katikati tu ya maovu yao nao huteseka milele.

Kuangushwa huku katika kukata tamaa kwa sababu ya taabu na mateso siyo hali ya kawaida na ni kinyume cha kanuni ya

mbinguni na duniani na, kwa hiyo, mtu atateseka pote katika dunia hii na katika ulimwengu ujao.

Ni kweli kwamba kila kitu katika maisha haya ni cha mpito na kimejaa mashaka, bali itahuzunisha ikiwa mtu yeyote atadharau ukweli huu na kuendelea kutafuta starehe na kutosheleza tamaa zake.

5. Ni kawaida katika dunia hii ya mateso kwa watu kufikiri na kutenda kwa uchoyo na ubinafsi na, ambayo kwayo, ni kawaida kwa huzuni na mateso kufuata.

Watu hujipendelea na kutowajali wengine. Watu hutawaliwa na matakwa yao yawapelekayo katika tamaa na matendo maovu. Kwa sababu ya haya, watateseka bila kikomo.

Maisha ya starehe hayadumu muda mrefu bali hupita kwa haraka sana, hakuna kitu chochote kinachoweza kufurahiwa milele.

6. Kwa hiyo, watu yawapasa wakati bado wangali vijana wenye afya nzuri, kutupilia mbali uchoyo wao wote na mahusiano yao yote na mambo ya dunia, na inawabidi kutafuta kwa nguvu Uongofu wa kweli, kwa kuwa hakuna tumaini la kudumu au furaha mbali na Uongofu.

Watu wengi, hata hivyo, hawaamini au hawajali kanuni hii ya chanzo na matokeo huendelea na tabia zao za uroho na

ubinafsi, wakiwa wasahaulifu wa ukweli kwamba tendo bovu huleta taabu.

Wala hawaamini kuwa matendo ya mtu katika maisha haya huyaathiri maisha yafuatayo na huwahusisha pia wengine kwa adhabu na thawabu zitokanazo na dhambi zao.

Wanalia na kuomboleza juu ya mateso yao, bila kuelewa kabisa umuhimu wa matendo yao ya sasa, juu ya maisha yao yajayo na uhusiano kati ya mateso yao ya sasa na matendo yao katika maisha yao yaliyopita. Hufikiria tu tamaa zao za sasa na mateso ya sasa hivi.

Hakuna kitu chochote duniani kinachodumu; kila kitu kinabadilika kwa mara moja na bila kutabirika. Lakini watu ni wachoyo na wajinga; wanasumbukia tu tamaa na mateso yapitayo mara moja. Hawayasikilizi mafundisho mema wala hawajaribu kuyaelewa; wao husumbukia matakwa yao ya sasa ya utajiri na tamaa kuu.

7. Tangu zama za kale watu wasiohesabika wamezaliwa katika dunia hii ya madanganyo na mateso, na bado wanaendelea kuzaliwa. Ni bahati njema hata hivyo, kwamba dunia inayo mafundisho mema ya Buddha na watu wanaweza kuyaamini na kusaidiwa.

Hivyo basi, watu yawapasa kufikiri kwa makini, waweke mioyo yao safi na miili yao pia, na waepukane na choyo na

maovu, na wautafute wema.

Kwa bahati kwetu sisi, elimu juu ya mafundisho ya Buddha imetufikia ; tujitahidi kuyaamini na kutamani kuzaliwa katika Nchi Takatifu ya Buddha. Tukishajua mafundisho ya Buddha, tusiwafuate watu wengine katika njia za kichoyo na kidhambi, wala tusiyaweke mafundisho ya Buddha peke yetu, bali tuyashike mafundisho hayo na kuyarithisha kwa wengine.

SURA YA TANO

FARAJA ILETWAYO NA BUDDHA

I
NADHIRI ZA AMIDA BUDDHA

1. Kama ilivyokwishaelezwa, watu hutekwa na tamaa za kidunia, wakirudia kutenda dhambi juu ya dhambi na kubeba mizigo ya matendo yasiyovumilika, wasiweze kutumia hekima zao au nguvu zao kuacha tabia hizi za uchoyo na upendeleo wa anasa. Kama hawawezi kushinda na kuondoa tamaa za kidunia, watawezaje kutambua asili yao halisi ya u-Buddha?

Buddha, ambaye alielewa fika tabia za binadamu alikuwa na huruma nyingi kwa watu na kuapa kuwa atafanya kila linalowezekana, hata kama ni kwa gharama ya taabu kwake, ili kuwaondolea hofu na mateso. Kwa kutekeleza faraja hii alijibainisha kama Bodhisattva katika zama za kale na kuweka nadhiri kumi zifuatazo

a) "Ingawa nimepata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu mpaka kila mtu katika nchi yangu awe na uhakika wa kuingia katika u-Buddha na kupata Wongofu.

b) "Ingawa nimeupata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu hadi mwanga wangu wa uthibitisho umeenea dunia nzima.

c) " Ingawa nimeupata u-Buddha,sitakuwa mkamilifu

hadi maisha yangu yatakapodumu na kuendelea katika nyakati mbalimbali na kuokoa idadi kubwa ya watu.

d) "Ingawa numeupata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu hadi ma-Buddha wote katika pande kumi watakapoungana na kulitukuza jina langu.

e) "Ingawa nimeupata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu hadi watu wote wenye imani ya kweli wamejitahidi kuzaliwa upya katika ardhi yangu kwa kurudia jina langu mara kumi kwa imani ya kweli na hasa waweze kufaulu katika uzawa huu mpya.

f) "Ingawa nimeupata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu hadi hapo watu kila mahali wameazimia kupata Uongofu, kushika uadilifu, kutamani kikwelikweli kuzaliwa katika nchi yangu, hivyo nitatokea wakati wa kifo chao na kundi kubwa la Mabodhisattva kuwakaribisha katika Nchi yangu Takatifu.

g) "Ingawa nimeupata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu hadi watu kila mahali, walisikiapo jina langu,wafikirie nchi yangu na watamani kuzaliwa huko na, mwisho wake wapande mbegu za uadilifu kwa moyo safi, na basi waweze kutimiza yote katika matakwa ya mioyo yao.

h) "Ingawa nimeupata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu hadi wale wote wanaozaliwa katika nchi Takatifu wawe na hakika ya kuupata u-Buddha ili waweze kuwaongoza wengine wengi katika Uongofu na katika kufuata na kushika huruma kuu.

Faraja iletwayo na Buddha

i) "Ingawa nimeupata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu hadi watu duniani kote wamevutwa kwa roho yangu ya kupenda huruma abayo itawatakasa mioyo na miili yao na kuwainua juu ya vitu vyote vya dunia hii.

j) "Ingawa nimeupata u-Buddha, sitakuwa mkamilifu hadi watu kila mahali popote, walisikiapo jina langu, wajifunze mawazo sahihi juu ya uzima na kifo, na wapate hekima halisi ambayo itafanya mioyo iwe safi na tulivu kati ya tamaa na mateso ya kidunia.

"Hivyo naweka nadhiri hizi; naomba nisipate u-Buddha hadi hapo zitakapotimilika. Na niwe chanzo cha Mwanga usio na kikomo, ukiniweka huru na kumulika hazina za hekima yangu na faraja, nikiongoa nchi zote na kuwaweka huru watu wote wanaoteseka."

2. Kwa hiyo, Yeye, kwa kukusanya faraja zisizohesabika katika miaka mingi, aligeuka Amida au Buddha wa Mwanga usio Kikomo na Maisha yasiyo na Mpaka, na akakamilisha nchi yake ya Buddha ya Utakatifu, ambamo sasa anaishi, katika dunia ya amani, akiwaongoa watu wote.

Nchi hii Takatifu, ambapo hakuna mateso, hakika nchi ya amani na ya furaha. Chakula, mavazi na na vyote vizuri huonekana iwapo watu wanaoishi huko wanavihitaji, Wakati upepo mwanana uvumapo kupitia katika miti iliyojaa johari,

muziki wa mafundisho yake matakatifu huijaza hewa na kusafisha mioyo ya wote wasikilizao.

Katika nchi hii Takatifu kuna maua yanayonukia vizuri sana ya yungiyungi, na kila ua lina petali nyingi za thamani, na kila petali inang'aa kwa uzuri usioelezeka. Nuru ya maua haya ya yungiyungi huangaza njia ya Hekima na wale wausikiao muziki na mafundisho matakatifu huelekezwa katika amani kamili.

3. Sasa Ma-Buddha wa pande kumi wanatukuza faraja za Buddha huyu wa Mwanga usio na kikomo na Maisha yasiyo na Mpaka.

Yeyote alisikiaye Jina la Buddha hulipokea na kulitukuza kwa shangwe, Moyo wake huungana na moyo wa Buddha na atazaliwa katika Nchi ya ajabu ya Buddha, Nchi Takatifu.

Wale wazaliwao katika Nchi Takatifu huungana katika maisha ya Buddha yasiyo kikomo; mioyo yao hujazwa huruma mara moja kwa wote watesekao nao huenda hima kuidhihirisha njia ya wokovu ya Buddha.

Katika imani ya nadhiri hizi hufukuzia mbali mambo yote ya kidunia na hutambua kutokudumu kwa dunia hii. Hujitolea ujira wao kwa ukombozi wa fahamu za maisha yao yote; huunganisha maisha yao na mateso yao, lakini, kwa wakati ule ule wakitambua uhuru wao kutoka katika shauku na minyororo ya maisha haya ya dunia.

Wanajua vikwazo na matatizo ya maisha ya dunia, lakini wanafahamu pia nguvu za huruma ya Buddha isiyo na kikomo. Wana uhuru wa kwenda au kurudi, wana uhuru wa kusonga mbele au kusimama wapendavyo ila huchagua kubakia na wale ambao wana huruma ya Buddha.

Kwa hiyo, yeyote asikiaye jina hili la Amida Buddha akashawishika kuliita Jina hilo katika imani ya kweli, atashiriki katika huruma ya Buddha. Hivyo watu wote yawapasa kuyasikiliza mafundisho ya Buddha na kuyafuata hata kama yatawapitisha tena katika ndimi za moto ziufunikao ulimwengu huu wa kufa na kuishi.

Ikiwa watu kwa kweli na kwa moyo, watanuia kuupata Wongofu,yawalazimu kutegemea nguvu za Buddha. Haiwezekani kwa mtu wa kawaida kusadiki uasili wa Buddha ulio mkuu bila msaada wa Buddha.

4. Amida Buddha hayupo mbali na yeyote. Nchi yake Takatifu inasemekana kuwa magharibi ya mbali, lakini, pia, ipo ndani ya mioyo ya wale watumainio kuwa naye kwa moyo wote.

Wakati watu wakipiga picha ya sura ya Amida Buddha iking'aa katika mng'ao wa dhahabu, katika mioyo yao, picha hiyo hugawanyika katika sura au maumbo themanini na nne elfu, kila sura au umbo likitoa miale ya mwanga themanini na nne elfu, kila sura au muale wa mwanga, ukiangaza dunia bila kumwacha katika giza mtu yeyote alitajaye jina la Buddha. Hivyo Buddha huyu

huwasaidia watu kufaidika kwa wokovu autoao.

Kwa kuuona mfano wa Buddha, mtu husaidiwa kuutambua moyo wa Buddha. Moyo wa Buddha umejaa huruma kuu ambayo huwapokea wote, hata wale wasiofahamu huruma yake au walioisahau, na, kwa wingi wale waikumbukayo kwa imani.

Kwa wale wenye imani, huwapa bahati ya kuwa pamoja Naye. Kwa kuwa Buddha ni yeye katika mwili wa usawa wa yeyote amfikiriaye Buddha, na Buddha humfikiria yeye na huingia ndani ya moyo wake bila kusita.

Hii ina maana kuwa mtu amfikiriapo Buddha, anao moyo wa Buddha katika hali yake ya ukamilifu uliojaa utakatifu, furaha na amani. Kwa maneno mengine, moyo wake huwa moyo wa Buddha.

Kwa hiyo, kila mtu katika imani takatifu na ukweli yampasa kuuangalia moyo wake kama ni moyo wa Buddha.

5. Buddha ana maumbo mengi ya kugeuka sura au kubadili mwili na anaweza kijidhihirisha katika njia nyingi kutegemeana na uwezo wa kila mtu.

Buddha hudhihirisha mwili wake kwa kuutanua kuweza kufunika anga yote na kutanda anga ya nyota isiyo na mipaka. Pia hujidhihirisha katika vitu vidogo vya maumbile; katika umbo,

mara nyingine katika nguvu, mara katika uelekeo na mikabala ya mioyo, na mara katika haiba ya mtu.

Lakini, katika namna moja au nyingine, Atajitokeza kwa wale walitajalo jina la Buddha kwa imani. Kwao Amida hujitokeza akiambatana na Mabodhisattiva wawili; Avalokitesvara, Bodhisattva wa Huruma na Mahasthama-prapta, Bodhisattva wa Hekima. Udhihirisho wake huijaza dunia yote ili kila mmoja aweze kuona, lakini ni wale tu wenye imani wauonao.

Wale wenye uwezo wa kuuona ufunuo wake wa muda wanahitaji furaha na utoshelevu wa milele. Zaidi ya hapo, wale watu wanaoweza kumwona Buddha wa kweli hutambua bahati za furaha na amani zisizohesabika.

6. Kwa vile moyo wa Amida Buddha pamoja na wa mapenzi na busara yake isiyo na mipaka ni hekima yenyewe, Buddha ataweza kuwaokoa wote.

Wengi wa watu waovu - wale watendao maovu ya ajabu, ambao mioyo yao imejaa uroho, chuki na kupumbazika; wale waongopao, wapayukao, watukanao na wale wanaoua, wanaoiba na kutenda matendo ya ufisadi; wale waliopo mwisho wa maisha yao baada ya matendo maovu - ulelekeo wao ni kwenye maisha marefu ya adhabu.

Rafiki mwema huwajia katika nyakati zao za mwisho na kuwasihi, akisema, "Sasa mnapambana na kifo;hamwezi kuficha maisha yenu maovu, bali mnaweza kukimbilia katika huruma ya Buddha ya Mwanga usio na Mwisho kwa kulitaja jina lake.

Ikiwa watu hawa wenye dhambi watalitaja jina la Amida Buddha kwa moyo mmoja dhambi zao zote ambazo zingewapeleka katika dunia ya maovu zitasafishwa.

Ikiwa tu kulitaja jina takatifu kunaweza kufanya maajabu haya, ni mangapi basi yanaweza kutendeka kama mtu ataweza kuelekeza mawazo yake kwa huyu Buddha!

Wale watakaofaulu kulitaja jina takatifu, hao watapokelewa na Amida Buddha na Bodhisattva wa Huruma na Hekima na hawa watawaongoza hadi katika Nchi ya Buddha, watakapozaliwa upya katika weupe na utakatifu kama wa ua la yungiyungi.

Kwa hiyo kila mmoja yampasa kushika moyoni maneno, "Namu-Amida-Butsu" au kutegemea kwa moyo wote juu ya Buddha wa Mwanga usio na Mwisho na Maisha yasiyo na mipaka!

II
NCHI ILIYO TAKATIFU YA AMIDA BUDDHA

1. Buddha wa Mwanga usio na mwisho, wa maisha yasiyo na kikomo anaishi na anaangaza ukweli wake milele. Katika nchi yake Takatifu hakuna kuumwa wala hakuna giza na kila saa inapita kwa furaha; kwa hiyo nchi hiyo inaitwa Nchi ya Raha Mstarehe.

Katikati ya nchi hii kuna ziwa la maji matakatifu yang'aayo, yenye mawimbi yavumayo taratibu na kutoa sauti nyororo na ya kupendeza kwenye ufuko wa mchanga wa dhahabu. Hapa na pale kuna maua ya yungiyungi makubwa kama magurudumu ya toroli yenye mwanga na maua mbalimbali - mwanga wa samawati kutokana na rangi ya samawati, njano kutokana na rangi ya njano, mwanga mwekundu kutokana na rangi nyekundu, mweupe kwa nyeupe ambayo harufu yake nzuri huijaza hewa yote.

Katika sehemu mbalimbali kando kando mwa ziwa kuna vibanda vilivyopambwa kwa fedha na dhahabu na feruzi na zamaradi, na ngazi za marumaru ziendazo ukingoni mwa maji. Katika sehemu nyingine kuna vikuta na safu za viguzo vilivyojengwa juu ya maji na kufunikwa na pazia na nyavu za madini ya thamani na katikati yake kuna vichaka vya miti ya viungo na vichaka vya maua.

Ardhi inang'aa kutokana na uzuri wake na hewa inatikisika

kutokana na amani zilizopo mbinguni. Mara sita, usiku na mchana, petali za maua zilizopambwa kwa rangi nzuri hudondoka kutoka angani na watu huyakusanya na kuyaweka katika vyombo vya maua ili kuyasambaza katika sehemu nyinginezo za nchi ya Buddha na kuyatoa sadaka kwa ma-Buddha elfu kumi.

2. Katika nchi hii ya ajabu kuna ndege wengi. Wapo kunguru weupe, bata weupe, tausi waliopambwa vizuri na ndege wengi wa nchi za joto wakubwa kwa wadogo wakitumbuiza kwa sauti nyororo. Katika nchi Takatifu ya Buddha, ndege hawa waimbao kwa sauti nzuri na nyororo hutangaza mafundisho ya Buddha na kusifu uadilifu wake.

Mtu yeyote asikiaye na kuusikiliza muziki wa sauti hizi, huisikiliza sauti ya Buddha na huamshwa upya katika imani, furaha na amani katika ushirika wa kidugu wa wafuasi wa Buddha popote walipo.

Upepo mwanana hupita katika miti ya Nchi Takatifu na kupeperusha pazia za mabanda zenye harufu nzuri na kupita kwa sauti tamu za kimuziki.

Watu wasikiapo mwangwi wa sauti nyororo za muziki kutoka mbinguni humfikiria Buddha, wa Dharma (mafundisho) na wa Samgha (undugu). Haya mambo mazuri yote ni viakisio vya Nchi Takatifu.

3. Je ni kwa nini Buddha wa nchi hii anaitwa Amida akiashiria Buddha wa Mwanga usio na Mwisho na maisha yasiyo na mpaka? Hii ni kwa sababu uzuri wa ukweli wake hung'aa ndani na nje ya mipaka ya nchi ya Buddha; ni kwa sababu umuhimu wa Huruma yake inayoishi haupungui kwa watu wasiohesabika nyakati zote.

Ni kwasababu idadi ya watu wanaozaliwa katika Nchi Takatifu na wakaongoka hasa hasa hawahesabiki na hawatarudi kamwe katika dunia ya mauti na madanganyo.

Ni kwa sababu idadi ya watu wanaopata uamsho katika maisha mapya kwa mwanga wake hawahesabiki.

Kwa hiyo, watu wote wakituliza fikra zao kwenye Jina lake na, wanapoelekea kwenye mwisho wa maisha yao, hata kwa siku moja au saba, wakinena jina la Amida Buddha kwa imani ya kweli, na wakiwa hivyo kwa moyo mtulivu, watazaliwa katika Nchi ya Buddha ya utakatifu, wakiongozwa na Amida Buddha pamoja na watakatifu wengine wengi watakaotokea mnamo saa hii ya mwisho.

Ikiwa mtu atalisikia jina la Amida Buddha, akawa na imani katika mafundisho yake, ataweza kuupata Uongofu wa kweli usio na kifani.

NJIA YA UTENDAJI

SURA YA KWANZA

NJIA YA KUTAKATA

I
UTAKASO WA MOYO

1. Watu wana tamaa za kidunia ambazo huwaingiza katika mateso na madanganyo. Zifuatazo ni njia tano za kujikomboa kutokana na minyororo ya tamaa za dunia.

Kwanza hawana budi kuwa na mawazo sahihi juu ya mambo; mawazo yanayotokana na uchunguzi wa makini, na kuelewa sababu na matokeo au madhara yake na kutambua umuhimu wake. Kwa kuwa chanzo na sababu za mateso vipo ndani ya tamaa za moyo na shauku na kwa kuwa tamaa na shauku vinahusiana katika kupotosha mtazamo wa nafsi ya mtu bila kujali sheria ya chanzo na matokeo, na kwa sababu inatokana na mtizamo potofu, imani itapatikana tu moyo utakapoondokana na tamaa hizi za kidunia.

Pili, watu wanaweza kuondokana na mtazamo potofu na matokeo yake ya tamaa za kidunia kwa kuutawala moyo kwa utararibu na uangalifu. Kwa kuutawala moyo kwa utaratibu na uangalifu wanaweza kuepukana na tamaa zitokanazo kwa kuchochewa na macho, masikio, pua, ulimi, ngozi na taratibu nyingine za akili kama hizo na kwa kufanya hivyo, watu wanaikata mizizi inayochipua tamaa zote za kidunia.

Tatu, yawapasa kuwa na mawazo sahihi kuhusu matumizi ya vitu vyote. Hii ina maana kuwa, kuhusu chakula na mavazi, wasivifikirie katika upande wa raha na starehe ila katika mahitaji ya mwili. Mavazi ni ya lazima katika kuukinga mwili kutokana na baridi, au joto kali au kuusitiri aibu zake; chakula ni muhimu na lazima kuulisha mwili wakati mwili huo unapokea Uongofu na U-Buddha. Tamaa za dunia haziwezi kujitokeza katika fikra za namna hiyo.

Nne, watu yawapasa kujifunza uvumilivu; lazima wajifunze kuvumilia adha ya joto na baridi; kiu na njaa; lazima wajifunze kuwa wastahimilivu wanapopokea bezo na matusi; kwa vile tendo la kukubali uvumilivu ndilo lizimalo moto wa tamaa za kidunia unaounguza miili yao.

Tano, ili watu waepuke hatari lazima wajifunze kuona. Kama mtu mwenye hekima anavyokaa mbali na farasi pori au mbwa kichaa, vivyo hivyo yampasa mtu asiwe na marafiki waovu au kwenda kwenye sehemu zinazokwepwa na watu wenye busara. Ikiwa mtu atajenga na kushika tabia ya tahadhari na busara, moto wa tamaa za kidunia unaowaka katika viungo vya mwili wake utazimika.

2. Kuna makundi matano ya tamaa duniani. Tamaa zinazotokana na sura na maumbo yaonekanayo machoni; zinazotokana na sauti zisikiwazo na masikio, zinazotokana na harufu nzuri inuswayo na pua; zinazotokana na maonjo ya ulimi; zinazotokana na vitu vinavyokubalika kwa njia ya mguso.

Kutokana na milango hii mitano ya tamaa tunapata upendo wa faraja ya mwili.

Watu wengi wanaposhawishiwa na upendo wa faraja ya mwili, hawagundui maovu yanayoambatana na faraja na hukamatwa katika mitego ya ibilisi kama mnyama akamatwavyo na mtego msituni. Kwa hakika, milango hii mitano ya tamaa ni mitego ya hatari hasa. Watu wakamatwapo katika mitego hii huangaika katika maumivu na mateso ya kidunia. Yawapasa kutambua namna ya kuepukana na mitego hiyo.

3. Hakuna njia ya kuepuka mateso ya kidunia. Fikiria ukimkamata nyoka, mamba, ndege, mbwa, mbweha na nyani, viumbe sita vyenye hali tofauti na uwafunge pamoja kwa kamba ngumu na uwaachie waondoke. Kila mmoja wao atajaribu kurudi katika makao yake kwa njia yake: nyoka atatafuta nyasi ndefu, mamba atatafuta maji, ndege atahitaji kuruka angani, mbwa atatafuta kijiji, mbweha atatafuta nyika na nyani atatafuta miti ya msituni. Katika jitihada ya kutaka kujinasua kila mmoja aende vyake kutakuwa na mapambano, lakini kwa kuwa wote wamefungwa katika kamba moja, mwenye nguvu zaidi ya wote atawavuta wote.

Kama viumbe katika mfano huu, binadamu hujaribiwa kwa njia nyingi kwa tamaa za milango yake ya fahamu sita, macho, masikio, pua, ulimi, mguso na moyo, na vyote vinatawaliwa na tamaa.

Ikiwa viumbe hao sita watafungwa kwenye mlingoti, watajitahidi kujinasua hadi hapo kila mmoja atakapochoka na kulala chini ya mlingoti. Vivi hivi, ikiwa watu watajifunza na kuutawala moyo hapatakuwepo na milango mingine mitano ya fahamu. Ikiwa moyo utatawaliwa watu watakuwa na furaha tangu sasa hata siku zijazo.

4. Watu hupenda faraja ya binafsi ambayo ni mapenzi ya umaarufu na sifa. Lakini sifa na umaarufu ni sawasawa na ubani uunguao kwa nguvu na hatimaye kuisha. Ikiwa watu watatafuta utukufu na heshima kutoka kwa watu na kuacha njia ya ukweli, wako katika hatari kubwa na hatima yake watakuwa na sababu ya kujuta.

Mtu ambaye hutafuta sifa na utajiri na mambo ya mapenzi ni sawa na mtoto ambaye hulamba asali kutoka kwenye makali ya kisu. Anapoonja utamu wa asali kuna hatari ya kuumiza ulimi wake. Mtoto huyo anafananishwa na mtu abebaye mwenge akiukabili upepo; bila shaka miale ya moto itamuunguza uso na mikono yake.

Mtu asiamini moyo wake uliojaa uchoyo hasira na ujinga. Mtu asiruhusu moyo wake ukimbie ovyo bali autawale kabisa.

5. Kuupata uwezo wa kuutawala moyo ni jambo gumu sana. Wale wautafutao Wongofu yawapasa kwanza waondokane na moto wa tamaa zote. Tamaa ni moto uwakao kwa kishindo hivyo mtu atafutaye Wongofu yampasa kukwepa moto wa tamaa kama

mtu aliyebeba mzigo wa nyasi kavu anavyokwepa cheche za moto.

Lakini itakuawa ujinga mtupu kwa mtu kufumba macho eti kwa sababu ya kuogopa kujaribiwa kutokana na sura nzuri atakazoziona. Moyo ndio kiongozi kwa hiyo kama unaweza kutawaliwa tamaa ndogo zitakwisha.

Ni vigumu kutafuta njia ya Wongofu, lakini ni vigumu zaidi ikiwa watu hawana moyo wa kuitafuta njia kama hiyo. Bila ya Wongofu kuna mateso yasiyokoma katika dunia ya kufa na kupona.

Mtu anapotafuta njia ya Wongofu inakuwa kama ng'ombe abebaye mzigo mzito huku akipita katika tope zito. Ikiwa maksai huyo atajitahidi kwa nguvu zake zote bila kushughulikia mambo mengine anaweza akayavuka matope salama na akapumzika. Kwa hiyo, moyo ukitawaliwa barabara na kuelekezwa katika njia sahihi, hapatakuwepo na tope la uchoyo la kuuzuia na mateso yake yote yatakwisha.

6. Wote wafuatao njia ya Wongofu yawapasa kuondokana na aina zote za majivuno ya ubinafsi na wawe tayari kwa unyenyekevu kupokea mwanga wa mafundisho ya Buddha. Hazina zote za dunia, dhahabu yake yote na fedha yake yote na heshima, haviwezi kulinganishwa na hekima na uadilifu.

Ili kufurahia afya bora, kupata furaha ya kweli kwa familia

ya mtu, kuleta amani kwa wote, ni lazima mtu awe na nidhamu na atawale moyo wake. Mtu akiweza kuutawala moyo wake anaweza kuipata njia ya wongofu, na hivyo hekima na wema wote vitakuja kwake.

Kama hazina inavyochimbuliwa kutoka ardhini vivyo hivyo wema hutokana na matendo mema, na hekima hutokana na moyo safi wenye amani. Ili kutembea kwa usalama katika mashaka ya maisha ya binadamu, mtu anahitaji mwanga wa hekima na mwongozo wa uadilifu.

Mafundisho ya Buddha, ambayo yanaeleza watu jinsi ya kuondokana na uchoyo, hasira na ujinga ni mafundisho mema na watu wote wanaoyafuata hupata maisha mazuri na ya furaha.

7. Binadamu wanatabia ya kufuata uelekeo wa mawazo yao. Wanapokuwa na fikra za uchoyo nao huwa wachoyo; Wakiwa wana fikara za hasira, wanakuwa na hasira zaidi; Wakishiriki fikra za kijinga, wataelekea katika ujinga.

Wakati wa mavuno wakulima hufungia mifugo yao isije ikavunja ugo na kuingia katika mashamba ya watu ikasababisha malalamiko mengi au kuuawa; hivyo basi watu yawapasa kuchunga mioyo yao kutokana na udanganyifu na taabu. Lazima waondokane na fikra zinazochochea uchoyo, hasira na ujinga, Ila washawishi fikra zinazochochea huruma na fadhila.

Wakati wa mvua za vuli malisho hujaa nyasi na wafugaji

wakati huo hufungulia mifugo yao lakini hata hivyo mifugo hawaachwi bila mchungaji. Ndivyo ilivyo hata kwa mioyo ya watu: Hata wakati wa hali nzuri moyo lazima ulindwe.

8. Wakati fulani Shakyamuni Buddha aliishi katika mji wa Kausambi. Katika mji huo alikuwepo Bwana mmoja aliyemchukia Buddha hadi akachukua hatua za kuwahonga watu wabaya waeleze hadithi za owongo juu yake. Katika hali kama hiyo ilikuwa vigumu sana kwa wanafunzi wake kupewa chakula cha kutosha kila waombapo pia matusi mengi katika mji huo yaliwaandama.

Ananda alimwambia Shakyamuni; "Ni heri tuondoke katika mji huo. Kuna miji mingine bora tunakoweza kwenda. Afadhali tuondoke hapa."

Aliyebarikiwa alijibu: "Je ikiwa mji mwingine utakuwa kama huu tutafanyaje?"

"Basi tutakwenda katika mji mwingine"

Aliyebarikiwa alisema: Hapana, Ananda, katika hali hiyo hatutatulia. Afadhali tuendelee kukaa hapa tukayavumilie matusi hadi yatakapoisha ndipo twende katika mji mwingine.

Kuna faida na hasara, visingizio na heshima, sifa na matusi, mateso na furaha katika dunia hii. Mwongofu hatawaliwi na

mambo haya ya nje; yatatoweka kwa haraka sana kama yanavyokuja.

II
NJIA BORA YA KUTENDA MEMA

1. Wale waitafutayo njia ya Wongofu ni lazima wakumbuke umuhimu wa kuiweka safi miili yao, maneno na mioyo yao. Kuiweka miili yao nadhifu yampasa mtu asiue kiumbe chochote, asiibe, au kuwa mzinzi. Ili kuwa na lugha safi mtu yampasa asidanganye au kutukana au kuongopa au kujihusisha katika mazungumzo yasiyo na maana. Ili kuwa na moyo safi yampasa mtu aondokane na aina zota za uchoyo, hasira na maamuzi potofu.

Ikiwa moyo utakuwa mchafu, hakika hata matendo ya mtu yatakuwa machafu; ikiwa matendo yatakuwa machafu kutakuwepo na mateso. Kwa hiyo ni jambo la muhimu sana mwili, mdomo na moyo vikawekwa safi.

2. Zama zile kulikuwa na mjane aliyekuwa tajiri mwenye sifa ya huruma, adabu na ukarimu. Alikuwa na mfanyakazi mwenye hekima na juhudi.

Siku moja mfanyakazi wake alifikiri : "Mkuu wangu ana sifa nzuri sana; sijui kama ni nzuri kwa asili yake au ni nzuri kwa sababu ya mazingira yake. Nitamjaribu ili nijue ukweli."

Asubuhi iliyofuata mfanyakazi huyo hakuonekana machoni pa mkuu wake hadi adhuhuri. Mkuu wake alipatwa na ghadhabu akamsuta vikali bila huruma. Mfanyakazi alijibu:
"Ikiwa mimi ni mvivu siku moja au siku mbili, hupaswi kukosa subira". Hapo mkuu wake alipandwa na hasira.

Siku iliyofuata mfanyakazi huyo alichelewa tena kuamka mapema. Kitendo hicho kilimfanya mjane akasirike sana hata akaamua kumchapa kwa fimbo. Habari za tukio hilo zilienea kila sehemu, na majane huyo tajiri akawa amepoteza sifa yake njema.

3. Watu wengi wako kama mama huyo. Mazingira yao yanapojitosheleza wanakuwa na huruma, adabu njema na wakimya, lakini haielezeki ikiwa wanaweza kuendelea na tabia hiyo wakati hali ya mambo inapobadilika na ikawa hairidhishi.

Ni pale tu mtu anapoendelea kudumisha moyo safi na wenye amani na kutenda wema wakati maneno mabaya yanapoingia masikioni mwake, watu wengine wanapomchukia au anapokosa chakula cha kutosha, mavazi na nyumba , hapo huenda tukamwita mwema.

Kwa hiyo basi, wale watendao matendo mema na kudumisha moyo wa amani tu wakati mazingira yao yanajitosheleza hao hakika siyo watu wema. Ni wale tu waliyoyapokea mafundisho ya Buddha na wakayafunza kwa mioyo na miili yao mafundisho hayo hao wanaweza kuitwa watu wema na wenye adabu njema na amani.

4. Kuhusu ubora wa maneno ya kutumia, kuna jozi tano za kinyume: Maneno ambayo ni bora katika nafasi zake na yale yasiyo bora kwa nafasi hizo; maneno ambayo yanafaa kwenye ukweli na yale yasiyofaa; maneno yenye utamu na yale ya kejeli; maneno yenye faida na yale yenye hasara; na maneno yenye huruma na yale yenye chuki.

Maneno yoyote yale tunayozungumza ni bora tuyachague kwa makini kwa sababu watu watayasikia na huenda yakawashawishi kwa wema au ubaya. Ikiwa mioyo yetu itajaa huruma na utu wema, itahimili maneno maovu tuyasikiayo. Tusikubali kamwe maneno machafu kutoka midomoni mwetu yasije yakaamsha hisia ya chuki na hasira. Maneno tunayoyazungumza daima yawe ni ya upole na hekima daima.

Fikiria mtu anayekusudia kuzoa takataka kutoka kwenye uwanja. Akatumia beleshi na ungo na akafanya kazi kwa bidii akitawanya takataka huko na huko, lakini ni kazi ngumu. Kama mjinga huyo hatuwezi kutumainia kutupilia mbali maneno yote. Lazima tuizoeze akili yetu na tujaze mioyo yetu kwa upole na wema ili tusisumbuliwe na maneno yasemwayo na watu wengine.

Mtu anaweza akajaribu kuchora picha kwa maji ya rangi kwenye anga ya bluu, lakini hii haiwezekani. Vilevile haiwezekani kukausha mto mkubwa kwa joto la tochi iliyotengenezwa kwa nyasi kavu za kulishia ng'ombe, au kutoa sauti isababishayo mipasuko kwa kusugua vipande viwili vya

ngozi laini. Watu lazima wazoeze akili zao kama mifano hiyo miwili ili wasivurugwe na maneno yoyote wanayoweza kuyasikia.

Yawapasa kufunza akili na mioyo yao na kuipanua kwa mapana ya dunia, isiwe na mipaka kama mbingu, yenye kina kirefu kama mto mkubwa, na laini kama ngozi iliyotiwa dawa ya kuilainisha.

Hata kama adui yako akikukamata na kukutesa, ukipandwa na hasira hutakuwa unafuata mafundisho ya Buddha. Katika hali yoyote ile huna budi kujifunza kufikiri: "Moyo wangu hauteteleki. Maneno ya chuki na hasira hayawezi kutoka mdomoni mwangu. Nitamzungushia adui yangu mawazo yenye wema, upole,yanayotokana na moyo uliojaa huruma katika hali zote za maisha."

5. Kuna hadithi inayozungumzia juu ya bwana mmoja aliyepata kukiona kichuguu kilichokuwa kinaungua mchana, na usiku kinafuka moshi. Alikwenda kwa mtu mwenye busara na akamwomba ampe ushauri kuhusu jambo ambalo anaweza kutenda. Yule mtu mwenye busara akamwambia kuchimba katika kichuguu kwa kutumia sime. Yule bwana alifanya hivyo. Naye alipata kwa mpangilio vitu vifuatavyo:- Ufito wa chuma, mapovu ya maji, pande la chuma, sanduku, kobe, kisu kikali, kipande cha nyama na mwisho likatoka joka. Bwana huyo alikwenda kutoa taarifa kuhusu aliyoyaona. Mwenye busara alifafanua umuhimu wa mambo hayo na akasema, "tupilia mbali

kila kitu isipokuwa joka; liache hilo joka na wala usilisumbue."

Hii ni ngano ambayo kwayo "kichuguu" ina maana ya mwili wa binadamu. "Kilichokuwa kinaungua "mchana kutwa" ina maana kwamba wakati wa mchana watu hutenda matendo waliyoyafikiria usiku uliotangulia. "Kinafuka moshi usiku" inaelezea ukweli kwamba watu wakati wa usiku hukumbuka kwa furaha au hujuta kutokana na mambo waliyoyafanya wakati wa mchana.

Katika ngano hiyo hiyo, "Bwana " ina maana mtu atafutaye Wongofu. "Mtu mwenye busara" maana yake ni Buddha. "Sime" ina maana ya hekima. "Chimba katika kichuguu" inaeleza juu ya juhudi zinazohitajika ili kuupata Uongofu.

Tena katika ngano hiyo hiyo, "ufito wa chuma wa lango" ina maana ya ujinga; "Mapovu" ni vishindo vya sauti za mateso na hasira; "pande la chuma" inaashiria kusita na kutokuwa tayari, "Sanduku" ina maana uwekaji wa hasira, uchoyo, uvivu, ugeugeu, majuto na madanganyo; "kobe" ina maana ya mwili na roho; kisu kikali ina maana ya mchanganyiko wa tamaa tano za fahamu, na "kipande cha nyama" ina maana ya matokeo ya tamaa imfanyayo mtu kutamani baada ya kutosheka. Vitu vyote hivyo ni hatari kwa binadamu, kwa hiyo Buddha alisema, "Tupilia mbali kila kitu.

Zaidi ya hapo, "joka" inaashiria moyo ambao umetupilia mbali mateso ya duniani ikiwa mtu atachimba katika mambo yake

kwa singe ya hekima hatimaye atalifikia joka lake. "Liache joka hilo na wala usilisumbue" ina maana ya kufuatilia na kuuchimba moyo ambao uko huru na tamaa za kidunia.

6. Pindola, mwanafunzi wa Buddha baada ya kupata Wongofu alirudi kwao Kausambi kutoa shukrani kwa watu wa huko kutokana na wema waliomtendea. Katika kufanya hivyo alikuwa ameandaa shamba kwa ajili ya kupanda mbegu za ki-Buddha.

Katika viungo vya Kausambi kuna mbuga ndogo kandokando ya mto Ganges iliyofunikwa na sufu ndefu za minazi ikipulizwa na upepo mwanana.

Siku moja, wakati wa kiangazi, Pindola alikaa ili atafakari chini ya kivuli cha mti wakati mfalme Udayana alipofika katika mbuga hiyo akiwa ameambatana na wenzi wake ili wakastarehe huko, na baada ya starehe na muziki mfalme alijipumzisha chini ya kivuli cha mti mwingine.

Wakati Mfalme wao akiwa amelala usingizi, wake zake na mabibi waliomsubiri walitembeatembea na ghafla wakamkuta Pindola amekaa katika kutafakari. Walimtambua kama mtu mtakatifu, wakamuomba awafundishe nao wakasikiliza maubiri yake.

Mfalme alipozinduka usingizini aliondoka kuwatafuta bibi zake na akawakuta wamemzunguka huyo mwanamme na huku

wakisikiliza mafundisho yake. Akiwa na moyo wa wivu na tamaa ya wanawake, Mfalme alijawa hasira na akamtukana Pindola akisema; "Ni jambo lisilosameheka kwako, mtu mtakatifu kuwa katikati ya wanawake huku ukifurahia mazungumzo ya kipuuzi pamoja nao." Pindola alifumba macho yake kwa haraka na akakaa kimya.

Akiwa amejaa hasira, Mfalme alichomoa sime na kumtisha Pindola, lakini mtu huyo wa Mungu alikaa kimya na imara kama mwamba. Hii ilimfanya Mfalme akasirike zaidi kwa hiyo akapasua kichuguu na kumtupia takataka zote zilizotoka humo lakini bado Pindola aliendelea kukaa kimya akaendelea kukaa katika kutafakari, akivumilia matusi na maumivu.

Baadaye, Mfalme alishikwa na aibu kutokana na tabia yake ya kikatili hivyo akamwomba Pindola msamaha. Kutokana na tukio hili mafundisho ya Buddha yalipata njia ya kuingia katika ngome ya Mfalme na kutoka humo yalisambaa katika nchi nzima.

7. Siku chache baadaye Mfalme Udayana alimtembelea Pindola katika sehemu yake ya maombi msituni alipoishi na akamuuliza, "Mwalimu mwenye kuheshimika, inawezekanaje wanafunzi wa Buddha kutunza miili yao safi na mioyo yao safi bila ya majaribu ya uzinifu ingawa wengi wao bado vijana?"

Pindola alijibu: "Bwana Mheshimiwa, Buddha ametufundisha kuheshimu wanawake wa makamo kama mama zetu, kuwaheshimu wake wa rika letu kama dada zetu na wale

wadogo tuwaheshimu kama binti zetu. Kutokana na mafundisho haya wanafunzi wa Buddha wanauwezo wa kutunza miili yao safi na bila majaribu ya uzinifu ingawa ni vijana."

"Lakini mwalimu mheshimiwa mtu anaweza kuwa na mawazo machafu juu ya mwanamke mwenye umri wa mama yake au dada yake au binti yake. Je wanafunzi wa Buddha wanatawalaje tamaa zao?"

"Bwana mheshimiwa, Aliyebalikiwa alitufundisha kuiona miili yetu kama itoayo uchafu wa aina zote kama vile damu, usaa, jasho na mafuta; kwa kuwazia hivyo, sisi, ingawa tu vijana, tunaweza kutunza mioyo yetu kwa usafi."

"Mwalimu mheshimika," Mfalme aliendelea kusisitiza. "Hii inawezekana kwa kuwa umezoeza mwili na moyo wako na kusafisha hekima yako , bali itakuwa vigumu kwa wale ambao bado hawajapata mafundisho ya namna hiyo. Wanaweza kujaribu kukumbuka uchafu lakini macho yao yatafuatilia sura nzuri. Wanaweza kujaribu kuona ubaya wa sura, lakini watavutiwa kwa hali ile ile na sura nzuri sana. Lazima kuna sababu nyingine inayowafanya vijana kati ya wanafunzi wa Buddha kuwa na matendo safi."

"Bwana mheshimiwa," alijibu Pindola, "Aliyebarikiwa hutufundisha kuchunga milango mitano ya fahamu. Tunapoangalia maumbo mazuri na rangi kwa macho yetu, tunaposikia sauti nzuri kwa masikio yetu, tunaponusa harufu

nzuri kwa pua yetu, au tunapoonja vitu vitamu kwa ulimi wetu au kugusa vitu vyelolo kwa mikono yetu hatupaswi kutawaliwa na vitu hivi vinavyotamanisha wala hatuwezi kukomeshwa na vitu visivyo vutia. Tunafundishwa kulinda milango mitano ya fahamu kwa makini. Ni kutokana na mafundisho ya Aliyebarikiwa, ambayo kwayo hata wanafunzi vijana wanaweza kutunza miili na mioyo yao kwa usafi."

"Mafundisho ya Buddha ni ya ajabu kweli kweli. Kutokana na uzoefu wangu binafsi nafahamu kuwa nikumbanapo na kitu chochote kizuri, bila kujilinda nasumbuliwa na vishawishi vya milango ya fahamu. Ni jambo la msingi kulinda milango mitano ya fahamu wakati wowote ili kuwa na matendo safi."

8. Mtu anapokueleza mawazo ya moyo wake katika matendo hali ya malipizo hufuata. Mtu akikutupia matusi, kuna majaribu ya kujibu au kulipiza kisasi. Ni lazima mtu ajilinde kutokana na hali ya kawaida ya kutaka kulipiza mambo. Ni sawasawa na kutema mate katika upepo, hayampati mtu yeyote isipokuwa yule aliyeyatema, ni sawasawa na kufagia vumbi katika upepo, kujichafua mwenyewe. Misiba hufuata hatua za mtu anayetoa nafasi au njia ya tamaa ya kulipiza kisasi.

9. Ni tendo zuri sana kuachana na uchoyo na kuhifadhi upendano. Bado ni bora kulinda nia ya moyo juu ya kuheshimu Njia Bora.

Yampasa mtu kuondokana na moyo wa ubinafsi na kuwa

na moyo wenye unyenyekevu wa kuwasaidia wengine. Tendo la kumfanya mtu mmoja awe na furaha humtia moyo mtu mwingine kumpa furaha mwenzake, hivyo furaha huwepo kutokana na tendo la namna hiyo.

Maelfu ya mishumaa inaweza kuwashwa kutokana na mshumaa mmoja, na maisha ya mshumaa yatakuwa mafupi. Furaha haipungui kutokana na tendo la kuigawana.

Watu wanaoutafuta Uongofu lazima wawe makini kwa kila hatua wanayoichukuwa. Hata kama matakwa ya mtu yatakuwa makubwa sana lazima yapatikane hatua kwa hatua. Hatua za njia ya Wongofu lazima zichukuliwe katika hatua yetu ya kila siku.

10. Mwanzoni mwa njia ya Wongofu kuna mambo magumu katika dunia hii ambayo lazima tuyashinde, nayo ni:- 1. Ni vigumu kwa mtu maskini kuwa mkarimu. 2. Ni vigumu kwa mtu mwenye majivuno kujifunza Njia ya Uongofu. 3. Ni vigumu kuutafuta Uongofu kwa gharama ya kujitoa kafara. 4. Ni vigumu kuzaliwa wakati Buddha yuko duniani. 5. Ni vigumu kusikia mafundisho ya Buddha. 6. Ni vigumu kuwa na moyo safi kushindana na silika za mwili. 7. Ni vigumu kutotamani vitu vizuri na vinavyovutia. 8. Ni vigumu kwa mtu mwenye nguvu kushindwa kutumia nguvu zake kutosheleza tamaa zake. 9. Ni vigumu mtu kutopandwa na hasira wakati ameudhiwa. 10. Ni vigumu kukaa bila hatia mtu anapojaribiwa na mambo ya ghafla. 11. Ni vigumu mtu binafsi kuomba kujifunza kwa mapana na makini. 12. Ni vigumu kutomdharau mtu anayeanza. 13. Ni

vigumu mtu kuwa mnyenyekevu. 14. Ni vigumu kupata marafiki wema. 15. Ni vigumu kuvumilia nidhamu inayoelekeza kwenye Uongofu. 16. Ni vigumu kutokusumbuliwa na mambo ya nje. 17 Ni vigumu kuwafundisha wengine kwa kufahamu uwezo wao. 18. Ni vigumu kuwa na moyo wa amani. 19. Ni vigumu kutokubishana juu ya wema na ubaya. 20. Ni vigumu kubuni na kujifunza njia mpya.

11. Watu wema na wabaya hutofautiana katika hali zao. Watu wabaya hawayatambui matendo mabaya kama ni ya dhambi; ubaya wa matendo hayo unapoelezwa kwao, hawayaachi kuyatenda na hawataki mtu aendelee kuwaonya juu ya matendo yao mabaya. Watu wema huguswa sana na mema na mabaya; huacha kutenda jambo lolote lile walionalo kuwa ni baya; humshukuru mtu yeyote yule anayewaonya juu ya matendo mabaya hayo.

Kwa hiyo watu wema na wabaya hutofautiana vibaya sana. Watu wabaya hawatambui wema wanaotendewa, lakini watu wenye busara hutambua na kushukuru. Watu wema hujaribu kuwaeleza utambuzi wao, furaha na shukrani kwa kulipa wema, sio kwa wafadhili bali kwa mtu yeyote.

III
MAFUNDISHO KATIKA HADITHI ZA KALE

1. Hapo kale kulikuwa na nchi iliyokuwa na desturi ya pekee ya kuwatupa wazee porini na milimani kusikofikika.

Waziri mmoja wa Serikali aliona vigumu kufuata desturi hii kuhusu baba yake. Hivyo kwa siri alijenga pango chini ya ardhi akamtunza baba yake humo.

Siku moja muungu alimtokea Mfalme wa nchi hiyo na akampa fumbo la kutatanisha akisema kuwa akishindwa kufumbua fumbo hilo kwa ukamilifu, nchi yake itaaribiwa: Fumbo lilikuwa : "Kuna nyoka wawili hapa; nitajie jinsia ya kila mmoja."

Hakuna mtu hata mmoja aliyeweza kufumbua fumbo hilo; hivyo Mfalme alitoa zawadi kubwa kwa mtu yoyote katika miliki yake atakayefumbua fumbo hilo.

Yule waziri alikwenda kwenye maficho ya baba yake na kumuuliza jibu la fumbo hilo. Mzee alisema:- "Ni jibu rahisi sana. Waweke nyoka wawili kwenye zuria laini; yule atakayejongea ndiye dume, na yule atakayetulia ni jike." Waziri alimpelekea Mfalme jibu hilo na fumbo likawa limefumbuliwa.

Pia muungu aliuliza maswali mengine magumu

yaliyomshinda Mfalme pamoja na wafuasi wake, lakini baada ya waziri kushaurina na baba yake mzee aliweza kuyajibu.

Yafuatayo ni baadhi ya maswali na majibu yake "Ni nani huyo, anapokuwa amelala usingizi, huitwa aliye macho, na, anapokuwa macho, huitwa aliyelala?" jibu lake ni:- Ni yule anayepata mafundisho ya Uongofu. Yu macho anapolinganishwa na wale waliokwisha kupokea Uongofu.

"Unawezaje kupima uzito wa tembo mkubwa?"

"Mweke tembo katika mashua na weka alama kwenye mashua kuonyesha mzamo wake kisha ujaze mawe katika mashua hadi izamapo kufikia alama uliyoichora. Pima uzito wa mawe."

Nini maana ya methali, "kikombe cha maji ni bora kuliko maji ya bahari?" Hili ndilo jibu lake . "Kikombe cha maji kilichotolewa kwa roho njema na ya huruma kwa wazazi wa mtu au mgonjwa kina sifa ya milele, lakini maji ya bahari kuna siku moja yatakauka."

Tena muungu alitengeneza mtu anayekufa njaa, amebakia mifupa na ngozi tu, akilalamika, "Kuna mtu yeyote duniani mwenye njaa, kuliko mimi?" "Mtu mwenye ubinafsi na uchoyo kiasi kwamba haamini katika hazina Tatu za Buddha, Dharma, na Samgha, na ambaye hatambikii wazazi na walimu wake, sio kwamba ana njaa sana bali ataanguka katika dunia ya mapepo ya njaa na huko atapata mateso ya njaa milele."

"Hapa kuna ubao wa mti wa Chandana, ni sehemu gani ya ubao huo ambayo inaelekea kwenye kitako cha shina la mti?" "Weka ubao ndani ya maji; Sehemu ya ubao itakayo zama zaidi ndani ya maji itakuwa sehemu ya mwisho iliyokuwa karibu na shina la mti."

"Hapa kuna farasi wawili wanaolingana na kufanana. Utawezaje kutambua ni yupi mtoto na yupi ni mama?." "Wape majani kidogo, mama atasukuma majani hayo kwa mtoto."

Kila jibu la maswali haya magumu liliwafurahisha muungu na Mfalme pia. Mfalme alishukuru sana alipogundua kuwa majibu haya mazuri yalitoka kwa mzee baba yake waziri aliyekuwa amemficha pangoni na akafuta sheria ya kuwatupa wazee milimani na akaamuru watunzwe kwa upole na ukarimu.

2. Siku moja Malkia wa Videha wa India alimuota tembo mweupe mwenye meno sita. Alitamani pembe hizo na akamuomba mfalme amtafutie pembe hizo ingawa kazi ya kupata pembe hizo ilikuwa ngumu, Mfalme aliyempenda sana Malkia alitoa taarifa ya kumuona tembo wa namna hiyo.

Ilitokea kwamba kulikuwa na tembo wa namna hiyo katika Milima ya Himalaya aliyekuwa anajifunza u-Buddha. Wakati fulani tembo huyu aliokoa maisha ya mwindaji katika hali ya hatari katikati ya milima. Mwindaji huyo alipata bahati ya kurudi katika nchi yake salama salimini. Hata hivyo, akiwa amepofushwa

na ukubwa wa zawadi na usahaulifu wa wema aliotendewa na tembo huyo, mwindaji alirudi milimani ili amuue.

Mwindaji, akiwa anajua kwamba tembo alikuwa anatafuta u-Buddha, alijifunika katika vazi la utawa wa ki-Buddha, akamkaribia tembo bila matata, akamchoma kwa mshale wa sumu.

Tembo akitambua kwamba mwisho wake umekaribia na kwamba mwindaji alikuwa ametekwa na tamaa ya kidunia kwa ajili ya zawadi, alipatwa huruma juu yake, akamfunika katikati ya ghadhabu kali ya tembo wengine waliotaka kulipiza kisasi. Hapo tembo alimuuliza mwindaji kwanini alikuwa amemtendea tendo la kijinga kama hilo. Mwindaji alimwambia juu ya zawadi na akatubu kwamba alitamani meno sita. Mara moja tembo aliyakata meno yake kwa kuyagonga kwenye mti na kumkabidhi mwindaji akisema:- "Kwa sadaka hii nakamilisha mafundisho yangu ya u-Buddha na nitazaliwa tena katika nchi takatifu. Nitakapokuwa Buddha nitakusaidia kuondoa mishale mitatu ya sumu ya uchoyo, hasira na ujinga."

3. Katika msitu chini ya Milima Himalaya palikuwepo na kasuku aliyeishi pamoja na wanyama na ndege wengine wengi. Siku moja moto ulizuka katika msitu huo kutokana na msuguano wa mianzi kukiwa na upepo mkali na hivyo wanyama na ndege waliingiwa na hali ya hofu. Kasuku akiwa na huruma kwa hofu na mateso yao, na akiwa anataka kulipa wema aliokuwa akipata katika msitu wa mianzi uliokuwa ukimpatia hifadhi, alifanya kila

lililowezekana ili awaokoe. Akajizamisha katika bwawa lililokuwa karibu na akaruka juu huku akijitikisa na kudondosha matone ya maji juu ya moto akiwania kuuzima. Aliendelea kufanya hivyo kwa bidii, na kwa moyo wa huruma, na kutoa shukrani kwenye msitu.

Roho ya wema na ya kujitoa mhanga ilitambuliwa na muungu huko mbinguni aliyetelemka kutoka angani na kumwambia kasuku:-"Una moyo hodari, lakini unatarajia mafanikio yapi kutokana na matone machache uyadondoshayo juu ya moto mkubwa?" Kasuku alijibu:- "Hakuna jambo lisilowezekana kutokana na moyo wa shukrani na kujitoa mhanga. Nitajaribu tena na tena, zaidi na zaidi katika maisha yajayo." Muungu mkuu alifurahishwa na roho ya kasuku na kwa pamoja wakauzima moto.

4. Wakati fulani ndege mwenye vichwa viwili kwenye mwili mmoja aliishi katika milima ya Himalaya. Siku moja kichwa kimoja kilikiona chenzake kikila matunda matamu na kikaona wivu na kujisemea:- "Basi mimi nitakula tunda lenye sumu." Kwa hiyo kikala sumu na ndege mzima akafa.

5. Wakati mwingine pia kichwa na mkia wa nyoka viligombania kutangulia. Mkia alimwambia kichwa:- "Kila siku unatangulia; Sio usawa niachie nami nitangulie nyakati fulani." Kichwa alijibu:- "Ni sheria ya maumbile mimi kuwa kichwa; hatuwezi kubadilishana."

Katika maumbile ya dunia kuna utaratibu sahihi na kila kitu kina kazi yake maalum. Kanuni hii inapovurugwa, utendaji kazi unaingiliwa, na utaratibu mzima unaharibika.

6. Kulikuwa na mwanamme aliyekuwa anaghadhabika kwa urahisi. Siku moja watu wawili walikuwa wanazungumza mbele ya nyumba juu ya bwana aliyeishi humo. Mmoja alimwambia mwenzake:- "Ni mtu mwema lakini hana simile; ana gadhabu kali na hukasirika mara moja." Huyo bwana aliyasikia yale maneno, bila kukusudia, alichomoka ndani ya nyumba na kuwashambulia wale watu wawili kwa kuwachapa, kuwapiga mateke na kuwajeruhi.

Mtu mwenye busara anaposhauriwa juu ya makosa yake, atajirudi na kubadilisha mwenendo wake. Mtu mjinga anaposhauriwa juu ya tabia yake mbaya hatadharau tu ushauri bali atarudia kosa lilelile.

7. Hapo kale palikuwa na tajiri mmoja mjinga. Alipoiona nyumba nzuri ya bwana mmoja yenye ghorofa tatu akaona wivu na akakata shauri kujenga nyumba kama hiyo akifikiri kuwa mwenye nyumba naye ni tajiri. Alimwagiza fundi aijenge. Bwana fundi alikubaliana naye na mara moja akaanza kujenga msingi, ghorofa ya kwanza, ghorofa ya pili, na mwisho ghorofa ya tatu. Tajiri huyu aliangalia kazi yake kwa machukizo na kusema:- "Sihitaji msingi, ghorofa ya kwanza, au ghorofa ya pili; nataka ghorofa nzuri ya tatu. "Ijenge haraka"!

8. Siku moja mpumbavu alikuwa akichemsha asali. Ghafla alitokea rafiki yake na kwa kuwa huyo mpumbavu alitaka ampe asali, lakini kwa vile ilikuwa bado ikichemka aliamua kuipembea ili ipoe bila kuitoa motoni. Vivyo hivyo ni vigumu kupata asali ya hekima iliyotulia bila kuitoa kutoka katika moto wa mateso ya dunia.

9. Siku moja kulikuwa na mapepo wabaya wawili walioshinda kutwa wakibishana na kuzozana juu ya sanduku, henzerani na jozi ya viatu. Mpita njia mmoja aliuliza, "kwa nini mnabishana kuhusu mambo haya? Vitu hivyo vina nguvu gani za miujiza zinazowafanya muendelee kubishana na kuzozana kuhusu umilikaji wake." Mapepo yalimweleza kuwa kutoka katika sanduku yangeweza kupata chochote walichokihitaji-Chakula, mavazi au hazina, kwa kutumia henzerani yangeweza kuwashinda adui zao wote; na kwa kutumia jozi ya viatu wangeweza kusafiri kupitia angani.

Baada ya kuyasikia haya, yule mpita njia alisema:-"Kwa nini kuzozana? Kama mnaweza kutoweka hapa kwa dakika chache, naweza kufikiria mgawano ulio bora kwa vitu hivyo kati yenu." Kwa hiyo mapepo mawili yaliondoka na mara tu baada ya kuondoka mpita njia alivaa vile viatu, akachukua sanduku na henzerani na akatawanyika kupitia hewani.

"Mapepo" yanawakilisha watu wasiokuwa na dini. "Sanduku" ina maana ya zawadi zitolewazo kwa hisani; hawaelewi ni kiasi gani cha hazina kinachoweza kupatikana

kutokana na uhisani "Henzerani" ina maana ya mazoea ya kutuliza fikara kwa makini. Watu hawaelewi kuwa maisha ya roho ya kutuliza fikara kwa moyo wanaweza kushinda tamaa za kidunia. "jozi ya vitu ina maana nidhamu safi ya mawazo na matendo itakayo wavusha katika ng'ambo ya tamaa zote na mabishano. Bila ya kutambua hayo hubishana na kuzozana juu ya sanduku, henzirani na jozi ya viatu.

10. Zamani za kale bwana mmoja alikuwa anasafiri peke yake. Ilipokaribia jioni alifikia kwenye nyumba isiyokuwa na mtu akaamua kulala humo. Yapata usiku wa manane jini lilileta maiti ndani ya nyumba hiyo na kuiacha kwenye sakafu. Kitambo kidogo jini jingine lilitokea kudai kwamba maiti ilikuwa yake likaanzisha mzozo.

Kisha jini la kwanza lilisema kuwa ni kazi bure kuendelea kubishana na likashauri kesi hiyo ipelekwe kwa hakimu atakayeamua ni nani mwenye haki. Jini jingine lilikubaliana na wazo hilo ila kwa kumuona mtu aliyejibanza pembeni kwa woga yakamkamata atoe uamuzi. Mwanamme huyo alipatwa na hofu kwa kujua kuwa uamuzi atakao toa utalikasirisha jini mojawapo na hilo litakalokasirika huenda likaamua kulipiza kisasi. Hata hivyo aliamua kueleza ukweli alioushuhudia.

Kama alivyotarajia, uamuzi wake ulimuudhi jini wa pili na hivyo jini lilimshika mkono wake mmoja kwa nguvu likaurarua lakini jini la kwanza liliurudishia kwa kutumia mkono mwingine wa maiti aliyekuwa sakafuni. Jini la pili kwa hasira liliurarua

mkono wake wa pili lakini jini la kwanza likarudishia mkono mwingine wa maiti mara moja. Mambo yaliendelea vivyo hivyo hadi mikono yote, miguu yote, kichwa na kiwiliwili vikawa vimeraruliwa na kuwekewa sehemu kama zile za mwili wa maiti. Majini yalipoona vipande vya mwili wa yule bwana vimesambaa sakafuni yaliviokota yakavila vyote na kuondoka kwa kicheko cha kichini chini.

Maskini aliyekuwa amejificha katika nyumba alikaraishwa na mikasa iliyomsibu. Sehemu za mwili wake zilizoliwa na majini alizirithi kwa wazazi wake na sehemu alizokuwa nazo zilikuwa za maiti. Hivi yeye alikuwa nani? Kwa kutotambua yeye ni nani na kwa kuchanganyikiwa alitoka ndani ya nyumba hiyo na kutembeatembea nje. Alipoliona hekalu, aliingia ndani na akawaelezea watawa matatizo yake. Watu waliuona ukweli na maana ya kutokuwa na ubinafsi kutokana na masimlizi yake.

11. Siku moja mrembo mmoja aliyevalia maridadi alitembelea nyumba moja. Mwenye nyumba alimuuliza yeye ni nani naye akajibu kuwa yeye ni muungu wa utajiri. Mwenye nyumba alifurahi na akampatia mapokezi mazuri.

Kitambo kidogo, alitokea mwanamke mwenye sura mbaya na mavazi machakavu. Mwenye nyumba alimuuliza yeye ni nani naye akamueleza kuwa alikuwa muungu wa umaskini. Mwenye nyumba aliogopa sana na akajaribu kumfukuza lakini mwanamke huyo likataa kuondoka akidai, "muungu wa utajiri ni dada yangu.

Tuna mapatano ya kuishi pamoja; unaponifukuza ni lazima afuatane nami." Ni kweli kabisa yule mwanamke mwenye sura mbaya alipotoka nje na mrembo akatoweka.

Kuzaliwa huambatana na kufa. Bahati hufuatana na balaa. Mambo mabaya huambatana na mambo mazuri. Watu yawapasa watambue mambo haya. Wajinga huogopa mikasa na hukazana kupata bahati njema, lakini wao wautafutao Wongofu yawapasa kuepukana na yote na kuwa katika dunia ya mapendo.

12. Zama zile alikuwepo fundi fukara aliyeacha mji wake na mke wake kwenda kutafuta bahati. Baada ya miaka 3 ya kazi ngumu alijipatia vipande mia tatu vya dhahabu na akaamua kurudi nyumbani kwake. Akiwa njiani aliwakuta watu kwenye sikukuu ya kutoa sadaka katika hekalu kubwa. Hii ilimfurahisha sana na akajishauri, "Hadi leo, nimeyawazia mambo ya sasa, sijawazia juu ya furaha ya baadaye hata siku moja. Ni sehemu ya furaha yangu kuwa nimefika mahali hapa; yanipasa nitumie bahati hii kupanda mbegu za matumaini." Akitawaliwa na fikra hizo kwa furaha alitoa akiba yake yote hekaluni na kurudi nyumbani kwake bila senti yoyote.

Alipofika nyumbani kwake mke wake alimsuta kwa kutomletea msaada wowote wa fedha. Fundi fukara alimjibu kuwa alikuwa amepata fedha lakini ameiweka mahali penye usalama. Alipobanwa zaidi aeleze alipoficha hiyo fedha alikiri kuwa alikuwa amewapatia watawa katika hekalu fulani.

Jambo hili lilimkasirisha mke akambeza mume wake na hatima yake akapeleka shauri lake kwa hakimu. Hakimu alipotamka bwana fundi ajitetee, alisema kuwa hakufanya jambo la kijinga kwa kuwa alikuwa amejipatia fedha zake kutokana na mapambano magumu na alihitaji kuitumia kama mbegu ya bahati njema ijayo. Alipofika hekaluni ilielekea kwake kuwa ndicho kiwanja ambapo angepanda dhahabu yake kama mbegu yake ya bahati nasibu. Akaendelea kusema: "Nilipowapatia watawa dhahabu yangu ilikuwa kana kwamba nilitupilia mbali uchoyo na ubahili wote kutoka moyoni mwangu, na nimetambua kuwa utajiri halisi siyo dhahabu bali moyo."

Hakimu alisifu sana roho ya fundi huyo na wale wote waliosikia waliunga mkono kwa kujitolea kwa njia mbalimbali. Hivyo fundi na mke wake waliingia katika bahati njema ya milele.

13. Mtu aliyeishi karibu na makaburini siku moja alisikia sauti ikimwita kutoka makaburini. Alikuwa mwoga kuichunguza sauti hiyo yeye mwenyewe lakini kesho yake alimweleza jasiri rafiki yake, ambaye aliazimia kufuatilia sauti hiyo inapotoka mara sauti hiyo itakaposikika tena usiku ufuatao.

Wakati yule mwoga alipokuwa anatetemeka kwa woga, rafiki yake alikwenda hadi makaburini, na kwa hakika sauti ilisikika kutoka kaburini. Rafiki yake aliuliza ni nani na anataka nini. Sauti toka kuzimuni ilijibu. "mimi ni hazina iliyofichwa ambaye nimeamua kujitoa kwa mtu yeyote. Nilijitoa kwa bwana

mmoja usiku wa jana lakini alikuwa mwoga kufuatilia, kwa hiyo nitajitoa kwako anayeistahili. Kesho asubuhi nitafika nyumbani kwako na wafuasi wangu saba."

Rafiki yake alisema. "Nitakusubiri lakini tafadhali nieleze jinsi ya kukuhudumia" Sauti ilijibu. "Tutakuja tumevaa majoho ya watawa. Andaa chumba chenye maji; oga mwili wako na usafishe chumba, tuwekee viti na bakuli nane za uji wa mchele. Baada ya mlo utatuongoza mmoja mmoja katika chumba kilichofungwa ambapo tutageuka kuwa mitungi ya dhahabu."

Siku iliyofuata asubuhi yake bwana huyo alioga na kusafisha chumba kama alivyoagizwa akabaki akiwasubiri hao watawa wanne. Watawa hao waliwasili kwake na akawapokea kwa ukarimu. Baada ya chakula chao aliwaelekeza kwenye chumba kilichofungwa ambako kila mtawa alijigeuza kuwa mtungi uliojaa dhahabu. Kulikuwa na mtu mwenye choyo sana katika kijiji kilekile aliyesikia tukio hilo akahitaji naye mitungi ya dhahabu. Aliwakaribisha watawa wanne nyumbani kwake. Baada ya chakula aliwaelekeza kwenye chumba kilichofungwa, lakini badala ya kugeuka kuwa mitungi ya dhahabu walikasirika na kuwa wakali kisha wakatoa taarifa polisi ambao walifika kumkamata.

Naye yule mwoga alipopata habari kuwa ile sauti toka kaburini ilimpatia utajiri rafiki yake jasiri, alikwenda kwa rafiki yake na kwa uroho akadai kuwa dhahabu ilikuwa yake kwa kuwa sauti ilimwita kwanza yeye. Mwoga yule alipojaribu kuchukuwa

mitungi alikumbana na nyoka wengi wametokeza vichwa vyao tayari kumshambulia.

Mfalme aliposikia habari hii alitoa hukumu kuwa mitungi ilikuwa mali ya mtu jasiri na akasema: "Kila jambo ulimwenguni huenda hivi. Wajinga wana tamaa ya matukio mazuri tu, lakini ni woga sana kuyafuatilia, na kwa hiyo hushindwa kila mara. Hawana imani wala ushujaa kupambana na migongano ya ndani ya moyo na utulivu wa kweli."

SURA YA PILI

NJIA YA KUFAIDIKA KWA VITENDO

I
KUTAFUTA UKWELI

1. Katika kutafuta kweli kuna baadhi ya maswali yasiyokuwa ya muhimu. Ulimwengu umeumbwa na nini? Ni kwa njia zipi jamii za binadamu zimewekwa pamoja? Ni muundo au sura ipi ya uongozi ulio bora wa jamii ya binadamu? Ikiwa binadamu angeahirisha kutafuta na kutenda matendo ya Wongofu hadi hapo majibu ya maswali hayo yapatikane, angekufa kabla ya kugundua njia.

Fikiria mtu amechomwa na mshale wenye sumu, na ndugu zake na marafiki wamepata kumfuata daktari ili amtoe mshale na kutibu jeraha.

Ikiwa mtu aliyejeruhiwa atapinga akisema, "Subiri kidogo. Kabla ya kutoa mshale, nataka kujua aliyenichoma. Alikuwa mwanamke au mwanaume? Alikuwa mtu wa nasaba bora au mkulima? Uta umetengenezwa na nini? Upinde uliotumika ulikuwa mdogo au mkubwa? Ulikuwa umetengenezwa kwa mti au mwanzi? Kamba ya upinde ilitengenezwa na nini? Ilikuwa imetengenezwa kwa uzi, henzirani au matete? Ni manyoya gani yalitumika? Kabla hamjachomoa mshale nataka kujua yote haya. "Nini basi kitakachofuata?

Njia ya kufaidika kwa vitendo

Kabla ya taarifa yote hiyo haijapatikana, bila shaka sumu itakuwa imepata muda wa kusambaa katika sehemu zote za mwili na huenda huyo mtu akafariki. Kazi ya kwanza ni kuondoa mshale na kuzuia sumu isisambae mwilini.

Wakati moto wa mateso unahatarisha ulimwengu, umbile la dunia halina maana ya msingi, upi ni muundo au umbo lipi ni sahihi la jumuiya ya watu vilevile hiyo haina umuhimu wa kuihangaikia.

Kujiuliza juu ya ulimwengu kuwa na mipaka au kuwa ni wa milele kunaweza kusubiri hadi njia itakapopatikana ya kuzima mioto ya kuzaa, uzu, ugonjwa na kifo; katika hali ya taabu, huzuni, maumivu na mateso, mtu yampasa kwanza kutafuta njia ya kutatua matatizo haya na kujitolea kuishika na kuitafuta njia hiyo.

Mafundisho ya Buddha yanahusu mambo yaliyo muhimu kuyajua wala si yale yasiyo muhimu. Hii ina maana watu hawana budi kujifunza wanayopaswa kujifunza, waondoe wanachopasa kuondoa, wajizoeze yale watakayowaongoza.

Kwa hiyo watu yawapasa kuamua yapi ni muhimu, yapi yatatuliwe kwanza na ni jambo lipi lenye shinikizo kwao. Kufanya haya yote yawapasa kujibidiisha kuifunza mioyo yao; kupata kwanza uwezo wa kuitawala mioyo.

2. Kwa mfano mtu anakwenda msituni kutafuta roho iotayo

katikati ndani ya mti na anaporudi anarudi na mzigo wa matawi na majani akidhania kuwa amepata alichokiendea. Je, hatakuwa mjinga akitosheka na gome au ubao badala ya roho ya mti aliyokusudia kupata? Lakini hayo ndiyo wafanyayo watu.

Mtu hutafuta njia itakayomwepusha na uzazi, uzee, maradhi na kifo au taabu, huzuni, maumivu na mateso: na badala yake anafuata njia hiyo kwa muda, anagundua mafanikio kidogo, na mara moja anaanza kujivuna na kudeka kabisa. Mtu huyu naye anakuwa sawa na aliyekwenda msituni kutafuta roho ya mti na akiridhika kwa kurudi nyumbani na mzigo wa matawi na majani.

Mtu mwingine akiwa ametosheka kwa maendeleo yake aliyoyapata kwa juhudi zake kidogo, hupunguza nguvu zake na huanza kujivuna na kuwa na kiburi; amebeba tu mzigo wa matawi na majani badala ya roho ya mti aliyokusudia kupata.

Mtu mwingine pia anapogundua kuwa moyo wake umetulia na mawazo yake yanakuwa wazi, anapunguza juhudi yake na kuanza kujivuna na kuwa na kiburi; ana mzigo wa magome ya miti na wala siyo roho ya mti aliyokuwa akiitafuta.

Basi tena, mtu mwingine huwa na majivuno na kiburi kwa sababu amegundua anayo busara ya kutosha;ana mzigo wa nyuzi za miti badala ya roho ya mti. Watafutaji wote hawa wanatosheka kwa urahisi kwa juhudi zao kidogo na huanza kujivuna na kujitegemea; hupunguza juhudi zao na huanguka katika ulegevu. Watu wote hawa hatimaye watakumbwa na mateso tena.

Njia ya kufaidika kwa vitendo

Wale wote waitafutayo njia ya kweli ya Wongofu wasitegemee tuzo ya heshima, utukufu au upendo. Tena wasiende kwa nguvu kidogo, kwa hatua za kipumbavu katika utulivu, maarifa au busara.

Kwanza kabisa yampasa mtu kuelewa kabisa moyoni mwake hali halisi na ya msingi ya ulimwengu wa maisha na kifo.

3. Ulimwengu hauna asili ya pekee. Ni upatanifu mkubwa kwa sababu na hali ya maumbile yenye asili yake tu katika matendo ya moyo ambayo yameshawishiwa na ujinga, fikra potovu, tamaa na ghururi. Sio kitu cha nje ambachɵ moyo una fikira potofu juu yake ; haina hakika ya pekee kwa hali yoyote ulimwengu umejitokeza kwa mifumo ya akili yenyewe ikidhihirisha madanganyo yake. Imeanzishwa na kujengwa kutokana na tamaa za moyo, kutokana na maumivu, mateso na mapambano yaliyoibuka kutokana na maumivu yaliyosababishwa na uchoyo, hasira na ujinga. Watu wote waitafutayo njia ya Uongofu hawana budi kupambana na roho ya namna hiyo ili waweze kufanikisha malengo yao.

4. " Loh, Moyo wangu! Kwa nini unatangatanga bila kutulia juu ya hali ya mabadiliko ya maisha? Kwa nini unanifanya nichanganyikiwe nisiweze kutulia? Kwa nini unanihimiza nikusanye mambo mengi? Unafanana na plau inayovunjika kabla ya kuanza kulima; unafanana na usukani unaovunjika wakati unatarajia kuvinjari katika bahari ya kufa na kupona. Mageuzi yangu yana maana gani kama hatuwezi kufaidi maisha haya?

" Loh Moyo wangu! Ulinifanya nizaliwe kama Mfalme, halafu ukanifanya nizaliwe kama masikini na niishi kwa kuombaomba. Agharabu umenisababisha nizaliwe katika majumba makubwa ya miungu mbinguni na kuishi katika furaha na anasa; mwisho unanitupia katika tanuru la jehanam.

" Loh Moyo wangu! mjinga! Hivyo umenielekeza katika njia mbalimbali na nimekuwa mtiifu na mtulivu kwako. Lakini kwa kuwa sasa nimesikia mafundisho ya Buddha, usinisumbue tena wala kunifanya niendelee na mateso; bali kwa pamoja tuutafute Uongofu kwa unyenyekevu na utulivu.

" Oh Moyo wangu! Laiti ungejifunza kuwa kila kitu hakina hakika na ni cha kupita; kama ungejifunza kutoshikilia mambo, kutotamani vitu, kutotoa nafasi kwa choyo, hasira na ujinga; bila shaka tungeweza kusafiri katika utulivu. Basi kwa kuvunjavunja pingu na kamba za tamaa kwa sime ya hekima, bila ya kubughudhiwa na manzili yabadilikayo-faida au hasara au baya, baraka au balaa, sifa au bezo-huenda tukaishi kwa amani.

" Oh, moyo wangu mpendwa! Ni wewe uliyeamsha imani ndani yetu; ni wewe uliyetushauri kuutafuta Uongofu. Kwa nini unarahisika tena kufungua milango kwa choyo; kwa mapenzi ya starehe na mahangaiko.

" Oh, moyo wangu, kwa nini unahangaika hapa na pale bila dhumuni mahsusi? Hebu tuvuke hii bahari kubwa ya madanganyo. Hadi sasa nimekuwa nikitenda kama upendavyo na

kwa pamoja tutafuata mafundisho ya Buddha.

" Oh, moyo wangu mpendwa! Hii milima, mito, na bahari inabadilika na inasababisha maumivu. Ni wapi katika dunia hii ya madanganyo tutakapopata utulivu? Hebu tufuate mafundisho ya Buddha na tuvuke hadi pwani nyingine ya Wongofu."

5. Kwa hiyo wale waitafutao njia ya Nuru hasa huamrisha mioyo yao. Kisha huendelea kwa azma kuu. Ingawa wanatukanwa na kusutwa na baadhi ya watu, wanasonga mbele bila kukata tamaa . Hawakasiriki wanapopigwa ngumi au mawe au wanapokatwa mapanga.

Hata kama maadui watakata vichwa vyao na kuacha viwiliwili, moyo usihangaike. Wakiruhusu mioyo yao ifunikwe na mambo yawaumizayo, hawafuati mafundisho ya Buddha. Yawabidi kukata shauri bila kujali litakalowatokea, kusimama imara, bila kuyumba daima wakisambaza fikra na mawazo ya huruma na ukarimu. Wacha matusi yaje, wacha balaa ije na bado mtu haitambidi kutoyumbayumba bali moyoni kubaki amejaa mafundisho ya Buddha.

Kwa nia ya kuupata Wongofu, yampasa mtu kujaribu kukamilisha yasiyowezekana, kustahimili yasiyostahimilika. Yampasa mtu kutoa yote aliyo nayo. Ikiwa mtu ataambiwa kuwa ili kuupata Uongofu inabidi apunguze chakula chake hadi punje moja ya mchele kila siku, atakula punje moja tu. Ikiwa njia ya Uongofu inapitia motoni mtu atasonga mbele.

Lakini mtu asifanye haya yote kwa madhumuni ya kutenda kinyume. Mtu atende itakiwavyo kwa sababu ni jambo la busara na sahihi. Mtu atende mambo hayo kutokana na roho ya huruma kama mama amfanyiavyo mtoto wake mchanga, kwa mtoto wake mgonjwa, bila kuwazia nguvu zake au faraja.

6. Zama za kale alikuwepo mfalme aliyependa nchi yake na watu wake na aliwatawala kwa hekima na huruma na matokeo yake nchi hiyo ilipata maendeleo makubwa na amani. Kila mara alijitahidi kuongeza hekima yake na elimu; Wakati mwingine alitoa zawadi kwa mtu yeyote aliyeweza kumpa mafundisho ya busara.

Hekima na bidii yake hatimaye viliwafikia miungu walioapa kumjaribu. Muungu alijigeuza kuwa jini, akaenda langoni kwa Mfalme akaomba aonane naye ili ampatie mafundisho matakatifu.

Naye Mfalme aliyefurahia kusikia taarifa hiyo alilikaribisha jini hilo vizuri limpe mafundisho. Jini lilibadilika katika sura ya kutisha na likadai lipewe chakula linachotaka kabla ya kutoa mafundisho. Chakula kilipoletwa jini lilidai lipewe nyama na damu ya binadamu ambayo bado ina moto. Mwana wa Mfalme na malkia walitoa miili yao likawala lakini jini hilo halikuridhika hivyo likadai mwili wa Mfalme.

Mfalme alijiweka tayari kutoa mwili wake ila akadai asikie fundisho kwanza kabla ya kuutoa mwili wake.

Muungu alitoa fundisho la busara lifuatalo: Taabu hutokana na tamaa na woga hutokana na tamaa. Wale walioachana na tamaa hawana taabu wala woga." Mara moja Muungu akarudia sura yake na mwana wa Mfalme pamoja na malkia wakatokea katika maumbo yao.

7. Hapo kale kulikuwa na mtu aliyeitafuta Njia ya kweli ya kwenda Himalaya. Hakufikiria lolote kuhusu hazina ya duniani ama furaha za ahera bali alitafuta mafundisho yatakayomwondolea madanganyo akilini mwake.

Miungu walifurahishwa na bidii na unyofu wa mtu huyo na wakaamua kujaribu moyo wake. Hivyo mmoja wa miungu alijigeuza kuwa jini na akajitokeza katika milima ya Himalaya, akiimba: " Kila kitu hubadilika, kila kitu hutokea na kupotea."

Mtafutaji alipousikia wimbo huu alifurahi sana. Alijiwa na furaha kuu kana kwamba amepata kisima cha maji kwa kiu yake ama kama mtumwa aliyeachiwa huru bila ya kutarajia. Alijisemea, "sasa nimepata mafundisho ya kweli niliyokuwa nikitafuta kwa muda mrefu." Aliifuatilia sauti hadi alipofikia jini lenye sura ya kutisha. Kwa moyo wa wasi wasi aliliendea lile jini na kusema "je, ni wewe uliyeimba wimbo mtakatifu niliousikia? Kama ni wewe tafadhali endelea kuimba."

Jini lilijibu:" Ndiyo, ulikuwa wimbo wangu, lakini siwezi kuuendeleza hadi nitakapokuwa nimepata chakula; ninakufa kwa njaa."

Bwana huyo alimsihi sana kwa bidii aendelee kuimba, akisema, "Wimbo huo una maana takatifu kwangu na nimetafuta mafundisho yake kwa muda mrefu. Nimesikia sehemu yake tu; tafadhali niruhusu nisikie ziada yake."

Jini lilisema tena: Ninakufa kwa njaa lakini nikionja nyama mbichi ya binadamu na damu yake nitaumalizia wimbo."

Kwa kuwa mtu huyo alikuwa na nia ya kusikia mafundisho aliahidi kutoa mwili wake kwa jini baada ya kusikia mafundisho. Hapo jini liliimba wimbo wote.

Kila kitu hubadilika,
Kila kitu huonekana na kutoweka,
Kuna uhuru wa kweli,
Mtu anaposhinda maisha na kifo.

Baada ya kulisikia shairi hilo yule mtu aliliandika kwenye miamba na miti kisha akapanda juu ya mti ajitupe chini ya miguu ya jini, lakini wakati huo jini lilishatoweka na badala yake muungu aliyejaa furaha alimpokea bila kuumia.

8. Hapo kale kulikuwa na mtu mwenye bidii ya kutafuta njia ya kweli aliyeitwa Sadaprarudita. Alitupilia mbali majaribio yote kwa faida au heshima na kuitafuta njia kwa kujitolea maisha yake. Siku moja alisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, "Sadaprarudita! "Ondoka hapa uelekee Mashariki usifikirie joto au baridi, usijali sifa za kidunia wala bezo, usibughudhiwe na tofauti ya mema na

maovu ila kaza mwendo mbali utapata mwalimu wa kweli nawe utapata Uongofu."

Sadaprarudita alifurahi sana alipopata maelekezo ya hakika na akaondoka mara moja kuelekea Mashariki. Agharabu alilala popote pale, nyikani au milimani.

Akiwa mgeni katika nchi ya ugenini alipata maudhi mengi; Wakati fulani alijiuza utumwani, aliuza mwili wake kwa sababu ya njaa, lakini mwisho alipata mwalimu wa kweli akamwomba maelekezo.

Kuna methali isemayo " Vitu vizuri ni ghali" na Sadaprarudita alithibisha ukweli huu kwa kuwa alikumbana na vipingamizi vingi katika kutafuta njia.

Hakuwa na fedha yoyote ya kununulia maua na ubani wa kumpatia mwalimu. Alijitahidi kuuza huduma zake lakini mtu wa kumkodisha hakupatikana. Ilielekea kulikuwa na pepo mbaya akimkwamisha katika njia yoyote aliyojaribu. Njia ya kuelekea kwenye Uongofu ni ngumu inaweza kupoteza maisha ya mtu.

Mwisho Sandaprarudita alifika mahali alipokuwa mwalimu ila akawa na tatizo jipya. Hakuwa na karatasi wala wino au brashi ya kuandikia. Hivyo alichoma mkono wake kwa sime na akaandika kwa kutumia damu yake. Kwa njia hii alifaulu kuipata kweli ya thamani.

9. Zama zile kulikuwa na mvulana, jina lake Sudhana ambaye pia alihitaji Uongofu na kwa bidii aliitafuta njia. Kutokana na mvuvi alijifunza elimu ya bahari. Kutoka kwa daktari alijifunza huruma kwa wagonjwa katika maumivu yao. Kwa tajiri alijifunza kuwa kuweka akiba ya fedha ndiyo ilikuwa siri ya bahati yake na akapata wazo kuwa ni lazima kuweka akiba ya kila kitu kilichopatikana katika njia ya Uongofu.

Kutokana kwa mtawa anayetafakari alijifunza kuwa moyo safi na wa imani una nguvu za kimiujiza za kusafisha na kutuliza mioyo mingine. Siku moja alikutana na mwanamke wa haiba ya hali ya juu na akavutiwa na roho yake ya ukarimu na kutokana naye akajifunza kuwa hisani ni matunda ya hekima. Siku nyingine alikutana na mtembezi mmoja wa makamo aliyemwambia kuwa kufika mahali fulani itambidi apande mlima wa mapanga na kupitia katika bonde la moto. Kwa hiyo alijifunza kutokana na uzoefu wake kuwa kulikuwa na fundisho kutokana na kila kitu alichokiona au alichosikia.

Alijifunza uvumilivu kutoka kwa mwanamke kiwete, maskini; alijifunza somo la furaha isiyo na gharama kwa kuangalia watoto wakicheza barabarani; na kutoka kwa watu waungwana na wanyenyekevu, ambao hawakufikiwa kuhitaji jambo lolote litakiwalo na watu wengine, alijifunza siri ya kuishi kwa amani na ulimwengu wote.

Kutokana na kuangalia mchanganyiko wa sehemu za ubani alijifunza somo la mapatano, na kutokana na mpangilio wa maua

alijifunza somo la sadaka na shukrani. Siku moja alipokuwa akipita msituni, alijipumzisha chini ya mti bora na akaona mche mdogo ukiota karibu kutokana na mti ulioanguka pale ukaoza na akajifunza somo la maisha kutokuwa na uhakika.

Mwanga wa jua na kumetameta kwa nyota, mara kwa mara vilimburudisha sana. Kwa hiyo Sudhana alifaidika kutokana na uzoefu wa safari ndefu.

Hakika wale waitafutao Nuru Kuu yawapasa wafikirie mioyo yao kama ngome na waipambe. Yawabidi pia wafungue malango ya mioyo yao kwa Buddha, na kwa heshima na unyenyekevu wamkaribishe ili aingie katika mwandani wao ili wakamtolee yeye ubani wenye manukato ya imani na maua ya furaha na shangwe.

II
NJIA ZA MATENDO

1. Kwa wale waifuatao Nuru kuna njia tatu za utendaji ambazo zinapaswa kueleweka na kufuatwa: kwanza, taratibu ya tabia za utendaji; pili utulivu sahihi wa moyo; na tatu, hekima.

Taratibu ni zipi? Kila mmoja awe ni mlalahoi au mtafutaji wa njia, lazima afuate mafundisho kwa tabia nzuri. Lazima atawale vyote moyo na mwili wake, na alinde milango ya fahamu zake sita. Nilazima aogope hata ovu dogo, na mara kwa mara ajitahidi

kutenda matendo mema tu.

Utulivu wa moyo una maana gani? Una maana ya kuondokana haraka na uchoyo na tamaa mbaya zinapojitokeza, na kutunza moyo kwa usafi na utulivu.

Hekima ni nini? Ni uwezo wa kutambua kwa usahihi na kukubali kwa utaratibu wa ukweli bora, kujua chanzo cha mateso, kinachofanya mwisho wa mateso.

Wale wafuatao njia hizi tatu za utendaji kwa bidii wana haki ya kuitwa mitume wa Buddha.

Fikiria punda, ambaye hana umbo zuri, hana sauti wala pembe kama zile za ng'ombe anafuata kundi la ng'ombe na akitangaza, " Tazama mimi pia ni ng'ombe. "Je kuna mtu atakayemwamini? Ni ujinga mtupu pia mtu anaposhindwa kufuata njia tatu za utendaji lakini anapotakabari kuwa yeye ni mtafutaji wa njia, ama mtume wa Buddha.

Kabla ya mkulima hajakusanya mavuno inabidi kwanza alime ardhi, apande mbegu, amwagilie na apalilie magugu wakati wa masika. Vilevile, mtafutaji wa wongofu lazima afuate njia tatu za utendaji. Mkulima hawezi kutegemea kuona mbegu zinaota leo, kuona mimea kesho, na kukusanya mazao kesho kutwa. Kwa hiyo mtu aitafutaye Nuru hawezi kutegemea kuachana na tamaa mbaya kesho yake na kuipata Nuru kesho kutwa.

Njia ya kufaidika kwa vitendo

Kama mimea inayopata utunzaji bora kutoka kwa mkulima tangu mbegu inapopandwa na wakati wa kubadilika kwa hali ya hewa hata wakati wa kukua toka kuota hadi kutoa matunda, hivyo basi mtafutaji wa Uongofu ni lazima alime na kutifua udongo wa Uongofu kwa bidii na ustahimilivu kwa kufuata njia tatu za utendaji.

2. Ni vigumu sana kuendelea kufuata njia na starehe, na moyo ukisumbuliwa na tamaa za milango ya fahamu. Kuna tofauti kati ya starehe ya maisha na starehe ya Njia ya Kweli.

Kama ilivyokwisha elezwa, moyo ndiyo chanzo cha mambo yote. Moyo unapopenda mambo ya kidunia, madanganyo na mateso bila shaka, vitafuata, lakini moyo unapopenda na kufurahia Njia ya kweli, hakika furaha na mafundisho vitafuata.

Kwa hiyo watu wafuatao Uongofu yawapasa kuwa na mioyo safi na kwa uvumilivu wafuate njia tatu za utendaji. Ikiwa wafuasi watafuata mafundisho, kwa kawaida watapata utulivu wa moyo; na ikiwa watapata utulivu wa moyo itakuwa jambo la kawaida kwao kupata hekima, na hekima hiyo itawaelekeza kwenye Uongofu.

Kwa hakika hizi njia tatu(kufuata mafundisho, kushika utulivu wa moyo, na kila mara kufanya mambo kwa busara) ni njia za kweli za kuelekea kwenye Nuru.

Kwa kutozifuata hizo njia tatu, kwa muda mrefu watu wanakusanya madanganyo ya akili. Wasibishane na watu wa duniani, bali, kwa utaratibu na uvumilivu watafakari undani wa dunia yao ya moyo safi kuupata Uongofu.

3. Ikiwa njia tatu za utendaji zitachambuliwa, zitadhihirisha njia nane bora, mitizamo minne ya kufikiriwa, taratibu nne sahihi, vitivo vinne vya nguvu zitakazotumika na ukamilifu wa njia sita za utendaji.

Njia Nane Bora ina maana ya mtizamo sahihi, fikra sahihi, maneno sahihi, tabia sahihi, maisha sahihi, nguvu sahihi, utu sahihi na utulivu sahihi.

Mtizamo Sahihi ina maana ya kuelewa kwa ufasaha U-nne wa Ukweli, kuamini kanuni ya sababu na matokeo na kutokudanganywa na sura na tamaa.

Fikra Sahihi ina maana ya azima ya kutozienzi tamaa, kutokuwa mchoyo, kutokasirika na kutofanya jambo lolote la kudhuru

Maneno Sahihi maana yake ni kuepuka kusema uwongo, kuseng'enya, kutukana na kutokuwa kidhabidhabina.

Tabia sahihi ina maana ya kujiepusha na maisha yanayoweza kuleta aibu.

Nguvu Sahihi ina maana ya kujitahidi kwa uangalifu kufuata uelekeo sahihi.

Utu Sahihi ina maana kuwa na moyo ulio safi na wenye akili na mawazo mema.

Utulivu sahihi ina maana ya kuuweka moyo katika hali iliyo huru kuuwezesha kutulia, ili kupata utakaso halisi wa moyo.

4. Mitizamo minne ya kufikiria ni: kwanza kufikiria mwili kuwa mchafu, kujitahidi kuondoa mapendo yote kwake, pili kufikiria milango ya fahamu kama chimbuko la mateso bila kujali hisia zake za furaha au maumivu; tatu, kuufikiria moyo kuwa katika hali ya kutiririka daima, na nne, kufikiria kuwa kila mtu duniani ni matokeo ya sababu na hali ya maumbile na hakuna kitu kisichobadilika milele.

5. Taratibu nne sahihi ni: Kwanza ni kuzuia uovu wowote usitokee: pili kuondoa uovu wowote unapotokea; tatu ni kushawishi utendaji wa matendo mema, na nne ni kutia moyo ukuzaji na ustawishaji wa matendo mema yaliyokwisha jitokeza. Kila mtu yampasa ajitahidi kufuata taratibu hizi nne.

6. Misingi mitano ya nguvu ni: Kwanza ni Imani ya kuamini; pili ni nia ya kujitahidi; tatu ni msingi wa kusimama kidete; nne ni uwezo wa kutuliza moyo; na tano ni uwezo wa kulinda hekima safi. Misingi hii mitano ni nguvu za lazima ili kuupata Wongofu.

7. Ukamilifu wa mazoezi sita ya kufikia ukingo mwingine wa Nuru ni: njia ya matoleo na sadaka, njia ya kutunza mafundisho, njia ya utulivu wa moyo, na njia ya hekima. Kwa kufuata njia hizi, hakika mtu atavuka kutoka ukingo wa madanganyo kwenda ukingo wa Nuru.

Zoezi la matoleo linaondoa uchoyo; Zoezi la Mafundisho humfanya mtu afikirie haki na raha za wengine; Zoezi la uvumilivu humsaidia mtu kutawala moyo ulio hafifu na unaotangatanga; na zoezi la Hekima huubadilisha moyo uliochanganyikiwa na uliojaa giza katika moyo wa busara safi.

Matoleo na kushika Mafundisho hujenga msingi madhubuti ambao ni wa lazima kujengea ngome juu yake. Uvumilivu na Bidii ni kuta za kuizuia ngome isishambuliwe na maadui kutoka nje. Utulivu na Hekima ni silaha za kujilinda kutokana na mashambulizi ya maisha na kifo.

Ikiwa mtu hutoa zawadi pale inapowezekana au kwa vile ni rahisi kutoa kuliko kutokutoa, hayo ni Matoleo, lakini siyo Matoleo ya kweli. Matoleo ya kweli hutokana na moyo wa huruma kabla ya ombi lolote na Matoleo ya Kweli hutolewa mara kwa mara wala siyo kwa msimu.

Wala hayatakuwa Matoleo ya Kweli ikiwa baada ya tendo hilo kutazuka hisia za kujilaumu au kujitukuza; Matoleo ya Kweli ni yale yatolewayo kwa furaha, kwa kujisahau kama mfadhili (mtoaji) kama mpokeaji, na zawadi yenyewe.

Njia ya kufaidika kwa vitendo

Matoleo ya kweli hutoka bila kusudio la kupangwa kutoka kwa moyo wenye huruma, bila matumaini ya kulipwa au kurudishiwa fadhila ukitegemea kuingia pamoja katika Uongofu.

Kuna aina saba za matoleo ambazo zinaweza kutendwa hata na watu wasio matajiri. Ya kwanza ni matoleo ya nguvu. Huku ni kutoa huduma kwa kufanya kazi. Aina ya juu sana ya Matoleo haya ni mtu kujitoa maisha yake kama inavyoonekana katika hadithi ifuatayo: ya pili ni matoleo ya kiroho. Ya tatu ni matoleo ya macho. Hii ni kutoa mtizamo wa ukarimu. Ya nne ni matoleo ya wajihi. Hii ni kutoa uso laini na wa tabasamu kwa wengine. Ya tano ni matoleo ya kauli. Hii ni kutoa maneno ya upole. Ya sita ni matoleo ya kiti. Hii ni mtu kutoa kiti chake kwa wengine. Ya saba ni matoleo ya nyumba. Hii ni kuwakaribisha watu wengine kulala nyumbani kwake. Aina hizi za matoleo zinaweza kutolewa na mtu yeyote katika maisha ya kila siku.

8. Zama zile kulikuwa na mwana wa mfalme jina lake Sattva. Siku moja yeye na kaka zake walikwenda kucheza msituni. Huko walimwona chui jike aliyekuwa amekabwa na njaa na akishawishika kuwala makinda wake saba.

Kaka zake walikimbia lakini Sattva alipanda juu ya jabari akajiangusha miguuni pa chui jike ili aokoe maisha ya vitoto vya huyo chui.

Sattva, mwana wa Mfalme, alitenda tendo la hisani bila kupanga lakini moyoni mwake alikuwa akifikiri: "Mwili huu

unabadilika na siyo wa kudumu. Nimeupenda mwili huu bila wazo la kuutupa lakini sasa niutoe sadaka kwa chui jike huyu ili nikaupate Uongofu." Wazo hili la mwana wa Mfalme Sattva linaonyesha ujasiri wa kweli wa kupata Uongofu.

9. Kuna Hali Nne zisizo na kikomo za Moyo ambao kwanza mtafutaji wa Nuru anapaswa kuzilinda. Nazo ni huruma; Utu wema, uchangamfu na utulivu. Mtu anaweza kuepukana na hasira kwa utulivu. Mtu anaweza kuepuka tabia ya kuwatofautisha marafiki na maadui kwa kulinda moyo mwadilifu.

Ni huruma kubwa iwafanyao watu wafurahi na kuridhika; ni utu - mwema unaoondoa jambo lolote linalowakosesha watu furaha na kuridhika, ni uchangamfu unaomfanya kila mtu afurahi na kuridhika kwa moyo wa furaha, kuna wingi wa amani kila mtu anapofurahi na kutosheka na mtu anaweza kuwa na hisia sawa kwa kila mtu.

Kwa uangalifu mtu anaweza kulinda hizi Hali nne zisizokuwa na kikomo na akaweza kuondokana na choyo, hasira, mateso na moyo wa upendo-chuki, lakini hilo siyo jambo rahisi kutenda. Ni vigumu kuondoa moyo mwovu kama ilivyo vigumu kumuondoa mbwa kwenye lindo, na ni rahisi kuupoteza moyo sahihi kama kulungu msituni; ama ni vigumu kuuondoa moyo mwovu kama ilivyo vigumu kuyafuta maandishi yaliyoandikwa kwenye mwamba au jiwe, na moyo sahihi ni rahisi kuupoteza kama maandishi yaliyoandikwa kwenye maji. Kwa hakika, ni jambo gumu sana katika maisha mtu kujiongoza ili

kuupata Uongofu.

10. Kulikuwa na kijana mmoja jina lake Srona aliyezaliwa katika familia ya kitajiri lakini mwenye afya hafifu. Alikuwa na bidii ya kuupata Uongofu, akawa mtume wa Aliyebarikiwa. Katika njia ya Nuru alijitahidi hadi miguu yake ikavimba.

Aliyebarikiwa alimwonea huruma akasema "Srona kijana wangu, ulijifunza kinubi nyumbani kwenu? Unajua kuwa kinubi hakiwezi kutoa muziki ikiwa nyuzi zimevutwa sana au zimelegezwa sana? Kinubi kinatoa muziki ikiwa nyuzi zake zimevutwa kwa usahihi.

"Mafundisho ya Wongofu ni kama kurekebisha nyuzi za kinubi. Huwezi kuupata Uongofu ikiwa utavuta sana au kulegeza sana moyo wako. Yakupasa kuwa mwangalifu na mwenye busara."

Srona aligundua kuwa maneno haya yalikuwa ya faida na mwishowe akapata alichokitaka.

11. Zama zile kulikuwa na mwana wa Mfalme ambaye alikuwa bingwa katika matumizi ya silaha tano. Siku moja alipokuwa anatoka kwenye mazoezi alikutana na dubwana ambalo ngozi yake ilikuwa ngumu kupindukia.

Dubwana hilo lilimshambulia lakini mwana wa mfalme hakuogopa katu. Kwanza alilichoma kwa mshale lakini

haukuliumiza popote. Pili alilitupia mkuki lakini ulishindwa kutoboa ngozi yake. Tena alilitupia ufito na Sagai lakini vyote vilishindwa kuipenya ngozi yake. Tena akatumia sime yake lakini haikufaa kitu, kwani dubwana hilo lilimdaka kwa mamikono yake na kumbana kwa nguvu. Basi tena mwana wa mfalme alijitahidi kutumia kichwa chake lakini hakikumsaidia.

Dubwana lilisema " Ni kazi bure wewe kukataa, nitakumeza." Lakini mwana wa mfalme alijibu." Huenda ukafikiri kuwa nimetumia silaha zangu zote hivyo sina msaada wowote, bado nina silaha moja iliyobaki. Ukinimeza nitakuharibu niwapo ndani ya tumbo lako."

Ushupavu wa mwana wa Mfalme ulilibabaisha sana dubwana na likauliza " Unawezaje kufanya hivyo?" Mwana wa mfalme alijibu "Kwa uwezo na nguvu za kweli."

Kisha dubwana lilimwachia na likamwomba alipatie mafundisho juu ya ukweli."

Mafundisho katika hadithi ni kuwatia moyo mitume kuwa na bidii katika harakati zao na kutokuwa na hofu wapambanapo na vikwazo.

12. Tabia ya kukarahisha na kujitanguliza humkwaza binadamu lakini dharau na aibu huwalinda binadamu. Watu huwaheshimu wazazi wao, kaka zao na dada zao kwa sababu ni wepesi wa kutambua dharau na aibu. Baada ya kujichunguza ni jambo la

heshima kujiepusha na utukuzaji wa nafsi na kuona aibu tuwaangaliapo watu wengine.

Ikiwa mtu ana roho ya toba, dhambi zake zitatoweka, lakini kama ana roho asiyokuwa na toba ndani mwake dhambi zake zitaendelea na zitamwangamiza milele.

Ni yule tu ayasikiaye mafundisho ya kweli kwa usahihi na kutambua maana na uhusiano wa mafundisho hayo kwake atakaye yapokea na kufaidika.

Ikiwa mtu atasikia mafundisho ya kweli lakini hayapokei, atashindwa katika juhudi za kuitafuta Nuru.

Imani , adabu, unyenyekevu, bidii na hekima ni misingi ya nguvu kwa yule anayeutafuta Uongofu. Kati ya misingi hiyo, hekima ndiyo kubwa zaidi na mengineyo ni sura za hekima. Kama mtu atapenda mambo ya kidunia, atafurahia kuplga maneno au kulala usingizi, ataiacha njia ya Uongofu.

13. Wakati wa mafundisho ya Uongofu, baadhi ya watu wanafaulu kwa haraka kuliko wenzao. Kwa hiyo mtu asikate tamaa kuwaona wenzake wanatangulia kuongoka.

Mtu anapojifunza ufundi wa kupiga upinde, hategemei kufaulu kwa haraka bali anafahamu kuwa akifanya mazoezi kwa uvumilivu taratibu, atafaulu barabara . Mto huanza kama kijito lakini huendelea kupanuka hadi kutiririka katika bahari kuu.

Kama kwenye mifano hii, ikiwa mtu atajifunza kwa uvumilivu na kwa bidii ataupata Uongofu bila wasiwasi.

Kama ilivyokwisha elezwa, ikiwa mtu atafungua macho yake, atayaona mafundisho kila mahali na hivyo nafasi zake za Uongofu ni nyingi sana.

Wakati fulani kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa anaunguza ubani. Aligundua kuwa harufu ya manukato ilikuwa haiji wala haiendi; haikutokea wala kutoweka. Tukio hilo dogo lilimsaidia kuipata Nuru.

Siku za kale mtu mmoja alichomwa mwiba katika mguu wake. Alipata maumivu makali na wazo likamjia kuwa maumivu yalikuwa yanabainishwa na moyo. kutokana na tukio hilo wazo zito lilimjia kuwa moyo usipotawaliwa unaweza kupotea au unaweza kuwa mtakatifu mtu anapofaulu kuutawala. Kutokana na mawazo hayo baada ya kitambo kidogo, Uongofu ulimjia.

Kulikuwa na mtu mwingine aliyekuwa bahili. Siku moja alikuwa anawazia juu ya moyo wake wa uchoyo alipogundua kuwa mawazo ya uchoyo yalikuwa ni vidonda na takataka ambazo zingeweza kuchomwa na kuteketezwa na hekima. Huo ulikuwa ni mwanzo wa Nuru.

Kuna msemo usemao: "Weka akili yako sawasawa. Ikiwa akili yako iko sawa, dunia yote itakuwa sawa." Fikiria maneno haya. Elewa kuwa tofauti zote duniani zinasababishwa na

mpambanuo wa mawazo ya moyo. Kuna njia ya Nuru katika maneno hayo Hakika njia za Nuru ni nyingi sana.

III
NJIA YA IMANI

1. Wale wote wapatao hifadhi katika hazina tatu, Buddha, Dharma na Samgha wanaitwa mitume wa Buddha, hushika na kufuata sehemu nne za utawala -wa- Moyo-mafundisho, imani, matoleo na hekima.

Mitume wa Buddha hushika mafundisho matano: usiibe, usiue, usizini, usiseme uwongo na usinywe kileo cha aina yoyote.

Mitume wa Buddha wana imani katika hekima kamili ya Buddha, Hujitahidi kuepukana na tamaa na uroho na kuitoa sadaka. Wanaifahamu kanuni ya chanzo na matokeo wakiwekea maanani mpito wa maisha na kushika kanuni ya hekima.

Mti unaoegemea mashariki, ukianguka utaangukia Mashariki na vivyo hivyo wale wanaosikiliza mafundisho ya Buddha na kuyaamini hakika watazaliwa katika Nchi Takatifu ya Buddha.

2. Ni hakika ilivyosemwa kuwa watu wanaoamini hazina tatu za Buddha, Dharma na Samgha wanaitwa Mitume ya Buddha.

Buddha ndiye aliyeipata Nuru kamili na alitumia ushindi wake kuwafungua na kuwabariki binadamu wote. Dharma ni Ukweli, roho ya Uongofu na mafundisho yanayoielezea. Samgha ni undugu Sahihi wa waumini katika Buddha na Dharma.

Tunazungumzia u-Buddha, Dharma, Udugu, kana kwamba ni vitu vitatu tofauti, anajidhihirisha katika Dharma na anatambulikana katika Udugu. Kwa hiyo kuamini Dharma na kuuhifadhi udugu ni kuwa na imani katika Buddha, na kuwa na imani katika Buddha ina maanisha kuamini Dharma, kuhifadhi udugu.

Kwa hiyo watu wanaongoka na kuwa huru kwa kuwa na imani tu katika Buddha. Buddha ni Mwongofu wa kweli na Hupenda kila mtu kana kwamba kila mmoja ni mtoto wake wa pekee. Hivyo basi, mtu yeyote anayemtambua Buddha kama mzazi wake, amejitambulisha kwake na atapata Uongofu.

Wale watambuao Buddha watalindwa na hekima yake na kutiwa manukato kwa neema yake.

3. Hakuna kitu chochote duniani kiletacho manufaa kuliko kumwamini Buddha. Kusikia tu jina la Buddha, kuamini na kufurahi angalau kwa kitambo kidogo tu, kuna tuzo isiyokuwa na kifani.

Kwa hiyo mtu hana budi kufurahi kwa kutafuta mafundisho ya Buddha licha ya moto mkubwa ulioijaza dunia

nzima.

Siyo rahisi kukutana na mwalimu anayeweza kuifafanua Dharma; itakuwa vigumu kukutana na Buddha; Lakini itakuwa vigumu zaidi kuyaamini mafundisho yake.

Lakini kwa sasa umekutana na Buddha, ambaye ni vigumu kukutana naye na umeelezwa yale ambayo ni vigumu kusikika, unapaswa kuamini na kufurahi na kuwa na imani katika Buddha.

4. Imani ni mmojawapo wa marafiki aliye bora katika safari ndefu ya maisha ya binadamu; ni kiburudisho bora safarini na ni mali.

Imani ni mkono unaopokea Dharma, ni mkono mtakatifu unaopokea wema wote. Imani ni moto unaozunguka uchafu wote wa tamaa za dunia; inaondoa mzigo, na ni kiongozi aonyeshaye mapito.

Imani huondoa woga, choyo na majivuno, hufundisha ukarimu na kuwaheshimu wengine, humweka mtu huru kutoka katika utumwa wa manzili; humtia hamasa kuweza kupambana na matatizo; humpatia mtu nguvu za kushinda majaribu; humwezesha mtu kutenda matendo mema na matakatifu, na hujaza moyo hekima.

Imani ni faraja wakati njia ya mtu inapokuwa ndefu na ya kuchosha, na huelekea kwenye Nuru.

Imani hufanya tujisikie kuwa pamoja na Buddha na hutuleta pale mkono wa Buddha unapotushikilia. Imani huilainisha mioyo migumu na ya uroho na hutupa roho ya upendo na moyo wa kuelewa utu wema na huruma.

5. Watu wenye imani hupata hekima kutambua mafundisho ya Buddha kwa lolote wanalolisikia. Wale wenye imani hupata hekima ya kuona kuwa kila kitu si kingine bali ni uwepo ambao unatokana na kanuni ya sababu na hali ya maumbile, na tena imani huwapa unafuu wa kupokea kwa uvumilivu na uwezo wa kukubaliana na hali zao kwa amani.

Imani huwapa hekima ya kutambua mpito wa maisha na neema yakutoshtushwa au kusikitishwa na lolote linalowatokea au kwa maisha yenyewe yapitayo wakijua kuwa hata hali na maumbo vitabadilika, ukweli wa maisha daima kubakia bila kubadilika.

Imani inazo sura muhimu tatu: toba, heshima ya furaha na ukweli kwa wema wa watu wengine, na ukubali upeo wa kuwepo kwa Buddha.

Watu hawana budi kustawisha sura hizi za imani; yawapasa kuwa wepesi wa kuona kushindwa kwao na uchafu; yawapasa kuyaonea aibu na kutubu; yawapasa kujifunza kutambua tabia nzuri; matendo mema ya wengine na kuyapa sifa; pia yawapasa kila mara kutamani kutenda na kuishi na Buddha.

Njia ya kufaidika kwa vitendo

Moyo wa imani ni moyo wa ukweli; ni moyo wenye fikra nzito, moyo ambao umejaa uchangamfu wa kweli kuelekea katika Nchi Takatifu ya Buddha kwa Nguvu zake.

Kwa hiyo, Buddha huipa nguvu imani ambayo huwaongo za watu katika Nchi Takatifu, nguvu ambayo huwatakasa, nguvu ambayo huwalinda kutokana na madanganyo ya nafsi zao. Hata kama wameipokea imani kwa kitambo tu, walisikiapo neno lake Buddha likisifiwa duniani kote, wataelekea katika Nchi Takatifu.

6. Imani siyo kitu kinachoongezewa katika moyo wa kidunia, ni ya asili ya Buddha iliyomo ndani ya moyo. Yeyote amwelewaye Buddha naye ni Buddha, yeyote mwenye imani katika Buddha amekuwa Buddha.

Lakini ni vigumu kuitafuta na kuipata asili ya Buddha ya mtu, ni vigumu kutunza moyo mtakatifu katika mabadiliko ya kila mara ya choyo, hasira na mateso ya dunia; bali imani humwezesha mtu kutenda yote hayo.

Katika msitu wa miti ya Eranda yenye sumu, ni miti ya Eranda yenye sumu tu iotayo humo wala siyo miti ya Chandana yenye matunda matamu na ya harufu nzuri za manukato. Ni muujiza ikiwa miti ya Chandana itaota na kustawi ndani ya misitu ya Eranda. Vivyo hivyo ni muujiza, imani katika Buddha kuota na kustawi ndani ya moyo wa watu.

Kwa hiyo, imani ya kumwamini Buddha inaitwa "imani isiyo na mizizi" yaani haina mizizi ya kuota kwenye mioyo ya binadamu bali ina mizizi ya kustawi katika moyo wa huruma wa Buddha.

7. Hivyo basi, imani ni takatifu na huzaa matunda. Bali ni vigumu kuamsha imani katika moyo mlegevu. Kwa usahihi, kuna mashaka matano ambayo hujificha katika vivuli vya moyo wa binadamu na hujitahidi kuikatisha imani tamaa.

Kwanza kuna mashaka katika hekima ya Buddha, pili kuna mashaka katika mafundisho ya Buddha; tatu kuna mashaka juu ya mtu anayeelezea mafundisho juu ya Buddha, nne kuna mashaka juu ya kuaminika kwa njia na taratibu za kufuata Njia na taratibu za kufuata Njia Bora; na moyo wake wa maringo, na usio na uvumilivu ana mashaka juu ya uaminifu wa wale wanaoelewa na kufuata mafundisho ya Buddha.

Kwa hakika hakuna kitu kibaya sana kama mashaka. Mashaka huwatenganisha watu. Ni sumu inayobomoa urafiki na kuvunja mahusiano mema. Ni mwiba unaochoma na kuumiza; ni sime inayoua.

Vianzo vya imani tangu zamani vilipandikizwa kwa huruma ya Buddha. Mtu anapopata imani yampasa atambue ukweli huo na amshukuru Buddha kwa wema wake.

Mtu inabidi asisahau kuwa siyo kwa sababu ya huruma yake

ambayo imeamsha imani, ila kwa sababu ya huruma ya Buddha ambayo kwa muda mrefu imeongeza mwanga wake mtakatifu katika mioyo ya binadamu na kufukuzia mbali giza la ujinga wao. Yule afurahiaye imani ya sasa ameingia katika urithi wao.

Mtu anaweza kuzaliwa katika Nchi Takatifu hata kama anaishi maisha ya kawaida ikiwa ameamsha imani katika huruma ya kudumu ya Buddha.

Kwa hakika, ni vigumu kuzaliwa katika dunia hii. Ni vigumu kuisikia Dharma, ni vigumu zaidi kuamsha imani, kwa hiyo kila mmoja lazima ajaribu kwa kadri awezavyo kuyasikiliza mafundisho ya Buddha .

IV
METHALI TAKATIFU

1. " Alinitukana, alinicheka, alinipiga. "Hivyo ndivyo mtu anavyofikiria na kwa kuwa anaendelea kushikiria mawazo ya namna hiyo hasira yake huendelea kupanda.

Hasira haiwezi kuisha ikiwa kuna mawazo ya chuki katika moyo. Hasira itakwisha mara tu mawazo ya chuki yatakapo sahaulika. Kama paa ya nyumba imetengenezwa vibaya mvua itapenyeza hadi ndani; hivyo choyo hupenya ndani ya moyo ambao haukufunzwa vizuri.

Kuwa mvivu ni barabara fupi ya kuelekea kifoni na kuwa na bidii ni njia ya uzima; watu wajinga ni wavivu, watu wenye busara ni watendaji.

Mtengenezaji wa mishale hujitahidi kutengeneza mishale iliyonyooka vilevile mtu mwenye busara huweka moyo wake kwa unyoofu.

Moyo usumbukao hautulii kamwe; hurukaruka hapa na pale na ni vigumu kuutawala, lakini moyo wa starehe ni mtulivu; kwa hiyo ni busara kuutawala moyo.

Ni moyo wa mtu mwenyewe na wala siyo wa adui yake unaomshawishi mtu kumwelekeza kwenye njia za maovu.

Mtu auzuiaye moyo wake kutokana na choyo, hasira na ujinga ni yule aifurahiaye amani ya kweli na ya kudumu.

2. Kusema maneno mazuri bila ya kuonyesha matendo ni kama ua zuri lisilo na manukato.

Harufu nzuri ya ua haielei kupingana na upepo; lakini hasira ya mtu mwema huenda ikipingana na upepo katika dunia.

Usiku huonekana mrefu kwa mtu asiye na usingizi na safari huonekana ndefu kwa msafiri aliyechoka; kwa hiyo muda wa madanganyo na mateso huonekana mrefu kwa mtu asiyejua mafundisho sahihi.

Njia ya kufaidika kwa vitendo

Mtu awapo safarini yampasa kusafiri na rafiki yake mwenye moyo sawa na wake au mwenye moyo bora zaidi; heri mtu asafiriye peke yake kuliko kusafiri na mjinga.

Rafiki mwovu na asiye mwaminifu ni wa kuogofya kuliko mnyama pori. Mnyama pori anaweza kujeruhi mwili wako, lakini rafiki ataujeruhi moyo wako.

Ikiwa mtu hawezi kuutawala moyo wake ataridhikaje kwa kufikiria mawazo kama, " Huyu ni mwanangu" au " Hii ni hazina yangu?" Mtu mjinga huteswa na mawazo kama hayo.

Kuwa mjinga na mtu kutambua kuwa ni mjinga, ni bora kuliko kuwa kuwa mjinga na mtu kufikiria kuwa ana busara.

Kijiko hakiwezi kuwa na mwonjo wa chakula kinachokibeba. Hivyo, mjinga hawezi kuelewa hekima ya mtu mwenye busara hata kama atajihusisha na mtu mwenye hekima.

Maziwa mabichi hayagandi kwa urahisi, hivyo matendo maovu hayaleti matunda ya moja kwa moja. Matendo maovu ni kama makaa ya moto yaliyofichwa katika majivu na yakaendelea kufuka moshi na mwisho kutokea moto mkali.

Ni ujinga kwa mtu kutamani mapendeleo, kupandishwa cheo, faida au heshima kwa sababu tamaa kama hizo haziwezi kuleta furaha bali zitaleta mateso.

Rafiki mwema anayetangaza makosa na upungufu wa watu na kukemea maovu anapaswa kuheshimiwa kana kwamba amefichua siri ya hazina iliyofichwa.

3. Mtu anayefurahi anapopewa mafundisho mazuri atalala kwa amani, kwani kutokana nayo moyo wake umetakasika.

Fundi Seremala hujitahidi kunyosha mihimili yake; mtengeneza mishale hujitahidi kuitengeneza vizuri; mchimbaji mtalo wa maji hujitahidi kuutawala moyo wake ili ukafanye kazi kwa ufasaha na kweli.

Mwamba mkubwa hausumbuliwi na upepo; moyo wa mtu mwenye busara hausumbuliwi na heshima au bezo.

Kuiteka nafsi ni ushindi mkubwa kuliko kuteka maelfu ya watu katika uwanja wa vita.

Kuishi siku moja na kupokea mafundisho mazuri ni bora kuliko kuishi miaka mia moja bila ya kuyajua mafundisho hayo.

Wale wanaojiheshimu yawapasa kujichunga wasije wakaanguka tena katika tamaa mbaya. Katika wakati mmojawapo wa maisha yao; katika ujana, utu uzima au uzeeni yawapasa kuamsha imani zao.

Dunia daima inawaka moto, inawaka moto wa uchoyo, hasira na ujinga; mtu yeyote yule anapaswa kuwa huru kutokana na hatari hizi mapema iwezekanavyo.

Dunia ni kama povu, ni kama matando ya buibui, ni kama najisi katika mtungi mchafu; yampasa mtu kujitahidi kila mara kulinda utakatifu wa moyo wake.

4. Kiini na asili ya mafundisho ya Buddha ni; kuepuka ubaya wowote, kutafuta wema, na kutunza moyo katika utakatifu; hiki ni kiini cha mafundisho ya Buddha.

Uvumilivu ni mojawapo kati ya taratibu ngumu lakini ni yule yule mvumilivu atakayepata ushindi.

Ni vema mtu kuondoa chuki anapojisikia kuchukizwa; ni vema kuondoa masikitiko anaposongwa na masikitiko; ni vema kuondoa uchoyo anapozama katika uchoyo. Ili kuishi maisha yasiyo na uchoyo yampasa mtu asijihesabie lolote katika mali yake.

Kuwa na afya njema ni faida kubwa; kutosheka na kile mtu alichonacho ni bora kuliko kuwa na utajiri mkubwa, kuwa wa kuaminika ni alama ya kweli ya urafiki; kuupata Wongofu ni furaha ya hali ya juu.

Wakati mtu ana hisia ya kuchukia maovu, wakati mtu anajisikia huru, wakati mtu anaona furaha ya kusikiliza mafundisho mema, wakati mtu ana hisia hizi na kuzithamini, yeye hana woga tena.

Usifungamane na mambo uyapendayo; usiepukane na mambo uyachukiayo. Huzuni, woga na kufungamana vyote

hutokana na yale mtu anayoyapenda na asiyoyapenda.

5. Kutu inayoharibu chuma huota kwenye chuma chenyewe; vivyo hivyo ubaya huota ndani ya moyo wa binadamu na kumharibu.

Maandiko matakatifu yasiyosomwa kwa uaminifu hayakawii kufunikwa na vumbi; nyumba isiyopata ukarabati wakati inahitaji matengenezo itaharibika na kuchafuka; vivyo hivyo mtu mvivu hakawii kunajisika.

Matendo mabaya humnajisi mtu; ubahili hunajisi matoleo; kwa hiyo matendo maovu hunajisi siyo tu maisha ya sasa bali hata maisha yajayo.

Lakini najisi iliyo mbaya zaidi ni najisi inayotokana na ujinga. Binadamu hawezi kutumaini kutakatisha mwili wake au moyo wake hadi atakapoondokana na ujinga.

Ni rahisi kuangukia kwenye upungufu, kuwa fadhili na jasiri kama kunguru, kuwaumiza watu wengine bila kuwa na fikra ya majuto.

Ni vigumu mno mtu kuwa mnyenyekevu, kuijua heshima na tahadhima, kuepukana na mapendo, kuwa mtakatifu katika mawazo na matendo na kuwa na busara.

Ni rahisi kuyaona matendo ya watu wengine bali ni

vigumu kukubali makosa yako. Binadamu hutangaza madhambi ya watu wengine bila kujali, lakini huficha dhambi zake kama mcheza kamali anavyoficha dadu yake ya ziada.

Anga haionyeshi nyayo za ndege, moshi au dhoruba; Mafundisho maovu hayana Uongofu ndani yake; hakuna kitu chochote katika ulimwengu huu ambacho ni imara; bali moyo wa Uongofu hauteteleki.

6. Kama askari alindavyo lango la ngome yake, ndivyo mtu impasavyo kulinda moyo wake kutokana na hatari za ndani na hatari za nje; mtu asisahau hilo hata kidogo.

Kila mtu anajitawala; ni chemichemi anayoweza kutegemea; kwa hiyo kila mmoja ajitawale mwenyewe.

Hatua za kwanza kuelekea kwenye uhuru wa kiroho kutoka kwenye pingu na vifungu vya dunia ni kutawala moyo, kuacha maneno yasiyo na maana na kuwa na mawazo ya kadri.

Jua huangaza, mchana mbalamwezi huufanya usiku upendeze, nidhamu hukuza heshima ya mpiganaji hivyo kutabaruku kimya kimya hubainisha mtafutaji wa Nuru/ Uongofu.

Yule asiyeweza kulinda na kutawala milango mitano ya fahamu za macho, masikio, pua, ulimi na mwili, na anajaribiwa na mazingira yake si mmojawapo wa watu wanaoweza kujifunza

kuushika Uongofu. Yule anayechunga vizuri malango ya njia kuu za fahamu na kuutawala moyo wake ndiye atakayefaulu kushika Nuru.

7. Mtu anayeshawishiwa na mapenzi yake na machukizo yake hawezi kuelewa kwa ufasaha umuhimu wa neema na huelekea kutekwa; yule asiyetawaliwa na mapendo anaelewa kwa uhakika neema na kwake vitu vyote vinakuwa vipya na vya maana.

Furaha hufuatwa na huzuni, huzuni hufuatwa na furaha lakini mtu anaposhindwa kutofautisha furaha na huzuni, tendo bora na tendo baya huyo ana uwezo wa kuupata uhuru.

Kuwa na wasiwasi katika matumaini au kuyahifadhi masikitiko ya wakati uliopita ni sawa na matete yaliyokatwa na kunyauka.

Siri ya afya ya mwili na moyo siyo ya kuomboleza kwa ajili ya nyakati zilizopita. Siyo kuwa na wasiwasi na mambo ya baadaye au kutarajia matatizo bali kuishi kwa busara na juhudi katika wakati uliopo.

Msihangaikie yaliyopita wala kuota yajayo bali tuliza moyo katika wakati uliopo.

Ni vema kufanya kazi iliyopo sasa kwa ukamilifu bila kushindwa; msihangaike kuikwepa au kuihairisha kazi hiyo hadi kesho. Utaweza kuishi maisha mema leo kwa kutenda sasa.

Njia ya kufaidika kwa vitendo

Hekima ni kiongozi bora na imani ni mwenzi mwema. Ni lazima mtu alikimbie giza la ujinga na mateso na autafute mwanga wa U-ongofu.

Ikiwa mwili na moyo wa binadamu vimesimamiwa barabara, yampasa mtu atoe ushuhuda kwa matendo yake maadilifu. Hii ni kazi takatifu. Imani ndipo itakapokuwa utajiri wake, ukweli utayapa ladha nzuri maisha yake, na kukusanya maadili litakuwa jukumu lake takatifu.

Katika safari ya maisha imani ni chakula, matendo ya uadilifu ni hifadhi, hekima ni mwanga wa mchana na uangalifu wa kweli ni kinga wakati wa usiku. Mtu akiishi maisha matakatifu hawezi kuharibiwa na kitu chochote; ikiwa ameuteka uchoyo uhuru wake hauwezi kuwa na kizuizi cho chote.

Yampasa mtu kusahau nafsi yake kwa ajili ya familia yake; yampasa mtu kusahau familia yake kwa ajili ya kijiji chake; yampasa mtu kusahau kijiji chake kwa ajili ya taifa; na yampasa mtu kusahau kila kitu kwa ajili ya Uongofu.

Kila kitu hubadilika, kila kitu huwepo na kutoweka; hakuna amani na kikomo hadi mtu avukapo mipaka ya maumivu makali ya maisha na kifo.

UNDUGU

SURA YA KWANZA

WAJIBU WA UDUGU

I
NDUGU WASIO NA MAKAO

1. Mtu anayetaka kuwa mwanafunzi wangu yampasa awe tayari kuacha mahusiano na familia yake, awe tayari kuacha maisha ya starehe za kidunia na kutegemea mambo yote ya utajiri.

Mtu aliyeacha mausiano hayo yote kwa ajili ya Dharma na hana mahali pa kuishi kwa ajili ya mwili au moyo wake amekuwa mwanafunzi wangu na ataitwa ndugu asiye na makazi.

Ingawa miguu yake huacha chapa yake katika nyayo zangu na mikono yake hubeba vazi langu, ikiwa moyo wake unasumbuliwa na choyo, huyo yupo mbali na mimi. Ingawa anavaa kama mtawa, iwapo hawezi kuyapokea mafundisho hayo hanioni.

Lakini ikiwa ameondoa choyo yote na moyo wake ni wenye amani na ni mtakatifu, yu karibu nami hata kama yupo maelfu ya maili kutoka kwangu. Akipokea Dharma ataniona ndani mwake.

2. Wanafunzi wangu, ndugu wasio na makao ni lazima watii sheria nne na wajenge maisha yao juu yake.

Kwanza wanavaa matambara, pili wanapata chakula chao kwa kuomba omba; tatu makao yao ni popote pale usiku unapowakuta kama vile chini ya mti au juu ya mwamba; na nne, wanatumia dawa maalum iliyotengenezwa kwa mkojo uliowekwa na undugu.

Kubeba bakuli mkononi na kutembea kutoka nyumba moja hadi nyingine, ndiyo maisha ya ombaomba, lakini ndugu halazimishwi na wenzake kufanya hivyo, halazimishwi na hali ya mambo au kwa majaribu; anafanya hivyo kwa utashi wake mwenyewe kwa sababu anajua kuwa maisha ya imani yatamwepusha na madanganyo ya maisha, yatamsaidia kuepukana na maumivu, na yatamwelekeza kwenye Uongofu.

Maisha ya ndugu asiye na makao siyo rahisi; hana sababu ya kuyafuata kama hawezi kuumiliki moyo wake au milango yake mitano ya fahamu.

3. Anayejiamini kuwa ndugu asiye na makao na kuweza kujibu anapoulizwa juu yake awe tayari kusema:

" Nipo tayari kutenda jambo lolote lililo la lazima ili kuwa ndugu asiye na makao. Nitakuwa mkweli na nitajaribu kutimiza madhumuni ya kuwa ndugu asiye na kwake. Nitawashukuru wale wote wanipao misaada na nitajaribu kuwafurahisha kwa bidii ya moyo wangu na maisha yangu mema."

Ili kuwa ndugu asiyekuwa na makazi ni lazima ajifunze njia

nyingi, awe mwepesi kuona aibu na dharau anaposhindwa, aweke mwili wake, kauli na moyo wake mtakatifu ikiwa moyo wake utakuwa mtakatifu; ni lazima alinde milango yake mitano ya fahamu, asipoteze uwezo wa kuutawala moyo wake kwa sababu ya furaha ya muda; asijisifu wala kuwakemea wengine na asiwe mvivu au mpenda usingizi mnono.

Mnamo saa za jioni inabidi awe na muda wa kukaa na kutafakuri na kufanya matembezi mafupi kabla ya kulala. Ili kupata usingizi mtulivu ni lazima alalie upande wa kulia na aweke miguu yake pamoja, na wazo lake la mwisho liwe juu ya ya muda anaokusudia kuamka kesho yake asubuhi na mapema. Asubuhi na mapema inabidi awe na muda mwingine wa kukaa na kutabaruku na baadaye afanye matembezi mafupi.

Siku nzima inambidi adumishe moyo mkakamavu, akiutawala mwili na moyo, akipinga vishawishi vya choyo, hasira, usingizi, kutokujali majuto, shutuma na tamaa zote za kidunia.

Kwa hiyo, akili yake ikiwa imetulia, itampasa apalilie hekima na akusudie kupata Wongofu wa hakika.

4. Ikiwa ndugu asiye na makazi, atajisahau na kunywea katika choyo, hasira, chuki, wivu, majivuno, kujitukuza au kutokuwa mwaminifu ni sawa na mtu anayebeba jambia kali lenye makali pande zote lakini limefunikwa kwa kitambaa chepesi.

Huyo si ndugu asiye na makazi kwa kuwa anavao mavazi ya

kitawa, na anabeba bakuli la ombaomba; huyo si ndugu asiye na kwake kwa sababu tu ananena maandiko kwa urahisi, huyo ni mtu tu anayetapatapa wala hakuna la ziada.

Hata kama sura yake ya nje ni ya mtawa hawezi kuondokana na tamaa za kidunia. Yeye si ndugu asiye na makazi, hazidiani na mtoto mchanga aliyevishwa nguo za mtawa.

Wale wanaoweza kutuliza na kutawala moyo; waliojaa hekima, walioondokana na tamaa za dunia na ambao madhumuni yao ni kuupata Wongofu tu ni hao tu wanaoweza kuitwa ndugu wasio na makazi.

Ndugu wa kweli asiye na makao anaazimia kufikiria lengo lake la Wongofu hata kama atamwaga damu yake yote na mifupa yake kuvunjikavunjika na kusagika. Mtu anayejitahidi namna hiyo, hatimaye atafikia lengo lake na kutoa ushuhuda juu yake kwa kutenda matendo yenye sifa ya ndugu asiye na makao.

5. Kazi ya ndugu asiye na makao ni kueneza mwanga wa mafundisho ya Buddha. Yampasa ahubiri kila mtu, awaamshe waliolala, asahihishe mawazo batili; hana budi kuwasaidia watu wawe na mtizamo sahihi, aende kila mahali akieneza mafundisho ya Buddha bila kujali maisha yake.

Kazi ya ndugu asiye na makao ni ngumu, kwa hiyo anayeitamani hana budi kuvaa nguo za Buddha, akalie kiti cha Buddha na kuingia katika chumba cha Buddha.

Kuvaa nguo za Buddha ina maana ya kuwa mnyenyekevu na kuwa mvumilivu, kukalia kiti cha Buddha ina maana ya kuona jambo na kulidharau kama siyo kitu chochote na kutokuwa na uhusiano na mambo, kuingia katika chumba cha Buddha yamaanisha kushiriki katika huruma kuu ya Buddha na kuwa na huruma kwa kila mtu.

6. Wale wanaohitaji kufundisha mafundisho ya Buddha kwa hiari lazima wajishughulishe na mambo manne:- Kwanza wahusike na tabia zao; pili lazima wayaangalie maneno wachaguayo wanapowaendea na kuwafundisha watu; wajihusishe na nia zao za kufundisha na kutimiza lengo la mafundisho hayo na nne hawana budi kujihusisha na huruma kuu.

Kwanza, ili kuwa mwalimu mzuri wa Dharma, ndugu asiye na makao yampasa kusimama imara kwenye uwanja wa uvumulivu, lazima awe na uadilifu, asiwe na majivuno na asitamani sifa; yambidi mara kwa mara afikirie upuuzi wa vitu; Asijishikamanishe na jambo lo lote. Iwapo atawajibika ipasavyo bila shaka atakuwa na tabia itakiwayo.

Pili yambidi awe Mwangalifu anapowaendea watu au hali. Yampasa aepuke watu wenye maisha mabaya au watu wenye madaraka; ni lazima awaepuke watu wa jinsia tofauti.

Tena, yambidi awaendee watu kwa upole na wema; hana budi kila mara kukumbuka kuwa vitu hutokana na mafumbato ya chanzo na hali, na akiwa na msimamo huo asiwalaumu watu wala

kuwasuta au kuwaseng'enya, au kuwadharau.

Tatu, yambidi awe na moyo mtulivu, akimwona Buddha kama baba yake wa kiroho, awaone ndugu wengine wasio na makao wanaofuata Nuru kama walimu wake na amwangalie kila mmoja kwa moyo wa huruma. Kisha awafundishe wote bila ubaguzi.

Nne, adhihirishe roho yake ya huruma kwa wote kama alivyofanya Buddha. Hasa hasa ajitahidi roho yake ya huruma iwafikie watu wasiokuwa na habari za Wongofu. Awatakie heri nao watafute Wongofu pia naye ayafuatilie matakwa yake akijipa moyo kwa nguvu zote zimwezeshe kuamsha ari yao.

II
WAFUASI WA ULEI

1. Imekwishaelezwa kwamba ili kuwa mwanafunzi wa Buddha yampasa mtu aamini katika hazina tatu; Buddha, Dharma na Samgha.

Kuwa mfuasi wa ulei mtu inamlazimu awe na imani isiyotingishika katika Buddha, ayaamini mafundisho yake, ajifunze na kuyaweka mafundisho katika matendo na kuulinda udugu.

Wafuasi wa ulei yawapasa kufuata mafundisho matano:-

kutoua, kutoiba, kutozini, kutosema uwongo au fitina, kutotumia vileo.

Wafuasi wa ulei wasiamini tu katika hazina tatu na kuyashika mafundisho, bali kwa kadri ya uwezo wao wawasaidie watu wengine kuyatafakari mafundisho haya, hasa hasa ndugu na marafiki zao; wakijitahidi kuamsha imani isiyotingishika ya Buddha ndani mwao na Dharma na Samgha, ili nao washiriki kugawiwa huruma ya Buddha.

Wafuasi wa ulei yawapasa daima kukumbuka kuwa sababu yao kuamini katika hazina tatu na kuyatunza mafundisho ni kuwawezesha hatimaye kuupata Uongofu, na kwa sababu hiyo na ingawa wanaishi katika dunia ya madanganyo yawapasa kujizuia kujihusisha na madanganyo hayo.

Wafuasi wa ulei wanapaswa kuweka maanani kuwa ni kitambo kidogo tu kijacho watapaswa kuwaacha wazazi wao na familia zao na kutupilia mbali maisha haya ya kuzaliwa na kufa; kwa hiyo wasijihusishe na vitu vya maisha haya bali waelekeze mioyo yao katika dunia ya Nuru ambamo kwayo hakuna kitu kipoteacho.

2. Endapo wafuasi wa ulei watataka kuamsha imani ya kweli katika mafundisho ya Buddha inabidi ndani ya mioyo yao wajenge furaha iliyo makini itakayo-ng'ara katika mazingira yao na nuru yake kuakisiwa kwao tena.

Moyo huu wa imani ni safi na mtaratibu, daima ni wa kusubiri na kuvumilia, kamwe hauna mabishano, kamwe hausababishi mateso kwa wengine lakini kila wakati unazifikiria zile hazina tatu: Buddha, Dharma na Samgha. Hivyo basi furaha hufunuliwa na kukua katika mioyo yao, na mwanga wa Nuru, unaweza kupatikana kila mahali.

Kwa vile wametulia katika himaya ya Buddha kwa imani, basi wametenganishwa mbali na moyo wa uchoyo, mbali na kufumbatanishwa na mali zao, na, kwa hiyo hawana woga katika maisha yao ya kila siku wala hawatishiki kwa kusutwa.

Hawataogopa kifo kitakachowajia kwa kuwa wanaamini kuzaliwa kwenye Nchi ya Buddha. Kwa kuwa wanaamini katika ukweli na utakatifu wa mafundisho, wote wanaweza kujieleza kwa uhuru bila hofu.

Kwa kuwa mioyo yao imejaa huruma kwa watu wote, hawatakuwa na tofauti kati yao bali watatendeana wema sawa, na kwa kuwa mioyo yao iko huru kutokana na mapenzi na machukizo, itakuwa safi, adilifu na yenye furaha kwa kutenda jambo lolote zuri.

Kama wanaishi kwa dhiki au kwa neema haileti tofauti yoyote katika kuongeza imani yao. Ikiwa watahifadhi uvumilivu, ikiwa watayaheshimu mafundisho ya Buddha, kama ni waangalifu katika mazungumzo na matendo, ikiwa mioyo iko imara kama milima, basi watatembea salama na kwa uhakika katika njia ya

Nuru.

Na ingawa wanalazimika kuishi katika hali ngumu na kati ya watu wenye mioyo michafu, iwapo wataweka imani yao katika Buddha daima watazidi kuwaongoza wenzao kwenye matendo mema.

3. Kwa hiyo, mtu yambidi kwanza awe na hamu ya kusikiliza mafundisho ya Buddha.

Ikiwa mtu yeyote atamweleza kuwa itakuwa lazima kupitia kwenye moto ili kuipata nuru, basi awe radhi kupita kwenye moto huo.

Kuna kutosheka katika kulisikia jina la Buddha ambako kuna thamani zaidi ya kupita katika dunia iliyojaa mioto kama hiyo.

Kama mtu ana nia ya kufuata mafundisho ya Buddha yampasa asijipende nafsi yake, au kuwa kaidi, lakini alinde hisia ya nia njema kwa watu wote; mtu awaheshimu wote wanaostahili heshima, awahudumie wanaostahili huduma na kutenda wema sawa kwa kila mtu.

Hivyo basi wafuasi wa ulei yawabidi kuandaa mioyo yao kabla ili wasibughudhiwe na matendo ya wengine. Katika hali hii watapokea mafundisho ya Buddha na wayashike na kuyafanyia kazi bila ya kuwaonea kijicho wengine, bila ya kushawishiwa na

wengine na bila kuwazia njia nyinginezo.

Wale wasioamini mafundisho ya Buddha wana mtizamo finyu, na kwa sababu hiyo wana mioyo isiyotulia. Lakini wale wanaoyaamini mafundisho ya Buddha wanaamini kwamba kuna hekima kuu na huruma kuu ikumbatiayo kila kitu na katika imani hiyo hawasumbuliwi na vitu visivyo na thamani.

4. Wale wanaoyasikia na kuyapokea mafundisho ya Buddha wanajua kwamba maisha yao ni ya kupita na kuwa miili yao ni mkusanyiko wa mateso na chanzo cha maovu yote, na hivyo basi hawajihusishi navyo.

Wakati uleule hawaachi kuitunza miili yao; Sio kwa sababu ya kufurahia anasa za mwili, lakini kwa sababu mwili unahitajika kwa muda tu ili waweze kupata hekima na kuwawezesha wawe mitume wa kuielezea njia kwa watu wengine.

Ikiwa watashindwa kuitunza miili yao wataishi maisha mafupi. Kama hawataishi maisha marefu hawatayatendea kazi mafundisho hayo wao wenyewe au kuyaeneza kwa watu wengine.

Ikiwa mtu anataka kuvuka mto anachunga sana chelezo chake, ikiwa ana safari ya mbali anamwangalia sana farasi wake. Vivi hivi, ikiwa mtu anataka kuipata Nuru ni lazima autunze mwili wake.

Wajibu wa udugu

Wanafunzi wa Buddha hawana budi kuvaa nguo kwa ajili ya kuikinga miili yao kwa joto kali na baridi kali na kusetiri sehemu zao za siri na wasivae nguo kwa sababu ya kujipamba.

Yawabidi kula chakula kwa ajili ya miili yao ili wapate uwezo wa kusikia, kupokea na kuelezea mafundisho, lakini wasile chakula kwa ajili ya starehe tu.

Inabidi waishi katika nyumba ya Nuru, ili walindwe kutokana na wezi wa mateso ya duniani na kutokana na mawimbi ya mafundisho mabaya, na waitumie nyumba hiyo kwa madhumuni halisi siyo kwa maonyesho au maficho ya matendo ya uchoyo.

Hivyo, mtu ni lazima athamini vitu na avitumie tu kwa uhusiano wake na Nuru na mafundisho. Asivimiliki au kijihusisha navyo kwa sababu za uchoyo ila kwa kuwa tu vinatimiza dhumuni ya kupeleka mafundisho kwa wengine.

Kwa hiyo, mawazo yake yahusike na mafundisho hata kama yupo pamoja na familia yake. Awatunze wenzake kwa moyo wa busara na huruma,akitafuta njia mbalimbali za kuamsha imani katika mioyo yao.

5. Wana ulei wa Samgha ya Buddha inawapasa kila siku kujifunza masomo yafuatayo: jinsi ya kuwahudumia wazazi wao, jinsi ya kuishi na wake zao na watoto, jinsi ya kujizuia na kujilinda na namna ya kumtumikia Buddha.

Ili kuwahudumuia wazazi ni lazima wajifunze kutenda wema kwa viumbe vyote vyenye uhai. Ili kuishi kwa furaha na wake zao na watoto wao ni lazima waepuke tamaa na mawazo ya starehe za uchoyo.

Wakiwa wanausikiliza muziki mzuri wa maisha ya familia wasisahau muziki mtamu sana wa mafundisho, na wakati wanaishi katika himaya ya nyumba, wajitahidi kila mara kutafuta himaya salama ya matendo ya zen, mahali ambapo watu wenye busara hupata hifadhi kuepukana na uchafu na masumbuko.

Walei wanapotoa sadaka yawapasa kuondoa choyo yote katika roho zao: wakiwa katikati ya umati, mawazo yao yawe karibu na watu wenye busara; wanapopatwa na mikasa, hawana budi kutuliza mioyo yao kwa furaha na kuiweka mbali na vipingamizi.

Wanapopata kimbilio katika Buddha yawabidi kutafuta hekima yake.

Wanapopata hifadhi katika Dharma, ni lazima waufuate ukweli wake ambao ni kama bahari ya hekima.

Wanapopata hifadhi katika Samgha, ni lazima wautafute ushirika usio na ghasia inayozuiwa na matakwa ya uchoyo.

Wanapovaa nguo, wasisahau pia kuvaa vazi la wema na unyenyekevu.

Wajibu wa udugu

Wanapotaka kujifariji, ni lazima wanuie kabisa kutupilia mbali choyo, hasira na ujinga kutoka katika mioyo yao.

Wanapofanya kazi ngumu kwenye barabara ielekeayo mlimani waifikirie kama njia ya Uongofu ambayo itawavusha ng'ambo ya dunia ya madanganyo. Wanapofuata barabara nyepesi na rahisi inawapasa watumie bahati ya unafuu wake ili kuleta maendeleo makubwa katika U-Buddha.

Wanapoliona daraja ni lazima watamani kulijenga daraja la mafundisho ili kuwapa fursa watu kulivuka.

Wanapokutana na mtu mwenye masikitiko, yawabidi kusikitikia uchungu wa dunia hii inayobadilikabadilika.

Wamwonapo mtu mchoyo, wawe na hamu kubwa ya kuwa huru kuepukana na madanganyo ya maisha haya na kupata utajiri wa kweli wa Nuru.

Waonapo chakula kitamu, wawe macho; waonapo chakula kibaya yawabidi kutamani choyo isije tena.

Wakati wa joto kali la majira ya kiangazi, ni lazima watamani kuwa mbali na joto la tamaa za kidunia na kupata ubaridi safi wa Uongofu wakati wa baridi kali isiyovumilika ya masika hawana budi kufikiria joto la huruma iliyoko ndani ya Buddha.

Wanaponena maandiko matakatifu yawabidi wawe wameamua kutoyasahau na wadhamirie kuyaweka katika vitendo.

Wanapofikiria Buddha, yawabidi kuchunga takwa lao kuu la kuwa na macho kama Buddha.

Pindi walalapo usingizi wa usiku, watamani miili yao, maneno na mioyo yao itakaswe na kuchangamshwa; wanapoamka asubuhi , ombi lao liwe kuwa katika siku nzima mioyo yao iwe myepesi kuelewa vitu vyote.

6. Wale wanaofuata mafundisho ya Buddha kwa sababu wanaelewa kuwa kila kitu kina sifa ya "kutokuwa na asili", hawadharau vitu vinginevyo katika maisha ya binadamu, ila huvipokea kwa jinsi vilivyo na kisha hujaribu kuvifanya viwe zana sahihi za Nuru.

Wasifikirie kuwa dunia hii haina maana yoyote na imejaa machafuko, wakati ukweli ni kwamba dunia ya Wongofu imejaa maana na Heri. Bali waonje njia ya Wongofu katika mambo yote ya dunia hii.

Mtu anapouangalia ulimwengu kwa macho machafu yaliyochanganyikana na ujinga atauona umejaa makosa, lakini akiuangalia kwa hekima sahihi, atauona kama ulimwengu wa Nuru, ambao ndio ukweli wake.

Wajibu wa udugu

Ukweli ni kwamba kuna dunia moja tu wala siyo mbili, moja isiyo na maana na ya pili yenye maana au moja nzuri nyingine mbaya. Watu hufikiria tu kwamba kuna dunia mbili, kutokana na ubaguzi wa akili yao.

Iwapo wangeondokana na ubaguzi huo pamoja na kutunza na kuweka mioyo yao safi kwa mwanga wa hekima, basi wangeiona dunia moja ambayo kwayo kila kitu kina maana.

7. Wale wanaomwamini Buddha huonja utakatifu huu wa umoja wa ulimwengu wote katika kila kitu, katika hali hiyo huona huruma kwa wote na huwa na uelekeo wa kumhudumia kila mmoja.

Kwa hiyo, inawabidi waisafishe mioyo yao kuondoa kiburi na kulinda unyenyekevu, ukarimu na huduma. Mioyo yao iwe kama ardhi yenye faida irutubishayo kila kitu bila upendeleo, itoayo huduma bila kinyongo, yenye shauku kila siku, ambayo hupata furaha kuu kwa kuwahudumia maskini wote kwa kupandikiza mafundisho ya Buddha ndani ya mioyo yao.

Hivyo basi, moyo wenye huruma kwa maskini huwa mama kwa watu wote, huwaheshimu watu wote, watu wote huwaona kama marafiki, na huwaheshimu kama wazazi.

Kwa hiyo, ingawa maelfu ya watu wanaweza kuwa na mawazo magumu na kukuza chuki kwa walei wamfuatao Buddha, hawawezi kuwadhuru, kwani madhara kama hayo ni sawa na

tone la sumu katika maji ya bahari kuu.

8. Mfuasi wa ulei atapendezwa na furaha yake kwa tabia za kukumbuka, kufikiri na kushukuru. Atatambua kuwa imani yake ni huruma ya Buddha na kwamba ameipata kutoka kwake Buddha.

Hakuna mbegu za imani katika tope la dunia ya mateso, lakini kwa ajili ya huruma ya Buddha, mbegu za imani zinaweza kupandwa na zitasafisha moyo hadi utakapokuwa na imani katika Buddha.

Kama ilivyokwisha semwa, mti wa chandana wenye harufu ya marashi hauwezi kuota katika msitu wa miti ya Eranda. Vilevile mbegu za imani katika Buddha haziwezi kuwa katika kifua cha madanganyo.

Lakini, hasa ua la furaha linachanua huko,hivyo ni lazima tuhitimishe kuwa wakati maua yake yapo katika kifua cha madanganyo, mizizi yake iko mahali pengine; hasa katika kifua cha Buddha.

Ikiwa mfuasi wa ulei atajipenda nafsi yake; atakuwa na kijicho, husuda, chuki na uharibifu kwa sababu moyo wake umechafuliwa na choyo, hasira na ujinga. Lakini kama atarudi kwa Buddha; atapata hata huduma kubwa ya Buddha kama ilivyotajwa hapo juu. Kwa hakika, haiwezi kuelezeka.

SURA YA PILI

MWONGOZO WA KUISHI KWA VITENDO

I
MAISHA YA FAMILIA

1. Ni makosa kufikiri kuwa balaa hutokea Mashariki au Magharibi; hutoka ndani ya moyo wa mtu mwenyewe. Kwa hiyo ni ujinga kuzuia balaa kutokea katika dunia ya nje na kuacha undani wa moyo bila kusimamiwa na kutawaliwa.

Kuna desturi ambayo imerithiwa toka zamani sana ambayo watu wa kawaida bado wanaifuata. Wanapoamka asubuhi, kwanza huosha nyuso zao na kusafisha midomo yao, kisha husalimu kwa kuinamia pande sita - Mashariki, Magharibi, Kusini, Kaskazini, juu na chini - wakiomba kuwa balaa yoyote isiwafikie kutoka upande wote na pia wawe na siku njema.

Lakini ni tofauti katika mafundisho ya Buddha. Yeye hufundisha kuwa inatubidi kutoa heshima kwa pande sita za ukweli na pia kuwa inatubidi kufanya mambo kwa busara na uadilifu na hivyo kuzuia balaa zote.

Ili kulinda milango ya pande hizi sita, watu watapaswa kuondoa uchafu wa "matendo manne, " kutawala na kulinda" mioyo minne michafu, " na kuziba "mashimo sita " ambayo husababisha upoteaji wa utajiri.

Kwa "matendo manne" humaanisha kuiba, kuua, uzinzi na uongo.

" Mioyo michafu minne" ni choyo, hasira, ujinga na woga.

"Mashimo sita" yanayosababisha upoteaji wa utajiri ni tamaa ya pombe na kuishi kijinga, kutolala mapema na kupoteza moyo katika upuuzi, kujishughulisha na mambo ya muziki na starehe, kucheza kamali, kushirikiana na marafiki wabaya na kukwepa wajibu.

Baada ya kuondoa najisi hizi nne, kuepukana na hali hizi nne za uovu wa moyo, na kuziba mashimo sita ya takataka, mitume wa Buddha huzicha pande sita za kweli.

Sasa ni zipi pande sita za ukweli? Nazo ni; Mashariki ni njia ya wazazi na mtoto, kusini ni njia ya mwalimu na mwanafunzi; Magharibi ni kwa njia ya mtu na rafiki yake, chini kwa ajili ya bwana na mtumishi na juu ni njia ya wanafunzi wa Buddha.

Mtoto anapaswa kuwaheshimu wazazi wake na kuwatendea yote yampasayo. Hana budi kuwahudumia, kuwasaidia katika kazi zao, kulinda ukoo wa familia, kulinda mali ya familia na kufanya ibada za kumbukumbu baada ya kifo chao.

Wazazi wawafanyie watoto wao mambo matano yafuatayo:- Waepuke kutenda mabaya, wawe mfano wa matendo mema, wawapatie elimu, wawafanyie mipango ya kuwaoza na

kuwapa fursa ya kurithi mali za familia katika wakati unaofaa. Ikiwa wazazi na mtoto watafuata masharti haya familia itaishi kwa amani kila wakati.

Mwanafunzi yambidi kusimama wakati mwalimu wake anapoingia, amtegemee, afuate mafundisho yake vizuri na amkumbuke katika kumpa sadaka, na kusikiliza mafundisho yake kwa makini.

Wakati uleule mwalimu yampasa kutenda matendo ya haki ili awe mfano mwema kwa mwanafunzi wake; amfundishe vizuri elimu aliyojifunza; yampasa atumie njia nzuri na amwandae kwa ufanisi wa hali ya juu; asisahau kumtunza mtoto kutokana na mabaya kwa njia yoyote ile. Ikiwa mwalimu na mwanafunzi wake wanashika masharti haya uhusiano wao utakuwa mzuri sana.

Mwanamme amheshimu, amkarimu na amwamini mke wake. Amkabidhi shughuli za utunzaji nyumba mkewe na kumpatia mahitaji yake pamoja na ziada. Vile vile, mke achukue jukumu la nyumba awachunge wafanyakazi wake kwa busara, alinde maadili mema kama atendavyo mke mwema. Asipoteze kipato cha mme bali aitunze nyumba kwa utaratibu na uaminifu. Ikiwa masharti haya yatafuatwa kutakuwa na nyumba yenye furaha isiyokuwa na ugomvi.

Masharti ya urafiki yana maana kuwa yapasa kuwepo upendo kati ya marafiki, kila mmoja akampatia mwenzie kile anachokikosa na kwa njia hiyo wakijaribu kusaidiana kwa

maneno matamu na ya kweli.

Mtu amsaidie rafiki yake asianguke katika njia mbaya, alinde mali na utajiri wake na amsaidie katika matatizo yake. Ikiwa rafiki yake amepatwa na mkasa inabidi ampe msaada yeye pamoja na familia yake kama italazimu. Kwa njia hiyo wataendelea kuishi kwa furaha na urafiki wao utadumishwa.

Bwana anapomshughulikia mtumishi wake azingatie mambo matano. Ampe kazi kulingana na uwezo wake; ampatie fidia anayostahili; ampe huduma anapokuwa mgonjwa, amgawie vitu vizuri na ampe mapumziko anayostahili.

Mtumishi naye lazima azingatie mambo matano. Awe wa kwanza kuamka na wa mwisho kulala, awe mwaminifu, afanye kazi yake kwa bidii na uangalifu na ajitahidi kutovunja heshima ya bwana wake. Iwapo kanuni hizi zitafuatwa amani itakuwepo na hapatakuwepo na migongano kati ya bwana na mtumishi wake.

Mwanafunzi wa Buddha hana budi kuhakikisha kuwa familia yake inayafuata mafundisho ya Buddha. Inawapasa wanafunzi wa Buddha kulinda heshima na fikira juu ya mwalimu wao wa u-Buddha, ni lazima wamkarimu, wafuate na kushika mafundisho yake huku wakimtolea sadaka.

Tena mwalimu wa mafundisho ya Buddha hana budi kuyaelewa fika mafundisho, akizikataa tafsiri potofu, akisisitiza wema na akijitahidi kuwaongoza waumini katika njia nyoofu.

Mwongozo wa kuishi kwa vitendo

Kwa maana familia inayofuata njia hii ikaweka maanani msingi wa mafunzo ya kweli itaishi kwa furaha.

Mwanamme anayesujudia pande sita hafanyi hivyo kwa nia ya kuepuka balaa za nje. Anafanya hivyo akiwa imara kuzuia maovu yasichipuke kutoka ndani ya moyo wake.

2. Binadamu hana budi kubainisha kati ya marafiki wake, wapi wa kuhusiana nao na wapi wa kutohusiana nao.

Wale wanaopaswa kuepukwa ni wachoyo, wajanja na wadanganyifu.

Wale anaoweza kushirikiana nao ni wale wanaoweza kumsaidia, waliotayari kuwa pamoja katika furaha na huzuni, wanaotoa ushauri mzuri na wenye roho ya huruma.

Rafiki wa kweli, ambaye mtu anaweza kushirikiana naye kwa usalama, kila mara atafuata njia ya kweli, atajihusisha na kuwa na wasi wasi juu ya mambo ya rafiki yake, atamliwaza katika shida, atampatia msaada utakaohitajika, atamtunzia siri zake na atampa ushauri mzuri.

Siyo rahisi kumpata rafiki kama huyo, na kwa hiyo mtu yambidi ajaribu kuwa na rafiki wa namna hiyo. Kama jua linavyotia joto ardhi ndivyo rafiki mwema anavyong'ara katika jamii kutokana na matendo yake mema.

3. Itakuwa vigumu kwa mtoto kuwalipa wazazi wake kwa wema wao, hata kama angeweza kumbeba baba yake kwenye bega lake la kulia na mama yake kwenye bega la kushoto kwa muda wa miaka mia moja.

Na hata kama angewaoshea wazazi wake kwa manukato yanukiayo vizuri sana kwa muda wa miaka mia moja ili awe mfano wa mtoto mzuri, na awapatie anasa zote za dunia; hata hapo bado hawezi kuwalipa fadhila zao kulingana na zile walizomtendea kwa vyovyote vile.

Lakini awaongozapo wazazi wake kwa Buddha na kuwaeleza mafundisho ya Buddha, na kuwashawishi kuziacha njia mbaya na kufuata njia ya kweli, ili iwasaidie kuachana na choyo na kufurahia tabia ya kutoa sadaka, hapo atakuwa kama anawalipa zaidi na zaidi.

Baraka za Buddha hujaa katika nyumba ambamo wazazi wanapewa thamani na heshima.

4. Familia ni mahali ambapo mioyo inakutana. Ina maana kuwa mioyo ikipendana, nyumba itakuwa nzuri kama bustani ya maua. Ina maana kuwa mioyo ikifarakana huwa kama tufani iletayo uharibifu bustanini.

Panapotokea kutoelewana katika familia, mtu asiwalaumu wenzake bali auchunguze moyo wake na kufuata njia ya kweli.

5. Wakati fulani kulikuwa na mtu mwenye imani kubwa. Baba yake alifariki wakati yeye angali mdogo; aliishi vizuri sana na mama yake, baadaye akaoa mke.

Mwanzoni waliishi pamoja vizuri ila kutokana na tofauti ndogo iliyojitokeza mke na mama mkwe walitokea kutopendana. Machukio yalipozidi kati yao mama yao aliamua kuwaacha wanae na kuishi peke yake.

Baada ya mama mkwe kuondoka walimzaa mtoto wa kiume. Mama mkwe alipata tetesi kuwa mke wa mwanae amesema, " Mama mkwe wangu alikuwa ananiudhi na muda wote alipoishi nasi hakuna jema lolote lililotokea, na mara tu alipoondoka tukio hili jema limetokea".

Habari hizi zilimuudhi mama mkwe aliyepaliza sauti na kusema "Ikiwa mama wa mume amefukuzwa kwenye nyumba na tukio jema limetokea ndani ya nyumba, basi mambo yameingia katika mpito mwema. Uadilifu utakuwa umetoweka duniani."

Kisha mama huyo alipiga kelele akisema " sasa yatubidi tuwe na mazishi ya uadilifu huu", Kama mwanamke kichaa, alikwenda kufanya ibada ya mazishi makaburini.

Mzimu aliposikia tukio hili, alimtokea mwanamke huyo na akajitahidi kumshauri lakini ilishindikana.

" Ikiwa hivyo ndivyo ilivyo," mzimu alimwambia, " nitachoma moto mtoto na mama yake: Je hilo litakuridhisha?".

Kwa kusikia hivyo, mama mkwe aligundua kosa lake, akaomba samahani kwa hasira yake na akambembeleza mzimu kuokoa maisha ya mtoto na mama yake. Wakati ule ule mke wa mwanae na mume wake walitambua udhalimu wao kwa mama kizee na wakaenda makaburini kumtafuta. Mzimu aliwapatanisha na tangu siku hiyo walianza kuishi pamoja kwa furaha kifamilia.

Wema haupotei kamwe labda mtu mwenyewe autupilie mbali. Wema unaweza kuelekea kupotea mara kwa mara, lakini ukweli ni kwamba wema haupotei. Wema unapoelekea kupotea, ni kwa sababu mtu anapoteza uadilifu wa moyo wake.

Mawazo ya utengano na fitina mara nyingi huleta maafa. Kutoelewana kidogo tu kunaweza kuambatana na balaa kubwa. Hii hasa inapaswa kuepukwa katika maisha ya kifamilia.

6. Swali la namna ya kugharamia matumizi ya kila siku katika familia lahitaji uangalifu. Kila mmoja yampasa kufanya kazi kwa bidii kama mchwa na nyuki. Pasiwepo mtu anayeishi kwa kutegemea nguvu za wenzake, au kutumaini misaada yao.

Kwa upande mwingine mtu asifikirie kuwa pato analochuma ni lake peke yake. Sehemu nyingine itumike kwa ajili ya mahitaji ya jumuiya na taifa na sehemu nyingine itengwe kwa ajili ya mahitaji ya walimu wa dini.

Ni vema mtu kukumbuka kuwa hakuna kitu chochote katika dunia kinaweza kuitwa "changu" hasa. Anachokipata mtu anakipata kutokana na mchangamano wa hali na maumbile; anaweza kukitunza kwa muda, kwa hiyo asikitumie kwa uchoyo au kwa madhumuni mabaya.

7. Wakati Syamavati, mwandani wa Malkia wa mfalme Udayana, alipompatia Anada mavazi mia tano, Anada aliyapokea kwa furaha.

Mfalme aliposikia habari hiyo, alimtuhumu Anada kwa udanganyifu na hivyo alimwendea na kumhoji ni jinsi gani anaweza kuyatumia haya mavazi mia tano.

Anada alijibu: " Ah mfalme, ndugu zangu wengi wanavaa matambara nitayagawa mavazi haya kwao.

"Utafanya nini na mavazi yaliyochakaa?
" Tutatengeneza matandiko"
" Mtafanya nini na matandiko machakavu?"
" Tutatenganeza foronya".
" Mtafanyia nini foronya chakavu?"
" Tutatengenezea mazuria".
" Mtafanyia nini mazuria machakavu?"
" Tutatengenezea vitambaa vya kufutia miguu".
" Mtafanyia nini na vitambaa vya kufutia miguu vichakavu?"
" Tutatengenezea mifagio ya kusafisha sakafu".
" Mtafanyia nini mifagio ya sakafu michakavu?"

"Mtukufu, tutaichanachana vipande vipande navyo tutavichanganya na tope ili tukapige lipu kuta za nyumba.

Kila kifaa tulichokabidhiwa ni lazima tukitumie kwa uangalifu, kwa kuwa siyo chetu bali tumekabidhiwa kwa muda tu."

II
MAISHA YA WANAWAKE

1. Kuna aina nne za wanawake. Aina ya kwanza ni ya wale wakasirikao kutokana na kisa kidogo sana, wenye mioyo ibadilikayo, wenye choyo na wivu kwa furaha za wengine na wasiokuwa na huruma na mahitaji ya wenzao.

Aina ya pili ni ya wale wanaojenga hasira juu ya mambo hafifu, ambao ni vigeugeu na waroho lakini wasio na husuda kwa furaha za wenzao na wenye huruma juu ya mahitaji ya watu wengine.

Aina ya tatu ni ya wale wenye moyo wa usikivu na hawashikwi na hasira mara kwa mara, wanafahamu kutawala moyo wa tamaa lakini hawawezi kuepuka hisia za wivu na wasio kuwa na huruma juu ya mahitaji ya watu wengine.

Kundi la nne ni la wale walio wasikivu, wanaoweza kuzuia mawazo ya choyo na kuwa na moyo wa utulivu, wasioonea

kijicho furaha ya watu wengine na wenye huruma kwa mahitaji ya watu wengine.

2. Msichana anapoolewa inampasa aazimie mambo yafuatayo:- "Nitawaheshimu na kuwahudumia wazazi wa mume wangu. Wametupatia mafao yote tuliyonayo na ni walinzi wetu wa hekima, kwa hiyo sina budi niwatunze kwa shukrani na nitakuwa tayari kuwasaidia kila inapowezekana.

"Nitamheshimu mwalimu wa mume wangu kwa kuwa amempatia mume wangu mafunzo matakatifu na tusingeweza kuishi kama binadamu bila mwongozo wa mafundisho haya mema.

"Nitauandaa moyo wangu ili niweze kumwelewa mume wangu ili kuweza kumsaidia katika kazi zake. Sitaenda kinyume na yale apendeleayo kwa kudhani kuwa hayo ni mambo yake na siyo yangu.

"Nitaelewa asili, silika, uwezo na maonyo kwa huruma. Nitatunza mapato ya mme wangu bila ya kuyafuja kwa matumizi yangu yoyote ya binafsi yasiyo na maana.

3. Uhusiano wa mme na mke haukupangwa kwa maana tu ya wao kuwa pamoja. Uhusiano huu una umuhimu mkubwa zaidi ya miili miwili katika nyumba moja. Mume na mke ni lazima wafaidi undani wa uhusiano wao kwa kusaidiana kuifunza mioyo yao katika mafundisho matakatifu.

Wana unyumba uliokomaa, "unyumba hasa" kama walivyoitwa, siku moja walikwenda kwa Buddha na kumwambia, " Bwana, tulioana baada ya kukaa na kuelewana tangu utotoni na hapakuwahi kutokea wingu la dosari katika furaha yetu. Tafadhali twambie ikiwa tunaweza kuoana tena katika maisha ya baada ya kifo.
Buddha aliwapa jibu la busara - "endapo nyote mna imani sawa, ikiwa nyote mlikuwa wote mnatoa hisani inayolingana na kama mna hekima inayolingana, basi mtakuwa na moyo sawa katika uzao ujao.

4. Sujata, alikuwa mke mdogo wa mwana mkubwa wa tajiri mmoja, aitwaye Anathapindada, alikuwa na majivuno, hakuwaheshimu wenzake na hakuyasikiliza maelekezo ya mme wake na ya wazazi wake na kwa sababu hiyo ugomvi ulizuka katika familia hiyo.

Siku moja Aliyebarikiwa alikuja kumtembelea Anathapindada na akagundua hali ya mambo hayo. Alimwita kwake mke mdogo, Sujata, na kumweleza kwa upole akisema:

"Sujata, kuna aina saba za wake. Kuna mke anayefanana na muuaji. Ana moyo mchafu, hamweshimu mme wake na kwa hiyo huelekeza moyo wake kwa mwanamume mwingine.

" Kuna mke anayefanana na mwizi. Haelewi kamwe kazi ya mumewe bali hufikiria tu tamaa yake ya anasa. Hupoteza mapato ya mumewe kwa kushibisha hamu yake na kwa kufanya hivyo

humwibia mumewe.

" Kuna mke afananaye na Bwana mkubwa. Humkaripia mumewe, hajali utunzaji wa nyumba na daima humkemea mumewe kwa maneno makali.

" Kuna mke afananaye na mama. Humtunza vizuri mume wake kama vile ni mtoto mdogo, humlinda kama mama amlindavyo mwanae, na hutunza mapato ya mumewe".

" Kuna mke afananaye na dada. Ni mwaminifu kwa mume wake na humtunza kwa makini na staha".

" Kuna mke afananaye na rafiki. Hujaribu kumbembeleza mumewe kama vile alikuwa rafiki aliyerejea kitambo tu baada ya kutoweka kwa muda mrefu. Ni makini, mwenye tabia njema na humheshimu sana mumewe".

" Mwisho, kuna mke ambaye ni kama mtumishi wa nyumbani. Humhudumia mme wake vizuri na kwa uthabiti. Humweshimu na kutii amri zake, hana matakwa ya kwake, hana mawazo mabaya, hana chuki na kila mara hujitahidi kumfurahisha mumewe".

Aliyebarikiwa aliuliza, " Sujata, unafanana na aina gani ya mke au ni aina gani ya mke ungempenda ufanane naye?" Alipoyasikia maneno haya, Sujata aliona aibu ya tabia yake ya zamani na akajibu kuwa angependa awe kama mke wa mfano wa

mwisho, mtumishi - mwanamke. Tangu hapo alibadilisha tabia yake na akawa msaidizi wa mume wake, na kwa pamoja waliitafuta Nuru.

5. Amrapali alikuwa kahaba tajiri na mashuhuri wa Vaisali na aliwamiliki makahaba wengi wenye umri mdogo na warembo. Alikwenda kwa Aliyebarikiwa na akamwomba ampatie mafundisho mema.

Aliyebarikiwa alisema, " Amrapali, moyo wa mwanamke hubabaishwa na kupotoshwa kwa urahisi. Mwanamke hutawaliwa na tamaa zake na kutekwa na wivu kwa urahisi zaidi kuliko mwanamume.

" Kwa hiyo ni vigumu zaidi kwa mwanamke kuifuata njia bora. Hii ni kweli hasa kwa mwanamke kijana na mrembo. Yakupasa kusonga mbele kufuata njia Bora kwa kuishinda tamaa na majaribu.

" Amrapali, yakubidi siku zako ukumbuke kuwa ujana na urembo havidumu bali hufuatwa na maradhi, uzee na maumivu. Tamaa ya utajiri mali na mapenzi ni majaribu yawasongao wanawake, lakini, Amrapali, hizo siyo hazina za milele. Nuru ni hazina pekee inayodumisha thamani yake. Afya njema hufuatwa na maradhi, ujana ni lazima ufuatwe na uzee; uzima lazima ukipishe kifo.

Mtu aweza kulazimika kumwacha mpenzi wake ili aishi na

yule amchukiaye, mtu aweza kushindwa kukipata kile akipendacho kwa muda mrefu. Hii ni kanuni ya maisha.

Kitu ambacho kinalinda na kumleta mtu katika amani ya kudumu ni Wongofu. Amrapali inakubidi uitafute Nuru mara moja".

" Amrapali alimsikiliza, akawa mwanafunzi wake na akatoa bustani yake nzuri kwa ndugu, kama sadaka.

6. Hakuna tofauti ya jinsia katika njia ya Wongofu. Ikiwa mwanamke ataamua kuutafuta Wongofu, atakuwa shujaa wa Njia ya Kweli.

Malkia wa mfalme Prasenajit na Malkia wa mfalme Ayodhya aliupata ushujaa huo. Alikuwa na imani kubwa katika mafundisho ya Aliyebarikiwa na akatoa ahadi kumi mbele yake.

" Bwana wangu, hadi niupatapo wongofu sitayakiuka mafundisho matakatifu; sitakuwa na majivuno mbele ya watu wote wanaonizidi umri, sitamkasirikia mtu yeyote.

"Sitawaonea kijicho wengine au kuwa na wivu juu ya mali yao; sitakuwa na ubinafsi moyoni mwangu au katika mali yangu; nitajitahidi kuwafurahisha maskini kwa vitu nivipokeavyo na sitahodhi vitu kwa manufaa yangu binafsi. "Nitawapokea watu wote kwa huruma, kuwapa mahitaji yao, kuongea nao kwa unyenyekevu, kuangalia hali zao bila ya kujali hali niliyonayo na

kujaribu kuwafurahisha bila ubaguzi."

" Nitakapowaona watu katika hali ya ukiwa, kifungoni, Katika maumivu ya magonjwa au shida nyinginezo, nitajitahidi kuwafariji na niwawezeshe kuwa na furaha kwa kuwaeleza sababu na sheria.

" Ikiwa nitawaona watu wakiwakamata wanyama hai kuwatendea vitendo vya ukatili au kwenda kinyume cha mafundisho yoyote, nitawaadhibu ikiwa wanastahili adhabu au nitawafundisha kama wanastahili kufundishwa, kisha nitawajibika kurekebisha waliyoharibu na kusahihisha makosa yao kwa uwezo wangu wote.

" Sitasahau kusikiliza mafundisho ya kweli, kwa kuwa ninajua kwamba mtu anapokwepa mafundisho ya kweli kwa haraka huachana na ukweli uliotanda kila mahali na atashindwa kuifikia pwani ya Nuru."

Kisha alipendekeza matakwa matatu yafuatayo ya kuwaokoa watu maskini;" Kwanza nitamfanya kila mtu awe na amani. Nina imani, ombi hili, katika maisha yawayo yoyote nitakayoishi litakuwa msingi wa wema utakaoota ndani ya hekima ya mafundisho safi.

" Pili, baada ya kupokea hekima ya mafundisho mema, nitawafundisha watu wote bila kuchoka;

" Tatu nitayalinda mafundisho mema, hata kama ni kujitoa kafara mwili wangu, maisha au mali."

Umuhimu wa kweli wa maisha ya familia ni nafasi familia itoayo kuleta faraja ya pamoja na msaada wa kuelekea katika njia ya Wongofu. Hata mwanamke wa kawaida, kama anao moyo sawa wa kuitafuta Nuru, na akatoa nadhiri na matarajio sawa, anaweza kuwa mwanafunzi mkubwa wa Buddha kama alivyokuwa Mallika."

III
MAISHA YA HUDUMA

1. Kuna mafundisho saba yanayoifanya nchi istawi vema; Kwanza yawabidi watu wakutane mara kwa mara kujadili mambo ya kisiasa na kujiandaa kwa usalama wa taifa.

Pili, watu wa aina zote wakutane pamoja kujadili mambo ya kitaifa.

Tatu, ni lazima watu waheshimu mila zao za zamani na siyo kuzibadili bila sababu za msingi, pia inawalazimu kufuata sheria na ibada na kuiheshimu haki.

Nne ni lazima watambue tofauti za amri pamoja na za jinsia, na kuheshimu ubora wa familia na jumuiya zilizopo.

Tano, ni lazima wawapende wazazi wao na wawe waaminifu kwa walimu wao na wazee wao.

Sita, ni lazima kuheshimu makaburi ya mababu zao na kufanya ibada za kila mwaka.

Saba, ni lazima kuthamini maadili ya jamii, kuheshimu mwenendo safi, kuwasikiliza waheshimiwa walimu na kuwatolea sadaka.

Ikiwa nchi itafuata mafundisho haya vizuri, itastawi na itaheshimiwa na nchi nyingine zote.

2. Nyakati fulani kulikuwa na mfalme aliyesifika kwa kuitawala nchi yake vizuri na kutokana na hekima yake aliitwa mfalme mwanga - mkuu. Alielezea kanuni ya utawala wake kama ifuatavyo:-

Njia bora ya mtawala kumiliki vizuri nchi yake ni kwanza kabisa ajitawale yeye mwenyewe. Kiongozi lazima awaendee watu wake kwa moyo wa huruma na awafundishe na kuwaelekeza kuondokana na uchafu mioyoni mwao. Furaha itokanayo na mafundisho mema hakika inazidi starehe na raha ambayo mali na vitu vyote vya duniani vinaweza kutoa. Hivyo basi angeliweza kuwapatia watu wake mafundisho mema yakaiweka mioyo na miili yao katika raha mstarehe.

Maskini wanapomwendea angeweza kuwafungulia ghala

lake na kuwaruhusu wachukue chochote, na hivyo angeweza kuchukua nafasi hiyo kuwafundisha hekima ya kuondokana na tamaa na maovu yote.

Kila mtu ana mtizamo tofauti kulingana na hali ya moyo wake, watu huuona mji wao wanamoishi kuwa safi na wa kupendeza, bali wengine huuona kuwa mbovu na chakavu. Yote hutegemea na hali ya mioyo yao.

Watu wayashikao mafundisho mema na kuyaheshimu, wanao uwezo wa kuona uwiano kati ya miti na mawe ya kawaida, mwanga mzuri na rangi safi za marumaru. Lakini wale wenye tamaa mbaya wasiokuwa na maarifa ya kuitawala mioyo yao, ni vipofu wa kutoweza kuona hata mwanga wa jumba la mfalme lililojengwa kwa dhahabu.

Kila kitu katika maisha ya kila siku katika taifa kiko hivyo hivyo. Moyo ndiyo chimbuko la kila kitu hivyo mtawala yampasa kwanza ajitahidi kuwafanya watu wake waifunze mioyo yao.

3. Kanuni ya kwanza katika utawala wa busara ni sawa na kanuni ya Mfalme Mwanga Mkuu; Kuwaagiza watu kuelimisha mioyo yao.

Kuelimisha mioyo yao ni kuutafuta wongofu, kwa hiyo, mtawala wa busara hana budi kuelekeza juhudi zake kwanza katika mafundisho ya Buddha.

Ikiwa kiongozi ana imani na Buddha na anafuata mafundisho yake barabara, anatambua na kuheshimu watu waadilifu na wenye masikitiko, hapatakuwepo na upendeleo wowote kwa marafiki au maadui na nchi yake itaendelea kustawi.

Ikiwa nchi imestawi hakuna maana ya kushambulia nchi nyingine na haina haja ya kuwa na silaha za kufanyia mashambulizi.

Watu wawapo na raha na kutosheka, tofauti zao za kitabaka hupotea, matendo mema hukuzwa, wema na uadilifu huongezeka pia na watu hueshimiana. Kisha kila mmoja hustawi; Majira na hali ya joto huwa kawaida; Jua, mwezi na nyota hung'aa kama kawaida; Pepo na mvua hutokea katika nyakati zake; na maafa yote ya kiasili hutoweka.

4. Wajibu wa mtawala ni kuwalinda watu wake. Ni mzazi wa watu wake na huwalinda kwa sheria zake. Anapaswa kuwalea watu wake kama wazazi wawaleavyo watoto wao, akimbadilishia nguo kavu kwa nguo iliyolowana bila kusubiri mtoto alie kwanza. Vivyo hivyo mtawala yampasa awaondolee mateso watu wake na kuwapa furaha bila kusubiri walalamike kwanza. Hakika utawala wake hautakuwa sahihi hadi hapo watu wake wawapo na amani. Watu ndiyo hazina ya nchi yake.

Kwa hiyo Mtawala mwenye busara huwafikiria watu wake wakati wowote na hawasahau katu. Hufikiria shida zao na

kupanga ustawi wao. Ili kutawala kwa busara lazima ashauriwe juu ya mambo yote:- Juu ya maji, ukame, dhoruba na mvua; analazimika kujua mambo ya mazao, uwezekano wa kupata mavuno mazuri, starehe na masikitiko ya watu. Ili kuwa na uwezo wa kutuza, kuadhibu au kusifu kwa usahihi inambidi ajue na kuelewa kwa undani kabisa ubaya wa mkosaji na uzuri wa mtu mwema.

Mtawala mwenye busara huwatunza watu wake wanapokuwa na mahitaji na hukusanya kutoka kwao wanapokuwa wameneemeka. Ni lazima aamue kwa busara anapotoza kodi na kuhakikisha kuwa ushuru autozao si mzigo ili watu wake waishi bila manung'uniko.

Mtawala mwenye busara atawalinda watu wake kwa nguvu zake na hekima yake. Mtu anayewatawala watu wake namna hiyo ana haki ya kuitwa mfalme.

5. Mfalme wa kweli ni mfalme wa wafalme. Nasaba yake ni bora na ya juu. Hatawali tu kambi nne za dunia, bali yeye pia ni Bwana wa Hekima na Mlinzi wa mafundisho Maadilifu.

Popote aendapo, ugomvi huisha na chuki hutoweka. Hutawala kwa haki kwa nguvu za kweli, kwa kuyashinda maovu huleta amani kwa watu wote.

Mfalme wa kweli kamwe si muuaji au mwizi au mzinzi. Daima hasemi uongo, hatukani watu, wala hadanganyi au

kuseng'enya. Moyo wake hauna tamaa wala hasira na ujinga. Huondoa maovu haya kumi na badala yake hujenga maadili kumi.

Kwa kuwa utawala wake umejengwa juu ya kweli yeye hawezi kushindwa. Kweli anapotokea mahali popote ugomvi huisha na chuki hutoweka. Hakuna utengano kati ya watu wake, na kwa hiyo wanaishi kwa usalama na utulivu; kuwepo kwake tu huleta amani na furaha kati yao. Hivyo ndiyo sababu anaitwa Mfalme wa Kweli.

Kwa kuwa Mfalme wa Kweli ni mfalme wa wafalme, watawala wengine wote hutukuza jina lake tukufu na hutawala milki zao kwa kumwiga yeye.

Hivyo basi mfalme wa kweli ni mtawala wa wafalme wote na katika njia yake nyoofu. Wafalme huwapa watu wao usalama na kutimiza wajibu wakiwa pamoja na Dharma.

6. Mtawala mwenye busara atatoa hukumu yake kwa huruma. Atajitahidi kufikiria kila shauri kwa hekima na kutoa hukumu yake kwa kufuata kanuni tano.

Kanuni tano ni: Kwanza, ni lazima achunguze ukweli wa mambo yalivyoelezwa.

Pili atahakikisha kuwa mambo hayo yapo chini ya mamlaka yake. Kama akitoa hukumu kwa mamlaka yake yote, hukumu

yake iwe ni ya msingi, lakini akifanya hivyo bila mamlaka atazidisha matatizo, hana budi kusubiri wakati hali itakaporuhusu.

Tatu, ni lazima ahukumu kwa haki: hii ina maana kuwa ni lazima aingie katika moyo wa mshtakiwa. Akigundua kuwa kosa lilitendeka bila kukusudia hana budi kumwachia huru mshtakiwa.

Nne, inampasa atangaze hukumu yake kwa upole wala siyo kwa ukali; yaani aweze kutoa adhabu inayostahili na asivuke mipaka. Mtawala mzuri humwelekeza mhalifu kwa upole na humpa muda kufikiria makosa yake.

Tano, ahukumu kwa huruma lakini siyo kwa hasira; alaani kosa wala siyo mkosaji. Atoe hukumu yake katika misingi ya huruma na atumie nafasi hiyo kumsaidia mhalifu ajutie makosa yake.

7. Ikiwa waziri mashuhuri katika serikali hatajali wajibu wake, akafanya kazi kwa faida yake binafsi, au akapokea rushwa, hiyo italeta uozo katika uadilifu wa umma. Watu watadanganyana, mwenye nguvu atamvamia asiye na nguvu, mwenye cheo atamwonea asiyenacho, tajiri atamwonea maskini na hapatakuwepo na haki, fujo zitazuka na matatizo yataongezeka.

Katika hali kama hiyo, mawaziri waaminifu watajihuzuru katika utumishi wa umma, watu wenye busara kwa hofu ya kuhusishwa katika migogoro watakaa kimya na walaghai watachukua nafasi katika serikali na kutumia uwezo wao wa

kisiasa kujitajirisha bila kujali shida za watu.

Katika hali ya mambo kama hayo serikali hupoteza nguvu zake na sera zake nzuri uharibika.

Maofisa wasio waaminifu kama hao ni wezi wa furaha za watu, na kumbe ni wabaya zaidi ya wezi kwa sababu hawa humdanganya mtawala wao pamoja na watu na ni chanzo cha matatizo katika taifa. Mfalme anapaswa kuwafukuza kazi mawaziri kama hao na kuwaadhibu.

Hata katika nchi inayotawaliwa na mfalme mzuri kwa sheria nzuri pia, kuna aina nyingine ya wakorofi. Kuna waume wavutwao zaidi na mapenzi ya wake na watoto wao na kusahau kabisa wema wa wazazi wao waliowalea na kuwatunza kwa muda wa miaka mingi. Hawajali wazazi wao, huwanyang'anya mali zao na kutojali mafundisho yao. Wana kama hao hawana budi wajumuishwe kati ya watu walio waovu kuliko wote.

Je ni kwa nini? Ni kwa sababu wamejitenga kwa wazazi ambao upendo wao wa muda mrefu ulikuwa upendo ambao hauwezi kulipwa hata kama wana hao wangewaheshimu na kuwatendea mema matupu katika maisha yao yote. Wote wasio waaminifu kwa mtawala wao na waliojitenga na wazazi wao hawana budi kuadhibiwa kama wahalifu wa hali ya juu.

Tena, katika nchi ambayo inatawaliwa na mfalme nzuri

kwa sheria safi kuna aina nyingine ya ukorofi. Kuna watu ambao wamesahau kabisa hazina tatu, Buddha, Dharma na Samgha. Watu hawa huaribu sehemu takatifu za kuabudia, huchoma maandiko matakatifu, huwatumikisha walimu wa haki na hivyo huenda kinyume na mafundisho matakatifu ya Buddha. Na hao pia ni kati ya wahalifu wakubwa.

Je, ni kwa nini? Ni kwa sababu wao huvunja imani ya roho ya taifa lao ambayo ndiyo msingi na chimbuko la maadili yake. Watu hao kwa kuunguza imani ya wengine wanajichimbia kaburi.

Dhambi nyinginezo zinaweza kuonekana nyepesi zikilinganishwa na ukorofi huu. Wahalifu wakorofi kama hao wanapaswa kuadhibiwa vikali sana.

8. Inawezekana kuwepo njama juu ya mfalme anayetawala nchi yake vyema kulingana na mafundisho mazuri au pengine maadui wa nje wanaweza kuivamia nchi. Katika hali kama hiyo mfalme yamlazimu aamue mambo matatu.

Aamue: Kwanza hawa wakorofi au maadui wa nje wanatishia amani na ustawi wa nchi yetu, nitawalinda watu na nchi yangu hata kwa majeshi.

" Pili, nitajitahidi kutafuta njia ya kuwashinda bila kutumia silaha.

" Tatu, nitajitahidi kuwateka wakiwa hai na kuwanyang'anya silaha zao ikiwezekana bila kuwaua."

Kwa kufuata maamuzi haya matatu Mfalme atasonga mbele kwa busara baada ya kuandaa kambi za lazima na kutoa maelekezo.

Kwa kufuata utaratibu huu, nchi na askari wake watatiwa moyo kwa hekima na heshima ya Mfalme na wataheshimu msimamo wake. Ikiwa ni lazima askari kwenda vitani wataelewa sababu na misingi ya kufanya hivyo. Kwa hali hiyo watakwenda mstari wa mbele kwa moyo na utii, wakiheshimu na kutii utawala wa busara wa mfalme. Vita kama hiyo haitaliletea ushindi tu kwa Taifa bali pia italitengenezea wema na uadilifu.

SURA YA TATU

UJENZI WA NCHI YA BUDDHA

I
UDUGU WENYE MASIKILIZANO

1. Hebu tufikirie nchi ya jangwa ikiwa imetandwa na giza huku ndani yake kukiwa na viumbe hai wakiparamiana gizani.

Kwa kawaida viumbe hao wataogopa sana na kadri wanavyokimbia hapa na pale bila kuelewana wakati wa usiku, kutakuwepo na upweke na kutahayari kwingi. Kwa hakika hili ni tukio la kusikitisha.

Hebu tufikirie kwamba ghafla mtu mmoja mashuhuri anatokea akiwa na tochi na kila kitu katika eneo hilo kinamulikwa na kinaonekana wazi.

Viumbe hai katika upweke wa giza mara hujikuta katika faraja kubwa wanapotambuana na kuanza kufurahia kuwa pamoja.

Kwa "nchi ya jangwa" inamaanisha dunia watu waishimo ikakaa kuwa katika giza la ujinga. Wale wasio na mwanga wa hekima katika mioyo yao hutangatanga katika woga na ukiwa. Walizaliwa pekee na kufa pekee; hawajui jinsi ya kuishi na wenzao kwa amani na utulivu, na kawaida huwa ni woga na hukata tamaa.

Kwa "mtu mmoja mashuhuri mwenye tochi" inamaanisha Buddha akiwa katika hali ya binadamu, na kwa hekima yake na huruma huiangazia dunia.

Katika mwanga huu watu hujitambua pamoja na wenzao na hufurahia kuanzisha urafiki na mahusiano ya kidugu.

Maelfu ya watu wanaweza kuishi katika jumuiya lakini siyo hasa ya kirafiki hadi hapo wanapofahamiana na kuhurumiana.

Jumuiya ya kweli ina imani na hekima vinavyoimulika. Ni mahali ambapo watu hufahamiana na kuaminiana na ni penye uelewano kijamii.

Ama kweli, amani ni maisha na maana halisi ya ushirika au jamii ya kweli.

2. Katika vyama na mashirika kuna aina tatu. Kwanza kuna vile ambavyo vinaundwa katika msingi wa uwezo, mali, utajiri na matakwa ya viongozi wakuu.

Pili, kuna vile ambavyo vimeundwa kwa sababu ya manufaa ya wanachama wake na vitadumu endapo wanachama wake wataendelea kunufaika bila ugomvi.

Tatu, kuna vile vilivyoundwa katika msingi wa mafundisho mema na utulivu ukiwa ndiyo maisha yake.

Bila shaka aina ya tatu au ya mwisho ndicho chama na ushirika wa kweli kwa kuwa ndani mwake wanachama huishi katika roho moja ambayo kwayo umoja wa roho na aina mbali mbali za maadili huchipuka. Katika ushirika wa namna hii kutakuwepo na masikilizano, kutosheka na furaha kwa wingi.

Uongofu/Nuru ni kama mvua inyeshayo juu ya mlima ikajikusanya katika michirizi ambayo hukusanyika katika vijito na vijito navyo hujikusanya na kuwa mito ambayo mwisho wake hutiririka baharini.

Mvua ya mafundisho matakatifu hunyesha kwa watu wote bila kujali mazingira yao. Wale wanaoyapokea hujikusanya katika vikundi vidogo vidogo, kisha huunda shirika mbali mbali,na jumuiya nyingi hujengeka ambazo hujikuta kati ya bahari kubwa ya Wongofu.

Mawazo ya watu hao huchanganyika kama maji na maziwa na hatimaye hujiunga katika udugu wenye masikilizano.

Kwa hiyo mafundisho ya kweli ndilo sharti la msingi la ushirika sahihi na kama nilivyosema ni mwanga unaowezesha watu kuelewana na kurekebishana na kufuta ukakasi uliopo katika mawazo yao.

Kumbe ushirika uliojengwa juu ya mafundisho sahihi ya Buddha waweza kuitwa udugu.

Ni vema kufuata mafundisho haya na kuifundisha mioyo yao. Kwa hiyo udugu wa Buddha utamhusisha kila mmoja kinadharia lakini ukweli ni wale tu wanaofuata imani moja ambao ni washirika.

3. Udugu wa Buddha utakuwa na washirika wa aina mbili:- Kutakuwa na wale wawafundishao washiriki walei na wale wanaowafadhili wahuburi kwa kuwapatia chakula na mavazi. Kwa pamoja watadumisha na kueneza mafundisho.

Tena, kuukamilisha udugu lazima kuwepo na masikilizano kati ya washiriki. Wahubiri huwafundisha washiriki nao washiriki huwaheshimu wahubiri ili kuwepo na masikilizano kati yao.

Washirika wa uchungu wa Buddha waungane pamoja kwa upole uliojaa upendo wakifurahia kwa kuishi pamoja na wafuasi wenzao na kupenda kuwa pamoja kiroho.

4. Kuna mambo sita yatakayosaidia kumwongoza mwana udugu katika masikilizano. Kwanza ukweli wa kauli; pili, ukweli na wema wa matendo; tatu, unyoofu na wema wa roho; nne, mgawanyo sawa wa mali ya wote; tano, kufuata sawa maandiko matakatifu; na sita, wote kuwa na mawazo sahihi.

Kati ya mambo haya, la sita au " wote wakiwa na mawazo sahihi" hujenga kiini, na mengine matano yakifanya kazi ya kukifunika na kukisetiri.

Ujenzi wa nchi ya Buddha

Kuna mafungu mawili ya sheria saba ya kufuata kama undugu unataka kufanikiwa. Fungu la kwanza ni kama kundi:

1. Wakutane mara kwa mara kusikiliza mafundisho na kuyajadili.

2. Wawe huru kuchanganyikana na kuheshimiana.

3. Wayatii mafundisho na kuziheshimu sheria bila kuzibadili.

4. Wazee na vijana waishi kwa utii na ustahifu.

5. Ukweli na utii viwe ishara ya mwelekeo wao.

6. Waitakase mioyo yao katika mahali patulivu ambapo watawapatia watu wengine utulivu wa moyo huu kabla ya kumiliki wa kwao.

7. Wawapende watu wote, wawakarimu wageni na kuwahimiza wagonjwa kwa huruma na upole.

Undugu anaofuata sheria hizi daima hautarudi nyuma wala hautaanguka. Fungu la pili linamhitaji kila mmoja:

(1) awe na roho safi na asiombe vitu vingi, (2) awe mwaminifu na mnyofu na aachane na uchoyo, (3) awe

mvumulivu bila ubishi, (4) awe mkimya wala si msengenyaji (5) afuate taratibu zilizopo wala asiwe jeuri; (6) awe na moyo wa makini kwa maisha ya kila siku.

Ikiwa washarika watafuata sheria hizi, undugu utadumu bila kutetereka.

5. Kama ilivyosemwa hapo juu, udugu hudumisha masikilizano na amani katika msingi wake; kwa hiyo, yule asiye na masikilizano hawezi kuitwa mwana udugu. Kila mshiriki ajichunge ili asiwe chanzo cha ugomvi na fitina. Fitina na ugomvi vinapojitokeza vifutiliwe mbali kabisa, kwa sababu fitina huvunja na kubomoa ushirika wowote ule. Madoa ya damu hayawezi kuondolewa au kufutwa kwa damu, chuki haiondolewi kwa chuki, chuki inaweza kuondolewa tu kwa kuisahau.

6. Palikuwepo na mfalme aliyeitwa Maafa, ambaye nchi yake ilitekwa na mfalme Brahmdatta. Mfalme Maafa, baada ya kujificha kwa muda pamoja na mwanae na mkewe alikamatwa ila kwa bahati njema mwanae wa kiume alitoroka.

Mwana wa mfalme alijitahidi kutafuta njia ya kumwokoa baba yake bila mafanikio. Siku ya kunyongwa kwa baba yake alijipenyeza kwa uficho hadi kwenye uwanja wa kunyongea ili ashuhudie kwa hasira na uchungu kifo cha baba yake kwa kuwa hakuwa na lolote la kufanya zaidi ya hilo.

Baba alimtambua mwanae katika kundi la watu na

akatamka kama kwamba anajisemea mwenyewe, " usitafute kwa muda mrefu, usitende kwa haraka, chuki inaweza kupozwa kwa kuisahau.

Baadaye mwana wa mfalme alitafuta njia yo yote ya kulipiza kisasi kwa muda mrefu. Hatimaye aliajiriwa kama mhudumu katika jumba la mfalme Brahmadatta ambaye alipendezwa naye.

Siku ambayo mfalme alikwenda kuwinda mwana huyo wa mfalme alitafuta njia ya kulipiza kisasi. Mwana wa Mfalme alimwongoza mfalme Brahmadatta hadi kwenye sehemu pweke na kwa kuwa Mfalme alikuwa amechoka alilala usingizi kichwa chake akakilaza juu ya mapaja ya mwana wa mfalme kutokana na kumwamini kwake.

Mwana wa mfalme alichomoa sime na kuiweka juu ya shingo la mfalme na kisha akasita. Maneno aliyoyasema baba yake wakati wa kunyongwa yalimjia moyoni na ingawa alijaribu tena na tena hakuweza kumuua mfalme. Mara moja mfalme alizinduka usingizini na kumwambia mwana wa mfalme kuwa ameota ndoto mbaya; alimwota mwana wa mfalme Maafa akijaribu kumuua.

Mwana wa mfalme huku akitetemesha sime mkononi mwake kwa haraka alimkamata mfalme, na akajitambulisha kama mwana wa mfalme Maafa, akatamka kuwa wakati wa kulipiza kisasi cha baba yake ulikuwa umefika. Hata hivyo hakudhubutu kulipiza kisasi alitupa sime yake chini ghafla na akapiga magoti mbele ya mfalme.

Mfalme aliposikiliza hadithi ya mwana wa mfalme na maneno ya mwisho ya baba yake aliguswa sana na akamwomba radhi mwana wa mfalme. Baadaye, alimrudishia, milki ya baba yake na nchi zao ziliendelea kuishi kwa urafiki kwa muda mrefu.

Maneno ya mwisho ya mfalme Maafa, " Usitafute kwa muda mrefu" ina maana kuwa uchungu usihifadhiwe kwa muda mrefu na "usitende kwa haraka" yamaanisha kuwa urafiki usiharibiwe kwa haraka.

Uchungu hauwezi kumalizwa na uchungu; unaweza kumalizika tu kwa kuusahau.

Katika ushirika wa udugu uliojengwa juu ya masikilizano ya mafundisho ya kweli, kila mshiriki lazima athamini maana ya hadithi hii.

Sio washiriki wa udugu tu wanaothamini na kutambua maana hii katika maisha yao ya kila siku bali watu wote.

II
NCHI YA BUDDHA

1. Kama ilivyoelezwa, kama udugu hausahau wajibu wao wa kueneza mafundisho ya Buddha na kuishi pamoja kwa masikilizano, udugu huo utapanuka na mafundisho yake yataenea sana.

Hii ina maana kuwa watu wengi watatafuta Nuru, pia ina maana kuwa majeshi ya uovu, ya uchoyo, hasira na ujinga, ambayo yanaongozwa na shetani wa ujinga na tamaa, yataanza kurudi nyuma, na hekima, mwanga, imani na furaha vitashamiri.

Utawala wa shetani umejaa ulafi, giza, mapambano, mapigano, mapanga na umwagaji damu, pia umejaa wivu, dhuluma, chuki, udanganyifu, uwongo, kujipendekeza, siri na shutuma.

Sasa kwa mfano mwanga wa hekima uiangazie milki hiyo na mvua ya huruma iinyeshee, na imani ianze kuota, na maua ya furaha yaanze kusambaza manukato yake. Basi milki hiyo ya shetani itabadilika kuwa Nchi Takatifu ya Buddha.

Kama upepo mwanana na maua machache katika tawi yatoayo ishara za ujio wa majira ya machipuo, ndivyo mtu aipatapo Nuru, majani, miti, milima, mito na vitu vingine huanza kunawili kwa msukumo wa maisha mapya.

Mawazo ya mtu yakiwa safi hata mazingira yake yatakuwa safi pia.

2. Katika nchi yenye mafundisho ya kweli, kila mwanachi ana moyo safi wenye amani na raha. Kwa hakika, huruma ya Buddha huwanufaisha watu wote, na roho yake ng'avu husafisha uchafu wote toka mioyoni mwao.

Moyo safi punde si punde hubadilika kuwa moyo wa makini, moyo unaolingana na Njia Bora, moyo unaopenda kutoa, moyo unaopenda kutunza mafundisho, na moyo wa uvumilivu, wa matumaini, utulivu, busara, upole na moyo uwapelekao watu kwenye Nuru kwa njia mbali mbali za kiufundi. Kwa hivi, vivyo Nchi ya Buddha itajengeka.

Nyumba yenye baba, watoto na mama, hugeuka kuwa nyumba ya Buddha, nchi yenye tofauti za kijamii nayo pia hugeuka katika ushirika wa roho za kidugu.

Jumba la dhahabu lenye madoa ya damu haliwezi kuwa makazi ya Buddha. Kibanda chenye matundu yapitishayo mbalamwezi kwenye paa chaweza kubadilishwa kuwa makazi ya Buddha ikiwa moyo wa mwenye kibanda hicho ni safi.

Nchi ya Buddha inapopatikana katika moyo wa mtu mmoja, moyo huo mmoja huvuta mioyo ya ukoo mzima katika ushirika wa kindugu. Imani katika Buddha huenea kutoka mtu mmoja hadi kwenye familia, kutoka familia huanza kwenye kijiji, kutoka kijiji hadi mjini, kutoka mijini hadi nchi mbalimbali na mwishowe hadi dunia nzima.

Kwa hakika, uaminifu na unyenyekevu katika kueneza mafundisho ya Dharma ndio ujengayo Nchi ya Buddha.

3. Ili kuhakikisha, ukiangalia dunia kwa upande mmoja ikiwa imejaa choyo na tamaa, dhuruma na umwagaji damu inaonekana

hasa nchi ya ibilisi, lakini watu wanapoamini wokovu wa Buddha, damu hugeuka maziwa na choyo na tamaa hugeuka kuwa huruma, na hapo nchi ya ibilisi hubadilika kuwa Nchi Takatifu ya Buddha.

Inaelekea kuwa ni kitu kisichowezekana kuikausha bahari kwa kijiko kidogo, lakini azma ya kufanya hivyo, hata kama itachukuwa maisha ya watu, watu wengi sana, azma hiyo ni moyo huo ambao mtu atapaswa kuwa nao katika kuupokea Wokovu wa Buddha.

Buddha anasubiri ng'ambo ya pili; kwa maana katika dunia yake ya Wokovu ambamo hakuna choyo, hakuna hasira, ujinga, mateso, maumivu, bali ni penye mwanga wa hekima na mvua ya huruma.

Ni nchi ya amani, kimbilio la wanaoteseka na wenye dhiki na maumivu, mahali pa mapumziko kwa wale wanaohitaji kupumzika wakati wakieneza mafundisho ya Dharma.

Katika Nchi hii Takatifu kuna Mwanga usio na mpaka na Maisha ya milele. Wafikao katika mbingu hii hawatarudi tena katika dunia ya madanganyo.

Hakika, Nchi hii Takatifu ambamo manukato ya maua hupamba hewa kwa hekima na ndege huimba Dharma takatifu, hayo ndio makao ya mwisho wa watu wote.

4. Ingawa Nchi hii Takatifu ni mahali pa kupumzika, siyo mahali pa uzembe. Vitanda vya maua ya manukato siyo vya kupumzishia uzembe, bali ni mahali pa maburudisho na mapumziko ambapo mtu hupata nguvu na nia mpya ya kuendeleza kazi ya Wokovu wa Buddha.

Kazi ya Buddha ni ya milele. Kwa kuwa binadamu na viumbe wanaendelea kuishi, na ili mradi uchoyo na mioyo najisi huumba dunia zao na manzili, hapatakuwepo na mwisho wa kazi yake.

Wana wa Buddha waliovuka hadi katika Nchi Takatifu kwa njia ya nguvu kuu ya Amida, wanaweza kutamani kurudi katika nchi zao ambako bado walitoka na ambako bado wana mahusiano. Hapo nao watashiriki kufanya kazi ya Buddha.

Kama mwanga wa mshumaa ueneavyo kutoka mshumaa mmoja hadi mwingine vivyo hivyo mwanga wa Buddha wa huruma utaenea toka moyo mmoja hadi mwingine bila kikomo.

Wana wa Buddha, waitambuapo roho yake ya huruma hurithi jukumu lake la Wokovu na utakaso na kuvirithisha vizazi kutoka kizazi hadi kizazi kingine ili kuifanya Nchi ya Buddha itukuzwe milele na milele.

III
WALE WALIOUPOKEA UTUKUFU KATIKA NCHI YA BUDDHA

1. Syamavati, mwanadani wa Mfalme Udayana alikuwa mfuasi mkubwa wa Buddha.

Aliishi katika viwanja vya ndani katika jumba la Mfalme na hakuweza kutoka nje lakini kijakazi wake, Uttara, aliyekuwa na kumbukumbu nzuri alikuwa akitoka kuhudhuria mihadhara ya Buddha.

Kijakazi huyo aliporudi nyumbani, alimsimlia Malkia mafundisho ya Aliyebarikiwa, na hivyo Malkia alipanua busara na imani yake.

Mke wa pili wa Mfalme aliona kijicho juu ya mke wa kwanza na akatafuta njia za kumuua. Alimchongea kwa Mfalme na baada ya kukubaliana na uchonganishi huo, Mfalme akapania kumuua mke wake wa kwanza, Syamavati.

Malkia Syamavati alisimama kwa utulivu mbele ya Mfalme kiasi kwamba Mfalme hakuwa na nia ya kumwua tena. Kwa kujikaza, mfalme aliungama mbele ya Malkia kwa tuhuma zake.

Choyo ya mke wa pili ilizidi kuongezeka na akawatuma watu wabaya kuchoma nyumba za ndani katika ikulu wakati Mfalme alipokuwa amesafiri. Malkia Syamavati alikaa kimya na

akawatia moyo vijakazi wake waliojawa na hofu, na bila woga, alikufa kwa amani kutokana na imani aliyojifunza kutoka kwa Aliyebarikiwa. Uttara alikufa pamoja naye motoni.

Kati ya wanawake wengi waliokuwa mitume wa Buddha wanawake hawa wawili waliheshimiwa sana. Malkia Syamavati alitukuzwa kama moyo wa huruma na kijakazi wake Uttara kama mwenye usikivu mzuri.

2. Mahanama, mwana wa Mfalme wa ukoo wa Shakya na binamu yake Buddha naye alikuwa na imani katika mafundisho ya Buddha na mmoja wa wafuasi wake waaminifu.

Wakati huo mfalme mkali aitwaye Virudaka wa Kasala aliteka ukoo wa Shakya. Mahanama mwana wa Mfalme alikwenda kwa mfalme kumwomba awaachie watu wake aliowateka lakini Mfalme hakumsikiliza. Hatimaye alimwambia Mfalme aachie kiasi cha mateka watakaoweza kukimbia haraka wakati yeye amejizamisha ndani ya bwawa lililokuwa karibu.

Mfalme alilikubali haraka shauri hili akidai kuwa itamchukua muda mfupi sana kwake kuwa ndani ya maji.

Mahanama alipozama, langoo la ngome lilifunguliwa na watu walikimbia haraka kwa usalama wa maisha yao. Lakini Mahanama hakutokeza nje ya maji kwa sababu alikuwa amezifunga nywele zake kwenye mzizi wa mti ulio ndani ya maji ili ajitoe kafara lakini aokoe maisha ya watu wake wote.

3. Utpalavarna alikuwa mtawa wa kike mashuhuri sana ambaye hekima yake ililinganishwa na ya Maudgalyayana, mtume mashuhuri wa Buddha. alikuwa mtawa hakika na alikuwa kiongozi wa wenzake akiwafundisha bila kuchoka.

Devadatta alikuwa mwanamme hasidi na katili aliyepotosha moyo wa Mfalme Ajatasatru kwa kumshauri kupinga mafundisho ya Buddha. Ila baadaye, mfalme Ajatasatru alitubu, akavunja urafiki wake na Devadatta, akawa mwanafunzi mtiifu wa Buddha.

Wakati fulani Devadatta alipokuwa akifukuzwa kutoka katika lango la ngome, katika juhudi zake za kuonana na mfalme, alikutana na Utpalavarna akitokea ndani ya ngome. Hii ilimchukiza sana akamgonga Utpalavarna na kumjeruhi vibaya.

Utpalavarna alirudi katika nyumba yake ya watawa akiwa na maumivu makali na watawa wengine walipojaribu kumliwaza aliwaambia; " Dada zangu, maisha ya ubinadamu hayatabiriki, kila kitu kinapita na hakina nafsi wala kujipendelea. Dunia ya Uongofu ndiyo tu yenye amani na utulivu. Lazima mwendelee na mafunzo yenu." Kisha akakata roho kimya.

4. Angulimalya, aliyekuwa jambazi mkubwa na aliyeua watu wengi, aliokolewa na Aliyebarikiwa na akawa mmojawapo wa wanafunzi wake.

Siku moja alikwenda kuombaomba mjini na kutokana na matendo yake mabaya ya zamani alipata matatizo na mateso.

Wanavijiji walimvamia na kumpiga vibaya sana, lakini alirudi kwa Aliyebarikiwa, akiwa bado anavuja damu, akaanguka chini ya miguu yake akimshukuru kwa bahati aliyoipata ya kupata mateso kutokana na matendo yake ya zamani ya kikatili.

Alimwambia "Uliyebarikiwa jina langu la asili niliitwa ' Hapana Madhara,' lakini kwa sababu ya ujinga wangu, nilipoteza maisha ya thamani ya watu wengi, na kutoka kwa kila mtu nilikata kidole kimoja; kutokana na matendo hayo, nilipewa jina la Angulimalya, mkusanyaji wa vidole.

" Hivyo basi, kutokana na huruma yako, nilijifunza hekima na nikajitoa kwa hazina tatu za Buddha, Dharma na Samgha. Mtu anayeswaga farasi au ng'ombe hutumia kamba au mjeredi lakini wewe Uliyebarikiwa, uliutakasa moyo wangu bila kutumia mjeredi, kamba au ndoano.

" Leo hii, Uliyebarikiwa, nimepata malipo yangu sahihi, sitamani kuishi wala sitamani kufa. Nasubiri tu muda wangu utimie."

5. Maudgalyayana, pamoja na mheshimiwa Sariputra, alikuwa mmojawapo wa wanafunzi wawili maarufu wa Buddha. Walimu wa madhehebu mengine walipoona jinsi maji safi ya mafundisho ya Buddha yalivyokuwa yakisambaa kwa watu na kunywewa kwa hamu, walipandwa na wivu hivyo wakaweka vikwazo mbalimbali dhidi ya mafundisho hayo.

Hata hivyo hapakuwa na kizuizi chochote kilichoweza kuzuia mafundisho yake kuenea kwa mapana. Wafuasi wa madhehebu mengine walijaribu kumuua Maudagalyayana.

Mara mbili aliweza kukwepa lakini mara ya tatu alivamiwa na wapagani na kuishia kwenye kipigo chao.

Akiongozwa na Nuru, akiwa kimya na kwa utulivu alipokea kipigo, na ingawa mwili wake ulikuwa umekatwakatwa na mifupa yake kupasukapasuka, alikufa kwa amani.

CHIMBUKO LA REJEA ZA "MAFUNDISHO YA BUDDHA"

Majina kwa kifupi: DN-Dīgha Nikāya
MN-Majjhima Nikāya
SN-Saṃyutta Nikāya
AN-Aṅguttara Nikāya

BUDDHA

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
Sura ya 1			
1	2	1	Mafundisho mbali mbali
	4	19	AN 3-38, Sukhumālā-sutta
	5	8	MN 3-26, Ariyapariyesana-sutta
	5	13	Mafundisho mbali mbali
	6	13	MN 9-85, Bodhirājakumāra-sutta
	6	17	Mafundisho mbali mbali
	7	5	Sutta-nipāta 3-2, Padhāna-sutta
	7	11	Mafundisho mbali mbali
	7	6	Vinaya, Mahāvagga 1
	9	6	DN 16, Mahāparinibbāna-sutta
2	10	3	DN 16, Mahāparinibbāna-sutta
	10	16	Parinibbāna-sutta
	12	12	Parinibbāna-sutta
	12	19	DN 16, Mahāparinibbāna-sutta
Sura ya 2			
1	14	1	Amitāyur-dhyāna & Vimalakīr-ti-nirdeśa sūtras
	14	5	Śūraṃgama-sūrta

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
	14	9	Vimalakīrti-nirdeśa & Mahāparinirvāṇa sūtras
	15	2	Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 16
	15	17	Mahāyāna-jātaka-cittabhūmi-parīkṣa-sūtra
	15	22	Mahāparinirvāṇa-sūtra
2	17	11	Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 3
	18	11	Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 4
	18	22	Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 5
3	21	3	Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 16
Sura ya 3			
1	24	1	Avataṃsaka-sūtra 5
	25	1	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	25	6	Avataṃsaka-sūtra
	25	13	Suvarṇaprabhāsottamarāja-sūtra 3
2	27	14	Avataṃsaka-sūtra
	27	19	Avataṃsaka-sūtra 34, Gaṇḍavyūha
	28	3	Smaller Sukhāvatīvyūha-sūtra
	28	6	Avataṃsaka-sūtra
	28	11	SN 35-5
	28	15	Mahāparinirvāṇa-sūtra
3	30	11	MN 8-77, Mahāsakulūdayi-sutta
	31	4	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	31	15	Laṅkāvatāra-sūtra
	32	1	Avataṃsaka-sūtra 32

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
	32	15	Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 25
	32	20	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	33	7	Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 2
	33	13	Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 2

DHARMA

Sura ya 1

1	36	1	Vinaya, Mahāvagga 1-6 & SN 56-11-12, Dhammacakra-pravartana-sutta
	37	13	Itivuttaka 103
	37	23	MN 2, Sabbāsava-sutta
	38	5	Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 18
	38	17	Śrīmālādevīsiṃhanāda-sūtra
3	40	10	Avataṃsaka-sūtra 22, Daśa-bhūmika

Sura ya 2

1	44	1	MN 4-35, Cūḷasaccaka-sutta
	46	3	AN 5-49, Rajah-muṇḍa-sutta
	46	13	AN 4-185, Samaṇa-sutta
	46	18	AN 3-134, Uppāda-sutta
2	47	1	Laṅkāvatāra-sūtra
	47	5	Avataṃsaka-sūtra 2
	47	13	Avataṃsaka-sūtra 16
	48	2	Avataṃsaka-sūtra 22, Daśa-

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
			bhūmika
	48	13	Laṅkāvatāra-sūtra
	48	18	AN 4-186, Ummagga-sutta
	48	22	Dhammapada 1, 2, 17, 18
	49	12	SN 2-1-6, Kāmada-sutta
3	49	22	Avataṃsaka-sūtra 16
	50	6	Laṅkāvatāra-sūtra
	50	21	MN 3-22, Alagaddūpama-sutta
	51	17	Laṅkāvatāra-sūtra
	51	21	Laṅkāvatāra-sūtra
4	54	3	Vinaya Mahāvagga 1-6
	54	13	SN 35-200, Dārukkhandha-sutta
	55	7	Laṅkāvatāra-sūtra na nyinginezo
	55	21	MN 2-18, Madhupiṇḍika-sutta
	56	9	Laṅkāvatāra-sūtra
	56	22	Laṅkāvatāra-sūtra
	57	16	Vimalakīrti-nirdeśa-sūtra
	59	18	Avataṃsaka-sūtra 34, Gaṇḍavyūha
	60	2	Laṅkāvatāra-sūtra na nyinginezo
Sura ya 3			
1	61	1	Vinaya Mahāvagga 1-5
	61	14	Vinaya, Cūḷavagga 5-21
	62	1	Śūraṃgama-sūtra

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
2	66	18	Śūraṃgama-sūtra
	68	13	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	68	20	Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 7 & Śūraṃgama-sūtra
	69	11	Avataṃsaka-sūtra 32
	69	16	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	69	20	Brahmajāla-sūtra
	70	6	Mahāparinirvāṇa-sūtra
3	71	1	Mahāparinirvāṇa-sūtra
Sura ya 4			
1	76	1	Śrīmālādevīsiṃhanāda-sūtra
	77	7	AN 2-11
	77	11	Itivuttaka 93
	77	18	Vinaya, Mahāvagga
	78	4	AN 3-68, Aññātiṭṭhika-sutta
	78	18	AN 3-34, Āḷavaka-sutta
	79	9	Vaipulya-sūtra
	79	14	Vinaya, Mahāvagga 1-6, Dhammacakrapravartana-sutta
	79	17	MN 2-14, Cūḷadukkhakkhandha-sutta
	80	9	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	81	6	Itivuttaka 24
2	83	3	MN 6-51, Kandaraka-suttanta
	83	16	AN 3-130
	83	22	AN 3-113

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
3	84	12	Itivuttaka 100
	85	1	Saṃyuktaratnapiṭaka-sūtra
	85	20	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	87	4	AN 3-62
	87	17	AN 3-35, Devadūta-sutta
	88	23	Therīgāthā Aṭṭhakathā
4	89	1	Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 2
Sura ya 5			
1	96	1	Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 1
	99	8	Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 2
	100	16	Amitāyur-dhyāna-sūtra
2	104	1	Sukhāvatīvyūha-sūtra ndogo

NJIA YA MATENDO

Sura ya 1			
1	108	1	MN 2, Sabbāsava-sutta
	109	21	MN 3-26, Ariyapariyesana-sutta
	110	10	SN 35-206, Chapāna-sutta
	111	6	Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 41-2
	113	13	MN 2-19, Dvedhāvitakka-sutta
	114	4	Dhammapada Aṭṭhakathā
2	115	3	AN 3-117
	115	15	MN 3-21, Kakacūpama-sutta
	118	15	MN 3-23, Vammīka-sutta

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
	120	4	Jātaka IV-497, Mātaṅga-Jātaka
	123	13	Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 9
	123	21	Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 11
	124	12	Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 13
	125	8	AN 2-4, Samacitta-sutta
3	126	1	Saṃyuktaratnapiṭaka-sūtra
	134	16	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	135	9	Saṃyuktaratnapiṭaka-sūtra
Sura ya 2			
1	139	1	MN 7-63, Cūḷamālunkya-suttanta
	140	23	MN 3-29, Mahāsāropama-sutta
	142	7	Mahāmāyā-sūtra
	142	19	Theragāthā Aṭṭhakathā
	144	6	MN 3-28, Mahāhatthipadopama-sutta
	144	19	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	145	6	Avadānasátaka-sūtra
	146	6	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	147	18	Pañcaviṃśati-sāhasrikā-prajñāpāramitā-sūtra
	149	1	Avataṃsaka-sūtra 34, Gaṇḍa-

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
			vyūha
2	150	14	AN 3-88
	151	10	AN 3-81
	151	16	AN 3-82
	152	7	Parinibbāna-sutta vol. 2
	153	5	MN 14-141, Saccavibhanga-sutta
	154	7	Parinibbāna-sutta vol. 2
	154	19	AN 5-16, Bala-sutta
	155	1	Avataṃsaka-sūtra 6
	155	16	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	156	4	Saṃyuktaratnapiṭaka-sūtra
	156	17	Suvarṇaprabhāsa-sūtra 26
	157	5	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	158	2	Theragāthā Aṭṭhakathā
	158	17	Jātaka 55, Pañcāvudha-Jātaka
	159	20	Itivuttaka 39 & 40
	160	6	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	160	9	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	160	11	AN 5-12
	160	16	Parinibbāna-sutta
	161	1	Śūraṃgama-sūtra
3	162	3	SN 55-21 & 22, Mahānāma-sutta
	162	17	AN 5-32, Cundī-sutta
	163	5	Vimalakīrti-nirdeśa-sūtra

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
	163	16	Śūraṃgama-sūtra
	163	22	Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 2
	164	8	SN 1-4-6
	164	11	Avataṃsaka-sūtra 33
	165	5	Avataṃsaka-sūtra 24
	165	16	Suvarṇaprabhāsa-sūtra 4
	166	1	Amitāyur-dhyāna-sūtra
	166	4	Sukhāvatīvyūha-sūtra
	166	9	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	167	5	MN 2-16, Cetokhila-sutta
	167	20	Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 2
4	168	12	Dhammapada
	176	1	SN 1-6-59
	176	14	AN
	176	19	Mahāparinirvāṇa-sūtra

UNDUGU

Sura ya 1

1	178	1	Itivuttaka 100 & MN 1-3, Dhammadāyāda-sutta
	178	7	Itivuttaka 92
	178	16	Vinaya, Mahāvagga 1-30
	178	16	MN 4-39, Mahā-assapura-sutta
	180	19	MN 4-40, Cūḷa-assapura-sutta
	181	16	Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 10
	181	21	Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 10

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
	182	7	Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 14
2	183	15	SN 55-37, Mahānāma-sutta
	184	3	AN 3-75
	184	9	SN 55-37, Mahānāma-sutta
	184	14	SN 55-54, Gilāyanaṃ-sutta
	184	20	Avataṃsaka-sūtra 22
	186	6	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	188	20	Avataṃsaka-sūtra 7
	191	10	Mahāmāyā-sūtra
	192	8	Avataṃsaka-sūtra 21
	193	2	Mahāparinirvāṇa-sūtra
Sura ya 2			
1	194	1	DN 31, Siṅgālovāda-sutta
	199	1	AN 2-4, Samacitta-sutta
	199	17	AN 3-31
	200	1	Jātaka 417, Kaccāni-Jātaka
	201	15	DN 31, Siṅgālovāda-sutta
	202	1	Dhammapada Aṭṭhakathā 1
2	203	6	AN 4-197
	204	3	AN 5-333 Uggaha-sutta
	204	19	(Maoni ya Wa-Burma)
	205	11	AN 7-59, Sujāta-sutta
	207	4	DN 16, Mahāparinibbāna-sutta
3	208	8	Śrīmālādevīsiṃhanāda-sūtra
	210	9	DN 16, Mahāparinibbāna-sutta
	211	10	Avataṃsaka-sūtra 34, Gaṇḍav-

Kifungu	*Ukurasa*	*Mstari*	*Chimbuko*
			yūha
	212	17	Suvarṇaprabhāsa-sūtra 12
	213	15	Bodhisattva-gocaropāya-viṣa-yavikurvana-nirdeśa-sūtra
Sura ya 3			
1	220	1	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	221	13	AN 3-118, Soceyyan-sutta
	223	5	SN
	223	15	Vinaya, Mahāvagga 10-1 & 2
	224	1	DN 16, Mahāparinibbāna-sutta
	225	6	Vinaya, Mahāvagga 10-1 & 2
2	227	16	SN
	228	13	Antarābhava-sūtra
	228	19	Vimalakīrti-nirdeśa-sūtra
	229	22	Mahāparinirvāṇa-sūtra
	230	17	Sukhāvatīvyūha-sūtra ndogo
	231	1	Sukhāvatīvyūha-sūtra
	231	14	Vimalakīrti-nirdeśa-sūtra
3	232	1	Dhammapada Aṭṭhakathā 1
	232	14	AN 34-2
	233	8	Dhammapada Aṭṭhakathā 1
	234	1	AN 5-1
	234	5	Sarvāstivāda-saṃghavedaka-vastu 10
	234	19	MN 9-86, Aṅgulimāla-sutta
	235	18	AN 26

VIAMBATISHO

HISTORIA FUPI YA UBUDDHA

1. INDIA

Mojawapo ya matukio maalum ya kukumbukwa, katika historia ya kiroho ya binadamu lilijitambulisha wakati "mwanga wa Asia" ulipoangaza katika sehemu ya kati ya India, au kwa maneno mengine chemchem ya Hekima Kuu na Huruma ilipobubujika kule, ambayo imetokea kustawisha moyo wa binadamu kwa muda wa karne nyingi hadi sasa.

Buddha Gautama, aliyekuja kujulikana kwa wafuasi wa baadaye kama Shakyamuni au " Mtu wa Hekima katika ukoo wa Shakya" aliacha mji wake akawa mwombaji na akafunga safari kuelekea kusini hadi magadha. Inakisiwa na kuaminiwa kuwa Buddha aliupata Uongofu (Nuru) katikati ya karne ya tano KK chini ya mti uitwao Bodhi. Kuanzia hapo aliendelea na juhudi zake bila kuchoka kwa muda wa miaka 45 akihubiri mafundisho ya hekima, na Huruma hadi alipokutana na " Kifo chake kikuu" ambapo aliingia Maha - pari- Nirvana, wakati wote akiwa anafundisha juu ya hekima na huruma. Matokeo yake, Mabuddha waliendelea kujitokeza katika falme na makabila mbalimbali katikati ya India.

Mnamo nyakati za utawala wa Mfalme Asoka (aliyetawala: 268 - 232 K.K) mtawala wa tatu wa ufalme wa Maurya, mafundisho ya Buddha Gautama yalienea katika nchi yote ya India na hata nje ya mipaka yake.

Maurya ilikuwa ya kwanza katika muungano wa falme za India. Wakati wa mtawala wake wa kwanza, Chandragupta (alitawala : 316 - 293 K.K au nyakati kama hizo) ufalme huu ulikuwa ukitawala milki kubwa kuanzia milima ya Himalaya Kasakazini hadi katika Ghuba ya Bengal Mashariki, kutoka katika milima ya Hindu Kush Magharibi na ng'ambo ya milima ya Vindhya sehemu ya Kusini.

Mfalme Asoka aliendelea kuipanua milki hii hadi nyanda za Deccan alipoiteka Kalinga na Sehemu nyinginezo.

Mfalme huyu anasemekana kuwa alikuwa na tabia ya gadhabu, watu wakimwita Chandāsoka (Harara Asoka). Lakini tabia yake ilibadilika aliposhuhudia maafa mabaya yaliyotokana na vita vya kuiteka Kalinga. Alipindukia kuwa mfuasi mzuri wa mafundisho ya Hekima na Huruma. Baada ya hapo, alitenda mambo mengi kama muumini wa Buddha, kati yake kazi mbili zifuatazo ni za kukumbukwa.

Kwanza, zilikuwa ni " sheria za Asoka," au dhana za utawala zilizojengwa juu ya mafundisho ya Buddha zilizochorwa juu ya nguzo za mawe, alizoamrisha zichorwe katika sehemu nyingine mbalimbali ili kueneza mafundisho ya Buddha. Pili, alituma wajumbe nje ya milki yake katika nchi mbalimbali wakieneza mafundisho ya Hekima na Huruma pande zote. Jambo la kukumbukwa ni kwamba baadhi ya wajumbe walitumwa sehemu za Syria, Misri, Krene, Makedonia na Epeiro kueneza UBuddha kwa marefu na mapana Magharibi ya dunia. Waama, Mahendra (Mahindo katika lugha ya Pāli) mjumbe aliyepelekwa Tāmraparni au Siloni (Ceylon) alifanikiwa katika " Kuanzisha mafundisho mema juu ya Lankādvīpa (Pāli, Lankādīpa) njema" na hivyo akaweka msingi wa mahali pa kuanzia kueneza mafundisho ya Buddha kwa mafanikio kisiwani.

2. KUSTAWI NAKUENEA KWA U - BUDDHA WA MAHAYANA

" Mkondo wa Mashariki na U - Buddha" umezungumziwa sana na wafuasi wa Buddha wa siku za kale. Lakini mnamo karne za kabla ya Kristo, sura ya U - Buddha ilielekezwa Magharibi. Ilikuwa wakati wa mwanzo wa muhula wa ukristo "sura" Ya U - Buddha ilipoanza kuelekezwa Mashariki. Walakini kabla ya kurejea kwenye jambo hili, tuzungumzie mageuzi yaliyotokea katika U - Buddha. Badiliko hili lilikuwa si jingine bali "Wimbi jipya" Inavyojulikana kama U - Buddha

wa Mahayana au Gari Kuu la U - Buddha, ambao ulikuwa unajiimarisha barabara na kujitokeza wazi katika mafundisho ya wakati huo.

Nani, lini na vipi "Wimbi jipya" lilianzishwa? Hadi sasa hakuna mwenye uwezo wa kujibu kwa usahihi maswali haya. Tunachokifahamu ni: Kwanza, mkondo ulioibuka utakuwa katika kiti kinachoitwa kizazi - fikirika sehemu ya mchanganyiko wa shule ya Mahāsaṁghika kwa makasisi waliofanikiwa wa wakati huo; Pili, ukweli ni kwamba yalikwisha kuwepo baadhi ya maelezo ya msingi ya maandiko matakatifu ya Mahayana kuanzia karne ya kwanza au ya pili BK hadi karne ya kwanza ya muhula wa ukristo. Hata wakati wazo zuri la Nāgārjuna likiungwa mkono na maandishi ya Mahayana, lilikuzwa, uwaziwazi u-Buddha wa Mahayanaa, ulizidi kujitokeza mbele katika jukwaa la historia ya dini.

Kazi iliyotendwa na U - Buddha wa Mahayana ilikuwa kubwa sana katika historia ndefu ya U - Buddha. Sasa, kwa Uchina na Japan, U - Buddha kwa nchi hizi kwa karibu historia yake yote, umestawi kwenye msingi wa Mafundisho ya Mahayana. Hili halielekei kuwa jambo geni kwani kulishakuwepo na wazo adilifu kwa wokovu wa umma, likioanisha watakatifu hai katika mtizamo wa Bodhisattvas kueneza wazo hili; zaidi ya hapo, katika kuwaunga mkono, matokeo ya kielimu katika uwanja wa elimu au saikolojia yaliyokuwa yameletwa na wanagenzi wa Mahayana yalikuwa ya maana. Katika hali hii ingawa ilihusishwa na mafundisho ya Buddha Gautama kwa upande mmoja awamu mpya za hekima na maadili ziliongezewa. Kwa nyongeza hizi mpya U - Buddha ulipata nguvu na harufu mpya zilizoboresha nchi za Mashariki kama kasi ya mkondo wa mto mkubwa.

3. MASHARIKI YA KATI

China ilipata habari za U - Buddha kutoka katika nchi za Asia ya kati. Hivyo basi tunapozungumzia mafundisho kuenea kutoka India hadi

Uchina, hatuna budi kuzungumzia Barabara ya Hariri. Barabara hii ikipitia katika nchi zisizo na mipaka katikati ya Asia kuunganisha Magharibi na Mashariki, na ilikuwa katika umri wa Mfalme Wu wa Nasaba ya Han (aliyetawala 140 - 87 K.K), njia hii ilipofunguliwa. Wakati huo milki ya Han ilienea hadi Magharibi na katika nchi zilizoipakana kama Ferghana, Sogdiana, Tukhara, na hata Parthia, na moyo wa kibiashara uliokuwa umeingizwa na Alexander mkuu ulikuwa bado unapamba moto. Katika njia hii iliyopita katika nchi hizo, hariri ilichukua nafasi muhimu sana na ndiyo sababu ikaitwa Barabara ya Hariri. Kuanzia labda muda kidogo kabla au baada ya muda wa mwanzo wa muhula wa ukristo India na Uchina zilianza uhusiano wa kiutamaduni kwanza kwa njia ya barabara ya biashara. Kwa hiyo barabara inaweza kusemwa kuwa imekuwa njia ya U - Buddha vilevile.

4. UCHINA

Historia ya U - Buddha wa Kichina inaanza na wao kukubali maandiko ya Buddha na tafsiri yake iliyofuata. Maandiko ya zamani sana yasemekana kuwa ni "Ssu - Shih - êr - châng - ching"
(Sutra katika sehemu arobaini na mbili zilizotamkwa na Buddha)". Tafsiri iliyofanywa na Kāśyapamātaṅga na wengine wakati wa kipindi cha Ying - P'ing (58 - 76 B.K) cha Mfalme King Ming wa milki iliyofuatia ya Han ya Mashariki ingawa sasa inadhaniwa kuwa hadithi hiyo siyo ya kweli. Mtizamo wa pamoja sasa unatoa shukrani kwa An - shih - kao aliyeshughulika katika kutafsiri huko Lo - yang kuanzia mwaka 148 hadi 171 B.K. Kuanzia sasa hadi wakati wa Nasaba ya Kaskazini ya Sung (960 - 1129 B.K) kazi ya kutafsiri iliendelea kwa zaidi ya miaka elfu moja.

Mnamo miaka ya mwanzo watu waliofanya kazi za Uhasisi maandiko na kufanya tafsiri zake wengi wao walikuwa makasisi kutoka nchi za katikati ya Asia. Kwa mfano An - shih - kao, aliyetajwa hapo juu, alitoka Parthia, K'ang - sêng - k'ai, kutoka eneo la Samarkand alikwenda Lo - yang mnamo karne ya tatu na akatafsiri

"Sukhāvativyūha" (Kitabu cha maisha yasiyo na kikomo). Aidha, Chu - fa - hu au Dharmaraksha, anayejulikana kama mfasiri wa "Saddharma - puṇḍarīka" alitoka Tukhāra na aliishi Lo - yang tangu mwisho wa karne ya tatu hadi sehemu ya mwanzo ya karne ya nne. Wakati alipojitokeza kumārajīva, kutoka Kucha, mnamo mwanzoni mwa karne ya tano, kazi ya kutafsiri ilikuwa imefikia kiwango cha juu sana huko Uchina.

Kuanzia wakati huo, makasisi kutoka Uchina walianza kuitembelea India kujifunza Sanskrit. Mtangulizi wa makasisi hao alikuwa Bwana Fa-hsien (339-420? BK). Aliondoka Ch'ang-an mnamo 399 kwenda India na alirudi nyumbani baada ya miaka kumi na mitano. Kasisi mteule kati ya wale walioitembalea India alikuwa Hsuan - chuang (600-664 BK) aliyefika huko mwaka 627 na kurudi nyumbani katika mwaka 645 baada ya miaka kumi na tisa. Tena I - ching (635 - 713 B.K) (bila ya kumchanganya na jina la kitabu I - ching) alifunga safari kwenda India kwa njia ya bahari mnamo 671 na alirudi nyumbani kwa njia hiyo hiyo baada ya miaka ishirini na mitano

Makasisi hawa waliitembelea India wao wenyewe kujifunza Sanskrit na kurudi nyumbani na maandiko waliyokuwa wameyachagua, wakiwa watangulizi katika kazi za kutafsiri. Uwezo wa kiisimu wa Lugha aliokuwa nao Hsuan - chuang ulikuwa wa hali ya juu na kwa juhudi zake, kazi ya kutafsiri maandiko ilikuwa imepiga hatua kubwa. Kazi za awali zilizofanywa na watangulizi kama vile Kumārajīva inaitwa "Tafsiri za kale" na kazi za Hsuan - chuanga na wafasiri waliofuata zinaitwa "Tafsiri mpya" na wanagenzi wa U-Buddha katika nyakati zilizofuatia.

Kutokana na wingi wa juzuu walizokuwa wamezitafsiri kutoka Sanskrit mwelekeo wa fikra na shughuli za kidini za wanazuoni hawa, taratibu, ingawa kwa nguvu ziligeukia katika shari. Ilijitokeza dhahiri hali ya ujamii na tabia halisi ya mahitaji na kujiamini. Ukweli kwamba makasisi katika hatua za mwanzo walielekeza mioyo yao kwenye imani ya msingi wa "Hakuna kinachodumu" hasa inayozungumziwa katika Prajñā ya Sutra ilikuwa ni udhihirisho wa mwelekeo huu. Baadaye

walitupilia mbali kile kilichoitwa "Hinayana", au Gari kuu. Waama mwelekeo huu taratibu ulijitokeza katika dhehebu la Tendai na inasemekana kuwa ulikuwa umefikia kilele chake lilipojitokeza dhehebu la Zen.

Ilikuwa katika sehemu ya pili ya karne ya Sita wakati Dhehebu la Tendai liliposhuhudia ukamilifu wake katika Uchina, iliyokamilishwa na Tendai Daishi, Chih - i (538 - 597 B.K) mzee wao mkuu wa tatu. Alikuwa mmojawapo wa watu mashuhuri sana katika imani ya U-Buddha na uchambuzi wa makini katika mafundisho ya Buddha katika Vipindi vitano na kanuni nane alizozitengeneza mtakatifu huyu yamekuwa na mvuto mkubwa katika U - Buddha wa China pamoja na Japan.

Uchambuzi utaonyesha kuwa katika Uchina, Sutras nyingi zililetwa Uchina bila kujua wala kujali mpangilio wa asili au chimbuko lake na Sutras hizo zilitafsiriwa kama zilivyopokelewa. Katika mlundikano wa Sutras hizi lilijitokeza tatizo la kuelewa asili na tathimini zao. Ilikuwa muhimu kuupokea U - Buddha kwa ujumla na kuonyesha jinsi mtu atakavyosimama kufuatana na uelewa wake. Katika tathmini ya Sutras, muelekeo wa mtizamo wa Kichina, kwanza ni kwa watangulizi. Juu ya yote, ile ya Chih - i ilikuwa imepangwa kimantiki na hivyo rahisi kusadikika. Lakini baada ya kazi za uchambuzi wa U - Buddha wa kisasa kujitokeza, kazi yake Chih - i ilipoteza umaarufu wake.

Ndani ya historia ya U-Buddha katika Uchina "Lilokuwa la Mwisho" ilikuwa Dhehebu la Zen. Mwanzilishi wake inasemekana kuwa ni Śramana, kutoka nchi ya ugenini, au Bodhidharma (-528 B.K); lakini, mbegu aliyoipanda ilichanua maua baada ya Hui - nêng (638 - 713 B.K) mzee wa sita katika historia hii. Baada ya karne ya nane dhehebu hili katika Uchina lilishatoa makasisi wengi wenye vipaji wakifuatana huku ustawi wa Zen ukidumishwa kwa muda wa karne nyingi.

Inaonekana wazi kuwa kulikuwa na fikra mpya katika U - Buddha, iliyoweza kuzama katika asili ya Wachina. Haikuwa kitu kingine ila U

- Buddha uliopambwa na mtizano wa fikra wa kichina. Na kumbe mtiririko wa mafundisho ya Buddha Gautama pamoja na wimbi hili jipya lililoongezeka, yalifanya mto upanuke na ukatokea kurutubisha nchi zote za Mashariki.

5. JAPAN

Historia ya U - Buddha katika Japan ilianza katika karne ya sita. Mnamo mwaka 538 B.K, Mfalme wa Paikche (au Kudara, Korea) alituma ujumbe wake kuwasilisha sura ya U - Buddha na vitabu vya Sutras kwenye Baraza Tukufu la Mfalme Mkuu Kinmei. Huu ulikuwa mwanzo wa U - Buddha katika nchi hii. Kwa hiyo historia ya dini katika Japan ina umri wa zaidi ya miaka 1,400 sasa.

Katika historia hii ndefu tunaweza kufikiria U - Buddha wa Japan kwa kuihusisha na mitizamo mitatu. Wa kwanza unaweza kuwekwa kwenye U - Buddha wa mnamo karne ya saba, na nane. Kuonyesha hii kwa wazi ni ushahidi wa Hekalu la Horyuji (607 B.K) na Hekalu la Todaiji (752 B.K) yaliyojengwa wakati huo. Tukichunguza wakati huu kuna ukweli ambao hauwezi kusahaulika kuwa mkondo wa utamaduni ulikuja juu kuliko kawaida katika Asia yote, na ustaarabu wa Magharibi ulitupwa gizani. Msukumo imara na wa ajabu ulianza kujengeka kwa nguvu katika Asia. Katika Uchina, Mashariki ya katikati, India na nchi za Bahari ya Kusini, Shughuli za izidathira, kidini na kisanaa ziliendelea kwa nguvu. Kuunganisha misukumo hii U - Buddha ulikuwa ukitakasa nchi za Mashariki kwa mkondo wake mkuu wa huruma na utu. Na msukumo huu mpya wa utamaduni wa Kijapani kama unavyodhihirishwa na ujenzi wa mahekalu mazuri ya Horyuji na Todaiji, na pia kazi nzuri za kidini na kisanaa zilizojitokeza kwa kuhusiana na utamaduni ulivyoingia ndani hadi kingo za ncha ya Mashariki ambao ulikuwa unaikumba sehemu kubwa ya Asia.

Watu wa nchi hii, ambayo haikuwa na ustaarabu kwa miaka mingi, sasa waliogelea katika wimbi la utamaduni mkubwa; na ua la ustaarabu

lilichanua ghafla. Hii ilikuwa bahati iliyozungukia Ujapani katika karne hizo. Na mshindi mkuu mhusika wa kukua kwa utamaduni huu ni u - Buddha, mahekalu ya u - Buddha ya wakati ule yalikuwa vituo mashuhuri vya jamii, na makuhani walikuwa viongozi wa elimu mpya. Kuliinukia utamaduni mkubwa na usiokuwa wa kidini tu. Hii ilikuwa hali halisi ya u - Buddha ulioanziswa kwa mara ya kwanza katika nchi hii.

Katika karne ya tisa, makuhani wawili, Saicho (Dengyo Daishi 767 - 822) na Kukai (Kobo Daishi 774 - 835) walijitokeza na kuanzisha madhehebu mawili ambayo kwa pamoja yanaitwa u - Buddha wa Heia. Huku kulikuwa kuanziswa kwa u - Buddha wa Kijapani hasa. Walipokea u - Buddha katika msimamo na ufuasi wake halisi na wakawa watawa kuanzisha makazi ya kati ya watawa katika Milima ya Hiei na Koya. Katika muda wa miaka mitatu baada ya kuanzishwa, hadi kipindi cha Kamakura, madhehebu haya mawili Tendai na Shingon, yalikuwa na mahusiano, na yalistawi vizuri katikati ya watawala na katika viwanja na nyumba za kifalme.

Tunaweza kuupata mtizamo wa pili kwa kuangalia U-Buddha wa karne ya kumi na mbili na kumi na tatu. Walijitokeza makuhani wakuu kama Honen (1133 - 1212 B.K), Shinran (1173 - 1262 B.K) Dogen (1200 - 1253 B.K.) na Nichiren (1222 - 1282 B.K). Tunapozungunzia u - Buddha wa Japani hatuwezi kusita kutaja majina ya makuhani hawa watatu. Je, ni kwa nini karne hizo zilizotajwa zikawa na watu mashuhuri? Ni kwa sababu walikuwa wanakabiliwa na tatizo linalofanana kwa nyakati zile. Je walikabiliwa na tatizo gani? Huenda ilikuwa ni kukubalika kwa u - Buddha lakini katika njia ya pekee ya Kijapani.

Hii inaweza kutuleta kwenye swali, " Kwa nini haikuwa kweli kwamba u - Buddha ulikwishaingizwa katika nchi hii zamani kabla ya wakati huu? Ndivyo ilivyo kihistoria. Lakini ni kweli pia kuwa mamia ya miaka ilihitajika ili watu wa nchi hii waichambue na kuiumba vyakutosha dini ya kigeni ili kuifanya mali yao.

Kwa kifupi ilikuwa katika karne ya saba na nane wakati juhudi za kuukubali u - Buddha zilipoanza katika nchi hii, na matokeo yake dini ilichanua kwa nguvu kutokana na Mabuddha wa karne ya kumi na mbili na kumi na tatu.

Baada ya hapa, u - Buddha katika Ujapani iliyosimama juu ya msingi uliojengwa na makuhani maarufu, umezilinda kazi zake hadi leo. Tangu wakati ule walipojitokeza wateule, hakuna un'gavu wowote wa karne hizo umeishajitokeza tena katika historia ya u - Buddha nchini Ujapani. Hata hivyo, inaelekea kwa mwandishi wa leo kuwa kuna kitu kingine kinachotuvutia, nacho ni matunda ya uchunguzi wa kisasa katika u - Buddha wa asili.

Tangu kukubalika kwake kwa mara ya kwamza, kwa kweli u - Buddha wote katika Japani ulikuwa Mahayana, kwa mvuto na ushawishi wa u - Buddha wa kichina. Hasa baada ya kujitokeza kwa walimu mashuhuri katika karne za kumi na mbili na kumi na tatu, mafundisho ya Mahayana yalijenga wimbi kubwa na waasisi wa madhehebu wakiwa kitovu chake; Mtizamo huo unadumu hadi leo hii.
Katika historia ya u - Buddha katika Japani, uchambuzi wa uchunguzi juu ya u - Buddha wa asili ulianza baada ya kipindi cha kati cha Meiji. Sura ya Buddha Gautama ilijitokeza barabara kwa wale wote waliokuwa wanaelekea kusahau kuwa kulikuwa na Muasisi wa u - Buddha mbali na waanzilishi wa madhehebu, na pia ilidhihirishwa kwa wale ambao hawakukubali lolote lile mbali na mafundisho ya Mahayana, kwamba kulikuwa na taratibu za imani za u- Buddha. Hatua hizi mpya bado zipo katika uwanja wa wasomi na bado hazina nguvu kuamsha shauku ya kidini kwa umma. Lakini inaonekana maarifa ya watu wa nchi hii juu ya u - Buddha yanaelekea kupinda. Mwandishi angependelea kudhihirisha hatua hii na kuiita ya tatu au ya mwisho kati ya mitizamo mitatu iliyozungumziwa hapo juu.

KUENEZWA KWA MAFUNDISHO YA BUDDHA

U-Buddha ni dini iliyojengwa juu ya mafundisho ya Shakyamuni aliyokuwa ameyafundisha kwa muda wa miaka arobaini na tano ya maisha yake. Kwa hiyo maneno aliyoyatumia katika mafundisho yake ni madhubuti na sahihi katika dini hii, na ingawa kuna milango 84,000 ya dharma na shule nyingi vyote vinatokana na maandiko ya Shakyamuni. Vitabu vile yalimoandikwa mafundisho ya Buddha vinaitwa Issaikyo au Daizokyo, maana yake mkusanyo kamili wa maandiko matakatifu.

Shakyamuni alidai usawa wa binadamu kwa bidii sana na alifundisha kwa lugha nyepesi ili kila mmoja aweze kumwelewa kwa urahisi. Aliendelea kuhubiri kwa manufaa ya watu wengi hadi dakika ya mwisho alipokufa akiwa na umri wa miaka themanini.

Baada ya kifo cha Shakyamuni, wanafunzi wake walihubiri habari ya kweli kama walivyokuwa wamesikia. Hata hivyo, kadri mafundisho yalivyoenezwa na kusimuliwa ndivyo baadhi ya tofauti zilivyojitokeza kutokana na makosa yasiyo kusudiwa yaliyotokana na hali ya wafuasi katika yale waliyodhani kuwa wameyasikia au kuyaelewa. Na kumbe, maneno ya Shakyamuni yanapaswa kuenezwa kwa usahihi na watu wote bila ubaguzi. Kwa hiyo, wengi wa makuhani wakuu walikaa pamoja kwa nia ya kurekebisha, kuunganisha na kuimarisha maneno na mafundisho wakieleza kila mmoja alichofikiri alikuwa amekisia na kwa njia hiyo wakakaa miezi na miezi wakibadilishana mawazo. Kazi iliyotokana na mkusanyiko huo inajulikana kama Ketsuju au Mafungamano. Hii inaonyesha jinsi walivyojaribu kwa uchaji wao kueneza maneno yale yale yaliyokuwa yamezungumziwa na mwalimu mkuu.

Mafundisho yalipokwisharekebishwa yaliandikwa. Kwenye maandiko yaliyoandikwa ziliongezwa tafsiri na fafanuzi na makuhani wasomi wa miaka iliyofuata na wakaiita Ron au fafanuzi. Mafundisho

ya Buddha mwenyewe, fafanuzi zilizoongezwa baadaye, na maagizo ya Buddha, yote yalikuja kuitwa Sanzokyo (Sehemu tatu za maandiko ya Buddha) au Tripitaka katika Sanskrit.

Sanzokyo au Tripitaka ina Kyozo, Ritsuzo na Ronzo; neno Zo yamaanisha chombo au mfuko. Kyo ina maana ya maandiko ya u - Buddha, Ritsu yamaanisha maagizo ya undugu ya Buddha, na Ron ni fafanuzi zilizoandikwa na makuhani wakuu.

Kulingana na desturi, u - Buddha unasemekana kuwa uliingizwa Uchina mnamo mwaka 67 B.K wakati wa utawala wa mfalme Ming katika miongozo ya mwisho ya Nasaba ya Mashariki ya Han (25 - 220 B.K). Lakini kwa uhakika ilikuwa miaka themanini na minne baadaye maandiko ya u - Buddha yalipoingizwa ndani ya Uchina na kutafsiriwa (mwaka 151 B.K) na Mfalme Huan wa nasaba ile ile. Kwa muda wa miaka 1700 kuanzia hapo juhudi za kutafsiriwa kwa maandiko katika kichina ziliendelea. Idadi ya vitabu na juzuu vilivyotafsiriwa vilifikia maandiko 1440 na juzuu 5586. Juhudi za kuhifadhi maandiko yaliyotafsiriwa ulianza mapema katika nasaba ya Wei,ila ilikuwa mnamo Nasaba ya Kaskazini ya Sung upigaji chapa wake ulipoanza. Lakini kuanzia wakati huo kazi za makuhani wakuu wa Kichina zilianza kuongezwa kwenye maandiko ya Buddha na haikuwa tena sahihi kuviita Tripitaka vitabu hivi. Ilipotawala Nasaba ya Suei vilipewa jina la Issaikyo au mkusanyo wa maandiko yote matakatifu, na ilipotawala Nasaba ya Tang viliitwa kwa jina jipya la Daizokyo au makusanyo ya maandiko yote ya u - Buddha, sheria na nyaraka.

U - Buddha uliingia Tibeti mnamo karne ya saba B.K, na muda kama miaka 150 katika karne ya tisa hadi kumi na moja B.K; juhudi ya kuyatafsiri maandiko ya Buddha iliendelea, na hakika maandiko yote yalitafsiriwa kwa wakati huo.

Kutokana na ukweli kwamba maandiko yalikuwa yametafsiriwa siyo tu katika Kikorea, Kijapani, Kisiloni, Kikambodia, Kituruki na Kiarabu, lugha zote za Mashariki na hata katika lugha za Kilatini, Kifaransa,

Kiingereza, Kijerumani na Kiitalia, tunaweza kusema kwa usahihi kuwa baraka za mafundisho ya Buddha sasa yameenea ulimwengu mzima.

Ila katika fikra nyingine, tukitafakari kuanzia kwenye aina ya tafsiri na historia ya mwanzo na chimbuko la kuenea na kustawi kwa dini hii muda wa miaka elfu mbili, kukiwa na tafsiri za vitabu zaidi elfu kumi na mbili inakuwa vigumu kupata maneno halisi na kweli yaliyozungumzwa na Shakyamuni hata kama tutatumia msaada wa Daizokyo." Kwa hiyo ni lazima kutafuta maelezo makuu kutoka " Daizokyo" na yawe msingi ambapo mtu anaweza kusimamia katika imani yake ya kidini.

Katika u - Buddha, mamlaka ya juu yamo katika maneno aliyoyasema Shakyamuni. Hivyo basi mafundisho ya u - Buddha hayana budi kuwa ni mafundisho yanayoendana na hali halisi ya maisha ya kila siku; vinginevyo yatashindwa kuamsha moyo wa mtu kutoka katika kilindi chake kuelekea kwenye kuyaamini mafundisho. Katika hali hii ili mafundisho tuweze kuyaita yetu yanahitajika yawe rahisi na wazi, maadilifu na yakutosheleza katika kuwakilisha mawazo yote yakiwa sahihi kwa maneno yanayotumika katika maisha ya kila siku.

Kitabu hiki ni matokeo ya fikra za hapo juu kikirithi " mkondo" wa Daizokyo yake ya zaidi ya miaka elfu mbili na mamia kadhaa. Ni kweli, kitabu hiki hakichukuliwi kuwa sahihi katika mahudhui yake. Maneno ya Buddha yana maana yenye kina kisicho kikomo na Uadilifu wake hauna kikomo kiasi kwamba mtu hushindwa kuyathamini kwa urahisi.

Kwa hiyo inaaminiwa kwamba kitabu hiki kitazidi kukuzwa na kuzidi kuwa chenye ukweli na thamani kubwa kwa kadri nakala zirudiwavyo na kutolewa siku za usoni, kama ilivyoazimiwa.

HISTORIA YA "MAFUNDISHO YA BUDDHA"

Kitabu hiki kinafuata chapa ya asili ya Kijapani iliyokusanywa na kupitiwa, iitwayo Newly Translated Buddhist Text kilichochapishwa mnamo Julai, 1925, na Shirika la Kueneza Kitabu cha "Newly Translated Text" lililoongozwa na kasisi Muan Kizu. Chapa hii ya kwanza ya Kijapani ilikusanywa na kuandikwa na Profesa Chizen Akanuma, wakishirikiana na wasomi wengi wa ki - Buddha katika Ujapani na ikachukua karibu miaka mitano kukichapisha.

Katika kipindi cha Showa (1926 -) kitabu cha Popular Edition of Buddhist Text katika Kijapani pia nacho kilichapishwa na shirika na kuenezwa pote katika Ujapani .

Julai, 1934 wakati wa vijana wa ki-Buddha wa Pan Pacific walipokutana Ujapani, The teaching of Buddha, tafsiri ya kingereza ya Popular Edition of Buddhisttda Text ilichapishwa na Fungamano la vijana wote wa Ki - Buddha katika Ujapani kwa msaada wa Bwana D . Goddard ikiwa ni kama kazi mojawapo ya fungamano hilo. Wakati wa kusherehekea miaka 70 tangu kuanzishwa kwa u - Buddha katika Marekani mwaka 1962, Bwana Yehan Numata, Mwanzilishi wa kampuni ya Mitutoyo, alichapisha toleo la Kiingereza la The Teaching of Buddha yeye binafsi.

Mwaka 1965 wakati Bw. Numata alipoanzisha shirika la kuendeleza u - Buddha katika Tokyo mojawapo ya kazi za shirika hilo zilizopangwa ni kuenezwa kwa toleo la kiingereza dunia nzima.

Ili kutimiza mpango huo kamati ya kupitia The Teaching of Buddha iliundwa mwaka 1966. Wajumbe wa kamati hiyo walikuwa Maprofesa, Kazuyoshi Kino, Shuyu Kanaoka, Zenno Ishigami, Shinko Sayeki, Kodo Matsunami, Shojun Bando, na Takemi Takase. Wengine waliohusika ni Profesa Fumio Masutani, Bw. N.A Wadell, na Bw Toshisuke Shimizu. Kwa hiyo toleo lote la Kiingereza - Kijapani la The Teaching of Buddha lilichapishwa katika mtindo mpya.

Mwaka 1972, Maprofesa Shuyu Kanaoka, Zenno Ishigami, Shoyu Hanayama, Kwansei Tamura, na Takemi Takase walifanya masahihisho ya makosa.

Tena, mnamo 1974 ili kusahihisha misemo isiyo sahihi katika toleo la Kiingereza iliyokuwa imebainishwa na Bw. Richard K. Stainer, kwa shirikisho, chini ya ushauri wake, Maprofesa Shojun Bando, Kodo Matsunami, Shinko Sayeki, Kwansei Tamura, Doyu Tokunaga na Shoyu Hanayama (Mhariri Mkuu) walikipitia kitabu. Katika mwaka 1978 na 1980 kulikuwapo na mkutano juu ya mada zilizopendekezwa na Bw. Shinroku Inouye, wajumbe wa kamati ya uhariri hapo juu pamoja na Profesa Shigeo Kamata na Yasuaki Nara walikutana tena kukipitia kitabu hicho tena. Hivyo basi, toleo la kiingereza-Kijapani la The Teaching of Buddha ilichapishwa katika mtindo wa sasa yakiwa matunda ya kazi yao.

Katika mwaka 1980 ilikubalika kuwa Muda umefika wa kutafsiri kitabu hiki katika lugha zaidi ya nne (Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kihispania) zilizokuwepo. Kwa hiyo, kwa mara nyingine shirika lilimuomba Bw. Steiner kukihakiki kiingereza katika kitabu hicho ili kutafsiriwa katika Kijerumani, Kiitalia, Kigriki, Kichina, Kiholanzi na Kinepali.

Tena, mnamo 1981 ili kukifanya kitabu hiki kiwe rahisi tuliwaomba wanafunzi wa Kijapani na Kimarekani wakisome. Baadaye wahariri walikutana na kuzungumzia mabadiliko pamoja na wanafunzi hawa , na matokeo yake kitabu kilirudiwa na kutolewa upya. May, 1986

REJEA YA
"MAFUNDISHO YA BUDDHA"

	Ukurasa	Mstari
Maisha ya binadamu		
Maana ya maisha	5	7
Hali halisi za dunia hii	90	20
Njia adilifu ya maisha	228	17
Maoni potofu juu ya maisha	42	6
Dondoo sahihi la maisha	39	1
Maisha ya mashaka	54	3
Kwa wale waliodanganyika (mfano)	118	14
Maisha ya mtu (mfano)	85	1
Ikiwa mtu ataishi maisha yenye uchafu na tamaa (mfano)	84	6
Yapi yatafundishwa na wazee, wagonjwa na wafu (hadithi)	87	14
Kifo hakiepukiki (hadithi)	88	22
Mambo matano ambayo hakuna ye yote awezaye kuyatimiza duniani	46	2
Kweli nne katika dunia hii	46	11
Madanganyo na Wongofu vyote chimbuko lake ni katika moyo	47	1
Vitu ishirini vya thamani ambavyo ni vigumu mtu wa kawaida kutimiza	124	12
Imani		
Imani ni moto	164	6
Imani ina vitu vitatu muhimu	165	15

	Ukurasa	Mstari
Imani ni matendo	166	17
Imani hujitokeza ndani ya moyo adilifu	165	5
Ni vigumu kutafuta ukweli kama ilivyo vigumu kwa kipofu kujaribu kusimulia sura ya tembo kwa kugusa (mfano)	70	6
Mahali ambapo uasili Buddha upo huonyeshwa kwa mafundisho ya kweli ya u - Buddha (mfano)	71	12
Uasili - Buddha umefichwa na tamaa (mfano)	72	17
Mashaka huzuia imani	167	4
Buddha ni baba wa dunia yote na binadamu ni watoto wake	33	13
Hekima ya Buddha ni pana na yenye kina kirefu kama bahari kuu	32	6
Roho ya Buddha imejaa huruma kuu	14	1
Buddha hana mwili halisi	15	1
Buddha alihubiri katika maisha yake yote	13	1
Buddha alitumia matukio ya maisha na kifo kuwashawishi watu	21	20
Buddha aliokoa watu kutokana na mateso yao kwa kutumia matendo yaliyo kwenye (mfano)	22	2
"	17	13
"	18	11
Dunia ya Uongofu	230	8
Kuwa wafuasi wa Buddha, Dharma na Samgha	163	5

	Ukurasa	Mstari
Kujifunza njia za kuyatunza maandishi, kujaribu kuutuliza moyo na kutenda kwa uadilifu	150	14
Njia nne takatifu	153	9
Njia sita za kufikia ng'ambo nyingine ya wokovu	155	1
Taratibu nne za haki	154	14
Vigezo vinne vya kufikiria	154	6
Vitivo vitano vya nguvu ya kupatia Wongofu	154	19
Hali nne za moyo zisizo na kikomo	157	5
Wale waelewao hali nne takatifu	37	13
Kifo cha binadamu na maisha ya mpito	12	3
Watazaliwa katika nchi yake takatifu	106	11
Jifanye ni mwanga, jiamini	10	3
Mafunzo ya akili		
Yampasa mtu kuyashika yale yaliyo muhimu kwake mwenyewe (mfano)	139	7
Kuwa makini na hatua za mwanzoni	124	8
Usisahau unachokitafuta (mfano)	140	21
Ili kufanikiwa katika jambo lolote yampasa mtu kuvumilia vikwazo vingi (hadithi)	146	6
Jipe moyo hata wakati unapozidi kutofanikiwa (Hadithi)	158	16
Usifanye moyo wako usumbuliwe hata wakati wa hali zisizoridhisha (hadithi)	115	13
Wale waelewao na kufuata njia takatifu ni sawa na kwenda gizani ukiwa na taa	38	5

	Ukurasa	Mstari
Mtu atakuta mafundisho juu ya maisha ya binadamu popote aendapo (Hadithi)	149	1
Watu huelekea upande waelekezwao na moyo wao	113	13
Maana ya kujifunza ni kumiliki moyo wako mwenyewe	10	19
Umiliki moyo wako kwanza	194	1
Iwapo utamiliki moyo wako	113	17
Hali tofauti za moyo (mfano)	110	10
Moyo si nafsi ya mtu	44	12
Usiruhusu moyo ukuyumbishe	10	6
Uteke moyo wako	142	18
Uwe mtawala wa moyo wako	11	4
Maovu hutoka kwenye mwili, mdomo na moyo	78	18
Uhusiano kati ya moyo na maneno	117	1
Mwili huu si kitu bali jambo la kupotoshwa (Hadithi)	133	8
Mwili huu umejaa kutu za kila aina	122	8
Usitamani chochote	10	6
Takasa mwili, mdomo na moyo	115	10
Usiwe na upendeleo na weka jitihada (hadithi)	158	1
Mateso ya binadamu		
Mateso ya binadamu hutokana na moyo wa kufungamana/kupambanua	41	9
Namna ya kuzuia mateso	12	12

	Ukurasa	Mstari
Madanganyo na ujinga hutengeneza milango ya Uongofu	56	3
Namna ya kujikomboa kutokana na mateso	108	1
Wakati moto mkali wa tamaa unapozimwa, Uongofu wa kustarehesha unaweza kupatikana	132	1
Ngoa ndio hasa chanzo cha madanganyo	80	8
Fikiria ngoa, ufuska kama ni nyoka aliyejificha ndani ya maua	80	9
Usishikamane na nyumba iunguayo (mfano)	17	13
Tamaa ni chanzo cha maovu	110	3
Dunia hii ni moto uunguzao	77	17
Iwapo watu watatafuta umaarufu na heshima, ni sawa na kujiunguza wenyewe	111	8
Mtu akitafuta utajiri na uzinzi, atajiharibu mwenyewe	111	12
Watu wenye busara na wajinga hutofautiana katika asili zao	125	8
Wajinga hawayatambui makosa yao (mfano)	131	12
Ujinga huonea wivu bahati njema ya wengine kwa kuangalia tu matokeo (mfano)	136	15
Njia ambayo wajinga huelekea kufuata (mfano)	131	16
Maisha ya kila siku		
Toa sadaka na kusahau	155	21
Aina saba za sadaka bila utajiri	156	4
Namna ya kupata utajiri (Hadithi)	135	9
Jinsi furaha iletwavyo	123	24
Usisahau kamwe wema uliotendewa (hadithi)	129	19

	Ukurasa	Mstari
Utofauti katika tabia za watu	83	16
Balaa huandamana pamoja na hatua apitiazo mtu atoaye nafasi kwa tamaa ya kulipiza kisasi	123	12
Namna ya kupoza hasira	225	13
Usisumbuliwe na bezo kutoka kwa wengine (hadithi)	114	4
Hamuishi kwa ajili ya mavazi, chakula au malazi	188	7
Chakula na mavazi sio kwa ajili ya raha au starehe	109	1
La kufikiria unapokula	190	15
La kufikiria unapovaa nguo	189	21
La kufikiria wakati unapokwenda kulala	191	6
La kufikiria wakati wa joto au baridi	190	17
La kufikiria katika maisha yako ya kila siku	189	5
Serikali		
Njia ya kuelekeza taifa katika fanaka	210	9
Njia kwa mtawala	213	14
Mtawala ajitawale	211	14
Ukweli wa utawala ni kuifunza mioyo ya watu	212	15
Tabia wapaswayo kuwa nayo mawaziri na maofisa	216	13
Namna Jaji apaswavyo kushughulikia wahalifu	215	16
Athari za kuwafunza watu wa taifa	213	8
Namna ya kukabiliana na mapambano ya maisha	218	13

	Ukurasa	Mstari
Uchumi		
Vitu lazima vitumike vizuri (Hadithi)	202	6
Hakuna kitu kilicho mali ya mtu milele	202	1
Mtu asihodhi vitu kwa ajili ya manufaa yake binafsi	208	16
Namna ya kuongeza utajiri (Hadithi)	135	9
Maisha ya familia		
Familia ni mahali ambapo mioyo ya wanajamii huunganishwa pamoja	199	17
Vitu ambavyo vitavuruga familia	194	15
Njia za kulipa fadhila mtu atendewazo na wazazi wake	199	10
Njia nzuri za mtoto kufanya kwa wazazi wake	195	14
Njia sahihi za mume na mke	196	14
Mume na mke lazima wawe na imani sawa (Hadithi)	205	1
Maisha ya wanawake		
Aina nne za wanawake	203	5
Aina mbali mbali za wake	205	19
Mafundisho kwa wake wachanga (Hadithi)	204	3
Kwa manufaa ya wanawake kuolewa	204	3
Kwa manufaa ya wanawake wachanga na warembo	207	12
Ni vipi wanaume wanaweza kuheshimu wake zao	121	21
Tabia ya wanaume kwa wanawake	204	19

	Ukurasa	Mstari
Viapo na matakwa ya mwanamke halisi	208	13
Mke mbaya ni yupi?	205	19
Njia ya Ndugu wasio na makazi		
Mtu hawi ndugu asiye na makazi kwa vile tu anavaa kama mtawa na kutamka maneno matakatifu ya Sutras	180	23
Ndugu wasio na makazi sio warithi wa hekalu na vifaa vyake	178	1
Watu wenye tamaa hawawezi kuwa watawa wa kweli	178	7
Maisha halisi apasayo kuishi ndugu asiye na makazi (kwao)	179	23
Maisha ya jamii		
Maana ya maisha ya jamii	221	8
Hali halisi ya dunia hii	90	20
Aina tatu za uongozi	221	13
Maisha ya kweli ya jamii	222	1
Mwanga mkuu umulikao giza	220	7
Uelewano katika mahusiano ya watu	222	15
Mambo yatakayosaidia kuiongoza jamii	223	15
Uhalisi wa udugu	222	17
Ujamaa halisi wa wafuasi wa u - Buddha	229	22
Wale wavurugao sheria ya amani Wataharibikiwa (mfano)	130	19
Wale walio na uvivu na wagombanao na wenzao wataharibikiwa (mfano)	130	19
Watunze wazee kwa heshima (Hadithi)	126	1

	Ukurasa	Mstari
Mwanafunzi apaswavyo kumtendea mwalimu na mwalimu apaswavyo kumtemdea mwanafunzi	196	4
Kanuni za urafiki	196	22
Namna ya kuchagua rafiki wazuri	198	6
Namna ya mtumishi na mtumikiwa wapaswavyo kutendeana	197	7
Namna ya kuwakabili majambazi	209	2
Mambo ya kufikiriwa na wale wanaodhamiria kufundisha Dharma	182	7

REJEA YA SANSKRIT (kufuata mpangilio wa herufi)

ANĀTMAN (pasipo -nafsi/u-mimi)

Hii ni mojawapo ya mambo ya msingi katika U - Buddha. Vitu vyote na uhai wote havina maana wala hakika. Ni jambo la kawaida kwa u - Buddha, unaohubiri kutokudumu kwa kila kitu, kusisitiza kuwa kutokudumu kwa vitu vyote hakuwezi tena kuwa na hakika ndani yake. Anātman inaweza kutafsiriwa pia kama isiyo na Roho.

ANITYA (Hali ya mpito au kutodumu)

Jambo jingine la msingi katika u - Buddha. Uhai, maisha na vitu, katika ulimwengu huu vinabadilika mara kwa mara bila kukoma angalau kwa kitambo kidogo. Kila kitu lazima kife au kifikie mwisho wake katika siku za usoni mwake, na matazamio haya ndiyo chanzo halisi cha mateso. Dhana hii isitafsiriwe kwa mtizamo wa chuki , au ubaya, kwa sababu uzazi na maendeleo vyote ni udhihirisho wa mabadiliko hayo ya mara kwa mara.

BODHISATTVA (Anayejitahidi kuipata NURU/ Wongofu)

Mwanzoni jina hili lilitumika kuonyesha Gautama Siddhārtha kabla hajaipata NURU. Baada ya kutokea u - Buddha wa Mahāyāna wale wote waliojibiidisha na u- Buddha wakajulikana kwa jina hili. Mwisho wale wanaojaribu kuwaelekeza wenzao kwenye udugu wa ki - Buddha kwa njia za huruma kuu huku wakijibiidisha kuelekea kwenye lengo lilelile, wametambulishwa kwa Ishara ya Wabodhisattva; Avalokiteśvara (Kwannon), Kṣitigarbha (Jizō) Mañjuśrī (Mon-ju) ni kati ya wachache wanaojulikana vizuri.

BUDDHA (Aliyemwongofu)

Mwanzoni kabisa, Gautama Siddhārtha (Śākyamuni) muasisi wa u - Buddha aliitwa kwa jina hili kwa kuwa ni yeye aliyeipata NURU miaka 2,500 iliyopita, akiwa na umri wa miaka 35 huko India. Shabaha kuu ya wafuasi wa Buddha wote bila kujali mkondo au shule waliomo ni kuwa ma - Buddha. Kwa sababu ya utofauti wa njia za kufikia hali hii, u - Buddha umegawanyika katika madhehebu na shule mbali mbali. Katika u - Buddha wa Mahāyāna mbali na Śākyamuni, Buddha wa kihistoria, Śākyamuni, Mabuddha wengi kama vile Amitābha (Amida),

Mahāvairocana (Dainichi), Vaiṣajyaguru (Yakushi) n.k. wanakubalika kama alama za mafundisho ya u - Buddha. Wakiwa wameathiriwa na dhana ya u - Buddha wa imani ya Nchi Takatifu katika Ujapani (mtu anakuwa m - Buddha baada ya kuzaliwa tena katika Nchi Takatifu) wale wote waliokufa wanaitwa "ma - Buddha," au HOTOKE katika kijapani.

DHARMA (Mafundisho ya Kweli)

Haya ni mafundisho aliyofundisha Buddha, Aliyebarikiwa. Kuna aina tatu za kanuni katika mafundisho: Sūtras, (Mafundisho ya Buddha mwenyewe), Vinayas, (maadili yatolewayo na Buddha),na Abhidharmas, (fafanusi na mazungumzo juu ya Sūtras na Vinayas zilizotolewa na wasomi katika vipindi vya baadaye). Kanuni hizi tatu zinaitwa Tripiṭaka. Dharma ni moja kati ya hazina tatu za u - Buddha.

KARMAN (Matendo)

Ingawa maana ya asili ya neno hili ni "matendo", katika kuhusiana na nadharia ya chanzo limetokea kutambuliwa kama namna ya uwezo/ nguvu iliyotokana na kila tendo lililotendwa na mtu siku za nyuma. Hii ina maana kuwa kila moja ya matendo yetu hutokea katika wema au ubaya, mateso au furaha ikitegemeana na tendo lenyewe na lina uwezo wa kuathiri maisha yetu ya ahera, na hii inatambuliwa kama Karma ya mtu. Kuna kuamini kuwa tendo jema likirudiwa, wema utajumuishwa na uweza wake na utatenda kazi juu ya maisha ya ahera kama athari yenye manufaa. Kuna aina tatu za matendo; ya mwili, ya kauli na ya akili katika dhana hii.

MAHĀYĀNA (Gari Kuu)

Katika uelekeo wa historia ya u - Buddha ilitokea mikondo miwili ya mawazo, Mahāyāna na Theravāda (au Hīnayāna). U - Buddhawa ki - Mahāyāna ulienea Tibeti, Uchina, Korea, Ujapani n.k wakati u - Buddha wa Theravāda ulienea Burma, Śrī Lanka (Ceylon), Thailand n.k. Neno Mahāyāna lamaanisha "Gari kuu" linaloweza kubeba viumbe wote wanaoteseka katika dunia hii ya uzao na kifo, na linaloweza

kuwaongoza wote katika NURU bila kuwabagua.

NIRVĀṆA (Utulivu Kamili)

Maana yake ni "Kuungua". Hii ni hali ambapo uchafu wote wa binadamu na mateso vimeteketezwa kabisa kutokana na matendo na tafakuri kwa msingi wa Hekima Sahihi. Wote waliopata hali hii wanaitwa Mabuddha. Gautama Siddhārtha aliipata hali hii katika umri wa miaka 35 na akawa Buddha. Hata hivyo, inaaminika kwa sasa kuwa aliifikia hali ya raha mstarehe kamili baada ya kufa kwake, kwa sababu mabaki ya uchafu wa kibinadamu yangeendelea kuwepo ili mradi mwili wake halisi unaendelea kuishi.

PĀLI (Lugha)

Hii ni lugha iliyotumika katika u - Buddha wa Theravāda. Fungu la kanuni za zamani za u - Buddha ziliaminika kwa kuwa ziliandikwa katika Lugha hii. Kwa kuwa hii ni namna ya Praknt, lahaja ya Sanskrit, hakuna tofauti kubwa kati ya Pāli na Sanskrit, Dharma katika Sanskrit. Dharma katika Pāli, Nirvāṇa katika Sanskrit, Nibbāna katika Pāli, (Angalia - Sanskrit).

PĀRAMITĀ (Kuvuka hadi ng'ambo ya pili)

"Kuvuka hadi ngambo ya pili" ina maana ya kufikia katika nchi ya Buddha kwa kushika na kutenda maadili mbali mbali ya Buddha. Kwa kawaida maadili sita ya utendaji yafuatayo yanatambuliwa kuwa ni yale yanayomfanya mtu avuke kutoka katika ulimwengu huu wa uzawa na mauti hadi kwenye ulimwengu wa NURU. Sadaka (Matoleo), Uadilifu, uvumilivu, juhudi, umakini na Uamuzi sahihi (au Hekima). Majuma ya HIGAN katika utamaduni wa Kijapani katika majira ya kuchipua na vuli yanatokana na dhana hii ya ki - Buddha.

PRAJÑĀ (Hekima)

Ni mojawapo ya Pāramitās sita. Kazi ya akili inayomwezesha mtu kutambua maisha bila kukosea na kutofautisha kati ya ukweli na uwongo. Mtu alipatapo hili kwa usahihi huitwa Buddha. Kwa hiyo hii ni hekima iliyosafishwa na kutakaswa, tofauti na akili za binadamu za

kawaida.

SAṀGHA (Udugu wa ki - Buddha)

Ina - maanisha watawa wa kike na kiume, walei wa kike na kiume. Katika siku za kwanza iliwahusu watawa wa kike na kiume wasiokuwa na maskani. Baadaye, wakati mwamko wa Mahāyāna ulipoibuka, wale wote waliolenga kwenye Bodhisattva, bila kujali kama walikuwa walei au watawa, walijiunga pamoja katika undugu. Mojawapo ya hazina tatu za u - Buddha.

SANSKRIT (Lugha)

Lugha ya asili, ya kale ya India mojawapo ya lugha zilizotumiwa na familia za kihindi - Ulaya. Imegawanywa kwenye vedic na Sanskrit halisi. Maandishi ya asili ya Mahāyāna yameandikwa kwenye lugha hii katika mtindo ujulikanao kama U-Buddha uliobobea kwa Sanskrit (Buddhist Hybrid Sanskrit)

SAṀSĀRA (Kurudi katika mwili)

Marudio ya mara kwa mara ya uzawa na mauti kuanzia zamani, hadi leo na siku zijazo hupitia katika falme sita danganyifu: Jehanam, pepo zenye njaa, wanyama Aśura au Pepo zipiganazo, watu na peponi. Mpaka hapo mtu aipatapo nuru hawezi kukwepa gurudumu hili la kuhama kwa roho. Wale wote walio huru katika hii wanaweza kuitwa ma - Buddha.

ŚŪNYATĀ (Pasipo - Hakika) (Pasipo - Asili)

Hii ni dhana kuwa kitu hakina uhakika wa kudumu na ni mojawapo ya mambo ya msingi katika u - Buddha. Kwa kuwa kila kitu kinategemea sababisho haiwezekani kuwepo kwa nafasi ya kudumu kama asili au hakika. Lakini mtu asing'ang'anie kwenye dhana ya kwamba kila kitu kina hakika wala hakina. Kila kiumbe kiwe binadamu au si binadamu, kipo katika uwiano. Kwa hiyo ni ujinga kung'ang'ania wazo moja au dhana fulani au itikadi kana kwamba ndiyo kauli pekee. Haya ni maelekeo ya msingi katika maandiko ya Prajñā ya u - Buddha wa Mahāyāna.

SŪTRA (Maandiko)

Kumbukumbu za mafundisho ya Buddha Maana ya awali ni "Uzi," inayomaanisha kufunga maandiko kwa pamoja na kwa ufupi au muhtasari kutokana na mafunzo lukuki ya dini au elimu.

THERAVĀDA (au Hīnayāna : Watetezi wa Wazee)

Utamaduni wa kusini wa u - Buddha unawakilishwa na jina hili. "Thera" maana yake wazee. Hii ni shule ya wazee ambapo kihistoria kilikuwa ni kikundi cha watawa wenye kushikilia mambo ya kale na waliopendelea kuyafuata mafundisho kwa makini kinyume na kikundi kingine cha watawa kilichokuwa huru (ambao imani zao baadaye zilidhihirika katika Mahāyāna ndio utamaduni wa Kaskazini). Huu mkondo wa upinzani katika madhehebu ya Ukuhani wa ki - Buddha unasemekana ulianza mapema sana karne chache baada ya kifo cha Buddha, wakati Mahādeva mtawa mwenye mageuzi alipokazania tafsiri huria chini ya makundi matano ya mafundisho ya u - Buddha. Hii ilisababisha mgawanyiko katika Theravāda na Mahāsāṁghika ambapo ilikuwa chemuchemi ya Mahāyāna ya baadaye.

TRIPIṬAKA (vikapu vitatu)

Matawi matatu ya maandiko ya u - Buddha, Dharma, yana maana hii. Haya ni Sūtra, yenye mafundisho ya Buddha; Vinayas, yenye maadili yake, na Abhidharmas zenye fafanuzi na habari juu ya imani na mafundisho. Hapo badaye maandishi ya ki - Buddha yaliyoandikwa na makuhani - Wakuu wa kichina na Kijapani yaliingizwa katika kanuni za u - Buddha. Angalia - Dharma.

Watawa, kuna mtu mmoja ambaye uzawa wake katika dunia ni kwa manufaa ya wengi, kwa furaha ya wengi: aliyezaliwa kutokana na huruma kwa ajili ya dunia, kwa faida, manufaa na furaha ya viumbe wa mbinguni na binadamu. Mtu huyo ni nani? Ni Tathagata ambaye ni Arahat, huyu mtawa, ni mtu yule mmoja.

Watawa, ufunuo wa mtu mmoja ni nadra kuupata katika dunia. Wa mtu yupi? Tathagata ambaye ni Arahat, aliyeupata wokovu kamili. Ni yule mtu huyo mmoja.

Watawa vigumu kupatikana duniani ni mtu yule wa ajabu. Mtu yupi? Tathagata ambaye ni Arahat, aliyeupata wokovu kamili. Ni mtu huyo huyo mmoja.

Watawa, kifo cha mtu mmoja ni lazima kimsikitishe kila mmoja. Cha mtu yupi? Cha Tathagata ambaye ni Arahat, Aliyeupata wokovu kamili. Ni mtu yule mmoja.

Watawa, vigumu kupatikana duniani ni mtu yule wa ajabu. Mtu yupi? Tathagata aliye Arahat, aliyeupata wokovu. Ni mtu huyo mmoja.

Watawa, kuna mtu mmoja azaliwaye duniani ambaye hana ulinganisho wala usawa. Mtu huyo ni nani? Ni Tathagata ambaye ni Arahat, aliyeupata wokovu kamili. Ni mtu huyo mmoja.

Watawa, ufunuo wa mtu mmoja ni ufunuo wa jicho kuu, mwanga mkuu, nuru kuu. Wa mtu yupi? Wa Tathagata ambaye ni Arahat, Aliyepata wokovu kamili. Ni nani huyo mmoja (Aṅguttara Nikāya 1-13).

TAASISI YA KUENDELEZA NA KUENEZA
U-BUDDHA NA USAMBAZAJI WA

"MAFUNDISHO YA BUDDHA"

Katika kuendeleza u-Buddha ni muhimu kumzungumzia mfanyabiashara, na muungwana huyu ni Bwana Yehan Numata, mwanzilishi wa Kampuni ya uundaji ya Mitutoyo.

Alianzisha Kampuni ya kutengeneza zana za kuonyesha vipimo halisi katika mwaka 1934. Imani yake ni kuwa kufaulu kwa biashara hutegemea uhusiano wa karibu sana wa mbinguni, duniani na binadamu, na kwamba ukamilifu wa moyo wa binadamu unapatikana tu kwa uhusiano unaowiana wa hekima, huruma na ushupavu.

Kutokana na imani hii anafanya kila anachoweza kuendeleza ufundi wa utengenezaji wa zana za kupimia na kuendeleza moyo wa binadamu.

Ni imani yake kuwa kupata amani ya ulimwenguni kunawezekana tu kutokana na ukamilifu wa moyo wa binadamu kwa shabaha yenye mafundisho ya Buddha. Kwa hiyo mbali na kuongoza kampuni yake amekuwa akijibidiisha tangu mwanzo katika kueneza na kuboresha muziki wa kisasa wa ki-Buddha pamoja na kusambaza picha na mafundisho yake.

Desemba, 1965, aliimarisha taasisi kwa fedha zake binafsi katika shughuli za kutangaza u-Buddha na wakati ule ule kutoa msaada kwa ajili ya amani ya dunia. Kwa hiyo taasisi ya kueneza u-Buddha ikaanza kama taasisi ya umma.

Ni nini kinachofanyika katika kueneza mafundisho ya u-Buddha kwa marefu na mapana ili kila mmoja afaidike na kufurahia Mwanga na Hekima yake kuu na Huruma?

Ni kazi ya hii taasisi ya kuendeleza u-Buddha kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili, kwa kuzingatia wosia wa mwanzilishi wake. Kwa kifupi kila juhudi inayofanywa katika kutangaza mafundisho ya Buddha inakidhi haja ya Taasisi ya kuendeleza u-Buddha.

Kitabu hiki "Mafundisho ya Buddha" ni matokeo ya fikra zetu juu ya historia ya dini katika nchi hii, kwamba hapajakuwepo kitu chochote kilichoandikwa na tukakiita kitabu cha Mafundisho ya u-Buddha kama inavyotafsiriwa katika mtizamo wa Kijapani kwa uelekeo wake ingawa tumekuwa tukiheshimu utamaduni wa ki-Buddha kwa fahari kubwa.

Kitabu hiki kitatumika kama "chakula" cha kiroho kwa mtu ye yote atakayekisoma. Kimeandikwa jinsi kilivyo ili mtu ye yote aweze kukiweka katika meza yake au kwenda nacho na kukutana na mwanga wa kiroho kwa utashi wake.

Ingawa hakijafikia ukamilifu kama jinsi ambavyo tungependa, toleo la sasa la "Mafundisho ya Buddha" limetokea mbali, na limetokana na kazi na juhudi za watu wengi kwa nia ya kukidhi mahitaji ya watu wa kisasa kwenye kuanzisha u-Buddha unaokubalika na wenye maandishi yaliyo sahihi ambayo ni rahisi kusomeka na kueleweka, wakati ule ule yakawa ni mwongozo wa matendo na rejea ya kila siku na hamasa ya kweli.

Ni shauku na matumaini ya taasisi ya kueneza u-Buddha kuona siku inafika ambapo nyumba nyingi zinakuwa na kitabu hiki na watu wengi sana wanafurahi na kuoga katika mwanga wa Mwalimu Mkuu.

Maoni ya wasomaji yanakaribishwa.

Tafadhali jisikie huru kuiandikia taasisi ya kueneza na kuedeleza u-Buddha wakati wo wote.